# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

## Kikao cha Thelathini na Saba – Tarehe 28 Mei, 2019

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu!

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MHE. JAMES K. MILLYA - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti na Majukumu ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**MHE. JESCA D. KISHOA - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA NISHATI:**

Taarifa ya Msemeji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni juu ya Wizara ya Nishati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**SPIKA:** Ahsante sana. Katibu!

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Maswali Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Yahaya Omar Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi sasa aulize swali lake.

Na. 306

### Halmashauri ya Itigi kuwa Wilaya

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuza:-

Je, ni lini Serikali itaifanya Halmashauri ya Itigi kuwa Wilaya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Massare Mbunge wa Manyoni Mangharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza wakati majibu swali la Bunge Na. 287 kuhusu pendekezo la kugawa Mkoa wa Tanga, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikalli inatambua umuhimu wa kuanzisha maeneo mapya

ya utawala kwa ajili ya kusogeza huduma karibu na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa sasa Serikali imeweka kipaumbele cha kuhakikisha maeneo yalianzisha hivi karibuni yanaboresha na kuendelezwa kwa miundombinu na huduma mbalimbali zikiwemo Ofisi, makazi ya viongozi na watendaji, huduma za afya, elimu, maji, mawasiliano, barabara na umeme ili wananchi waanze kunufaika na huduma zinazotolewa na Serikali kupitia mamlaka hizo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahaya Massare swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, majibu haya Serikali ni mazuri na yana dhamira njema ya kuijenga nchi hii ifikie katika malengo mazuri. Lakini kuna majibu ya swali kama hili ambao niliuliza mwaka 2016 kama 2016/2017 na bahati nzuri kwenye hansard ninalo lilipata majibu ambao yalionyesha matumaini kwamba kuna siku Halmashauri ya Itigi inaweza kuwa Wilaya. Lakini kwa kuwa Halmashauri ya Itigi ni engeo ambao lina ukubwa wa *Squire* kilometa 17,000 ni sawa sawa baadhi ya mikoa ambao ipo katika nchi hii na ni tarafa moja.

Je, sasa Serikali ipo tayari kuwa tuachane na suala la kuongeza Wilaya tuondoe walau tuongeze tarafa ambazo hazitakuwa na ghamara kubwa za uendeshaji ikiwemo ofisi ya Wakuu na nini au madiwani?

La pili, katika eneo langu kuna kijiji kinaitwa Mitungu ambacho nacho kina eneo kubwa ukubwa wa eneo ni mkubwa sana lakini wananchi ni wengi. Kutoka katikati ya kijiji mpaka pembeni ni kilometa 40 upande mmoja na upande wa pili hivyo hivyo.

Je, Serikali iko tayari kufanya kazi nzuri kama nazofanya Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani ambaye anatamka jambo na linafanyiwa kazi na haraka unapata

matokeo. Je, kwenye kijiji hiki kimoja tu ambacho tunataka kugawanywa angalu kupata vijiji viwili kina watu zaidi elfu 30 Serikali ipo tayari angalu kusaidia na kunipa uwezekano wa mwaka 2020 kuona wepesi katika eneo hili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Mheshimiwa Mbunge tunakusudia na kutengependa apate wepesi mwaka 2020 na kwa kazi nzuri anayoifanya kuwasemea wananchi wake wa Manyoni tunaamini kwamba wataendelea kumwani na kumunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, ameuliza maswali mawili ya nyongeza kwa uchungu na akionyesha ukubwa wa nchi ulivyo na ameonyesha namna ambavyo alishapata majibu ya matumaini hapa Serikali inafanya tathimini kutoka mwaka hadi mwaka. Baada ya kufanya tathimini ya kuangalia maeneo ambayo bado yanazidi kuimarishwa kwa maana ya Ofisi na vitendea kazi vingine miradi ya maendeleo iliyopo na uwezo wa Serikali ndio maana tukaja na jibu la namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo amezungumza hapa kwanza maeneo haya yanafanya uchanguzi kwa mfano vijiji vya mwaka huu tayari timu yetu imeshatembelea maeneo mbalimbali kuangalia maeneo ya migoro mahali ambapo ilikubadilisha GN wameshafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tulipokee hili tuendelee kushauliana tuone kama haitaingiza gharama kubwa Serikalini. Kama ambavyo tunajua tukiongeza maeneo itakauwa gharama zaidi tutaona namna ambavyo kama kuna wepesi wa kuifanya ile kazi ili hawa wananchi waweze kupata huduma karibu. Lakini nawaomba waendelee kuwahimiza nia ya Serikali ni njema sana na Wabunge

watakubaliana na sisi kwamba kwa kweli kama unaanzisha maeneo mapya na kati ya hapa kuna watu ambao wadai ofisi za mikoa kuna ofisi za wilaya, Ofisi za Wabunge, Ofisi za kata vijiji na mitaa kwa kweli ukiangalia huo ukubwa na wingi wa shughuli hiyo unahitaji tutulie kuimalisha maeneo ambayo kweli tunayo sasa ili tuweze kuongeza baadaye ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nape Nnauye swali la nyongeza.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Pamoja na kutambua nia njema ya Serikali katika kusitisha kuongeza maeneno mengine mapya ya utawala hasa kwa maeneo ya mikoa na wilaya na halmshauri ambazo pengine gharama ya kuanzisha ni kubwa lakini kule chini kwenye kata na vijiji na mitaa hali ni mbaya sana na gharama yake sio kubwa kiasi hicho, badala kuyabeba yote pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Serikali kwa nini isifikirie hasa tunapokwenda kwenye uchaguzi wa Serikali za mitaa kwenye mitaa, kwenye kata na vijiji kwenda kuongeza maeneo ya kiutawala kwa sababu hali halisi inakataana na huo msimamo wa Serikali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema ni kweli kuwa tunaangalia gharama ni kubwa lakini naomba nikubaliane na maoni ya Wabunge walio wengi humu kwamba tuangalie kama nilivyomjibu Mheshimiwa Massare tuangalie kama kuna maeneo ambayo hatutakuwa na gharama kubwa tuyazingatie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu lengo la Serikali nikusogeza huduma karibu na wananchi na kuna maeneo kwa kweli wanatembea km 40, 30 kwenda kuomba barua

ya mtendaji wa kata kitendo ambacho sio sawa sawa. Kwa hiyo, tulipokee hili kwa niaba ya Bunge hili Tukufu na kwa niaba ya Serikali tumelifanyia kazi kwa pamoja na tutashirikisha Wabunge wa maeneo husika namna kuweza kulifanya hili kutekelezeka. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi wali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo Naibu Waziri amesema kwamba swali hili liliulizwa kuhusu Tanga wiki iliyopita ningependa kujua Mkoa ambao una halmashauri 11 na tunaposema pamoja na kupeleka maendeleo karibu na wananchi lakini lengo haswa ni kuboresha huduma. Huoni kama ni mzigo kubwa sana kwa mkoa mmoja kuwa na halmashauri nyinigi wakati baadhi ya mikoa halmashuri zake hazizidi nne hadi tano?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri nimewahi kuwa katibu wa vijana wa Chama cha Mapinduzi wa Mkoa wa Tanga, nina zifahamu halmashauri 11 na ukiangalia jiografia kwenda mpaka kule kilindi mpaka Tanga kule Nkinga ni jiografia kubwa. Lakini tunajua kuna mikoa mingine pia ni mikubwa sana ukiangalia kwa mfano Lindi, Ruvuma kule kwa kweli kuna maeneo makubwa sana kiuongozi labda kwa jibu la jumla tu ni kwamba msimamo wa Serikali ni kwamba kwa gharama iliyopo kama ilivyotajwa kwenye REA ujenzi wa miundombinu ya mkoa na wilaya ni kubwa sana ni mabilioni ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tulipokee tushauriane ndani ya Serikali tuone kama tunaweza kulifanya kesi *by* kesi kulingana na ukubwa wa eneo hili tuone kama tunaweza kulifanyika kazi kwa sasa siwezi kuahidi kama tutafanya kesho. Tunaona ile ku-*concern* ya huduma karibu na wananchi jiografia yetu kubwa mikoa ni mikubwa lakini tulipokee kama

maoni ya Wabunge tuendelee kuyafanyia kazi wakati ambapo ikiwa wakati muafaka hili litatekelezwa. Lakini hayo ndio majibu ya Serikali kwa sasa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko sasa aulize swali lake samahani ana swali la msingi.

Na. 307

**Kushuka kwa Ufaulu Katika Msomo ya Sayansi**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ufaulu wa wanafunzi katika maomo ya Sayansi na hisabati yanaonekana kushuka kila mwaka, mathalani mwaka 2015 asilimia 85 ya wanafunzi walifeli somo la hisabati matokeo ya kidato cha nne. Aidha, katika masomo mengine ya Kemia, Fizikia na Biolojia ufaulu bado ni duni sana.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuinusuru Halmashauri ya Mji wa Tarime na janga hili la ufulu duni katika masomo ya sayasi?

(b) Je, nini mkakati wa Serikali katika kuiwezesha maabara za shule za sekondari zilizojengwa kwa nguvu kubwa ya wananchi ndani ya Jimbo la Tarime mjini kuweza kupata wataalam na vifaa vya maabara ili kuinuka ufaulu kwenye masomo ya Sayansi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko Mbunge wa Tarime Mjini lenye sehemu (a) na (b) kama ifutavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza mipango mbalimbali ya uboreshaji wa elimu ya sekondari nchini ili kuinua kiwango cha ufaulu na ubora wa elimu kwa ujumla. Serikali imeipatia Halmashuri ya Mji wa Tarime walimu 59 wa masomo ya sayansi ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, Serikali katika mwaka wa fedha 2019/20 imepanga kutumia shilingi bilioni 58.2 kupitia EP4R kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya elimu ya sekondari nchini ikiwemo Halmshauri ya mji wa Tarime. Vilevile kupitia mradi mpya wa uboreshaji wa Elimu ya Sekondari nchini, Serikali imepanga kutumia shilingi bilioni 48.9 kwa ajili ya kuboresha elimu ya sekondari nchini.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika shule zote tisa za sekondari zilizopo katika Halmashauri ya Mji wa Tarime wanafunzi wanafanya mitihani ya masomo ya sayansi kwa vitendo kwa kutumia maabara zilizopo. Hata hivyo, maabara hizo ni kweli zinakabiliwa na upungufu wa vifaa vya maabara na huduma nyingine kama maji na gesi. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali kupitia mpango wa *EP4R* imepanga kutumia bilioni 58.2 kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya shule za sekondari ambapo jumla ya shule 70 zitapatiwa vifaa vya maabara zikiwemo shule za Halmashauri ya Mji wa Tarime.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko swali na nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nisikitike kwa majibu ya Serikali ambayo yametolewa na Naibu na Waziri sasa hivi Serikali ya Awamu ya Tano tunasema tunaelekea kwenye Tanzania ya Viwanda na kwa kasi kubwa sana ununuzi wa ndege ambao tuahitaji *pilot* na Ma-*engeneer*, mnajenga SGR, *stiegler's gorge* zote zitahitaji wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya majibu hayatoi uhalisia ni mwezi Mei mwaka huu tumepewa mwalimu mmoja wa sayansi sasa kama Mheshimiwa Naibu Waziri anazungumzia walimu toka Tanzania tupate uhuru kweli

tunao walimu 59, na upungufu ni mkubwa. Maswali yangu sasa.

Ningependa kujua katika sekondari tisa ambazo zipo ndani mji wa Tarime ni sekondari mbili ambayo ni *High School* ya Tarime na sekondari ya Mogabili ndio maabara zimekamilika sekondari saba zote maabara hazikamilia majengo ni yale ambao wananchi wamejenga na kwa kufanya hivi inazorotesha ufaulu wa wanafunzi. Ningependa kujua Serikali ni lini mtaleta fedha ili tuweze kukamilisha maabara ya hizi sekondari saba ambazo hazijakamilika zikisubiri Serikali ikamilishe pamoja na vifaa?

Katika Halmashauri ya Mji wa Tarime tuna sekondari moja tu *A-Level* na kama unavyojua kwamba tuna sekondari tisa. Wanapomaliza *form four* wanafunzi wetu wengi na hasa wasichana wanashindwa kupata nafasi kuendelea na *high school*. Ni lini sasa Serikali itapandisha hadhi walau Mogabili Sekondari au Nyandoto kuwa *A-level* nayo ili kuchukua wanafunzi mchanganyiko kwa maana wavulana na wasichana ili watoto wetu wa kike waweze kwenda *High School*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upole kabisa haya ndio majibu ya Serikali, yeye Mheshimiwa Esther kama ana majibu yake nadhani abaki nayo. Majibu ya Serikali majibu haya yanaandaliwa kutoka Halmashauri ya Tarime. Hakuna taarifa za uwongo ambazo zinatolewa hapa mbele ya Bunge letu Tukufu na ndio taarifa ya hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili suala la kupeleka walimu na kupeleka vifaa vya maabara haliwezi kabisa kulinganishwa na miradi mingine ya maendeleo kwa sababu kila kitu kinajitegemea na vyote ni muhimu sana na vinafanyika sambamba. Tumeajiri walimu awamu hii ya juzi

4500 ndio imepata walimu wachache, awamu iliyopita walimu walipelekwa Tarime lakini bahati nzuri na mimi nimefika wanazungumza ukifika Tarime pale tunazungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala shule kupandishwa hadhi Waheshimiwa Wabunge mnafahamu ni suala la mchakato ni lazima ninyi wenyewe kama Mbunge wa eneo husika kupitia halmashauri yako kupitia vikao vya halmashauri kamati ya fedha, bajeti ya ndani na wadau mbalimbali ikiwepo na mfuko wako wa jimbo mleta maoni TAMISEMI Wabunge walioleta maoni yakupandishwa shule zao kuwa *high school* yanafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ninaomba nitoe taarifa kuanzia mwezi mwaka huu tuna shule nyingi zinaanzishwa ambao tumepata maoni kutoka kwa Wabunge wenyewe kwa vyanzo vya ndani tumpelekee Serikali na walimu tunawapeleka katika maeneo hayo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susane Lyimo swali la nyongeza.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya Tarime ni matatizo ya nchi nzima. Na utakubaliana nami kutokana na matatizo maabara ndio maana wanafunzi wengi wanapofika kidato cha pili *majority* wana-*opt* kwenda masomo ya *Arts* kutokana na upungufu mkubwa wa maabara lakini vile vile upungufu mkubwa wa walimu wa sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri anapojibu hapo anasema kwamba wametenga takribani bilioni 59 mara nyingi fedha hizo tunatambua zinaenda walau nusu. Sasa nilitaka kujua Serikali ina mkakati gani mahususi katika miaka hii inayobakia mpaka tunapoenda kwenye Bunge la mwisho kuhakikisha kwamba wanatenga fedha kwa ajili ya kukamilisha maabara ili wanafunzi wetu wa *opit* kwenda masomo ya sayansi ili waendane na Tanzania ya viwanda.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, labda nitoe taarfa kwamba hapa tulipo sasa hivi tumepata shilingi bilioni 16.6 na tumeshaomba taarifa labda hili nisema inawezekana kuna tatizo la mawasiliano tukiomba maabara ambazo zimekamilika tunaomba kwa maafisa wetu wa elimu kuhamia mikoa na wilaya. Tumeshapata taarifa mbalimbali za halmashauri zote nchini. Mchakato unaendelea kupeleka vifaa tulitaja juzi hapa kwenye bajeti zaidi ya maabara 2500 nchi hii watapata vifaa vya maabara mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini fedha inayozungumzwa hapa kwenye bajeti hii inazungumzia 2019/ 2020 ndio inayozungumzwa hapa. Lakini tunazingatia maeneo lakini tumeeomba taarifa kama kuna maabara zimekamilika tupate taarifa zao. Lakini kuna halmashauri zinatofautiana kutoka moja kwenda nyingine na tunaanza kama tunapeleka vifaa au wataalamu wa maabara au walimu wa sayansi tunapeleka mahali ambapo kuna changamoto kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukipata taarifa zile labda niwaelekeze Waheshimiwa Wakurugenzi tunapoomba Taarifa kupitia Maafisa Elimu wa Mikoa, Msingi na Sekondari na Walimu, ni lazima wale watoe taarifa lakini pia na Waheshimiwa Wabunge mshirikishwe, maana yake tumepata kweli taarifa hapa hata ya maboma, ikaonekana tunapata taarifa ambazo ni *old fashion* Mbunge ana taarifa zake, na Mkurugenzi ameleta taarifa hapa zinatofautiana, ndiyo picha. Lakini, tukiomba taarifa ya Elimu au ya Afya au huduma nyingine kwenye halmashauri zetu, basi Wakurugenzi na Makatibu Tawala kabla ya kuleta taarifa kwenye Ofisi Kuu za Serikali wawasiliane na Waheshimiwa Wabunge ili wote tuwe kwenye line moja na tuweze kuzungumza lugha moja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shaaban Shekilindi swali la nyongeza.

**MHE. SHAABAN O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona, kutofaulu kwa wanafunzi hasa wa masomo ya sayansi kuna changiwa sana na kutomalizika kwa maabara, Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za kutosha katika maabara hizi ili ziweze kumalizika hasa katika Jimbo la Lushoto? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge, na anajua nimetembelea kwenye Jimbo lake, na anafanya kazi kubwa sana kuwasemea wananchi wake, na wananchi wa Lushoto wamejenga Shule nyingi ikiwepo shule ya *high school,* na nilienda akaniambia kuna upungufu wa Walimu, na namuahidi kwamba tulipomaliza kugawa mgao wa Walimu hawa wa Sekondari naye amepata mgao, na hili tumelipokea, vifaa ambavyo tumeelekeza, kama ile Shule ambayo nilitembelea ilikuwa na changamoto kubwa ya watoto wa kike wengi hawajapata vifaa ambavyo vya kuwasaidia ili waweze kusoma masomo ya sayansi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Ofisi Rais, Utumishi na Utawala Bora. Mheshimiwa Aida Joseph Khenani Mbunge wa Viti maalum sasa aulize swali lake.

Na. 308

### Kuajiri Wahitimu Wote wa Vyuo Nchini

**MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza:-

Je, kuna utaratibu wowote wa kuajiri watu wote waliohitimu Vyuo na kukidhi vigezo vya kuajiriwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Utumishi na Utawala Bora majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani Mbunge wa Viti maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu Serikali imekuwa Mwajiri Mkuu, wa Wahitimu wa Vyuo mbalimbali kutoka katika soko la Ajira nchini. Ajira hizi zimekuwa zikitolewa kwa kuzingatia mahitaji halisi ya raslimali watu katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala na Taasisi mbalimbali za Serikali kwa kuzingatia ikama na bajeti iliyotengwa kwa ajili ya kugharamia ajira mpya katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mabadiliko ya kijamii na kiuchumi, Serikali ilianzisha Sekretarieti ya ajira katika Utumishi wa Umma, kwa lengo la kuratibu mchakato wa ajira katika Utumishi wa Umma kwa uwazi na ushindani kwa njia ya usaili wa nadharia na vitendo pale inapobidi. Hivyo, wahitimu wanaofaulu usaili ndiyo wanaokidhi vigezo vya kuajiriwa na huwa wanaajiriwa kwa kada zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Duniani kote, Serikali siyo mwajiri pekee wa wahitimu wa vyuo mbalimbali vya elimu, kwani pamoja na kuajiriwa Serikalini, wahitimu hao huajiriwa pia katika Sekta binafsi, Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali, Asasi za Kiraia na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, wahitimu wengine huamua kujiajiri wenyewe na hivyo kutoa mchango wa maendeleo kwa Taifa kwa njia moja au nyingine. Aidha, kuhitimu Elimu ya juu, siyo kigezo pekee cha kuwezesha muhitimu husika ila sifa na ushindani wa kutosha ili kuweza

kuajiriwa na Serikali. Hivyo, Serikali haina utaratibu wa kuajiri wahitimu wote wa vyuo vya Elimu ya juu nchini. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, swali langu la msingi nilisema wahitimu wa vyuo vikuu waliokidhi Vigezo, sikusema waliohitimu tu ndiyo wote wanastahili kuajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Serikali, kila mwaka takribani Wahitimu laki nane, kwa mwaka, na wanaoajiriwa ni elfu arobaini peke yake, kwa hiyo laki saba na sitini wanabaki mtaani. Ningependa kujua Serikali ina Mkakati gani wa ziada, kwa sababu Mkakati uliopo umeshindwa kukidhi vigezo vya kuweza kuwaajiri vijana wengi ambao wamehitimu? Ni Mkakati gani wa ziada ambao Serikali inao kwa ajili ya kuwasaidia Vijana hawa ambao wengi wako mtaani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Kumekuwa na vikwazo mbalimbali kwa hawa wahitimu wanapokuwa wanaomba kazi, na kikwazo namba moja, ni kikwazo ambacho wanawaambia kwamba wawe na uzoefu, na wakiamini wametoka chuoni. Ningependa kujua, Serikali haioni ni kuna Mkakati ambao unahitajika wa ziada sana, kuwa na programu maalum ya kuwa andaa Vijana hawa kabla ya hawajakwenda kazini? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala na Bora majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba niseme kabisa kwamba kila Mtanzania ana haki ya kuomba ajira kwenye Utumishi wa Umma. Lakini vilevile, tuangalie kwamba ajira za Serikalini huzingatia sana *scheme of service*, huzingatia sana ikama, na bajeti iliyopangwa kwa wakati huo, na vilevile kutegemea na

vipaumbele vya Taifa wakati huo. Niwahase wahitimu wote nchini waendelee kuomba ajira kupitia sekretarieti yetu ya ajira ambayo tumeboresha sasa hivi inapitia ajira *portal* kupitia njia ya mtandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba niliambie Bunge lako Tukufu pia kwamba mwaka ule wa fedha 2018/ 2019 Serikali iliweza kuajiri ajira mbadala na ajira mpya zaidi ya elfu arobaini na moja na laki na sita na Kada ya Walimu ilikuwa elfu nne na mia tano. Lakini kwa mwaka huu wa fedha naomba niliambie Bunge lako Tukufu kabisa kwamba Serikali inatarajia kuajiri zaidi ya ajira elfu arobaini na nne na laki na nane, lakini kana kwamba hiyo haitoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niliambie Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ya Awamu ya Tano pia imejipanga tumeanzisha Sera ya *local content* ili *private sector* zote nchini ziweze kuajiri Watanzania na nichukue fursa hii kuwapongeza sana Mkoa wa Pwani kwa sababu wao wamezingatia sana Sera ya Viwanda na Uchumi na wameweza kuajiri zaidi ya Watanzania elfu hamsini, iwe ni *in direct* iwe ni *direct* na naomba nitoe Rai, Mikoa mingine pia iweze kuiga mfano wa Mkoa wa Pwani ambao wanaufanya mpaka sasa hivi, ili Watanzania wengi pia waweze kupata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili, la Mheshimiwa Mbunge Khenani anazungumzia Mikakati ya Serikali ambayo mingine nimeitaja, amezungumzia kuhusu uzoefu na naomba niseme katika Sera yetu mpya ya Utumishi 2004 Serikali imesema kabisa kwamba ajira mpya hazitazingatia uzoefu, uzoefu unakuja kwa wale ambao tayari wako kazini. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa. Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri

kwa majibu mazuri, lakini nirudi kwenye swali la nyongeza la pili la Mheshimiwa Aida Khenani na hasa eneo lile ambalo vijana wengi wa Kitanzania wamekuwa wakipata shida sana ya kigezo cha uzoefu, katika kutafuta ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na vijana, kweli limekuwa ni tatizo, Ofisi ya Waziri Mkuu inasimamia masuala ya Ustawi wa Vijana, na baada ya kugundua kwamba vijana wengi wamekosa sifa za kuajiriwa kwa sababu ya kigezo cha uzoefu, Ofisi ya Waziri ya Mkuu, iliamua kutengeneza mwongozo mpya, wa *internship* ili kuhakikisha vijana wanapomaliza masomo yao, waweze kupata maeneo ya kupata uzoefu kwenye *private sector* na maeneo mbalimbali, na zinapotoka nafasi za ajira kigezo cha uzoefu kiwe tena siyo kikwazo kwa ajili ya ajira zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa *program* hiyo sasa imekwisha kuanza, na Ofisi ya Waziri Mkuu imeshasimamia makundi ya kutosha ya vijana na kuwapeleka kwenye maeneo mbalimbali kwa ajili ya *internship programme* tayari kwa kuwafanya wawe na uzoefu wa kuajiriwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Ally Saleh Ally Mbunge wa Malindi sasa aulize swali lake.

Na. 309

### Wajibu wa Kulinda Haki za Binadamu Nchini

**MHE. ALLY SALEH ALLY** aliuliza:-

Katika masuala ya Haki za binadamu Tanzania ina wajibu wa ndani na nje na kila wajibu unahitaji kuonekana wazi ili kujenga imani kwamba haki za Binadamu zinatekelezwa katika viwango vya Kisheria, Kikatiba na Kimataifa?

(a) Je, Serikali itatimiza vipi matakwa haya ya ndani na nje?

(b) Je, ni kiasi gani Serikali imekuwa ikijenga misingi ya usimamizi, ufuatiliaji na utekelezaji wa Haki za Binadamu ndani ya nchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Saleh Ally (Malindi) lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sheria zetu za nchi, Mikataba ya Kimataifa na Kikanda, Serikali ina wajibu wa kuheshimu na kulinda haki za binadamu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutimiza wajibu huo, ndani ya nchi, Serikali imeweka mfumo wa Kisheria na Kitaasisi ili kuhakikisha kuwa masuala ya haki ya za binadamu nchini yanalindwa, yanatekelezwa na kuheshimiwa ipasavyo. Kwa kufanya hivyo, Serikali ilianzisha Chombo mahsusi, kitakachosimamia masuala ya haki za binadamu nchini ambacho ni Tume ya haki za binadamu na Utawala Bora iliyoanzishwa kwa mujibu wa Katiba na imewekwa ikifuatilia utekelezaji wa misingi ya haki za binadamu na Utawala bora na kuishauri Serikali namna bora ya kuboresha utekelezaji wa wajibu wake ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kama ilivyo kwa nchi nyingine duniani, ambazo zimeridhia Mikataba mbalimbali ya Kimataifa na Kikanda, inayohusu haki za binadamu imekuwa ikijenga misingi ya usimamizi, ufuatiliaji na utekelezaji wa haki za binadamu ndani ya nchi kwa kutunga Sheria mbalimbali na kuanzisha Taasisi na mfumo

inayosaidia utekelezaji wa misingi iliyowekwa kwa mkataba ya Kimataifa na Kikanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania, imekuwa ikiwasilisha taarifa zake kuhusu utekelezaji wa haki za binadamu nchini katika vyombo mbalimbali vya Kimataifa na Kikanda. Taarifa hizo hujadiliwa na mapendekezo ya kuboresha haki za binadamu nchini hupokelewa na kutekelezwa kwa kuzingatia Sheria za nchi, mila na desturi za Watanzania pia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Saleh Ally swali la nyongeza.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kuniruhusu kuuliza maswali mawili ya nyongeza, la kwanza ni kwamba kwa miaka miwili sasa, kumekuwa na matokeo ya kutisha ambayo kwa kweli, si asili ya Kitanzania, yakitokea kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu ni pamoja na kutekwa, kupigwa, kuteswa, kubamiza upinzani na mambo kama hayo, Je, Serikali kwa nini haijitokezi ikasimama ikahesabiwa ili tuone kama kweli haki zinalindwa Kikatiba na Kisheria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Kwa muda sasa takribani, pengine miaka miwili, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala bora, haina Uongozi, na kwa hivyo pengine kuna ombwe la kutazama matukio mbalimbali ya haki za binadamu. Najua hivi sasa kuna mchakato wa kutafuta hao watu wa kujaza nafasi za Tume ya Haki za Binadamu, lakini Je, kwa nini Serikali inaachia hali kudorora mpaka Tume muhimu kama hii ikakosa uongozi kwa zaidi ya miaka miwili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria majibu kwa maswali hayo.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, matukio ambayo umeyataja, na ambayo yametokea, yanajulikana Serikalini na Vyombo husika na hasa Jeshi la

Polisi na Vyombo vingine vya Usalama vimekuwa vikifuatilia matukio hayo. Mara nyingi tunapata taarifa na majibu yanaridhisha, lakini kazi upelelezi na kazi ya kufatilia vituko kama hivyo na vitendo kama kama hivyo, inaweza ikachukua muda na Serikali imekubali kuchukua majukumu hayo na maswali haya yanaulizwa na wananchi kama unavyouliza, yanaulizwa pia Kimataifa na tuko tayari kutoa taarifa sahihi hapo vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama vitakapokamilisha uchunguzi wa namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni kuhusu uongozi wa Tume ya Haki za Binadamu, Tume ile ina Bodi tayari, ina watendaji tayari mchakato wa kumtafuta Mwenyekiti, au Mtendaji Mkuu, imekamilika na kilichobakia sasa ni kufikisha jina hilo baada ya upekuzi kukamilishwa na Vyombo vya Usalama na kuipeleka kwa Mamlaka ya uteuzi na hiyo inaweza kutokea wakati wowote, lakini kazi imekwisha kamilika na inaweza kutokea wakati wowote. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene Mbunge wa Ileje, sasa aulize swali lake.

Na. 310

**Serikali Kusitisha Mikataba na Wadau mbalimbali**

**MHE. JANET Z. MBENE** aliuliza:-

Serikali iliingia Mikataba na Uwekezaji na Wadau mbalimbali kwenye Sekta tofauti ambayo kwa sababu mbalimbali imesitishwa na Serikali?

(a) Je, ni Mikataba mingapi imesitishwa na ni sekta zipi zinaongoza?

(b) Je, Serikali imeingia gharama kiasi gani, katika kesi zilizofunguliwa Mahakamani na kusitishwa kwa Mikataba hiyo?

(c) Je, Serikali imepata faida au hasara gani kwa kusitisha Mikataba hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene Mbunge wa Ileje, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ni kweli Serikali imekuwa ikisitisha Mikataba ya Uwekezaji kutokana na sababu mbalimbali, moja ikiwa ni kwa upande mmoja mwingine ni Mkataba wa kushindwa kutimiza masharti kwa mujibu wa Mkataba au makubaliano ama inapobainika kuwa kulikuwa na udanganyifu ambao haukuweka wazi taarifa za msingi wakati wa kuingiwa katika Mikataba hiyo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali bado inaendelea na mapitio ya Mikataba yote, iliyoingiwa na Serikali ili kutambua kama vigezo na masharti kama ya Mikataba hiyo vinatimizwa ipasavyo. Mara zoezi hili, likikamilika Serikali itakuwa na takwimu sahihi ya Mikataba yote, iliyosainiwa sambasamba na kuifanya tathmini ya gharama zake zilizotumika kwa kesi zilizofunguliwa kutokana na usitishwaji wa Mikataba husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Hati Idhini ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, iliyochapishwa katika gazeti la Serikali kwa Tangazo namba 48 la mwaka 2018 na Sheria ya marekebisho mbalimbali ya Sheria ambayo pamoja na mambo mengine imerekebisha majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambapo utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeboreshwa zaidi, kwa kuanzishwa kwa Idara itakayoishughulikia utekelezaji wa Mikataba yote baada ya kufanyiwa mapitio yaani *vetting*. Jukumu hili litawezesha kutambua na kupata takwimu sahihi za Mikataba yote

iliyositishwa, inayotakiwa kusitishwa na inayotakiwa kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pia, mabadiliko ya Sheria hiyo yameanzisha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambayo kwa sasa inasimamia mashauri yote ambayo Serikali inashtaki au kushtakiwa. Kwa sasa Ofisi hii inaendelea na kazi ya utambuzi wa mashauri yote dhidi ya Serikali kutoka katika Wizara na Taasisi zote za Serikali. Jitihada zote hizi, zina malengo ya kusaidia upatikanaji wa takwimu sahihi na mashauri yaliyofunguliwa kutokana na usitishwaji wa Mikataba na kutambua faida na hasara zake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene swali la nyongeza.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yaliyojibiwa kwa ufanisi, na weledi wa hali ya juu, pamoja na hayo naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza na kabla sijauliza maswali hayo nataka nipongeze sana Serikali kwa hatua iliyochukua kwa kusitisha mikataba yote ambayo ilikuwa inaonekana wazi haizingatii maslahi mapana ya wananchi wa Tanzania. Vilevile niipongeze Serikali kwa kuchukua hatua mbalimbali alizoziainisha Mheshimiwa Waziri za kuhakikisha kuwa sasa mikataba itakuwa inafatiliwa kwa ukaribu zaidi. Naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kutokana na mwenendo mzima na utaratibu wa malalamiko mengi yanayojitokeza katika sekta ya kilimo, uvuvi, ufugaji na katika sekta nyingine muhimu za kiuchumi ni dhahiri mikataba mingi iliyoingiwa imekuwa haiwanufaishi wadau wa sekta hizi hasa wakulima, wafugaji na wavuvi. Ningependa sasa Serikali

ituambie wana mkakati gani maalum wa kuhakikisha kuwa mikataba inayoingiwa na wawekezaji wa kilimo, ufugaji, uvuvi, uletwaji wa pembejeo mbalimbali, masoko n.k sasa hivi yanapitiwa upya na kuhakikisha kuwa yanazingatia maslahi mapana ya sekta hizo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili Mkoa wangu wa Songwe na hususani Wilaya ya Ileje ina migodi ya makaa ya mawe, wa Kiwira pamoja na ule Mlima Kabulo na kwa muda mrefu sasa mgodi ule haufanyi kazi kwa sababu mkataba wake ulisitishwa na mgodi ule ulikuwa unaajiri takribani watu 7000 na zaidi. Je, ni lini sasa mkataba ule utapitiwa upya ili ule mgodi uanze kufanya kazi? Naomba sana Serikali izingatie hilo kwa sababu tayari tunaathirika kiuchumi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria majibu kwa maswali hayo.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kila wizara na kila sekta inapeleka rasimu za mikataba ambayo wangependa waingie na wadau wao hapa nchini au nje ya nchi kwa Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo mwanzoni mikataba mingine ni mizuri, mingine ina mapungufu, mingine ni mibaya ile ambayo ni mizuri kila wizara ambayo tayari imeshatoa taarifa yake hapa wametueleza mafanikio yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana tu Wizara ya Madini imetueleza jinsi faida inavyopatikana kutoka sekta ya madini, kutokana na mikataba ya uuzaji madini yetu ulimwenguni. Na mashirika yote yaliyo chini ya Wizara ya Madini ikiwa ni pamoja na *STAMICO* wamekuwa wakirejesha Serikalini pato kubwa ambayo hiyo ni sehemu ya faida hiyo. Ni lazima tuangalie kwa makini mikataba mingi ina udanganyifu na tunaposaini mikataba hii tunaweza kudanganywa na ndio maana wizara yangu imeona kuna umuhimu wa kufanya marekebisho na kusahihisha mapungufu yote ya wizara zote na taasisi zote zoezi hilo linaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na madhumuni ya kumuweka wakili wa Serikali kumsaidia Mwanasheria Mkuu ni hilo kuangalia ubora wa mikataba yote ambayo Serikali na Wizara zake na taasisi zote inaingia na zoezi hilo linaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mgodi wa Kiwira ninaamini kwamba Mheshimiwa Mbunge jana ulisikiliza hotuba ya Waziri wa Madini alivyosifia ule mgodi mpya wa Kibulo ambao ulianzishwa mwezi Novemba, 2018 na ilipofika Machi, 2019 umeshatoa faida ya milioni 12.9 na kuilipa Serikali milioni 4.7 ni malipo mengine yanayofikia milioni 2.7. pia mgodi ule tayari umeshaleta kinu ambacho kinachakata mkaa unaouzwa katika nchi zifuatazo, Kenya Uganda, Rwanda, Burundi na China.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna sehemu ambazo lazima tuangalie mkataba huu ili tuweke maboresho hasa katika ajira lakini kipimo cha mikataba isiwe tu udhaifu wake lazima tutazame pia faida zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali kama haya tuanze kuyauliza je faida ni zipi na hasara ni zipi. Na nadhani katika mgodi wa Kiwira na migodi mingine ya makaa ya mawe tutaendelea kupata nishati mpya kabisa na imetathminiwa kimataifa kwamba mkaa unaotoka Tanzania na hasa unaotoka kule Liganga ni kati ya mikaa bora duniani ambayo haitosi gasi chafu kama mikaa mingine duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa kwamba tutatazama masuala ya ajira lakini nina hakika kutokana na faida kubwa tunayopata na mgodi wa Kiwira kama Waziri Biteko alivyotueleza jana tupo katika mwelekeo mzuri, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge sasa tunaelekea Wizara ya Nishati Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 311

**Utekelezaji wa *REA III*- Mbulu Vijijini**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Serikali aliahidi kupeleka umeme katika vijiji vyote vya Jimbo la Mbulu Vijijini kupitia *REA III* kwa sababu *REA II* haikufanya vizuri katika jimbo hilo:-

Je, vijiji vingapi vitafikiwa na umeme wa *REA* Awamu ya III?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati majibu

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Flatei Gregory Massay Mbunge wa Mbulu Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imedhamiria kufikisha umeme katika vijiji vyote visivyo umeme nchini ifikapo Juni 2021. Jimbo la Mbulu Vijijini lina vijiji vipatavyo 76 na kati ya vijiji hivyo 12 vimepatiwa umeme. Vijiji 13 vya Qaloda, Getesh, Endesh, Labay, Maretadu, Hayderer, Endanachan(Haydom), Muslur, Dirim, Simha, Yaeda Ampa, Endoji na Gidhim vimejumuishwa katika mradi wa REA III mzunguko wa kwanza. Mkandarasi Kampuni ya Angelique *International Limited* kutoka India anaendelea na kazi za kusambaza umeme katika Jimbo la Mbulu Vijijini. Kazi ya kupeleka umeme katika vijiji vilivyopelekewa umeme zitakamilika mwezi Juni, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zinazoendelea kwa sasa ni pamoja na kusimika nguzo, kuvuta nyaya na kufunga transfoma katika Vijiji vya Qaloda, Getesh, Endoji, Endesh, Labay, Maghang Juu, Getagujo na Simahha. Kati ya vijiji hivyo, vijiji 6 vya Getesh, Endoji, Qaloda, Labay, Getagujo na

Maghang Juu vitawasha umeme mwisho wa mwezi Mei, 2019. Kazi za mradi zinahusisha ujenzi wa kilometa 45.87 za njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 na kilometa 35 za njia ya umeme wa msongo kilovoti 0.4, ufungaji wa transfoma 16 na uunganishaji wa wateja wa awali 347 na gharama za mradi ni shilingi bilioni 2.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vilivyobaki katika Jimbo la Mbulu vitapatiwa umeme kupitia mradi wa *REA III* mzunguko wa pili utakaoanzwa kutekelezwa mwezi Julai, 2019 na kukamilika mwezi Juni, 2021.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza pamoja na majibu aliyonipa Mheshimiwa Naibu Waziri umeme mahali ambako umekwenda kama alivyosema kwenye majibu ya swali maeneo ya taasisi na visima vya maji vimerukwa. Swali la kwanza kata za Mahitadu, Masieda, Endage Chan, Heda Chini, Getiree, Bashai, Endamillai, Rolward, Endargati, Esheshi, lini zinapata umeme?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru pia umefika kwenye jimbo langu na Mheshimiwa Waziri amefika na iko ahadi ya vijiji 22 kupatiwa umeme mwaka huu. Na leo ni bajeti ya wizara yako je, Mheshimiwa Waziri vijiji hivi na ahadi hii vipo katika bajeti hii au nitegemee nini niwaambie wananchi wa Mbulu Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri katika maswali ya msingi ya Mheshimiwa Mbunge. Nimpongeze sana Mheshimiwa Flatei Massay Mbunge wa Mbulu Vijijini alivyofuatilia masuala ya umeme vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli zipo kata sita ikiwemo Masieda, Yaendachini pia Endagi chan pamoja na Gorand, na Esheteshi pamoja na Bashi. Zipo umbali wa takribani kilometa 15 kutoka Ngoradi na kilometa 14 kutoka Mbulu Mjini. Lakini utaratibu tunaofanya sasa wananchi wa kata hizo *TANESCO* pamoja na *REA* wameshaanza kushirikiana na utekelezaji wa kupeleka umeme katika vijiji hivyo unaanza mwezi Julai mwaka huu na utakamilika Desemba mwaka huu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge wafikishie taarifa wananchi wa Mbulu Vijijini kwamba utekelezaji wa miradi hiyo katika kata hizo utafanyika kama kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili ahadi ni lini, taasisi pamoja na maeneo mengine tuwape uhakika. Mheshimiwa Mbunge anavyofuatilia masuala ya Mbulu Vijijini anavyo vijiji 76 na kati ya hivyo tayari vijiji 32 tumevipatia umeme, vijiji vinavyobaki nikupe taarifa na tathmini ya Serikali imekamilika vyote vitapelekewa umeme ifikapo mwezi Juni, 2021.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwenda kwa hiyo tumalizie maswali yaliyobaki. Mheshimiwa Desderious John Mipata Mbunge Nkasi Kusini sasa aulize swali lake.

Na. 312

**Mpango wa *REA III*- Vijiji vya Jimbo la Nkasi Kusini**

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Vijiji vya Sintali, Nkana, Nkomachindo na Katani viko kwenye mpango wa kupata umeme wa *REA* Awamu ya III lakini mpaka sasa hakuna kazi zinazoendelea:-

Je, ni lini kazi hiyo itaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata Mbunge wa Nkasi Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya vijiji 51 vitapatiwa umeme katika Wilaya ya Nkasi ikiwa ni pamoja na vijiji 12 vya Jimbo la Nkasi Kusini vya Ntuchi, Tambaruka, Chima, Chatelekesha, Isasa, Kingombe, Ntemba, Nkomolo II, Kasapa, Kisula, Namansi na Kasu B. hadi kufikia mwezi Mei, 2019 umeme tayari umeshawasha katika vijiji vya Chala, Chima, Chala Isasa na Ntemba. Jumla ya wateja wa awali 77 wameunganishiwa umeme. Aidha, mkandarasi anaendelea na kazi katika vijiji 9 viliovyosalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za mradi katika Jimbo la Nkasi Kusini vinahusisha ujenzi wa kilometa 29.65 za njia ya umeme wa msongo kilovoti 33; kilometa 28 za njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4; ufungaji wa transfoma 14 na uunganishwaji wa wateja wa awali 324. Gharama za kazi hiyo inakadiriwa kufikia shilingi bilioni 2.15.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vya Sintali, Nkana, Katani na Nkomachind vitapatiwa umeme kupitia mradi wa *REA* III mzunguko wa pili unatarijiwa kuanza mwezi Julai, 2019 na kukamilika mwezi Juni, 2021.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Desderius Mipata swali la nyongeza.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza vijiji nilivyovitaja vya Katani, Sintali, Nkana na Nkomachindo niseme na Malongwe pamoja na Wapembe nimeuliza kwenye swali la msingi ni lini hasa vitapata umeme? Hapa amesema viatapata kwenye mzunguko wa pili ambao utaisha mwaka 2021 na utaanza mwezi Julai mwaka huu. Sasa ni lini hasa nataka kujua kwa

sababu wananchi wa maeneo haya wamezungukwa na maeneo ya umeme?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili vijiji vya Kipande, Kundi kuna sekondari zetu lakini sekondari zote hazijaunganishwa na umeme, pia Kijiji cha Ntemba ambako kuna umeme unapelekwa safari hii hatua chache kama kilometa nne kuna Chuo cha Ufundi cha Mvima na kuna pia Kituo cha Afya cha Mvima. Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuja walitoa ombi la kuunganishiwa umeme na hadharani tulikubali kwamba tutawaunganishia umeme. Ni lini katika maeneo haya huduma za jamii yatapata umeme?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nilifanya naye ziara katika Jimbo la Nkasi Kusini na maeneo aliyoyataja hayo tulitembea kwa pamoja. Lakini nataka niseme kwamba katika swali lake la msingi kwa vijiji alivyovitaja ikiwemo cha Wampembe anaulizia ni lini hasa umeme utawaka. Kama ambavyo tumejieleza katika jibu la msingi kwamba mradi wa *REA* awamu ya tatu mzunguko wa pili unatarajiwa kuanza tarehe 01 Julai, 2019 na kwa kuwa leo ni bajeti yetu nimwombe Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako tukufu liridhie bajeti hii ili tuanze kutekeleza mradi huu na kwa kuwa hatua za awali zimeshafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili anaulizia umeme ambao unapelekwa katika Kijiji cha Ntemba ambako mita chache kuna Kituo cha Ufundi na Kituo cha Afya, ni kweli nilivyofanya ziara katika eneo lake jambo hili lilijitokeza na kwa kuwa ni sera ya Serikali ya Awamu ya Tano kwamba maeneo yote ya huduma za jamii ikiwemo vyuo, shule za sekondari na vituo vya afya vipatiwe umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kusisitiza ahadi hii ipo na kwamba eneo hili litapatiwa umeme na kama alivyosema Mheshimiwa Waziri katika majibu ya nyongeza

kwamba tumeelekeza *TANESCO* kufikisha umeme katika taasisi mbalimbali na kazi hiyo inaendelea. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 313

**Nafasi za Vijana Kujiunga na Jeshi**

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA** aliuliza:-

(a) Je, ni vijana wangapi kutoka Wilaya ya Kaskazini A na Wilaya ya Kaskazini B wamepata nafasi ya kujiunga na Jeshi kuanzia mwaka 2015?

(b) Je, mgawanyo wa idadi ya vijana wanaojiunga na Jeshi kwa kila wilaya nchini upoje?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita yaani kuanzia mwaka 2015 hadi 2018 vijana walijiunga na JKT kutoka Zanzibar kwa kujitolea ni kama ifuatavyo:-

(i) Mwaka 2015/2016 vijana 300;
(ii) Mwaka 2016/2017 vijana 300;
(iii) Mwaka 2017/2018 vijana 400 kwa hivyo jumla katika miaka hiyo mitatu ni vijana 1000.

Jukumu la kugawa nafasi hizo kwa wilaya liko chini ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa mwaka 2019/20 Zanzibar imetengewa nafasi 500.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mgawanyo wa idadi ya vijana wanaojiunga na JKT kwa kujitolea kwa kila mkoa huzingatia uwiano wa idadi ya watu kulingana na takwimu za sensa ya Taifa ya watu na makazi, elimu, jinsia na sifa nyingine zinazokuwa zimeainishwa na mkuu wa JKT. Zoezi hili ikiwa ni pamoja na mgawanyo wa vijana hadi ngazi ya wilaya huratibiwa na wakuu wa mikoa husika baada ya Makao Makuu ya JKT kuainisha idadi ya vijana kwa kila mkoa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Angelina Malembeka swali la nyongeza.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake japo hayajaniridhisha kwa sababu swali langu la msingi nilihitaji kujua ni vijana wangapi kutoka Wilaya ya Kaskazini A na Wilaya ya Kaskazini B ndani ya Mkoa wa Kaskazini Unguja ambao wamepata ajira katika jeshi kwa miaka mitatu, lakini amenipa jibu la jumla la Zanzibar yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilitaka kujua ni lini vijana wa Mkoa wa Kaskazini Unguja watapata ajira katika jeshi ili kuondoa malalamiko yaliyopo hivi sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili kwa kuwa manug'uniko ni mengi yanayotokana na vijana kujitolea kwa muda mrefu lakini hawapati ajira. Ni mkakati gani ambao Serikali umeupanga ili kuhakikisha vijana hawa wanapata ajira hiyo kwa kuzingatia pia jinsia maana hapa katika orodha yake inaonyesha wanaume 720 wanawake 280?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Malembeka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali la kwanza anasema sikumpa takwimu za ni vijana wangapi kutoka Wilaya ya Kaskazini A na B waliojiunga na JKT. Katika jibu langu la msingi nilitoa takwimu za jumla za vijana wanaochukuliwa kutoka Zanzibar na nikaeleza kwamba jukumu la kupanga idadi kwa Wilaya za Zanzibar linafanywa na SMZ. Kwa hivyo takwimu sina na Mheshimiwa akizihitaji itabidi azipate kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa sababu wao ndiyo wanapanga kwa mujibu wanavyoamua, sisi tunakabidhi kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wao wanagawa wanavyopenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, katika hilo hilo la kwanza alikuwa anauliza lini vijana watapata ajira ili kuondoa malalamiko. Nataka ieleweke kwamba kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa lazima vijana waelewe kwamba siyo ajira, kujiunga na JKT ni kwenda kupata mafunzo ya kijeshi pamoja na *study* za kazi. Wachache watapata ajira katika vyombo vya Ulinzi na Usalama, walio wengi watabidi wajiajiri wenyewe au waajiriwe na sekta binafsi. Hili ni muhimu lieleweke, wasielewe kwamba kujiunga na JKT ndiyo ajira. Tunachukua vijana wengi na nilitoa takwimu hapa wakati wa bajeti yangu kwamba tunachukua takribani vijana 20,000 kwa mwaka. Vyombo vya ulinzi na usalama havina uwezo wa ku-*observe* kuchukua wote hao katika ajira, watapata wachache na walio wengi watakuwa wamepata *study* za kazi ili waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ni mkakati gani wa kupatia ajira na kwa kuzingatia jinsia, hawa tuliowataja ni vijana wanaojiunga na JKT na siyo ajira. Kwa maana hiyo kule wanapofanya usaili kuna vigezo ambavyo vinafuatwa, mara nyingi wasichana hawajitokezi kwa wingi lakini wanaojitokeza wengine wanakosa sifa zinazotakiwa na ndiyo maana unaona kuna tofauti ya idadi hapa. Kwa hiyo, mkakati uliopo ni kuwasaidia vijana hawa, wale wanaokosa ajira

katika vyombo vya ulinzi na usalama kuweza kuwapa *study* za kazi ili waweze kuajiriwa na sekta nyingine pamoja na kujiajiri wao wenyewe.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Mbunge wa Welezo sasa aulize swali lake.

Na. 314

**Kuongezeka kwa Vitendo vya Mauaji Zanzibar**

**MHE. SAADA MKUYA SALUM** aliuliza:-

Kumekuwa na vitendo vya mauaji ya mara kwa mara kwa upande wa Zanzibar katika siku za hivi karibuni; mauaji hayo yanatokana na aidha kuuwawa kwa wanaoshukiwa kuwa ni wezi au mauaji mengine hayajulikani chanzo chake.

(a) Je, Serikali imeshafanya tathmini ya hali hiyo?

(b) Je, ni washukiwa wangapi kwa kipindi cha karibuni ambao wametiwa hatiani kutokana na vitendo vya mauaji kwa upande wa Zanzibar?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saada Mkuya, Mbunge wa Welezo lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwa kipindi cha hivi karibuni kumekuwa kukijitokeza mauaji ya aina mbalimbali yakiwemo yale ya wananchi kujichukulia sheria mkononi baada ya kuchukizwa na vitendo vifanywavyo na watu wanaowaua. Hali hii ni kosa kisheria na Serikali imeshafanya

tathmini ya kutosha ambapo kwa kipindi cha Juni, 2016 hadi Juni, 2017 jumla ya watu 34 waliuawa, 29 kati yao waliuawa kwa kutuhumiwa wizi, mmoja kwa tuhuma za ushirikina, wawili kwa tuhuma za wivu wa mapenzi na watatu kwa migogoro ya ardhi. Thathmini hii ya Serikali inakwenda sambamba na utoaji wa elimu kwa wananchi ili wasijichukulie sheria mikononi na badala yake wawafikishe watuhumiwa mbele ya vyombo vya sheria ili kuchukuliwa hatua stahiki za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya watuhumiwa 33 wamekamatwa kwa tuhuma za mauaji na kesi 36 zimefunguliwa na zipo katika hatua mbalimbali mahakamani na baadhi zikiwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, swali la nyongeza.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naishukuru Serikali, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri kabisa hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonekana kwamba utaratibu huu wa utoaji wa elimu hauko *effective* na ndiyo maana haya matukio yameendelea kwa kiasi hicho ambacho Mheshimiwa Waziri amekitaja.

Je, Serikali haioni kama kuna umuhimu wa kubadilisha utaratibu wa utoaji wa elimu kwa wananchi ili wasiendelee kuchukua sheria katika mikono yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, inawezekana kabisa yanatokea haya mauaji kwa sababu wananchi wenyewe wanakuwa wanakosa imani na jeshi la polisi na kwamba pengine wale watuhumiwa wakipelekwa katika vituo vyetu vya polisi, kesho yake wanawaona wako mitaani. Kwa hivyo, Serikali ina mkakati gani wa kuliondoa hili miongoni mwa jamii ili kuona kwamba haki inatendeka kwa kila ambaye amefanya kosa na wale ambao hawajafanya makosa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri kwamba swali lake la kwanza sijalisikia vizuri, alizungumzia utaratibu sikuweza kupata ...

**NAIBU SPIKA:** Ameuliza hamuoni sababu ya Serikali kubadilisha utaratibu wenu namna mnavyotoa elimu kwa maana ya kwamba elimu haiwafikii sawa sawa wale wananchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Sasa nijibu maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo; kuhusiana na utaratibu ambao tunatumia nadhani siyo utaratibu mbaya, hata hivyo tunachukua mapendekezo yake kama ni changamoto ili tuangalie jinsi gani tunaweza tukfikia zaidi wananchi waweze kupata taarifa. Hata hivyo nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi kwa kiasi kikubwa wana imani na jeshi lao la polisi na kutokana na amani na utulivu na upungufu wa takwimu za uhalifu nchini ambao unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikiri kwamba kwa wale wananchi ambao wanakosa imani na baadhi ya askari polisi wachache ambao pengine wamekuwa wakitekeleza majukumu yao kinyume na maadili, niwahakikishie wananchi kwamba wakati wote tunavyobaini askari wa aina hiyo tumekuwa tukichukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo bahati njema ni kwamba askari hao ni wachache, walio wengi wanafanya kazi zao vizuri kwa uadilifu na ndiyo maana nchi yetu inaendelea kuwa salama mpaka sasa hivi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunamalizia swali letu la mwisho. Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 315

**Ujenzi wa Jengo la Askari Polisi - Makunduchi**

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaunga mkono juhudi za ujenzi wa jengo jipya la kisasa la Askari Polisi wa Makunduchi?

**NAIBU SPIKA:** Meshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto ya uhaba wa nyumba za makazi ya askari katika eneo la Makunduchi na katika Mkoa wote wa Kusini Unguja. Eneo la Makunduchi lina jengo moja la ghorofa la makazi ya familia nne za askari lililorithiwa toka Serikali ya Mkoloni na Mahanga mawili yanayotumiwa kwa makazi ya askari. Makazi haya ni sawa na asilimia 10 tu ya mahitaji halisi. Kwa kutambua changamoto hii, Serikali imeanzisha ujenzi wa nyumba za makazi ya familia 12 za askari polisi katika Mkoa wa Kusini Unguja. Aidha, Serikali kwa kupitia jeshi la polisi na kushirikiana na wadau imeanzisha ujenzi wa kituo cha polisi cha Daraja B huko Dunga, kituo hiki kimefikia hatua za mwisho kumalizika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimwia Mwantumu Haji swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na yenye tija ndani yake na pia nakiri kwamba katika kituo cha Dunga ni kweli tayari hili jengo liko katika

kukamilisha mwisho wake kuwa zuri sana na lifanye kazi. Niseme maswali yangu mawili ya nyongeza, kwa kuwa jengo la Makunduchi la muda mrefu na mwaka 2015 waliamua polisi kuweka *foundation* pale ili wapate kituo chao cha uhakika, je sasa swali langu liko hapa; Serikali itamaliza ujenzi huu lini? Swali langu la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwamba eneo la Makunduchi ni eneo la utalii. Kila mwaka kule Makunduchi kunakuwa kunafanywa Mwaka Kogwa, na ukizingatia hata mwaka jana Mheshimiwa Waziri wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa yeye ndiyo mgeni rasmi alikwenda kule. Swali langu lipo hapa, Serikali ina mpango gani wa kuweka ulinzi katika eneo lile hasa sambamba na ujenzi wa vituo vya polisi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na swali lake la kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika maeneo ambayo tunayaangalia kwa karibu pale ambapo bajeti itakapokaa vizuri tuweze kumaliza ni hilo jengo ambalo amelizungumza la kituo cha polisi Makunduchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kuimarisha ulinzi hasa ukizingatia eneo la Makunduchi ni sekta ya utalii, nimhakikishie kwamba sasa hivi tunavyozungumza tuna mkakati kabambe wa kuimarisha usalama katika maeneo hususan Ukanda wa Pwani wa Zanzibar maeneo ambayo yamekuwa yanatumika kiutalii ili tuweze kuongeza imani ya watalii na wawekezaji katika ukanda huo. Kwa hiyo, tutakapokamilisha mkakati huo, sehemu ya Makunduchi ni moja katika maeneo ambayo yatafaidika.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu, sasa nitamkaribisha Mwenyekiti aje aendelee na ratiba yetu.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na matangazo hivi sasa. Tutaanza na matangazo ya wageni ambao wapo Bungeni leo hii, nitaanza na wageni wa Mheshimiwa Naibu Spika waliopo *Speaker's Gallery* kutoka Shirika la Ndege Tanzania *(ATCL)* ambao ni ndugu Edward Mkwabi, *Sales Director* karibu sana; ndugu Salome Seloyeka, Meneja *ATCL* Dodoma; ndugu Andrew Israel, *Traffic Lesson Officer*, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Spika waliopo *gallery* ya kawaida ni ndugu Emmanuel Mbasha na ndugu Patric Mbasha, karibuni wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni wengine wapo kwenye jukwaa la Mheshimiwa Spika ni wageni watano (5) ambao ni watumishi wa Bunge la Wawakilishi wa Nigeria waliokuja kwa ajili ya mafunzo ya siku tatu Mr. Ahmed Salisu Yard, *Director of Bill (Team Leader)* karibu sana; Mr. Ezennia Nwanekezie, *Chief Legislative Officer;* Mrs. Lauratu Idris Mohamed, *Assistant Chief Legal Draftsman*, karibu sana; Ms. Dora Ohene, *Chief Legislative Officer*, karibuni; Mr. Tordue Nyitse, *Assistant Chief Legislative Officer,* karibuni sana wageni wetu hao kwenye *gallery* la Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni 165 wa Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani, Mbunge, Waziri wa Nishati ambao ni Watendaji kutoka Wizara ya Nishati pamoja na familia yake. Dkt. Hamisi H. Mwinyimvua, Katibu Mkuu, karibu sana Katibu Mkuu wetu; Dkt. Alexander Kyaruzi, Mwenyekiti wa Bodi ya *TANESCO*; karibu Mwenyekiti; Profesa Sufian Bukurura, Mwenyekiti wa Bodi ya *TPDC*; Ndugu Michael Nyagoga, Menyekiti wa Bodi ya *REA*, Profesa Gasper Mhinzi, Mwenyekiti wa Bodi ya *PURA*, Dkt. Lutengano Mwakahesya, Menyekiti wa Bodi ya *PBPA*; Ndugu Fadhili Manonga, Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya *EWURA*; Ndugu Beatus Segeja, Mwenyekiti wa Bodi ya *TPDC*; Dkt. Tito Mwinuka, Mkurugenzi Mtendaji wa *TANESCO*; *Engineer* Amos Maganga, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa *REA*; *Engineer* Kapulya Musomba, Kaimu Mkurugenzi

Mtendaji wa *TPDC*; Ndugu Charles Sangweni, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa *PURA*; *Engineer* Kato T. Kabaka, Meneja Mkuu *TPDC*; Ndugu Nzinyangwa Mchany, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa *EWURA* na Ndugu Erasto Simon, Kaimu Mtendaji Mkuu wa *PBPA*. Hao wameambatana na Wakuu wa Taasisi, Idara zote zilizochini ya Wizara ya Nishati, Karibuni sana wageni wetu kutoka Wizara hii ya Nishati. *(Mkofi)*

Wageni wengine ni wageni 12 wa Mheshimiwa Dkt. Kalemani ni Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Chato wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Chato ndugu Rafael Masambo, karibuni sana wageni wetu kutoka Chato. *(Makofi)*

Pia wapo wageni 38 wa Mheshimiwa Dkt. Kalemani ni Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato wakiongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Batholomeo Manunga na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Chato Ndugu Eliud Mwaiteleke, karibuni sana wageni wetu kutoka Chato. Wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Kalemani ni familia yake wakiongozwa na Mke wake Ndugu Vaileth Kalemani, karibuni sana katika Bunge letu wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni tisa wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Mbunge, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni Machifu kutoka Mkoa wa Mara na Mkoa wa Singida, haya Machifu wetu wale pale karibu sana katika Bunge letu. *(Mkofi)*

Wageni 35 wa Mheshimiwa Deo Sanga, Mbunge ambao ni Wenyeviti, Makatibu na Wenezi wa Kata mbalimbali wa CCM kutoka Jimbo la Makambako, Mkoa wa Njombe wakiongozwa na ndugu Vasco Mugunda, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 23 wa Mheshimiwa Jesca Kishoa, Mbunge kutoka Hakirasilimali wakiongozwa na ndugu Rachel Chagonja, karibu. *(Makofi)*

Karibuni sana wageni watano wa Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge kutoka Same Mkoa wa Kilimanjaro wakiongozwa na Katibu wa Kata ya Mamba ndugu Dia Chikira, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Augustino Masele, Mbunge ambaye ni mtoto wake kutoka Mkoa wa Geita ndugu Victor Masele, karibu. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Mbunge ambao ni ndugu zake kutoka Mkinga Mkoa wa Tanga wakiongozwa na ndugu Mohamed Mbaruku, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Shabani Shekilindi, Mbunge ambao ni rafiki zake kutoka nchini Ujerumani, ndugu Chiara Zwaan na ndugu Natasha Swai, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa John Mnyika, Mbunge ambao ni viongozi wa CHADEMA kutoka Jimboni, Jimbo la Kibamba wakiongozwa na Diwani wa Kata ya Mbezi Mheshimiwa Humphrey Sambo, karibuni sana wageni wetu kutoka Mbezi. *(Makofi)*

Wageni 56 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mbunge ambao ni Kwaya ya Safina kutoka Kanisa la Anglikana Jijini Dodoma wakiongozwa na ndugu Paul Joel, karibuni hao naona hawapo. *(Makofi)*

Wageni 67 wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni wanamaombi kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na *Bishop* Dkt. Elia Mauza, karibuni sana wageni wetu. Wageni wengine watatu wa Mheshimiwa Ritta Kabati ni Masista kutoka Shirika la Theresia wa Mtoto wa Yesu kutoka Tosamaganga Mkoa a Iringa, karibuni sana Masista wetu kutoka Mkoani Iringa. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Sonia Magogo, Mbunge ambao ni ndugu zake kutoka Dar es Salaam ndugu

Shahada Omar na ndugu Irene Magoa. Karibuni wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni 29 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni kwaya ya Uinjilisti kutoka Usharika wa Segerea Mkoa wa Dar es Salaam wakiongozwa na Mchungaji Noah Kipingu. Karibuni sana wanakwaya wetu kutoka Mkoa wa Dar es Salaam huko Segerea. *(Makofi)*

Wageni wengine ambao wako katika Bunge kwa ajili ya mafunzo ni walimu 30 kutoka shule ya msingi Mwere B ya Mjini Morogoro, karibuni walimu 30 kutoka shule ya msingi, karibuni sana walimu. *(Makofi)*

Viongozi watano wa Bunge la Vijana la mwaka 2018 ambao ni ndugu Zephania Sane Spika wa Bunge la Vijana 2018, naona siwaoni. Ndugu Ashiruna Muhunzi, Naibu Spika wa Bunge la Vijana 2018, wapo, wale kule juu. Ndugu All Yanga, Waziri Mkuu wa Bunge la Vijana 2018, karibuni sana nawaona kule juu. Ndugu Mrisho Ndili kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bunge la Vijana 2018, karibu. Ndugu Shabir Bigirwa, Mwanasheria Mkuu wa Bunge la Vijana 2018, karibu, wapo kule juu. Ndugu Alphonsina Ambrosi Katibu wa Bunge la Vijana 2018, karibu. Ndugu Razaro Sabas, mnadhimu wa Kambi Tawala, Bunge la Vijana 2018 na ndugu Shaaban Mohamed Katibu Mezani Bunge la Vijana 2018, karibuni sana vijana wetu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Kuna tangazo kwa Waheshimiwa Wabunge, watumishi wa Bunge na Wakristo wote katika eneo la Bunge. Waheshimiwa Wabunge wote, watumishi wa Bunge pamoja na wakristo walioko kwenye eneo la Bunge wanatangaziwa kuhudhuria ibada katika eneo la wazi la *basement* leo siku ya Jumanne tarehe 28 Mei, 2019 saa saba mchana.

Aidha, Mchungaji Kipingu kutoka Usharika wa Segerea kanisa la KKKT atahudumu katika ibada hiyo. Waheshimiwa Wabunge wote na wakristo wote mnakaribishwa. Katibu!

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mwongozo wa Spika.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Nishati**

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mwongozo wa Spika.

**MBUNGE FULANI:** Hoja ya dharura.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Massay.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninayo Taarifa hapa kule Jimboni kwangu tembo wameingia Mjini na wameua watu wawili na wanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa sababu jambo hili linakuwa hatari na tembo wanaendelea na wawili wanaongezeka wako mjini na watu watano wako hospitali. Naomba unisaidie ili mambo haya yaende vizuri, Serikali inisaidie kule kwa sababu eneo hilo ni hatari sana na tembo wanaweza kuendelea kuua watu wengi jimboni.

**MBUNGE FULANI:** Hoja ya dharura.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kuomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) nikisoma na ile Kanuni ya 46(1). Leo nilikuwa na swali langu Na. 307 ambalo siwezi nikalisema lakini lilikuwa linahusu kufifia kwa ufaulu kwa masomo ya sayansi kwa wanafunzi wetu

ambako kunachangiwa na upungufu wa walimu wa sayansi na maabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anatoa majibu yake, sio tu ametumia lugha ya dhihaka dhidi ya Wabunge, lakini ametoa majibu ambayo ni ya uongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge tunapokuja kuuliza maswali hapa kwanza itambulike kwamba tulikuwa tumeshiriki vikao vya halmashauri zetu na tunaelewa matatizo yaliyoko kwenye halmashauri zetu na tupo *in contact* na watendaji wa Halmashauri zetu. Kwa hiyo, tunavyoandika swali na hili swali nimeliandika muda mrefu sana, 2016, nilitarajia Wizara ingekuwa na majibu ya kukidhi na Naibu Waziri nimekuwa nikim uona akifanya ziara nyingi sana Tarime kwa hiyo nilitegemea atakuwa na majibu yenye kukidhi maana Serikali imeleta majibu ambayo hayana uhalali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kiti chako kiongoze sasa, kwanza itambulike kwamba tunashiriki vikao na tunajua shida lakini Halmashauri ya Mji wa Tarime wamejibu kwamba Sekondari zote zina maabara kitu ambacho ni uwongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ningependa kujua utoe mwongozo Serikali sasa iende ilete majibu ya kina kwa mustakabali wa wananchi wa Tarime na Tanzania kwa ujuma. *Plus* niliuliza swali kuhusu kupeleka fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa hizi maabara, Naibu Waaziri hakujibu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwanza kiti chako kiagize ni kwanini Serikali inajibu uwongo licha ya kukaa na maswali muda mrefu na umuagize aende ahakikishe uhalisia ulioko Tarime na ahakikishe ametekeleza kwa ajili ya wanafunzi wetu wa kule na alete majibu yenye uhalisia Bunge hili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lwakatare.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nasimama kwa mujibu wa Kanuni 47(1) na 48(3)(a)na 48(4). Hivi sasa ninaposimama hapa wananchi wa Manispaa ya Bukoba wako kwenye taharuki kubwa kufuatia mvua ambazo zimeanza kunyesha tangu siku ya juzi na nyingine kuendelea jana kwamba kuna mafuriko makubwa sana katika Manispaa ya Bukoba ambapo mtu mmoja mtoto wa miaka 11 amefariki na nyumba zaidi ya 75 zimepata maafa makubwa lakini pia maji yale yamesambaa ndani ya mji kiasi cha kusababisha hali ya watu kutoka kwenye mtaa kwenda kwenye mtaa kutumia mtumbwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naleta hoja kwamba unikubalie hoja hii iweze kujadiliwa kwa maslahi mapana ya watu wa Bukoba na Mji wa Manispaa ya Bukoba ili hali inayoendelea ambayo ni tete ambayo imewaweka katika wasiwasi na kufikiria kwamba sasa ule mji umelaaniwa kwa sababu matukio yote yanaendelea kutokea tu katika mji huo huo ili tuweze kulijadili kwa muda utakaoupanga wewe mwenyewe. Naomba kuwasilisha. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimepata miongozo mitatu kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko. Kwanza kutoka kwa Mheshimiwa Massay kuhusu tembo ambao wanaingia huko kwenye mji wake naamini hili Serikali wameshalisikia na wao ndiyo wana vitengo vinahusikana na hilo jambo, naamini kwamba watalifuatilia.

Lakini kuhusu Mheshimiwa Esther Matiko, Kanuni yake aliyitumia kuhusu swali lake ambalo anasema hakuridhika na majibu basi kama ni uwongo kweli, Serikali itatuletea ili tuone kama kuna uwongo lakini kama ni ukweli ambayo ameyazungumza Mheshimiwa Waziri basi Mheshimiwa Esther Matiko itabidi uthibitishe.

Mheshimiwa Waitara, atajibu sasa hivi kama itathibitika kwamba aliyoyasema Waziri ni ya kweli, Mheshimiwa Esther Matiko itabidi wewe sasa uthibitishe uwongo huo uko vipi.

Suala la mwisho wa Mheshimiwa Lwakatare hatuwezi kujadili kwa sababu suala la mvua linatokea maeneo mengi ya nchini na hilo ni jukumu la Serikali kuangalia maeneo hayo na kuyafanyia kazi kama ambavyo kawaida ilivyo. Nimkaribishe Mheshimiwa Waitara aweze kujibu swali la Mheshimiwa Esther.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba niendele kurudia kwamba majibu ambayo nimetoa hapa hasa majibu ya msingi ni majibu sahihi na sababu yake ni kwamba swali limekuja katika ofisi yake tunafanya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichozungumzwa hapa ni kwamba waliuliza habari ya kumalizia maabara lakini pia na ufaulu na mikakati iliyopo. Kwa hiyo, tumetaka kujua halmashauri ambayo nimezungumza, Mheshimiwa Mbunge ni mjumbe wa vile vikao. Wilaya ya Tarime wanafanya kazi nzuru sana Maafisa wetu wa elimu na hasa sekondari, wanasema ufaulu kwanza hata kwenye mkoa ukilinganisha, sio kwamba Tarime ni wilaya ya mwisho, Wilaya ya Rorya ndiyo wilaya ya mwisho, wilaya ya Tarime inafanya vizuri kuliko wilaya zingine pale katika Mkoa wa Mara. Lakini wanatuambia maabara hazitoshi kweli kwa maana ya kila shule wanafunzi wanafanya mazoezi kwa vitendo kutumia maabara zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi anayozungumza Mheshimiwa Mbunge, tumesema tumetoa maagizo katika halmashauri zote walete maabara zilizokamilika ili tupeleke vifaa. Tumeshapokea taarifa, mchakato unaendelea. Kama kuna taarifa anazo tuwasiliane ili tuweze kuzilinganisha. Nimetoa tamko hapa kwamba inawezekana kuna taarifa ambazo Wabunge wanazo, wataalam wana zingine, wakurugenzi wanapata taarifa wawasiliane kwa pamoja ili iende sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya mwisho ambayo naizungumza hapa ya kupeleka fedha na kumalizia

maboma, nimejibu tumeanza kupeleka vifaa vya maabara, tumepata taarifa, tumepeleka vifaa vya maboma shule ya msingi. Itakapofika wakati wakugawa hizi fedha, tutazingatia maombi ya Waheshimiwa Wabunge, lakini tuangalie pia mahali ambapo kuna upungufu mkubwa katika eneo hilo. Taarifa hizi ambazo zimetolewa hapa ni taarifa sahihi kwa sababu huwa tunawasiliana katika vyombo vyote na katika vikao wamepitisha, wametuletea hapa. Taarifa za kwake za kwake ndiyo sina uhakika nazo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Esther Matiko, huo ndiyo mwongozo ambao umetoka Serikalini na kama hujaridhika basi utapeleka malalamiko yako kwa mujibu wa utaratibu.

Tunaendelea na hoja za Serikali. Sasa namkaribisha Waziri wa Nishati aweze kuja kutoa hoja yake.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Nishati

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba Taarifa za Bajeti ambazo tumewasilisha hapa Bungeni pamoja na ambayo nitasoma hivi sasa zote ziingie katika Bunge lako tukufu kwa maana ya Hansard za rekodi za kumbukumbu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2019/2020 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuendelea kuwajaalia afya njema viongozi wetu wakuu wa

Kitaifa. Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, Waheshimiwa Wabunge na viongozi wengine mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe salamu na kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge na hasa Kisekta katika Sekta ya Nishati na leo mbele yako nawasilisha katika Bunge lako tukufu hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tupunguze sauti, tuongee taratibu ili tumsikilize Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niungane na Mawaziri wenzangu, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo yake thabiti yanayosaidia kusimamia vyema Sekta ya Nishati. Ni dhahiri kwamba Rais wetu amekuwa chachu katika kutekeleza mipango mikubwa na yenye tija katika Sekta ya Nishati hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango hiyo ni pamoja na kuanza kutekeleza mradi mkubwa wa kielelezo wa kuzalisha umeme kwa kutumia maporomoko ya maji ya mto Rufiji *megawatt* 2115. Napenda kuwaahidi Watanzania kuwa Wizara yangu kwa kushirikiana na Bunge lako tukufu na wadau mbalimbali tutasimamia vyema mradi huu ili ukamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwashukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mbunge) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kwa miongozo mbalimbali wanayonipatia katika kusimamia Sekta ya Nishati. Nakiri kuwa maelekezo na miongozo ya watu hawa pamoja na mambo mengine yamenisaidia sana kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ally Mohammed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kusimamia vyema ufanisi na utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kuwapongeza Mawaziri walioteuliwa hivi karibuni na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nampongeza Profesa Palamagamba John Aidan Kabudi aliyeteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Angella Jasmine Kairuki aliyeteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji, Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustine Phillip Mahiga aliyeteuliwa kuwa Waziri wa Sheria na Katiba, Mheshimiwa Dotto Mashaka Biteko (Mbunge) aliyeteuliwa kuwa Waziri wa Madini, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga aliyeteuliwa kuwa Waziri wa Kilimo na Mheshimiwa Joseph George Kakunda aliyeteuliwa kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuwapongeza pia Naibu Mawaziri akiwemo Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Kilimo na Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara aliyeteuliwa kuwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukupongeza wewe mwenyewe, pia Wenyeviti wa Kamati za Bunge, Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge katika umahiri wao katika kulishauri. Kwa namna yapekee natoa shukurani zangu

za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Dunstan Kitandula (Mbunge), Makamu Mwenyekiti, Mariam Ditopile Mzuzuri na wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa ushauri na maelekezo waliyotupatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri kuwa Kamati imefanya kazi kubwa ya kuishauri Wizara katika masuala mbalimbali na kuchambua kwa kina mapendekezo ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2019/2020. Wizara itaendelea kushirikiana na Kamati katika kusimamia kwa ajili ya ufanisi wa Sekta ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Mapato, Matumizi na utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Nishati kwa mwaka 2019/2020 pamoja na Makadirio ya Mapato na Mapato kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti iliyopitishwa kwa ajili ya Wizara ya Nishati pamoja na Taasisi zake kwa mwaka 2018/2019 ni jumla ya shilingi trilioni 1.692 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, bajeti ya miradi ya maendeleo ilikuwa shilingi trilioni 1.665 sawa na asilimia 98.4 ya bajeti yote ya Wizara ambapo matumizi ya kawaida ni shilingi bilioni 27.15 sawa na asilimia 1.6 ya bajeti yote ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 Wizara ilikuwa imepoke ajumla ya shilingi trilioni 1.227. fedha hizi zinajumuisha shilingi bilioni 688.65 ambazo ni malipo ya awali yaani *advance payment* kwa mkandarasi wa ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa Rufiji ambao ni bilioni 169.71 ambazo ni fedha za nje zilizopelekwa katika miradi hiyo ni pamoja na miradi ya *REA, TANESCO* pamoja na miradi mingine ya maendeleo. Kiasi hicho kilichopokelewa na WIzara ni sawa na asilimia 87 ya fedha zilizotarajiwa kupokelewa katika kipindi hicho ambazo ni shilingi trilionni 1.410.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Nishati katika mwaka 2018/2019 ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 394.45 hadi kufikia tarehe 15 May 2019 Wizara kupitia *TPDC* na utafiti wa mafuta jumla ya mauzo imekusanya shilingi bilioni 484.33. Makusanyo haya ni sawa na shilingi bilioni 123 ya lengo la makusanyo ya asilimia 394.54. Kwa mwaka 2019 sababu ya kuvuka lengo ni kuongezeka kwa matumizi ya gesi asilia yanayotokana na kuunganishwa kwa kituo cha kuzalisha umeme wa Kinyerezi II pamoja na kiwanda cha Dangote kinachotumia umeme wa gesi katika kutengeneza saruji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makisio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2019/2020 ni shilingi bilioni 602.35 sawa na ongezeko la asilimia 52.6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 394.45 lililokuwa lengo la mwaka 2018/2019. Ongezeko hili, linatokana na makusanyo ambayo yameongezeka kutokana na matumizi ya rasilimali ya gesi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya kipaumbele ya Wizara kwa mwaka 2018/2019 yalikuwa ni pamoja na kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutekeleza miradi mikubwa ikiwemo mradi wa kuzalisha umeme wa Mto Rufiji *megawatt* 2115 na miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia Kinyerezi I *extension megawatt* 185 pamoja na Kinyerezi II *megawatt* 240.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ya kipaumbele ilikuwa ni kuimarisha mifumo ya kusafirisha umeme nchini, kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Mradi Kabambe wa kusambaza umeme vijijini. Kadhalika, ni kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima hadi Tanga Tanzania na pia kuimarisha shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi na kuendeleza miradi ya nishati jadidifu ikiwepo joto ardhi, upepo na umeme jua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa kutokana na utekelezaji wa maeneo hayo ya kipaumbele Wizara imepata mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na nchi kutokuwa na mgao wa umeme katika kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2018/

2019. Aidha, pamoja na kutokuwa na mgao wa umeme, Taifa letu limeanza kuwa n a ziada ya umeme wa wastani wa *megawatt* 300 kwa siku kwa mwaka 2018/2019 tofauti na awali tulipokuwa na upungufu wa *megawatt* 100 kwa mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio makubwa 21 ni kama yafuatayo; kwanza kwa utekelezaji wa mradi mkubwa wa kuzalisha umeme kutoka Mto Rufiji *megawatt* 2115 utakaokamilika mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa bwawa hili utaifanya Tanzania kuwa na umeme wa uhakika unaotabirika na wenye gharama nafuu. Aidha, ujenzi wa bwawa la mradi huu utaifanya Tanzania kushika nafasi ya kwanza Afrika Mashariki kwa kuwa na bwawa kubwa, nafasi ya nne kwa Afrika na kati ya mabwawa 70 Duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya pili makubwa ni kukamilika kwa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 220 kutoka Makambako, Madaba hadi Songea, pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Madaba na Songea na upanuzi wa kituo cha Makambako. Kukamilika kwa njia hii ya kusafirisha umeme kumefanya mikoa ya Njombe na Ruvuma kuunganishwa katika Gridi ya Taifa na hivyo kusitishwa kwa matumizi ya mitambo ya mafuta ambayo ilikuwa ikigharimu *TANESCO* na kuokoa wastani wa shilingi bilioni 9.8 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zilikuwa zikitumika sana kununua mafuta katika Vituo vya kuzalisha umeme vya Madaba, Ludewa, Songea, Mbinga na Namtumbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio makubwa ya tatu ni kuongezeka kwa kasi ya kusambaza umeme vijijini ambapo hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 Serikali ilipeleka umeme katika vijiji 7,127 vya Tanzania Bara ikilinganishwa na vijiji 2,018 vilivyokuwa vimeunganishwa umeme mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni sawa na ongezeko la vijiji 5,109 kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 253 ya vijiji vilivyokuwa na umeme kufikia mwaka 2015. Aidha, ifikapo mwezi Juni, 2020 vijiji zaidi ya 10,278 kati ya 12,268 vya Tanzania Bara vitaunganishwa umeme sawa na asilimia 84 ya vijiji vyote na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza Afrika Mashariki na nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara kuwa ya kwanza kupeleka umeme vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Wilaya na Halmashauri 15 za nchi yetu zimefikishiwa umeme katika vijiji vyake vyote na kazi inayoendelea ni kuunganisha umeme katika vitongoji vyake. Wilaya pamoja na Halmashauri hizo ikiwemo ni Mafia, Isimani, Pangani, Rufiji, Bahi, Siha, Moshi, Hai, Mwanga, Rombo, Madaba, Buhigwe, Makambako pamoja na Korogwe Mjini. Pamoja na kukamilisha wilaya na halmashauri hizo, kwa sasa kazi zinazoendelea ni kuunganisha umeme katika maeneo ya vitongoji vya vijiji hivyo, ambapo zoezi hili litakamilika mwezi Juni, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya nne Serikali kupitia *TANESCO* kuanza kuunganisha umeme kwa Shilingi 27,000 kuanzia Mei, mwaka huu 2019 katika maeneo yote nchini katika vijijini vyote vya nchi yetu, sawa na kutekeleza mpango wa *REA* unaoendelea hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya tano ni kuunganisha Gridi ya Taifa katika maeneo mbalimbali yakiwemo Tunduru, Mreba na Liwale na hivyo kuokoa jumla ya Shilingi bilioni 7.33 kwa mwaka zilizokuwa zikitumika kununua mafuta mazito ya kuendesha mitambo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya sita ni kukamilika kwa ujenzi wa mradi wa Kinyerezi II na kuongeza jumla ya MW 248.22 katika Gridi ya Taifa. Kituo cha Kinyerezi II ni cha kwanza hapa nchini kutumia teknolojia ya kisasa yaani *combined cycle*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya saba ni kuendelea kutumia vifaa vya ndani katika ujenzi wa miundombinu ya kuunganisha na kusambaza umeme ikiwemo nguzo, mashineumba *(transfoma),* nyaya na mita za LUKU na hivyo kulipunguzia gharama kubwa Shirika letu la *TANESCO* na kuokoa takribani Shilingi bilioni 162.57 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu umetengeneza ajira kwa watanzania wapatao 3,520 na kuharakisha utekelezaji wa miradi ya umeme. Kutokana na mafanikio hayo, kwa sasa kuna zaidi ya viwanda vitatu (3) vya kuzalisha transfoma badala ya kimoja kilichokuwepo, lakini kuna viwanda tisa (9) vya nguzo badala ya vitatu (3) vilivyokuwepo awali, lakini viwanda pia vingine vitano (5) badala ya kiwanda kimoja cha *East African Cables* kwan ajili ya nyaya. Pia kumekuwepo na viwanda vitatu (3) kwa ajili ya kutengeneza LUKU za Mita zinazotumika kusambaza umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya nane ni kuanza kutekeleza mradi wa kujenga njia ya kusafirisha umeme kV 132 ili kuunganisha mikoa ya Kigoma na Katavi katika Gridi ya Taifa. Mradi huu utasafirisha umeme kutoka Tabora – Urambo - Kaliua, Nguruka hadi Kidahwe umbali wa kilomita 391 na kutoka Tabora – Ipole, Inyonga hadi Nsimbo (Katavi), umbali wa kilomita 381.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya tisa ni Shirika la Umeme nchini kutohitaji ruzuku ya Serikali katika shughuli zake za uendeshaji kutokana na *TANESCO* kujiendesha lenyewe na kuokoa wastani wa Shilingi bilioni 133 zilizokuwa zikitumika kama ruzuku kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya kumi ni kuimarika kwa mapato ya *TANESCO* kwa kiwango cha ongezeko la asilimia 1.5 mwaka 2017/2018 hadi kufikia asilimia 7.6 mwaka 2018/2019 kutokana na makusanyo ambayo pia imefanya kwenye shughuli zake za uendeshaji. Hivyo ni

matarajio kuwa *TANESCO* itaweza kuanza kutoa ruzuku Serikalini kuanzia sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuunganishiwa umeme kwa wateja wapya 9,882 katika kipindi cha kuanzia Julai, 2015 hadi tarehe 15 Mei, 2019 na kufikia jumla ya wateja bilioni 2.4 kutoka bilioni 1.4 iliyokuwepo mwaka 2015. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 66 kwa miaka mitatu iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya 12 ni kuongeza mtandao wa kusambaza gesi asilia viwandani na majumbani, mtandao huu utawezesha kuunganisha wateja wa awali wa gesi asilia majumbani wapatao 500 katika Jiji la Dar es Salaam. Mpango huu wa usambazaji wa gesi nyumbani una punguzo la asilimia 40 la bei ya kawaida ya mtungi wa sasa. Kwa upande wa viwanda, viwanda vya Dangote pamoja na vingine vya Knauf na Rorya vimesambaziwa gesi katika kipindi hiki. Aidha, matumizi ya gesi katika magari yameongezeka kutoka magari 80 mwaka 2018 na kufikia magari zaidi ya 200 kwa mwaka 2019 ikiwa ni ongezeko la zaidi ya asilimia 150.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya 13 ni kukamilika kwa ukarabati wa vituo vya kupoza umeme vya Kigamboni na Kurasini na hivyo kuimarisha hali ya upatikanaji umeme katika Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya Kigamboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio mengine ya 14, kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya kupeleka umeme katika Mji wa Serikali eneo la Mtumba, ambapo pia tumeunganisha umeme katika Wizara zote na makao yao mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya 15 ni kuanzisha utaratibu mpya wa Mawasiliano baina ya wateja na *TANESCO* kupitia mitandao ya kijamii kuanzia katika magrupu yao kwa njia ya *whatsapp* na hii inaharakisha upelekaji wa huduma ka wateja na kuimarisha mapato ya shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya 16 ni kuongezeka kwa ufanisi wa makusanyo na mapato ya Serikali

ambapo hadi kufikia tarehe 15 Mei, 2019 Wizara kupitia *TPDC* ilikuwa imekusanya Shilingi bilioni 484.33 sawa na asilimia 1.34, lengo hili limevukwa kwa sababu ilikuwa ni lengo la shilingi bilioni 394.45 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya 17 ni kuendelea kutekeleza kazi za awali za Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima hadi Chongoleani (Tanga) zikiwemo *Geotechnical* pamoja na majadiliano ya *HGA* yanaanza kukamilika. Kazi hizo zitakamilika mwezi Juni, mwaka huu na kazi nyingine za maandalizi ya ujenzi nazo zitaanza kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya 18 ni kuongeza uzalishaji wa gesi asilia kufikia Futi za Ujazo milioni 190 kwa siku kwa mwaka 2018/2019 kutoka Futi za Ujazo milioni 175 kwa siku mwaka 2017/2018. Ongezeko hilo ambalo ni sawa na asilimia 8.6 limewezesha upatikanaji wa gesi kwa matumizi ya viwandani, majumbani na katika masuala ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya 19 ni kupungua kwa muda wa kushusha mafuta katika Bandari zetu za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara kutoka kati ya siku 30 na 60 hadi kati ya siku 3 hadi 8 kutokana na Serikali kuendelea kuimarisha Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja na hivyo kupunguza gharama zilizokuwa zinatokana na gharama za meli kuchelewa kushusha mafuta bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya 20 ni kupatikana kwa mafuta ya kutosha na ya uhakika katika kipindi chote cha mwaka 2018/19 ambapo hadi sasa kuna ziada ya lita milioni 125.22 za dizeli, lita milioni 94.67 za petroli, lita milioni 18.95 za mafuta ya taa pamoja na mafuta ya ndege ambayo kwa pamoja yanatosheleza hadi kwa muda wa zaidi ya siku 32.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya 21 ni kukamilika kwa ujenzi wa jengo la awamu ya kwanza la Wizara na

kuhamia Ofisi mpya katika Mji wa Serikali eneo la Mtumba Jijini Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2019/2020, Wizara ya Nishati itaendelea kutekeleza maeneo ya vipaumbele yakiwemo; kuongeza uzalishaji wa umeme nchini ili kufikia lengo la kuwa na *MW* 10,000 mwaka 2025, lengo hili litafikiwa kwa kutekeleza miradi mikubwa ikiwemo, mradi wa kuzalisha umeme katika maporomoko ya Mto Rufiji *MW* 2,115 na mradi wa kufua umeme kwa kutumia gesi asilia wa Kinyerezi I MW 185, Miradi mingine ni pamoja na kuzalisha umeme wa Rusumo MW 80, mradi wa Rufiji pamoja na Ruhudji MW 358 lakini Rumakali MW 222, pamoja na kuimarisha njia za kusafirishaji wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine muhimu ni kuendelea kujenga njia za kusafirisha umeme katika upande wa *North - West Grid Extension* wa kV 400 yenye urefu wa umbali wa kilomita 1,384 inayojumuisha Iringa – Mbeya – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma hadi Nyakanazi. Mradi mwingine unaotoka Singida – Arusha– Namanga kV 400, umbali wa kilomita 414; Rufiji - Chalinze – Dodoma kV 400, umbali wa kilomita 512; Rusumo – Nyakanazi kV 220, kilomita 98; Geita – Nyakanazi kV 220, kilomita 133; Tabora – Urambo – Kaliua – Nguruka hadi Kidahwe Mkoani Kigoma umbali wa kilomita 391; na Tabora – Ipole – Inyonga hadi Nsimbo (Katavi) umbali wa kilomita 381.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ya kisekta yanayozingatiwa na Wizara ni pamoja na kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA),* katika vijiji ambavyo vimebakia sasa 1,990 vilivyobaki vitapelekewa umeme ifikapo mwezi Juni, 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya upatikanaji wa umeme nchini**,** hali ya umeme nchini imeendelea kuimarika katika kipindi chote cha mwaka 2018/2019. Aidha, mahitaji ya umeme nchini yameendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na kukua na kuongezeka kwa shughuli za

kiuchumi zinazohitaji nishati ya kutosha, uhakika inayotabilika, pamoja na gharama nafuu. Katika mwaka 2018/2019 uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme *(installed capacity)* nchini umeongezeka na kufikia MW 1,601.90 kutoka MW 1,517.47 zilizofikiwa mwaka 2017/2018 sawa na ongezeko la asilimia 5.6. Kati ya jumla ya MW 1,601 zilizopo nchini, MW 1,565.72 zimeunganishwa katika Gridi ya Taifa na MW 36.18 zipo nje ya Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Spika, matumizi ya juu ya umeme yamefikia MW 1,116.58 ikilinganisha na MW 1,551.02. Umeme uliozalishwa nchini uliongezeka kutoka GWh 7,114 mwaka 2017 na kufikia GWh 7,374 mwaka 2018 sawa na ongezeko la asilimia 3.7. Hadi kufikia mwaka 2015, nchi yetu ilikuwa na uwezo wa kuzalisha umeme wa MW 1,204 ikilinganishwa na uwezo wa sasa wa MW 1,601.90 sawa na ongezeko la asilimia 33. Katika kutimiza azma ya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa viwanda, Serikali kupitia Wizara ya Nishati imelenga kuzalisha umeme wa MW 10,000 ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Mto Rufiji MW 2,115. Mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 2,115 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rufiji. Mkataba wa ujenzi wa mradi ulisainiwa tarehe 12 Desemba, 2018 kati ya *TANESCO* na Mkandarasi Kampuni ya *Arab Contractors* na *Elsewedy* zote za kutoka Misri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2018/2019, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa miundombinu wezeshi ikijumuisha: njia ya kusafirisha umeme wa MW 8 yenye msongo wa kV 33 kutoka Msamvu, Morogoro hadi eneo la mradi; barabara za kiwango cha changarawe za Ubena – Zomozi na Kibiti – Mloka hadi eneo la mradi; maeneo mengine ni mifumo ya maji; mawasiliano ya simu; na nyumba za kuishi Mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2019/2020 Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi huu

muhimu ambapo kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kuanza ujenzi wa bwawa *(main dam)* pamoja na kuanza ujenzi wa njia za kupitisha maji *(tunnels)*; pia kazi zingine zitakuwa ni kukamilisha ujenzi wa njia ya pili ya umeme msongo wa kV 33 kutoka Gongo la Mboto na kuendelea kwenye eneo la mradi. Fedha za ndani Shilingi trilioni 1.443 zimetengwa kwa mwaka 2019/2020 kwa ajili ya kutekeleza mradi huu. Utekelezaji wa mradi umeanza mwezi Desemba, 2018 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2022 gharama ya mradi huu ni shilingi trioni 6.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Serikali imedhamiria kwa dhati kutekeleza Mradi huu bila kuyumbishwa, bila kucheleweshwa wala kukwamishwa na mtu yeyote, ama kutoka ndani ama nje ya nchi kwa maendeleo ya ustawi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Ruhudji – MW 358. Mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kufua umeme wa MW 358 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhudji mkoani Njombe. Ujenzi wa mradi huu utahusisha njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 400 yenye urefu wa kilomita 170 kutoka Ruhudji hadi kituo cha kupoza umeme cha Kisada mkoani Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019 kazi zilizofanyika ni pamoja na: Serikali kuanza majadiliano ya ufadhili na Serikali ya China kwa ajili ya kutekeleza mradi; pamoja na Mtaalam Mshauri kuanza kukamilisha kazi hizo. Ujenzi wa mradi unakadiriwa kugharimu Dola za Marekani milioni 407.40 sawa na takriban Shilingi bilioni 943.7, pia ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa kV 400 unakadiriwa kugharimu Dola za Marekani milioni 53.2 sawa na takriban Shilingi bilioni 123.23.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2019/2020 kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kukamilisha taratibu za ufadhili, lakini pia kuhuisha Upembuzi Yakinifu, kumpata Mtaalam Mshauri na kusimamia mradi, pamoja na kumpata Mkandarasi. Jumla ya fedha zitakazotumika ni bilioni 12.50,

fedha hizi zimetengwa katika mwaka 2019/2020. Mradi huu utaanza kutekelezwa mwezi Mei, 2020 na kukamilika mwezi Aprili, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Rumakali. Mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme MW 222 kwa kutumia maji ya Mto Rumakali mkoani Njombe, pia utahusu njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita 150 kutoka katika mitambo ya kupoza umeme. Gharama za mradi huu itakuwa ni pamoja Dola za Marekani milioni 344.22 sawa na takriban Shilingi bilioni 899.27. Katika kipindi cha mwaka 2018/2019 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kumtafuta Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kuhuisha Upembuzi Yakinifu na mradi unafadhiliwa na Serikali ya Tanzania pamoja na hisani ya Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2019/2020 kazi zitakazofanyika ni kuhuisha Upembuzi Yakinifu; kumpata Mtaalam Mshauri, lakini pia kumpata Mkandarasi na kuanza shughuli za ujenzi. Jumla ya mradi ni Shilingi bilioni 3.5 zimetengwa katika mwaka 2019/2020 ili kutekeleza kazi hizo. Ujenzi wa mradi unatarajiwa kuanza mwezi Januari, 2021 na kukamilika mwezi Juni, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Kakono – MW 87. Mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 87 kwa kutumia maji ya Mto Kagera na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 220 kutoka Kakono hadi Kyaka yenye urefu wa kilomita 38.8. Gharama za ujenzi wa mradi ni Dola za Marekani milioni 380 zitakazotolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika, Shirika la Maendeleo la Ufaransa, na Shirika la Maendeleo la Norway, pamoja na Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2019/2020 kazi zitakazofanyika ni kutwaa ardhi na kulipa fidia katika eneo la mradi, lakini pia kutafuta Wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mradi na njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV 220. Jumla ya Shilingi bilioni 2.5 zimetengwa katika mwaka

2019/2020 ili kutekeleza mradi huu. Mradi unatarajiwa kuanza mwezi Desemba, 2019 na kukamilika mwezi Desemba, 2022. Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Maji wa Malagarasi – MW 45, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 45 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Malagarasi mkoani Kigoma na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 132 kutoka Malagarasi hadi Kidahwe mkoani Kigoma na hii ni umbali wa takribani kilomita 53. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za utekelezaji wa Mradi huu ni Dola za Marekani milioni 150 sawa na takriban Shilingi bilioni 346.3. Katika kipindi cha mwaka 2018/2019 kazi zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha Upembuzi Yakinifu kwa ajili ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 132; usanifu, lakini pamoja na upimaji na uthamini wa maeneo ya kulipa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2019/2020 kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kutwaa ardhi na kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; kumpata Mtaalam Mshauri na Wakandarasi kwa ajili ya kuanza shughuli za ujenzi. Jumla ya Shilingi bilioni tatu zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza mradi huu. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2020 na kukamilika mwezi Septemba, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Asilia wa Kinyerezi II – MW 240. Ujenzi wa mradi huu ulianza mwezi Machi, 2016 kwa gharama ya Dola za Marekani sawa na takriban Shilingi bilioni 794.12. Mradi huu ulihusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 240 kwa kutumia gesi asilia katika eneo la Kinyerezi Jijini Dar es Salaam. Kituo hiki chenye jumla ya mitambo nane (8), mitambo sita (6) ni ya kutumia gesi asilia na mitambo miwili (2) ni ya kutumia mvuke *(steam turbines).* Kukamilika kwa kituo hiki kimeongeza jumla ya MW 248.22 katika Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi *I Extension – MW* 185. Mradi huu ambao upo katika hatua za mwisho za utekelezaji

wake, mradi huu utaanza kukamilika mwaka 2019 mwezi Agosti na utatoa takribani MW 188 ambapo pia utajumuisha na MW 250 na kufikia MW 338. Mradi huu unagharamiwa na Serikali kwa asilimia 100 kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 188 sawa na takriban Shilingi bilioni 435.48.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/19 kazi zilizofanyika ni pamoja na: kukamilika kwa utengenezwaji wa mitambo minne (4) na kuanza kufungwa kwa eneo la mradi; kukamilika kwa upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kinyerezi kV 220 na kuendelea na upanuzi *(upgrade)* wa njia ya msongo wa kV 132 kutoka Kinyerezi I hadi Gongo la Mboto. Ujenzi wa mradi huu ulianza mwezi Juni, 2016 na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka 2019/2020 kazi zitakazotekelezwa ni kukamilisha ufunguzi wa mitambo na kuingia jumla ya MW 185 katika Gridi ya Taifa, katika mwaka 2019/2020 jumla ya shilingi bilioni 60 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Mtwara MW 300. Mradi huu unahusu ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia katika Mkoa wa Mtwara. Gharama za mradi zinakadiliwa kuwa dola za Marekani milioni 360 sawa na takribani shilingi bilioni 833.90. Mradi huu pia utahusu kujenga njia ya kusafirisha umeme kV 400 kutoka Mtwara hadi Somanga Fungu umbali wa kilometa 253. Mradi huu utatekelezwa kwa ufadhili wa Serikali ya Japani kupitia Shirika lake la Maendeleo *JICA* kwa kushirikiana na Serikai. Kazi zilizofanyika katika mwaka 2018/2019 ni pamoja na kukamilika kwa upembuzi yakinifu yaani *feasibility study* kwa kituo cha kuzalisha umeme na miundombinu wezeshi ikiwemo barabara pamoja na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2019/2020 kazi zitakazofanyika ni pamoja kukamilisha uthamini wa kulipa fidia kwa wananchi wanaopisha mradi pia kumpata Mkandarasi na Mshauri wa mradi. Jumla ya shilingi bilioni 4.2

zimetengwa katika mwaka 2019/2020 kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Machi, 2020 na kukamilika mwezi Septemba, 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kufua Umeme utokanao na Jua, yaani MW 150, pia upepo wa MW 200 na Makaa ya Mawe MW 600. Mwezi Septemba mwaka 2018 Serikali kupitia *TANESCO* ilitangaza miradi ya nishati jadidifu yaani jua yenye MW 150, upepo MW 200, na Makaa ya Mawe MW 600 kwa ajili ya kuutekeleza. Lengo ni kupata miradi ya kuzalisha umeme wa jumla ya MW 950 kwa masharti nafuu kwa njia ya ushindani na kuingizwa katika Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2019/2020 *TANESCO* itakamilisha taratibu za kuwapata wawekezaji binafsi wenye bei nafuu na kuanza utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Kusafirisha Umeme, mradi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 kutoka Singida, Arusha hadi Namanga. Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 400 yenye urefu wa kilometa 414 kutoka Singida hadi Namanga kupitia Arusha. Mradi huu pia unahusisha ujenzi wa kituo kipya cha kupoza umeme katika eneo la Kisongo Mkoani Arusha, upanuzi wa Kituo cha kupoza umeme yaani *addition bay* cha Singida na usamabazaji umeme katika Vijiji 22 vinavyopitiwa na mradi huu. Gharama ya mradi huu ni dola za Marekani milioni 258.82 sawa na takribani shilingi bilioni 599 .53. Kazi zilizofanyika kwa mwaka 2018/2019 ni kulipa fidia pamoja na kuanza shughuli za ujenzi wa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zilizopangwa kufanyika mwaka 2019/2020 ni kuendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo vya kupoza umeme. Aidha, utekelezaji wa mradi huu ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa *Backbone* Awamu ya II unaohusu kuongeza uwezo wa vituo vya kupoza umeme kutoka kV 220 mpaka kV 400 katika Mikoa ya Iringa, Shinyanga, Singida na Dodoma. Utekelezaji wa mradi huu

ulianza mwezi Machi 2017 na unatarajiwa kukamilika mwezi Machi 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 kutoka Makambako hadi Songea. Mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 220 kutoka Makambako hadi Songea kupitia Madaba pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Madaba na Songea umekamilika mwezi Mei, 2016, na kimsingi umezinduliwa hivi karibuni na Mhehsimiwa Rais wetu. Gharama ya mradi huu ilikuwa ni shilingi bilioni 216 chini ya ufadhili wa Serikali ya Tanzania na Sweden. Mradi huu ulizinduliwa hivi karibu kama nilivyotaja kwa lengo la kuongeza umeme na kuimarisha miundombinu ya umeme Ukanda wa Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zilizopangwa kufanyika mwaka 2019/2020 ni kuendelea kuunganisha wateja ikiwemo Vijiji vya Lutikila, Ifinga pamoja na Mbangamawe Mkoani Ruvuma vilivyoongezeka katika mradi huu kwa ajili ya kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 Iringa, Mbeya, Tunduma, Sumbawanga, Mpanda hadi Kigoma, na Nyakanazi yaani *North*, *West* Gridi. Mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya ksuafirisha wa kV 400 kutoka Mbeya, Iringa, Tunduma, Sumbawanga, Mpanda, Kigoma hadi Nyakanazi yenye urefu wa kilometa 1384. Mradi huu unatekelezwa kwa Awamu III kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa Msongo wa kV 400 kutoka Iringa hadi Mbeya na Sumbawanga. Awamu hii inahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 400 kutoka Iringa kupitia Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga yenye urefu wa kilometa 624. Kazi zilizofanyika kwa mwaka 2018/2019 ni pamoja na kukamilisha taarifa ya awali ya upembuzi yakinifu kati ya Mbeya na Sumbawanga, kuanza kwa udhamini pamoja na mali za wananchi watakaopisha mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zilizopangwa kufanyika mwaka 2019/2020 ni kukamilisha tathimini pamoja na kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha eneo la mradi, kumpata Mtaalam Mshauri pamoja Mkandarasi wa kutekeleza mradi. Mradi utagharimu takribani dola za Marekani milioni 465 sawa na takribani shilingi bilioni 1.08. Awamu ya pili ya mradi ni ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa kV 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma yenye urefu wa kilometa 280, ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Kidawe Mkoani Kigoma yenye upanuzi wa kituo cha kupoza umeme Mnazi Bay pamoja Nyakanazi ambao ni usafirishaji wa kilometa za urefu 440. Mradi huu utasaidia sana katika kuongeza umeme katika maeneo ya Kigoma pamoja na Katavi. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2021 na kukamilika mwezi Juni 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Njia ya Kusafirisha umeme wa Msongo wa kV Rufiji, Chalinze Dodoma. Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 400 yenye urefu wa kilometa 512 kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha Rufiji hadi Dodoma kupitia Chalinze Mkoani Pwani. Mradi huu pia unahusisha upanuzi wa vituo vya kupoza umeme katika Mji wa Chalinze na Jiji la Dodoma pamoja na kusambaza umeme katika Vijiji 37 vitakavyopitiwa na mradi. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa dola za Marekani milioni 276.36 sawa na takribani shilingi bilioni 640.08.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zilizopangwa kwa mwaka 2019/2020 ni kukamilisha upembuzi yakinifu, kufanya uthamini wa mali za wananchi watakaopisha mradi na jumla ya shilingi bilioni 11 zimetengwa kwa mwaka 2019/2020. Mradi huu unatarajiwa kuanzia mwezi Machi 2020 na kukamilika mwezi Desemba mwaka 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Njia Kusafirisha Umeme wa Msongo wa kV 400 kutoka Kinyerezi hadi Chalinze. Mradi huu utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 400 yenye urefu wa kilometa 115 kutoka Kinyerezi Mkoani Dar es Salaam hadi Chalinze Mkoani Pwani pamoja na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme. Katika kipindi cha mwaka 2018/2019 kazi zilizofanyika ni pamoja na

kukamisha taratibu za kulipa fidia kwa wananchi wanaopisha mradi pamoja na kuanza taratibu za kumpata mtaalam Mshauri na Mkandarasi. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa dola za Marekani milioni 120 sawa na takribani shilingi bilioni 282.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zilizopangwa kwa mwaka 2019/2020 ni kukamilisha upembuzi yakinifu, kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi na jumla ya shilingi bilioni 15 zimetengwa katika mwaka 2019/2020 ili kutekeleza kazi hizi. Mradi huu unatarajiwa kuanzia mwezi Julai 2020 na kukamilika mwezi Desemba mwaka 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Njia ya Kusafirisha wa Msongo wa kV 132 kutoka Tabora, Kidahwe, Mkoani Kigoma, pia kutoka Tabora Nsimbo hadi Katavi. Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa kV 132 yenye urefu wa kilometa 391 kutoka Tabora hadi Kidawe Mkoani Kigoma kupitia Urambo, Kaliua, Nanguruka na vituo vyake vya kupoza umeme pamoja na ujenzi wa kusafirisha umeme wa msongo wa kV 132 ya umbali wa kilometa 581 kutoka Tabora hadi Nsimbo Mkoani Katavi. Mradi huu unapitia pia Ipole na Inyunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zilizofanyika kwa mwaka 2018/2019 ni pamoja na kukamilisha upembuzi yakinifu kuainisha mipaka Namkuza utakaopita mradi na upatikanaji wa eneo. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa dola za Marekani milioni 92 sawa na takribani shilingi bilioni 213.11.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zilizopangwa kwa mwaka 2019/2020 ni kufanya tathimini ya athari za mazingira, kufanya uthamini wa mali za wananchi watakaopisha mradi kulipa fidia na kuanza utekelezaji wa mradi. Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kuboresha Mfumo wa Usambazaji Umeme katika Jiji la Dodoma. Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 220 kutoka Zuzu hadi Msalato na kutoka Zuzu hadi Kikombo

pamoja na ujenzi wa vituo viwili vya kupoza umeme katika maeneo ya Msalato na Kikombo Mkoani Dodoma. Gharama ya mradi ni dola za Marekani milioni 167.7 sawa na takribani shilingi bilioni 388.46. Kazi zilizofanyika mwaka 2018/19 ni pamoja na kukamilisha upembuzi yakinifu kwa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 220 njia ya kusambaza umeme wa msongo wa kV 33, vituo vya kupoza umeme vya Haneti na Narco pamoja na kuendelea na taratibu za kumpata mfadhili kutoka Serikali ya Japani. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Juni mwaka 2020 na kukamilika mwaka 2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi hizo za ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme katika Jiji la Dodoma Serikali pia imedhamilia kuufanya Mji Mpya wa Serikali kuwa Mji wa Kisasa na wa Kimataifa; katika hatua hiyo Serikali kupitia *TANESCO* inadhamilia kusambaza umeme katika Mji huo kwa kutumia nyaya za chini yaani (*underground cable)*. Gharama ya mradi huo zinakadoriwa kuwa jumla ya shilingi bilioni 16.9. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijiji *REA* awamu ya III. Mradi wa kusambaza umeme Vijiji kwa Awamu ya III kupitia Wakala wa umeme Vijijini *REA* unaendelea. Mradi huu unalenga kufikisha umeme katia Vijiji ambavyo hadi kufikia Desemba mwaka 2015 vilikuwa havijafikiwa na umeme na miundombinu yoyote. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2016 hadi kufikia mwezi Mei 2019 jumla ya Vijiji vipya vilivyoongezeka kuunganishwa umeme ni kupitia mradi huu ambao vimefikia 5,109 zaidi ya Vijiji 2,018 vilivyokuwa vimefikiwa mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Vijiji vilivyopelekewa umeme vimefikia 7,127 vilivyounganishwa umeme badala ya 2,118. Mzunguko wa kwanza wa mradi huu unaendelea utakapokamilika mwezi Juni 2020 jumla ya Vijiji 10,278 vitakuwa vimeunganishiwa umeme kati ya Vijiji 12,268 sawa na asilimia 84 ya Vijiji vyote vya Tanzania Bara. Vijiji 1,999 vilivyobaki sawa na asilimia 16 vitaanza kupelekewa umeme

kuanzia mwezi Julai mwaka 2019 na kukamilika ifikapo mwezi Juni mwaka 2021. Na hivyo kuifanya Tanzania kufikia miundombinu ya Vijijini katika maeneo yote kwa asilimia 100. Aidha hadi sasa jumla ya Taasisi za Elimu 3,165 maeneo ya biashara 3,451 pampu za maji 210, Taaisi za Afya 1,211na nyumba za ibada 984 zimefikishiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta Ndogo ya Nishati Jadidifu, Serikali katika mwaka 2018/2019 imeendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya nishati jadidifu ambayo ni pamoja na nishati inayotokana na nguvu ya jua, upepo na maporomoko madogo ya maji. Aidha, Serikali inaendelea kuhamisha matumizi ya nishati yatokanayo na nguvu ya *solar* yaani *(solar home system),* katika nyumba za Taasisi na maeneo ya makazi. Kupitia mfumo huu matumizi ya nishati ya jua iliongezeka kwa jumla ya MW 10 na hivyo kufanya matumizi ya nishati hivyo kufikia hadi sasa MW 26.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uendelezaji wa Rasilimali za Jotoardhi, katika kutimiza azma ya nchi yetu kuwa na usalama wa nishati kwa kuzalisha umeme wa kutosha Serikali pia inaendelea na kutumia vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupata MW 200 zitokanazo na Jotoardhi ifikapo mwaka 2025. Pamoja na uzalishaji wa umeme rasilimali ya Jotoardhi ina manufaa mengine mengi kupitia mchango wake katika maendeleo ya sekta nyingine za kiuchumi, manufaa mengine ni pamoja na ufugaji wa samaki, mabwawa ya maji, na moto pamoja kuogelea, uchakataji wa bidhaa za viwandani na hivyo kuboresha pato na kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta Ndogo ya Mafuta na Gesi Asilia, hadi kufikia mwezi Mei 2019 jumla ya futi za ujazo triioni 57.54 za gesi asilia zimegunduliwa hapa nchini. Katika kipindi cha mwaka 2018/2019 shughuli za utafutaji, uendelezaji, na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia zimeendelea kutekelezwa na Shirika la Maendeleo la Petroli *TPDC* kwa kushirikiana na Kampuni za Kimataifa za mafuta *(IOCs).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa gesi asilia nchini katika vitalu vya Mnazi Bay na Songosongo umeongezeka hadi kufikia fupi za ujazo milioni 190 kwa siku sawa kwa mwaka na hivyo kuongzeka kutoka futi za ujazo 175 kwa siku kwa mwaka 2017/2018. Hili ni sawa na ongezeko la asilimia 8.6. Ongezeko hili la uzalishaji wa gesi asilia limetokana na ongezeko la mahitaji katika matumizi ya viwandani, majumbani na kuzalisha umeme. Gesi asilia inachangia takribani asilimia 60 ya umeme unaozalishwa hapa nchini. Mahitaji ya gesi asilia katika kuzalisha umeme umeendelea kuongezeka ambapo imefikia futi za ujazo bilioni 50.53 kwa mwaka 2018 na kutoka futi za ujazo bilioni 42.79 kwa mwaka 2017, hii ni sawa na ongezeko la asilimia 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia katika Vitalu vya Kimkakati, utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia kupitia *TPDC* unaendelea kwa kutoa kipaumbele katika vitalu vya Eyasi-Wembere, 4/1B, Mnazi Bay pamoja na Songosongo Magharibi. Aidha, Serikali inaemdelea kukamilisha maandalizi ya mkakati pamoja na Mkataba Kifani kwa ajili ya uboreshaji wa shughuli za utafiti. Vitalu hivyo ni pamoja kitalu cha Eyasi-Wambere uchorongaji wa kisima cha kitalu cha Mnasi Bay Kaskazini, uchukuaji wa *data* za mitetemo katika vitalu vya 4/1B, na Mnazi Bay Kaskazini na kitalu cha Songosongo Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Kusafirisha na Kusambaza Gesi Asilia Nchini, Serikali imeendelea na ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza gesi asilia pamoja na kuhakikisha kuwa gesi hiyo inatumika kwa matumizi mbalimbali yakiwemo viwandani, majumbani na katika magari na hata katika kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi hiyo ni pamoja na moja mradi wa kusambaza gesi asilia viwandani, moja mradi wa kusambaza gesi asilia viwandani, katika mwaka 2018/2019 *TPDC* imekamilisha ujenzi wa miundombinu ya kusambaza gesi asilia katika kiwanda cha Dangote Awamu ya II, viwanda vingine ni Lodhia, Cocacola, kiwanda cha vifungashio, kina

chomilikiwa na Goodwill Ceramic Tanzania na kazi ya kuunganisha kiwanda cha Knauf ambayo imefikia asilimia 80. Aidha, *TPDC* imekamilisha majadiliano na mauziano ya gesi asilia kwa kiwanda cha *Shreeji Silcates*. *TPDC* inatarajia kujenga *trunk-line* kutoka Mwenge hadi Tegeta kwa kuunganisha wateja mbalimbali wakiwemo *Estim Constraction*, pamoja na wadau wengine. Jumla ya shilingi bilioni 11.22 zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kusambaza Gesi Asilia Majumbani pamoja na kwenye magari, Serikali kupitia *TPDC* inaendelea kusambaza gesi asilia kwa wateja wa majumbani walio karibu na miundombinu iliyo katika Mkoa wa Dar es Salaam. Mradi wa kunganisha wateja wa majumbani ni endelevu kupitia *GASCO,* na kampuni tanzu ya *TPDC*. Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwaka 2018/2019, katika mwaka 2019/2020 Serikali kupitia *TPDC* imepanga kuunganisha wateja wa awali zaidi ya nyumba 1,000 katika Jiji la Dar es Salam na nyumba zaidi 300 Mkoani Mtwara. Maeneo yanayopelekwa kwa sasa ni pamoja na kuanzia Ubungo Maziwa, Shekilango, Mwenge, Survey, Mlalakua, Nyanganyikeni Makongo juu, Mikocheni na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mengine shughuli zilizopangwa kufanyika ni pamoja na kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kufanya tathimini ya athari za mazingira. Maeneo mengine ambayo yatakayopelekewa gesi ni pamoja na Kilwa *Road*, Mandela pamoja na maeneo mengine ya Kurasini. Kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya gesi asilia majumbani *TPDC* itaongeza kasi ya kusambaza gesi asilia katika maeneo mbalimbali nchini ili watanzania wote waanze kutumia rasilimali ya gesi majumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia *LNG*, Serikali kupitia *TPDC* imeendelea na maandilizi ya ujenzi wa mitambo ya mkakati ya kusindika gesi asilia iliyoko kina kirefu katika bahari ya kitalu namba moja, namba mbili na namba nne. Mitambo hiyo kwa ujumla itakuwa na uwezo wa kusindika tani milioni 10 za gesi asilia

kwa mwaka pamoja na gesi itayosindikwa kusafirishwa nje kipaumbele ni kupatikana kwa gesi ya kutosha kwa ajili ya matumizi ya hapa ndani. Ili kuhakikisha mradi unatekelezwa kwa maslahi mapana ya Taifa *GNT i*naendelea na majadiliano na wawekezaji ambayo yameanza mwezi Aprili mwaka 2019 na yanatarajiwa kukamilika ndani ya miezi saba ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zitakazotekelezwa mwaka 2018/2019 ni kukamilisha tathimini ya athari za mazingira pamoja na kukamilisha mpango wa wananchi watakaopisha ardhi kwa ajili ya kufidiwa. Jumla ya fedha shilingi bilioni 6.7 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu, gharama za mradi ni dola za Marekani bilioni 30 sawa na takribani shilingi trilioni 69.49 kwa fedha za kitanzania, Mradi unatarajiwa kuanza mwaka 2022 na kukamilika mwaka 2028.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi Kutoka Uganda Tanzania, mradi huu unahusu ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Kabaale Nchini Uganda hadi Mkoani Tanga Tanzania gharama za mradi zinakadiliwa kuwa dola za Marekani bilioni 3.5 ambazo ni takribani shilingi trilioni 8.1 za Tanzania. Katika mwaka 2018/2019 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuendelea na majadiliano na mkataba yaani *HGA,* kuendelea na maandalizi ya majadiliano ya mkataba wa mawasiliano pamoja *Share Agreement* ambayo inategemea kukamilika mwezi Juni mwka 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yanayofanyiwa kazi kwa sasa ni pamoja na fidia pamoja na kipaumbele cha kupata eneo kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Mradi huu unatarajiwa kuleta manufaaa makubwa nchini ikiwemo kuongeza mapato ya Serikali kutokana na gawio la uwekezaji katika mradi wa *TPDC* na kodi mbalibali, kuongeza ajira kwa watanzania, pia kutoa fursa kwa watanzania kutoa huduma katika miradi itakayoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mikoa minane itakayotekelezwa Mikoa ambayo inahusika na utekelezaji wa

bomba hili ni pamoja na Mkoa wa Kagera, Mkoa wa Geita, Mkoa wa Tabora, Mkoa wa Shinyanga, Mkoa wa Manyara, Singida, Dodoma na Tanga. Mwaka 2019/2020 kazi iliyopangwa kutekelezwa ni kukamilisha majadiliano na mkataba yaani *SAG* pamoja na wadhamini wa nchi watakaofadhili mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama ambazo zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza mwaka huu kwa mwaka 2019/2020 Serikali imetenga shilingi bilioni 7 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu na mradi utaanza kutekelezwa kwa awamu kama ambavyo nimeeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Udhibiti wa Shughuli za Mkondo wa Juu, Mafuta na Gesi Asilia. Katika Mwaka 2018/ 2019 Serikali kupitia *PURA* imeendelea na udhibiti wa shughuli za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia hapa nchini. Jumla ya vitalu 11 kupitia mikataba ya uzalishaji na ugawanyaji mapato imefanyiwa mapitio na hili zoezi la kufanya mapitio linaloendelea. Mikataba hiyo ilisainiwa katika miaka ya 2001 hadi 2012 kabla ya Sheria ya Petroli ya mwaka 2015. Aidha, Sheria ya *Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act, 2017* pamoja na sheria ya *The Natural Wealth and Resources Contracts (Review and Re-negotiation of Unconscionable Terms) Act, 2017* zinahitaji mikataba hiyo ifanyiwe mapitio upya zoezi ambalo linaendelea hivi sasa. Kazi za kudurusu mikataba hiyo inaendelea kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Upatikanaji wa Mafuta Nchini. Hali ya upatikanaji wa mafuta nchini imeendelea kuimarika. Serikali kupitia Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja inaendelea kuagiza na kupokea mafuta ya kutosha wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya Mwezi Januari hadi Desemba Mwaka 2018 jumla ya lita bilioni 5.70 za mafuta ziliingizwa kupitia Bandari ya Dar es salaam, Tanga na Mtwara, sawa na ongezko la asilimia 6.3 ikilinganishwa na lita za mafuta bilioni 5.36 zilizouzwa kwa Mwaka 2017. Kati ya kiasi

hicho, lita bilioni 3.27 sawa na asilimia 5.7 ya mafuta yote yaliyoingizwa nchini yalikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya ndani, ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 2.5 ikilinganishwa na lita bilioni 3.19 zilizoingizwa katika Mwaka 2017. Kwa upande mwingine, lita bilioni 2.43 sawa na asilimia 42.6 ya mafuta yote yaliyoingizwa yalikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya nchi jirani *(on transit)* ambayo ni saw ana ongezko la asilimia 12 ikilinganishwa na mafuta ya *on transit* ya Mwaka 2017. Kiasi cha mafuta ya *Diesel* yaliyoingizwa kwa Mwaka 2017 ni asilimia 1.3 ya wakati wa mafuta ambayo yaliingizwa Mwaka 2018 yalikuwa asilimia 11.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia Mwezi Julai, 2018 Bandari ya Mtwara ilianza kupokea mafuta kwa ajili ya matumizi ya ndani sambamba na Bandari ya Dar es salaam na Tanga. Kuanza kutumika tena kwa Bandari hii kupokea mafuta kumeleta manufaa makubwa na unafuu wa bei ya upatikanaji wa mafuta katika Mikoa ya Lindi na Mtwara na hata Ruvuma. Unafuu huu wa bei umetokana na kuondolewa kabisa kwa gharama za usafirishaji kutoka Dar es salaam kwenda mikoa hiyo. Mathalani, kwa Mkoa wa Mtwara takribani shilingi 72 kwa lita zilizokuwa zinatumika kusafirisha mafuta kutoka Dar es salaam hadi Mtwara sasa zimeondolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ajira na Maendeleo ya Rasilimali Watu. Ili kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi baada ya kugawanywa kwa iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ya Nishati iliandaa na kutekeleza muundo wake ambao umeidhinishwa mwezi Juni, 2018. Ili kuongeza tija na motisha kwa wananchi katika Mwaka 2018/2019 Wizara iliwapandishwa vyeo watumishi 41 na kubadilisha kada watumishi watatu, watumishi 18 walipata fursa ya ufadhili wa masomo kutoka Serikali ya Jamhuri ya China. Aidha, Watanzania wengine 22 wanatarajiwa kwenda masomoni kupitia ufadhili wa Serikali ya China mwaka 2019/ 2020. Katika mwaka 2019/2020 Wizara inatarajia kubadilisha kada za watumishi wanne, kujaza nafasi 13 za uongozi na kuwapandisha vyeo watumishi 48.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa. Serikali kupitia Wizara ya Nishati inapenda kuwashukuru washirika wa maendeleo na nchi wahisani ambao wameendelea kutoa michango yao katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara. Kwa niaba ya Serikali napenda kutambua mchango wa Taasisi na mamlaka zifuatazo:-

(i)Benki ya Maendeleo ya Afrika;

(ii)Benki ya Dunia;

(iii)Benki ya Ushirikiano wa Kimataifa;

(iv)United Bank of Afrika;

(v)Economic Development (CDF);

(vi)Mfuko wa uendelezaji jotoardhi; pamoja na

(vii)Taasisi za Mashirika pamoja na JICA.

Aidha, napenda kushukuru pia Umoja wa Mataifa pamoja na Mashirika mengine ya Canada pamoja na Marekani. Aidha, natoa shukurani kwa Serikali za Uganda, Burundi, Canada, China, Finland, Iceland, Japan, Sweden, Ufaransa, Ujerumani, Norway, Korea ya Kusini, Misri, Rwanda na Zambia kwa ushirikiano katika kuendeleza sekta za nishati. Vilevile naishukuru Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) kwa ushirikiano katika masuala ya kikanda yanayohusu sekta hii. Kwa kipindi cha Mwaka 2019/2020, Wizara itaendelea kushirikiana kwa karibu na washirika hawa kwa maendeleo na mengine kutekeleza kwa ajili ya miradi iliyopangwa kwa ushirikiano na nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shukurani. Naomba kutumia fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu (Mb) kwa kunisaidia kwa kiasi kikubwa na kwa dhati kabisa katika kutekeleza

majukumu yangu. Aidha, napenda kumshukuru Katibu Mkuu, Dkt. Khamis Hassan Mwinyimvua kwa uchapakazi mahiri na ushirikiano anaonipa katika kutekeleza shughuli za Kiserikali za kila siku. Vilevile nawashukuru Makamishina, Wakuu wa Idara wa vitengo, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi za Taasisi za Wizara yetu, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara yetu, watumishi wote kwa ujumla kwa ushirikiano wao na juhudi zao wanazofanya kwa ajili ya kufanikisha maendeleo katika sekta ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Chato kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo ya jimbo. Nawaahidi kuwa sitawaangusha na nitaendelea kushirikiana nanyi katika kubuni mikakati mbalimbali ya kuendeleza shughuli za Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu tena nirudie hili. Kipekee napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Wananchi wangu wa Jimbo la Chato kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo ya jimbo. Nawaahidi kuwa sitawaangusha na nitaendelea kushirikiana nanyi katika kubuni mikakati mbalimbali ya shughuli za maendeleo ya jimbo. Naishukuru sana familia yangu ikiongozwa na mke wangu, Mama Vaileth Kalemani pamoja na watoto wangu kwa kuendelea kuniombea na kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu ya Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwisho. Bajeti ya mwaka 2019/2020 inalenga kutekeleza dhaira ya Serikali ya kuhakikisha kuwa inazalisha umeme wa kutosha, wa uhakika, unaotabirika na wenye gharama nafuu. Vilevile bajeti imelenga kuimarisha shughuli za utafutaji na biashara ya mafuta na gesi asilia kwa kuwezesha wananchi kunufaika na raslimali hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2019/2020 Wizara ya Nishati inakadiria kutumia jumla ya shilingi trilioni 2.142 ikilinganisha na shilingi trilioni 1.692 iliyotengwa Mwaka

2018/2019. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 26.6. Fedha nyingine za ndani ni pamoja na miradi ya mendeleo ambayo imetengewa kwa Mwaka 2019/2020 katika awamu tatu:-

(i) Shilingi Triliaoni 1.86 ambayo ni sawa na asilimia 95.1 ya bajeti yote ya ndani. Miradi hiyo ni miradi ya kuzalisha umeme katika Mto Rufiji Megawatts 2115 ambayo ni shilingi Trilioni 1.443.

(ii) Mradi kabambe za kusambaza umeme vijijini Awamu ya tatu, shilingi bilioni 363.11

(iii) Mradi wa kuzalisha umeme wa *Kinyerezi (I) extension magawatts* 185, shilingi bilioni 60.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa liidhinishe bajeti ya jumla ya shilingi trilioni 2,142,790,320,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Shilingi trilioni mbili bilioni mia moja kumi na sita elfu, milioni mia nne hamsini na nne elfu sawa na asilimia 98.8 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo za maendeleo, shilingi Trilioni 1,956,372,000,000 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 160,082,000,000 ni fedha za nje.

(ii) Shilingi bilioni 26,339,309,000 sawa na asilimia 1.2 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hiz, shilingi bilioni 15,025,821,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)*, na shilingi bilioni 11,313,880,000 kwa ajili ya mishahara *(PE)* kwa watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nitoe shukurani zangu za dhati kwako wewe, Wenyeviti wa Kamati za Bunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwa jinsi ambavyo tunashirikiana katika kutekeleza shughuli za Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati, hoja imeungwa mkono. Sasa namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini ili aweze kuwasilisha hoja yake. Mhehsimiwa Dustan Kitandula, Mwenyekiti karibu.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA – MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma ambaye ametuwezesha kuwa salama na tunawatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni, Kamati ilifanya kazi kuu mbili ambazo ni:-

(i) Kutembelea na Kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa Fedha kwa mwaka wa Fedha 2018/2019.

(ii) Lakini vilevile kufanya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilifanya ziara ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa chini ya Wizara ya Nishati, Fungu 58 katika Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka 2018/2019 na ikakagua kama ifuatavyo:-

(i) Mradi wa Kuzalisha Umeme katika Mto Rufiji;

(ii) Mradi wa Makambako-Songea ambao unatengeneza njia kuu ya Msongo wa Kilovolt 220; na

(iii) Mradi ya umeme Vijijini REA katika Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maelezo na Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 yanapatokana kuanzia ukurasa wa 13 hadi ukurasa wa 18 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta Ndogo ya Gesi Asilia na Hali ya Upatikanaji wa Mafuta; sekta ndogo ya gesi asilia ni sekta muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu kiuchumi. Kwa maeneo ambayo gesi asilia imeshaanza kuvunwa, yaani Mnazi bay, Songosongo na Killiwani, kiasi ambacho kimehakikiwa ni futi za ujazo trilioni 1.96. Hivyo ili nchi yetu iweze kunifaika ipasavyo na sekta hii ni lazima kuwekeza katika taasisi za usimamizi na uendelezaji kiteknolojia, kimtaji na katika rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi za umma zinazosimamia kimakakati sekta hii ndogo ya gesi asilia ni hizi zifuatazo:-

(i) Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu (PURA). Majukumu ya PURA yamebainishwa katika kifungu cha 12 cha Sheria ya Petroli, Sura ya 292; na PURA ni taasisi muhimu katika kudhibiti gharama za uzalishaji katika mkondo wa juu ambazo pia husaidia kudhibiti bei ya soko nchini. Hata hivyo, licha ya majukumu haya makubwa, Kamati imebaini kuwa tangu kuanza kwa PURA mwaka 2017 hadi sasa taasisi hii imekuwa haitengewi bajeti ya kutosha, haina watumishi wa kudumu na wala haina vitendeakazi hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuhakikisha PURA inawezeshwa kuwa na Jengo la Ofisi kwaajili ya kutekeleza majukumu yake ikiwemo utunzaji wa data zitokanazo na utafiti wa gesi asilia badala ya kutumia hifadhi ya majengo ya taasisi nyingine. Kuendelea kuacha utunzaji

wa data ufanyike na taasisi nyingine isiyo na wajibu kisheria ni hatari kwa usalama wa data hizo.

(ii) Kampuni ya Taifa ya Mafuta; Kifungu cha 8 cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392, kinatambua Shirika la Taifa la Maendeleo ya Petroli *(TPDC)* kama Kampuni ya Taifa ya Mafuta. Kifungu cha 9 cha Sheria hii kinaainisha majukumu ya *TPDC* ambayo ni pamoja na kushiriki kimkakati kwenye mnyororo wa utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa biashara ya mafuta na gesi asilia nchini, kusimamia Hisa za Serikali na kumiliki miundombinu ya kimkakati kwenye mnyororo wa mafuta na gesi asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti; uwezo wa *TPDC* kushiriki kwenye ukusanyaji wa mapato umeainishwa vyema katika Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015 lakini umeminywa sana kupitia Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi ya mwaka 2015.

Aidha, kifungu cha 17 cha Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi ya mwaka 2015, kimeainisha matumizi ya mfumo wa mapato ya taifa katika kukokotoa fedha za Mfuko wa Mapato ya Mafuta na Gesi, kwamba ili mapato husika yapelekwe kwenye Mfuko wa Akiba wa Mafuta na Gesi sharti makusanyo hayo kwa mwaka husika yawe yamefikia asilimia tatu ya Pato la Taifa na ziada ndiyo itakayohamishiwa katika mfuko wa akiba. Hivyo ili *TPDC* apate fedha kutoka mfuko huo ni lazima mapato ya gesi yafikie asilimia tatu ya *GDP.*

Kutokana na utaratibu huo ni wazi kuwa unaweka ugumu wa *TPDC* kuweza kupata fedha za kuwekeza katika miradi ya maendeleo. Mathalani, *TPDC* ina kasi ndogo ya kutekeleza mradi wa usambazaji gesi majumbani katika Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Mtwara kwa sababu ya kutokuwa na fedha za kutosha za kujenga miundombinu. Kamati inaishauri Serikali kufanya maamuzi ya kimkakati yatakayoiwezesha *TPDC* kupata fedha zitakazoiwezesha kushiriki kikamilifu kwenye uwekezaji kwa niaba ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi Madogo ya Gesi Asilia Nchini. Gesi asilia inayozalishwa nchini imekuwa ikitumika kuzalisha umeme viwandani, majumbani na kwenye Magari. Hadi kufikia Disemba 2018, gesi asilia iliyokuwa ikitumika katika uzalishaji umeme viwandani na matumizi mengine kwa Mwaka ni futi za ujazo trilioni 0.63 kati ya futi za ujazo trilioni 1.96 zilizohakikiwa**.** Hii inaonesha kuwa kwa mwaka Gesi inayotumika ni sawa na asilimia 4.14 ya kiasi kilichohakikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufuatiliaji wa Kamati umebaini kwamba sababu mojawapo ya kuwa na matumizi madogo ya gesi asilia nchini ni bei kubwa wanayouziwa watumiaji. Aidha, *TPDC* imekuwa ikiuza gesi kwa bei tofauti kwa wanunuzi wa gesi hasa viwandani. Mathalani Kiwanda cha Goodwill cha Mkuranga kinauziwa gesi kati ya Dola 5.57 hadi Dola 6.64 wakati ambapo kiwanda cha Dangote kimekuwa kikiuziwa kwa Dola za KImarekani 4.2. Licha ya kigezo cha umbali kuchangia katika upangaji wa bei Kamati inaona kuwa mkakati wa kuwa na bei zinazovutia watumiaji wengi kutumia gesi ungewezesha matumizi ya gesi kuongezeka kwa sekta ya uzalishaji na hivyo kupanua wigo wa mapato ya kikodi kwa Serikali kupitia sekta nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya upatikanaji wa umeme; nchi yetu imejiwekea lengo la kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa nchi ya uchumi wa kati unaochochewa na ukuaji wa viwanda ifikapo mwaka 2020/2025. Ili kufikia lengo hili, mchango wa sekta ya nishati una muhimu mkubwa wa kimkakati. Kwa kutambua hilo, Serikali imekusudia kuzalisha umeme wa megawatts 5,000 ifikapo Mwaka 2020 na Megawatts 10,000 ifikapo Mwaka 2020/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2018 hadi sasa, hali ya upatikanaji umeme nchini imeendelea kuimarika. Hali hiyo imetokana na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ya kuhakikisha kuwa miundombinu ya kuzalisha umeme Nchini inaimarishwa ili izalishe umeme kwa kwa wastani wake wa juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya jitihada zinazofanywa katika uzalishaji wa umeme nchini, Taarifa ya Wizara iliyowasilishwa kwenye Kamati inaonesha kuwa, upo uwezekano mkubwa wa kutpofikiwa megawatts 5000 ifikapo mwaka 2020. Taarifa inaonyesha kuwa uwezekano uliopo ni kufikia *megawatts* 2780 na hii itategema tu endapo majadiliano yanayoendelea sasa na wawekezaji binafasi yataweza kukamilika ndani ya mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuendana na kasi ya ujenzi wa uchumi wa viwanda, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha mradi wa kuzalisha umeme kwa Mto Rufiji unapewa fedha za kutosha na kusimamiwa kikamilifu ili ukamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya Miradi ya Umeme Vijijini *(REA)*; tathmini ya utekelezaji wa Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini (REA) mzunguko wa kwanza inaonesha kwamba mikataba ya kutekeleza miradi hii ilisainiwa Juni, 2017, lakini ufunguaji wa *LC* ulichukua takriban miezi 10 baada ya hapo yaani ulifunguliwa mwaka 2018 mwezi Mei. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa hali iliyojitokeza kwenye Mradi wa *REA III*, mzunguko wa kwanza haijirudii wakati wa kuanza utekelezaji wa Mradi wa *REA III* mzunguko wa pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika tathmini ya Wizara iliyofanyika mwaka 2017 mwezi Aprili inaonesha kuwa kati ya kampuni 29 yaliyopewa kandarasi ya kusambaza umeme vijijini ni kampuni 15 tu ndizo ambazo utekelezaji wa mikataba yao upo juu ya malengo yaliyotarajiwa. Aidha, kampuni saba ambazo utekelezaji wa mikataba yao hauridhishi zimeoneshwa kwenye taarifa yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaona ipo haja kwa Serikali kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Kampuni hizo ili kuhakikisha kuwa miradi hii inakamilika kwa wakati na kwa ubora uliokusudiwa kulingana na matakwa ya mikataba. Aidha, endapo jitihada za ufuatiliaji zitashindwa kuzaa matunda yanayotarajiwa, Kamati inaishauri Serikali

kutosita kuzichukulia kampuni hizo husika hatua stahiki na za haraka kulingana na matakwa ya mikataba ya kazi zao. Aidha, ikibidi *TANESCO* iweze kupewa jukumu la kukamilisha miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Uzingatiaji wa Maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2018/2019; Wizara ya Nishati katika mwaka 2018/2019 ilipanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 394.45. Kati ya makusanyo hayo, jumla ya shilingi bilioni 394 zilitarajiwa kukusanywa kupitia shughuli za mafuta na gesi. Mapato haya yanatokana na vyanzo mbalimbali vikiwemo; Shughuli za *TPDC* za utafiti wa mafuta, mauzo ya gesi asilia na mauzo ya nyaraka za zabuni. Hadi kufikia Februari 28, 2019, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya Shilingi bilioni 291.84.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo hayo yalitokana na shughuli za mafuta na gesi asilia nchini zinazoratibiwa na *TPDC*. Makusanyo hayo ni sawa na asilimia 131.7 ya lengo la hadi mwezi Februari, 2019 la makusanyo ya Shilingi bilioni 221.61**.** Ongezeko la kiasi cha makusanyo haya katika kipindi husika yanatokana na malipo ya gawio la faida katika shughuli za mkondo wa juu ikiwemo kampuni ya *Pan African Energy* ambayo imeanza kulipa baada ya kutofanya hivyo kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa usimamizi mzuri wa makusanyo ya maduhuli na hivyo kuvuka malengo ya makusanyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2019, Wizara ya Nishati (Fungu 58) ilikuwa imepokea kutoka Hazina jumla ya shilingi bilioni 345.22. Pamoja na mapokezi hayo, Hazina pia ilitenga jumla ya shilingi bilioni 688.65 ambazo zililipwa kwa Mkandarasi wa Mradi wa kufua umeme katika Mto Rufiji. Malipo haya yalifanyika tarehe 24 Aprili, 2019. Kutolewa kwa fedha hizo kumefanya Wizara kupewa jumla ya Shilingi trilioni 1.03, sawa na asilimia 92.1 ya fedha zote zilizotarajiwa kupokelewa kwa kipindi husika ambazo zilikuwa Shilingi trilioni

1.43. Kati ya Shilingi trilioni 1.5 zilizopokelewa na kutengwa, Shilingi trilioni 1.31 ni fedha za miradi ya maendeleo, sawa na asilimia 92 ya fedha za maendeleo zilizotakiwa kupokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati; katika uchambuzi wa Bajeti ya mwaka 2018/2019 Kamati ilitoa maoni kadhaa na ushauri na mapendekezo. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, sehemu kubwa ya ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa na baadhi bado haujazingatiwa kama ambavyo unaonekana kwenye taarifa yetu kuanzia ukurasa wa 41 hadi 42.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai ya Kamati kuwa Wizara iendelee kuyafanyia kazi maoni na ushauri unaotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2019/2020; katika mwaka 2019/2020, Wizara ya Nishati - Fungu 58 inakadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,142,793,309,000 ikilinganishwa na shilingi 1,692,286.14 zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019, hii ni sawa na ongezeko la asilimia 26.6. Ongezeko hili limetokana na kuanza kutekelezwa kwa miradi mikubwa ya kimkakati ikiwemo mradi wa umeme wa Mto Rufiji utakaozalisha Megawati 2,115 na bajeti ya mradi huu imeongezeka kutoka Sh.700,000,000,000 zilizotengwa mwaka jana hadi kufikia Sh.1,443,264,000,000 hili ni sawa na ongezeko la asilimia 106.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti iliyotengwa kwa mwaka 2019/2020 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ni shilingi 2,111,454,000,000 sawa na asilimia 98.8 ya bajeti yote ya Wizara. Bajeti ya fedha za ndani iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni Sh.1,956,372,000,000. Hii ni sawa na asilimia 92 ya Bajeti yote ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha nyingi za ndani za miradi ya maendeleo zimeelekezwa katika miradi minne ya kimkakati ambapo jumla ya Shilingi trilioni 1.88 sawa na asilimia 95.9 ya Bajeti yote ya ndani iliyotengwa zitatumika.

Miradi hiyo ni Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa maji ya Mto Rufiji, *megawatts* 2,115 (Shilingi trilioni 1.44); Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini, awamu ya tatu (Shilingi bilioni 363.11); Mradi wa kuzalisha Umeme wa Kinyerezi I *Extension megawatts* 185 (Shilingi bilioni 60) na Mradi wa Ruhuji wa *megawatts* 358 (Shilingi bilioni 10).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya Matumizi ya Kawaida; Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyotengwa kwa mwaka 2019/2020 ni shilingi 26,339,309,000 sawa na asilimia 1.2 ya bajeti yote ya Wizara. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 15 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi bilioni 11 zitatumika kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake. Aidha, Makisio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2019/2020, yanatarajiwa kuwa shilingi 602,059,798,000, ambalo ni ongezeko la asilimia 52.6 ikilinganishwa na shilingi 394,450,860,600 lililokuwa lengo la mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati; baada ya Kamati kutekeleza majukumu yake ya kikanuni ambayo ni ukaguzi wa miradi ya maendeleo na uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa fedha 2019/2020, Kamati ina maoni 14 yanayoambatana na ushauri wake kama yanavyoonekana kuanzia ukurasa wa 46 mpaka 52 na hapa nitataja machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni Utoaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo; katika kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati ni muhimu Serikali kuhakikisha kwamba utekelezaji wa miradi hiyo hausimami kwa sababu za ukosefu wa fedha.

Hivyo, Kamati inasisitiza na kuishauri Serikali juu ya umuhimu wa kujipanga kikamilifu na kuhakikisha kuwa inapeleka fedha za ujenzi na uendelezaji wa miradi kwa wakati kama zilivyotengwa na kuidhinishwa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni kasi ya usambazaji wa umeme wa vijijini *(REA).* Kasi ya usambazaji wa umeme ili iongezeke na iendane na matarajio ya wananchi ni lazima fedha ziweze kutengwa kimkakati na hivyo kuwezesha kufikia malengo yake. Kamati inaishauri Serikali kumaliza changamoto zinazosababisha usambazaji wa umeme kusuasua na hatimaye kuongeza kasi na ufanisi katika usambazaji wa umeme ili kuweza kufikia malengo ya miradi ya *REA* na vilevile kamati inaona ipo haja ya wakandarasi kusimamiwa kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni wigo wa utekelezaji wa Miradi ya Umeme Vijijini *(REA)*. Wakandarasi wanaotekeleza miradi ya *REA* wamekuwa wakipewa maeneo madogo wigo mdogo wa kufanyia kazi ambao haulingani na uhalisia kutokana na kutofanyika kwa upembuzi yakinikifu sahihi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia *TANESCO* ifanye upembuzi yakinifu na kwa usahihi kujua ukubwa wa kijiji kabla ya kumkabidhi mkandarasi ili kuepuka kumpa mkandarasi eneo dogo kuliko ukubwa halisi wa kijiji au eneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezeshwaji wa Wakala wa Udhibiti wa Mkondo wa juu wa Petroli *(PURA); PURA* ni taasisi muhimu katika udhibiti wa sekta ya gesi asilia katika mkondo wa juu. Licha ya kwamba taasisi hiyo ina zaidi ya miaka miwili tangu kuanzishwa kwake, lakini hadi sasa haina rasilimali watu wa kutosha katika maeneo muhimu, haina bajeti ya kutosha wala haina hata uwezo wa kuhifadhi takwimu za masuala ya gesi ingawa inasimamia kampuni za kimataifa zenye teknolojia ya hali juu na rasilimali watu wenye weledi mkubwa. Ili nchi iweze kunufaika ipasavyo na gesi ni lazima taasisi hii iweze kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa inaiwezesha Wakala wa Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli *(PURA)* kifedha, kiteknolojia na katika rasilimali watu ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni mfumo wa gawio la mapato yatokanayo na mafuta na gesi asilia; Sheria

ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi ya mwaka 2015, imeweka utaratibu wa mfumo wa *GDP* ili kuweza kuipatia *TPDC* fedha za kuwekeza katika sekta ya gesi. Kamati inaamini kuwa itachukua muda mrefu sana kwa Sekta Ndogo ya Gesi Asilia kuchangia Pato la Taifa kwa asilimia tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuzingatia kifungu cha 16(5) na (6) cha sheria hiyo kinachoelekeza jinsi ya kufanya marekebisho katika sheria hii; Kamati inaona upo umuhimu wa sheria hiyo kuangaliwa upya ili pamoja na mambo mengine ibadili mfumo wa kuigawia *TPDC* fedha za Mfuko wa Gesi Asilia na Mafuta kwa kutegemea uchangiaji wa pato la Taifa kwa asilimia tatu.

Vile vile Serikali inapaswa kuzingatia maoni ya Kamati Maalum ya Bunge kuhusu ushauri wa Kamati kuhusu Sekta Ndogo ya Gesi Asilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya kwamba Sheria ya Petroli, Sura ya 392 ilianza kutumika mwaka 2015 na sasa ni zaidi ya miaka minne na pia Sheria ya Mapato ya Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili ya Nchi kwa mwaka 2017 na Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Umiliki wa Madini ya Maliasili ya mwaka 2017 zimeanza kutumika tangu mwezi Julai. Hadi sasa yapata miaka miwili, Serikali ndio inafanya mapitio ya mikataba hii ili kubaini masharti yenye kasoro katika *PSA* hizo ili kuendana na masharti na matakwa ya sheria hizo.

Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mapitio ya mikataba hiyo. Aidha, ni rai ya Kamati kuwa Serikali iendelee kutekeleza maoni na ushauri uliopendekezwa na Kamati Maalum ya Bunge iliyoundwa na Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, naomba nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Spika,

Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge, kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge hili Tukufu. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza wajibu huu mkubwa tuliowakabidhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa Waziri wa Nishati Mheshimiwa Dkt Medard Matogolo Kalemani; Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Hamisi Mwinyimvua kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati yetu wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa weledi na umahiri waliouonesha wakati wote wa kutekeleza majukumu ya Kamati. Kwa heshima kubwa naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athuman Hussein; Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Michael Chikokoto; Makatibu wa Kamati Ndugu Felister Mgonja na Ndugu Omary Magwinza kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha taarifa hii kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 58 - Wizara ya Nishati kwa mwaka wa medha 2019/2020 ambayo ni Sh.2,142,793,309,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA NISHATI (FUNGU 58) KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Fasili ya 6(9) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati inao wajibu wa kusimamia majukumu yote ya kisera yanayotekelezwa na Wizara hii. Aidha, majukumu ya Kamati kuhusiana na Uchambuzi wa bajeti ya kila mwaka ya Wizara inazozisimamia yamefafanuliwa katika Fasili ya 7(1).

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni, Kamati ilifanya kazi kuu mbili ambazo ni:

a) Kutembelea na Kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa Fedha kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 **[*Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016*]**; na

b) Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 **[*Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016*].**

## 1.1 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara ya Nishati (Fungu 58) katika Mikoa ya Pwani (Rufiji), Njombe (Makambako), Ruvuma (Songea) na Iringa.

Kamati ilikagua Miradi iliyotengewa Fedha katika Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2018/2019. Miradi iliyokaguliwa ni ifuatayo:-

(i) Mradi wa Kuzalisha umeme katika Mto Rufiji (Rufiji HydroPower 2,115 MW);

(ii) Mradi wa Makambako-Songea Njia Kubwa ya Msongo wa 220kV*;* na

(iii) Miradi ya umeme Vijijini REA III Mkoa wa Iringa.

## 1.2 Maelezo na Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

### 1.2.1 Mradi wa Kuzalisha umeme katika Mto Rufiji (Rufiji HydroPower 2,115 MW);

**Mheshimiwa Spika,** mpango wa kujenga mradi wa kufua umeme kwa kutumia maji ya mto Rufiji katika eneo la Stiegler's Gorge ulianzishwa na Baba wa Taifa hayati Mwl. J. K. Nyerere. Mwaka 1976 Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Norway ziliipa Kampuni ya Norplan & Hafslund ya Norway kazi ya kufanya upembuzi yakinifu iliyokamilisha kazi hiyo Mwaka 1980. Upembuzi yakinifu uliangalia mradi mzima ukihusisha kuzalisha umeme, kudhibiti mafuriko na kuendeleza kilimo katika ukanda wa chini wa bonde pamoja na kuendeleza shughuli za uvuvi na utalii. Upembuzi yakinifu ulibainisha kuwa katika eneo hilo unaweza kujengwa mradi wa kufua umeme wenye uwezo wa **MW 2,115.** Gharama za

ujenzi wa Mradi wakati huo iliainishwa kuwa **Dola za Marekani Bilioni 1.38.**

Hata hivyo mradi haukuweza kuendelezwa kwa sababu kuu mbili:

i) Mahitaji ya umeme nchini yalikuwa madogo kiasi cha MW 100; na

ii) Gharama ya ujenzi kuwa kubwa ikilinganishwa na hali ya uchumi wa nchi katika kipindi hicho.

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 12 Disemba, 2018 Mkataba wa ujenzi wa mradi ulisainiwa kati ya TANESCO na Mkandarasi ambae ni Kampuni ya Arab Contractors ikiwa ni JV na Elsewedy Electric, zote za Misri. Tukio hilo la utiaji saini lilishuhudiwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Joseph Pombe Magufuli na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Misri. Ujenzi wa mradi huu utachukua kipindi cha miezi 42 ambapo miezi 36 ni ya ujenzi na miezi 6 ni kwa ajili ya maandalizi. Aidha, utekelezaji wa Mkataba huo umeanza toka tarehe 15 Disemba, 2018 na Serikali kupitia TANESCO ilikabidhi rasmi eneo la Mradi kwa Mkandarasi tarehe 14 Februari, 2019. Mradi wa Rufiji utafua umeme wa kiasi cha **MW 2,115** kwa kutumia maji ya Mto Rufiji.

**Mheshimiwa Spika,** kazi zilizotekelezwa kabla ya kuanza kwa mradi ni ujenzi wa miundombinu wezeshi ambayo ni pamoja na kupeleka umeme wa msongo wa kV 32 kwa kutumia nguzo za miti na kubadilishwa kuwa za zege, maji na mawasiliano ya simu, ujenzi wa barabara ya kiwango cha changarawe ya Kibiti – Mkongo – Mloka – Stiegler's Gorge na sehemu maalum ya kushushia mizigo katika Stesheni ya TAZARA katika kituo cha Fuga. Katika kutekeleza shughuli hizo jumla ya **shilingi bilioni 20.41** zimetumika.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kazi zilizoanza kutekelezwa katika mradi huu, Wakati wa ziara ya Kamati zilibainika changamoto zifuatazo:-

(i) Barabara kutokuwa za kiwango cha kuhimili mvua na mizigo mizito hali ambayo zisipo rekebishwa zinaweza kuchelewesha utekelezaji wa mradi. Hata hivyo, Kamati inatambua juhudi zinazoendelea kufanywa na Wizara pamoja na taasisi husika katika kuhakikisha wanaboresha hali ya barabara hizo kwa wakati;

(ii) Kukosekana kwa mpango wa kutenga eneo kwa ajili ya matenki ya kuhifadhia mafuta "*reserves tank*" wakati wa ujenzi wa mradi kwani ni wazi kwamba mafuta yatahitajika sana wakati wa ujenzi.

### 1.2.2 Mradi wa Makambako – Songea Njia kubwa ya Msongo wa 220KV

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa na Serikali ya Tanzania kupitia TANESCO na kwa ushirikiano wa Serikali ya Sweden kupitia Shirika la maendeleo la Sweden (Sida). Serikali ya Tanzania imechangia jumla ya Dola za kimarekani milioni 20 (ambapo kati ya fedha hizo TANESCO imechangia **dola milioni 7** na Serikali kuu **dola milioni 13)** kwa ajili ya ujenzi wa njia ya msongo wa kV 220 na Vituo vitatu vya kupozea umeme. Serikali ya Tanzania pia imetoa Fedha za ulipaji wa fidia kwenye njia kubwa ya msongo wa kV 220 kiasi cha **shilingi bilioni 7.** Serikali ya Sweden imetoa Jumla ya fedha za Sweden, **Krona milioni 620.** Kati ya fedha hizo Msaada ni **Krona million 578** na mkopo ni Krona **milioni 42.** Jumla kuu ya gharama za mradi kwa fedha za Tanzania ni sawa na **shilingi bilioni 216.**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Makambako-Songea umegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kV 220 yenye urefu wa kilomita 250 kutoka Makambako hadi Songea kupitia Madaba, ujenzi wa vituo vipya vitatu (3) vya kupoza umeme katika eneo la Makambako, Madaba na Songea Mjini na ujenzi wa njia za kusambaza umeme katika vijiji 122 vinavyopitiwa na njia ya umeme.

**Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa mradi umekamilika kama ilivyopangwa ambapo njia ya kusafirisha umeme yenye urefu wa km 250 ya msongo wa kV 220 pamoja na vituo vitatu vya kupooza umeme vya Makambako, Madaba na Songea umekamilika kwa **asilimia 100.** Mradi huu umewezesha mikoa ya Njombe na Ruvuma kuunganishwa katika Gridi ya Taifa ambapo iliungwa mwezi Novemba, 2018. Kazi zinazoendelea ni kusambaza umeme kwenye Vijiji vilivyopitiwa na njia ya umeme.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa usafirishaji umeme ulianza tarehe 12 Mei 2016 na ulikamilika 30 Juni 2018, Mradi wa ujenzi wa vituo vya kupozea umeme ulianza 26 Septemba 2016 na ulikamilika 15 Septemba 2018 na mradi wa usambazaji umeme ulianza Disemba 2018 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2019.

**Mheshimiwa Spika,** ziara ya kamati katika mradi huu ilibaini changamoto zifuatazo:

(i) Nguzo za umeme kuchomwa moto kutokana na shughuli za wananchi wakati wa kilimo;

(ii) Baadhi ya vijiji vilivyopitiwa na njia ya umeme kurukwa kuunganishiwa umeme;

(iii) Muitikio mdogo wa wananchi kuunganishwa na huduma ya umeme;

(iv) Ukosefu wa elimu kwa wananchi kuhusu gharama za kuunganishiwa huduma ya umeme;

(v) Uhaba wa mita za umeme na vifaa vya kuunganishia umeme kwa wateja;

(vi) Kasi ndogo ya kuunganisha huduma ya umeme kwa wananchi.

### 1.2.3 Miradi ya umeme Vijijini REA III Mkoa wa Iringa

**Mheshimiwa Spika**, Iringa ni miongoni mwa Mikoa itakayonufaika na miradi ya umeme vijijini awamu ya tatu inayotekelezwa katika Wilaya za Iringa Vijijini, Kilolo na Mufindi. Kwa Mkoa wa Iringa Miradi ya REA iko katika makundi matatu ambayo ni ;

(i) Ujazilishi "*densification*" unaotekelezwa na Mkandarasi **Namis Corporate Ltd**

(ii) Ujenzi wa njia kuu ya umeme ya Msongo wa Kilovolti **400(BTIP-VEI)** na;

(iii) Mradi wa REA III Mzunguko wa Kwanza unaotekelezwa na mkandarasi **Sengerema Engineering Group**.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia miradi hii katika mkoa wa Iringa inatarajiwa kuwa jumla ya **vijiji 179** vitanufaika ambapo itahusisha ujenzi wa njia za umeme mkubwa wa **kilomita 735.22,** ufungaji wa Mashine umba **(transformers) 288,** ujenzi **kilomita 580.03** wa njia za kusambaza umeme kwa wateja na uunganishaji wa **wateja 13,556** katika Mkoa wa Iringa kufikia Juni 2019. Aidha,hadi sasa Jumla ya **wateja 3,541** kati ya **wateja 13556** wameshafungiwa umeme katika **vijiji 67** vilivyowashiwa umeme katika mkoa wa Iringa.

(i) **Utekelezaji wa Mradi wa REA Awamu ya III (Ujazilizi)**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa REA awamu ya tatu wa kujazia maeneo ambayo yalirukwa kufikishiwa umeme **'densification'** kwa mkoa wa Iringa unatekelezwa na Mkandarasi M/s Namis Corporate Ltd kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1.2** na dola za kimarekani **milioni 1.098** katika Wilaya za Kilolo na Iringa Vijijini. Tayari Mkandarasi amekamilisha shughuli za kusimika nguzo maeneo yote, kuvuta waya na zoezi linaloendelea sasa ni uunganishaji wa wateja.

(ii) **Utekelezaji wa Mradi wa REA Awamu ya III Chini ya Mpango wa Kupeleka umeme kwenye Vijiji vilivyopitiwa na Njia kuu ya Umeme ya Msongo wa Kilovolti 400 (BTIP-VEI)**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imetekeleza Mradi mkubwa wa ujenzi wa njia kuu ya umeme yenye msongo wa Kilovolti 400 yenye urefu wa Kilomita 670 kutoka Iringa hadi Shinyanga, upanuzi wa vituo vya kupoozea umeme kwenye Miji ya Iringa, Dodoma, Singida na Shinyanga pamoja na kuvipatia umeme Vijiji vilivyo kandokando na njia hii ya umeme inayojengwa kutokea Iringa hadi Shinyanga. Mradi huu ni wa muhimu sana kwenye gridi ya Taifa kwa sababu umepanua uwezo wa kusafirisha umeme kutoka kanda ya Kusini Magharibi ambako kuna vyanzo vingi vya umeme na kupeleka kanda ya Kaskazini na Kaskazini Magharibi ambako kuna shughuli nyingi za kiuchumi ikiwemo migodi ya madini.

**Mheshimiwa Spika**, kupitia mradi huu Vijiji vyote 25 vya Mkoa wa Iringa vilivyo ndani ya kilomita 50 za Mradi vimepelekewa umeme **kwa gharama za shilingi bilioni 1.75 na dola za kimarekani milioni 3.43.** Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Norway, Sweden na Serikali ya Tanzania kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (REA). Aidha, kupitia Mradi huu kutafanyika na upanuzi wa kituo kidogo cha kupoozea umeme kwenye Kituo cha kufua umeme Mtera chenye ukubwa wa **10MVA** ili kukidhi ongezeko la usambazaji umeme.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya mafanikio haya upo umuhimu wa nchi kuwa na vyanzo mchanganyiko vya kuzalisha umeme kwenye maeneo tofauti ili kuepuka hasara ya upotevu wa umeme kwenda umbali mrefu.

(iii) **Utekelezaji wa Mradi wa REA Awamu ya III mzunguko wa kwanza**

**Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya tatu unatekelezwa na Mkandarasi M/S Sengerema Engineering Group na ulizinduliwa tarehe 21/03/2017 kwenye Mkoa wa Iringa. Mradi huu unagharimu **Shilingi bilioni 24.7** na **dola za kimarekani Milioni 6.2**

unahusisha usambazaji umeme kwenye **Vijiji 145** katika Wilaya za Mufindi, Kilolo na Iringa Vijijini. Utekelezaji wa mradi huu ulianza tarehe 21/06/2017 na unatarajiwa kukamilika Juni 2019. Jumla ya Vijiji 56 kati ya 145 vimewashwa umeme katika kipindi cha miezi takribani nane ya ujenzi kati ya miezi 24 ya mkataba na wateja wanaendelea kuunganishiwa huduma ya umeme.

**Mheshimiwa Spika**, **kwakuwa kasi ya kuunganisha umeme ni ya wastani wa kawaida kwa mkoa wa Iringa, ni rai ya Kamati kuwa Wizara iimarishe na kuongeza bidii ya usimamizi ili kuepuka kutokamilisha mradi huu kwa wakati.**

(i) **Ukaguzi wa utekelezaji mradi wa REA III**

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilikagua utekelezaji wa umeme mradi wa REA III katika vijiji viwili kama ifuatavyo:-

**a) Kijiji cha Ngano**; Wigo wa usambazaji katika kijiji hiki ulihusisha Ujenzi wa njia ya msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 7.1, njia ya msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 2.3 na ufungaji wa mashine umba moja(1) yenye uwezo wa 50Kva. Kamati iliridhishwa na kazi zilizofanyika katika kijiji hiki;

**b) Kijiji cha Ikuvala** - Wigo wa usambazaji katika kijiji hiki unahusisha Ujenzi wa njia ya msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 3.5, njia ya msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 4.6 na ufungaji wa mashine umba moja(1) yenye uwezo wa 50Kva.
Kamati haikuridhika na kazi zilizofanyika katika Kijiji hiki kwani baadhi ya nyumba zimerukwa kuunganishwa na huduma ya umeme ikiwemo maeneo ya kutoa huduma kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio katika miradi ya umeme mkoani Iringa, ziara ya kamati ilibaini changamoto zifuatazo:-

a) Baadhi ya Wakandarasi kutokuwa na vifaa vya kutosha katika kipindi cha mwanzo wa kazi zao mfano; Kukosekana

kwa nguzo katika kipindi cha miezi minne iliyopita kumesababisha baadhi ya miradi kutokutekelezwa kwa wakati;

b) Baadhi ya Maeneo/taasisi kuto kuunganishwa na huduma ya umeme licha ya miundombinu ya umeme kupita karibu na maeneo hayo mfano; Kanisa la Katoliki kijiji cha Ikuvala ambalo pia linatoa huduma ya Zahanati, Shule na sehemu ya kujisomea (library) kwa wakazi wa kijiji hicho;

c) Uchomaji wa mashamba katika kipindi cha kiangazi ambapo miundombinu hasa nguzo huathiriwa na moto na hivyo kuharibu miundo mbinu ya umeme;

d) Kurukwa kwa vijijiji ambavyo vimepitiwa na njia ya msongo wa umeme mfano; Vijiji vya Ivwanga, Ruhanzo na Malengi ambavyo umeme umepita ila Vijiji havijaunganishwa;

e) Wigo mdogo wa maeneo ya kazi kwa wakandarasi bado ni changamoto kubwa inayosababisha maeneo mengi kutofikishiwa huduma ya umeme.

f) Wakandarasi kupewa kazi ya kusambaza umeme kwenye vijiji kabla kufanyika utafiti na hivyo kupelekea Mkandarasi kupewa wigo mdogo wa kazi tofauti na uhalisia wa maeneo husika.

## 1.3 Maoni ya Jumla Kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

a) Mradi wa umeme wa mto Rufiji ni mradi mkubwa na muhimu sana kwa maendeleo ya nchi kiuchumi, hivyo kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa fedha zinapatikana kwa wakati muda wote wa ujenzi ili kuhakikisha mradi huo unakamilika kwa wakati.

b) Ujenzi wa mradi wa umeme wa Mto Rufiji unapaswa kuzingatia uwepo wa miundombinu na barabara imara ambazo zitahimili mizigo mizito na athari za mvua ili kuhakikisha miradi inaendelea kutekelezwa kwa nyakati zote. Mfano, licha ya jitihada zilizofanyika katika kutengeneza barabara za kufika katika mradi wa umeme wa Mto Rufiji bado barabara hizo zipo katika kiwango kisichoridhisha. Hivyobasi, ikiwa hali ya barabara itaendelea kuwa kama ilivyo sasa barabara hizo hazitapitika wakati wa mvua na hivyo kuchelewesha utekelezaji wa mradi.

c) Kutokana na mradi wa umeme wa Mto Rufiji kuwa ndani ya eneo la Hifadhi ni kweli kwamba umakini unahitajika ili kuhakikisha uharibifu wa mazingira usio wa lazima hautokei. Licha ya ukweli kwamba mafuta mengi yatahitajika kwa matumizi ya magari na mitambo itakayotumika katika ujenzi wa mradi huo hakuna eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa hifadhi ya mafuta (reserve tanks) wakati ni muhimu mafuta yakahifadhiwa kwa umakini na usahihi. Hivyo, kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kunajengwa hifadhi ya mafuta ikiwezekana katika eneo ilipo Stesheni ya reli ili kuzuia milipuko ambayo huenda ikaleta athari kubwa kwa viumbe hai katika eneo la mradi na hifadhi kwa ujumla.

d) Upelekaji wa umeme katika eneo la mradi wa umeme wa Mto Rufiji umetumia nguzo za zege na za miti, kwa kuwa mradi huo upo katika eneo la Hifadhi na wanyama mfano Tembo ambao huwa na tabia ya kuegemea nguzo kwa muda mrefu wakati wa mvua na kwa kitendo hicho ni rahisi kuangusha nguzo za miti na hivyo kuharibu miundombinu ya umeme, Kamati inaona ni vema katika mradi huo zikatumika nguzo za zege pekee ambazo huweza kuhimili hali zote na haziwezi kuanguka kwa urahisi.

e) Kutokana na maeneo mengi ya Vijiji na Vitongoji kurukwa wakati miundombinu ya umeme imepita katika maeneo hayo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza wigo (scope) wa maeneo ili kuweza kukidhi mahitaji ya wananchi kufikiwa na huduma ya nishati ya umeme.

f) Ni vema kabla Mkandarasi hajapewa mkataba wa kazi anayopaswa kufanya kwenye Vijiji mbalimbali kazi ya upembuzi yakinifu kwenye maeneo tajwa iwe imekwisha fanyika ili kuondoa tatizo la Wakandarasi kupewa wigo mdogo wa kazi kinyume na uhalisia wa maeneo/Vijiji husika.

g) Wananchi wengi wa vijijini hawana uelewa mpana wa namna huduma za umeme vijijini zinavyopatikana pamoja na gharama zake hali inayosababisha kuwa na muamko mdogo wa kuunganishwa na huduma za umeme. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya uunganishwaji wa huduma ya umeme ili wananchi wapate uelewa wa namna ya kuunganishwa na huduma ya umeme kwa kuhusisha gharama.

h) Licha ya nia njema ya Serikali kuhakikisha vifaa vinavyotumika katika Miradi ya umeme kama vile nguzo, mita za luku, mashine umba n.k zinazalishwa hapa nchini imedhihirika kuwa wazalishaji wameshindwa kwenda na kasi ya mahitaji ya vifaa kwa wakati na hivyo miradi ya umeme vijijini kukabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa vifaa kwa wakati hali inayosababisha miradi hiyo wakati mwingine utekelezaji wake kusimama na hivyo kurudisha nyuma juhudi za maendeleo kwa wananchi. Ni Rai ya kamati kuwa, wazalishaji wa ndani wataongeza mitaji yao na kuongeza uwezo ili kuwezesha miradi kukamilika kwa wakati;

Hatahivyo, Kamati inaishauri Serikali kujipanga na kuhakikisha vifaa vinapatikana kwa wakati na kwa gharama nafuu ili miradi hiyo ikamilike kwa wakati na hivyo kuchochea maendeleo katika maeneo husika.

i) Utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini katika baadhi ya maeneo umekuwa haushirikishi viongozi na wananchi wa maeneo husika na hivyo kutokuwa na uelewa wa pamoja kuhusu huduma ya umeme. Kamati inaishauri Serikali izingatie sana ushirikishwaji wa wananchi pamoja na viongozi wa maeneo wanaohusika.

j) Pamoja na kuwa TANESCO inafanya vizuri katika uzalishaji na usafirishaji wa umeme nchini bado kumekuwa na changamoto kubwa katika usambazaji wa umeme kwa wananchi na kusababisha wananchi wengi kukosa huduma ya umeme. Mathalani, katika mradi wa njia kuu ya umeme kutoka Makambako – Madaba - Songea ni **wateja 6708 tu kati ya 22700 sawa na asilimia 29** ya lengo ndio wameunganishiwa umeme hadi sasa. Aidha, mradi wa REA III mkoani Iringa ambao umelenga kuunganisha umeme kwa **wateja 13556** kufikia mwezi Juni, 2019 hadi sasa wameunganishwa **wateja 3541** tu sawa na **asilimia 26** ya lengo. **Kwa takwimu hizo maana yake ni kwamba uunganishwaji wa wateja katika miradi ya REA uko chini ya asilimia 30 ya lengo**.

Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi katika kutoa elimu kwa wananchi juu ya gharama za uunganishwaji wa umeme pamoja na kuongeza kasi katika usambazaji wa umeme ili wananchi wengi waweze kuunganishwa na kufikiwa na huduma hii na ikumbukwe kuwa kadri wananchi wengi wanavyounganishiwa umeme ndivyo ambavyo soko linavyopanuka na hivyo kukuza fursa ya kibiashara kwa TANESCO.

## 1.4 Sekta Ndogo ya Gesi Asilia na Hali ya Upatikanaji wa Mafuta Nchini

### 1.4.1 Sekta Ndogo ya Gesi Asilia

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ndogo ya Gesi asilia ni sekta muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu kiuchumi. Ili nchi iweze kunufaika ipasavyo na sekta hii ni lazima kuwekeza katika taasisi za usimamizi na uendelezaji ambazo zimewezeshwa kiteknolojia, kimtaji na katika rasilimali watu. Kwa maeneo ambayo gesi asilia imeshaanza kuvunwa yaani Mnazi bay, Songosongo na Killiwani, kiasi ambacho kimehakikiwa ni futi za ujazo **Trilioni 1.96.**

**Mheshimiwa Spika,** sekta ya ndogo ya Gesi Asilia inasimamiwa na kuendelezwa kimkakati na Taasisi mbili za umma zifuatazo:-

### 1.4.2 Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA)

**Mheshimiwa spika,** Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) majukumu yake yamebainishwa katika Kifungu cha 12 cha Sheria ya Petroli sura ya 392. PURA ni Taasisi muhimu katika kudhibiti gharama za uzalishaji katika mkondo wa juu ambazo pia husaidia kudhibiti bei katika soko nchini. Hatahivyo, Kamati imebaini kuwa tangu kuanzishwa kwa PURA mwaka 2017 hadi sasa haina bajeti ya kutosha, watumishi wa kudumu (waliopo wote wanakaimu) wala vitendea kazi na hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Moja ya jukumu la Wakala wa udhibiti wa Mkondo wa juu wa Petroli (PURA) ni kutunza Data zitokanazo na utafiti wa mafuta nchini. Jukumu hili hapo awali lilikuwa likifanywa na TPDC. Mpaka sasa PURA haina miundombinu wezeshi ya kutunzia Data hizo. **Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuhakikisha PURA inawezeshwa kuwa na Jengo la Ofisi kwaajili ya kutekeleza majukumu yake ikiwemo utunzaji wa data zitokanazo na utafiti wa gesi asilia badala ya kutegemea hifadhi za taasisi nyingine. Kuendelea kuacha utunzaji wa Data ufanywe na taasisi nyingine isiyo na wajibu kisheria ni hatari kwa usalama wa data hizo**.

### 1.4.3 Kampuni ya Taifa ya Mafuta (National Oil Company-TPDC)

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 8 cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392, kinatambua Shirika la Taifa la Maendeleo ya Petroli (TPDC) kama Kampuni ya Taifa ya Mafuta (*National Oil Company*). Kifungu cha 9 cha Sheria hii kina ainisha majukumu ya TPDC ambayo ni pamoja na kushiriki kimkakati kwenye mnyororo wa utafutaji, uendelezaji, uzalishaji na biashara ya Mafuta na Gesi Asilia nchini, kusimamia Hisa za

Serikali (*Government Commercial Participating Interest*), na kumiliki miundombinu ya kimkakati kwenye mnyororo wa Mafuta na Gesi Asilia.

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile Kifungu cha 125 cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392 kinaipa TPDC mamlaka ya kuwa mkusanyaji na msambazaji wa Gesi Asilia nchini (*Aggregator*) kupitia Kampuni Tanzu. Aidha, kwa mujibu wa Kifungu cha 6 cha Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi Asilia 2015, TPDC ina wajibu wa ukusanyaji wa mapato ya mfuko wa Mapato ya Mafuta na Gesi ambayo siyo ya kikodi.

**Mheshimiwa Spika**, Uwezo wa ushiriki kwenye ukusanyaji wa mapato wa TPDC pamoja na kuwa umeainishwa vyema katika Sheria ya Petroli ya mwaka 2015 lakini umeminywa sana kupitia Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi ya mwaka 2015. Aidha, kifungu cha 17 cha Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi ya mwaka 2015, kimeainisha matumizi ya Mfumo wa Pato la Taifa (GDP) katika kukokotoa fedha za Mfuko wa Mapato ya Mafuta na Gesi kwamba ili mapato husika yapelekwe kwenye Mfuko wa Akiba wa Mafuta na Gesi *(Oil and Gas Savings Account)* sharti makusanyo hayo kwa mwaka husika yawe yamefikia **asilimia 3** ya Pato la Taifa (GDP) na ziada ndiyo itakayohamishiwa katika mfuko wa akiba.

**Mheshimiwa Spika,** Hivyo ili TPDC apate fedha kutoka mfuko huo ni lazima mapato ya gesi yafikie asilimia 3 ya GDP. Kutokana na utaratibu huo wa GDP ni wazi kuwa unaweka ugumu kwa TPDC kuweza kupata fedha kuwekeza katika miradi ya maendeleo. Mathalani, TPDC ina kasi ndogo ya kutekeleza mradi wa usambazaji gesi majumbani katika mikoa ya Dar Es Salaam, Lindi na Mtwara kwa sababu ya kutokuwa na Fedha za kutosha za kujenga miundombinu.

Aidha, Wakala wa Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) hutoa ushauri kwa Waziri mwenye dhamana ya Nishati juu ya utoaji, ufutaji na uongezaji muda wa leseni. TPDC iliomba kupewa leseni ya utafiti wa Petroli katika vitalu vya Mnazibay North na Songo Songo West, ambapo kwa

kuzingatia kifungu Namba 85 na 86 cha Sheria ya Petroli Sura ya 392, PURA iliishauri Wizara kutoa leseni hizo baada ya kujiridhisha kuwa pamoja na mambo mengine TPDC ina uwezo kifedha na kitaalam kutekeleza shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi katika vitalu husika. Hivyo, TPDC haikupatiwa leseni kwa wakati huo kwakuwa katika masharti tajwa haikukidhi uwezo wa kuwa na mtaji wa kutosha.

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kufanya maamuzi ya kimkakati yatakayoiwezesha TPDC kupata fedha zitakazoiwezesha kushiriki kikamilifu kwenye uwekezaji kwa niaba ya watanzania. Kwa hali ilivyo sasa ufinyu wa mtaji umeifanya TPDC kushiriki kwa kiwango cha chini sana kwenye uwekezaji wa miradi mbalimbali.**

### 1.4.4 Matumizi Madogo ya Gesi Asilia Nchini

**Mhesimiwa Spika**, Gesi Asilia inayozalishwa nchini imekuwa ikitumika kuzalisha umeme, viwandani, majumbani na kwenye magari. Hadi kufikia Disemba 2018, gesi asilia iliyokuwa ikitumika katika uzalishaji umeme, viwandani na matumizi mengine kwa mwaka ni futi za ujazo **Trilioni 0.63.** kati ya futi za ujazo **trilioni 1.96** zilizohakikiwa**.** Hii inaonesha kuwa kwa mwaka Gesi Asilia inayotumika ni sawa na **asilimia 4.18** ya kiasi kilichohakikiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Ufuatiliaji wa Kamati umebaini kwamba sababu moja wapo ya kuwa na matumizi madogo ya Gesi Asilia nchini ni bei kubwa wanayouziwa watumiaji. Aidha, TPDC imekuwa ikiuza Gesi bei tofauti tofauti kwa wanunuzi wa Gesi hasa viwandani. Mathalani, Kiwanda cha Goodwill Mkuranga kinauziwa gesi kwa dola za kimarekani (USD) 5.57 mmBTU kwa ajili ya "*Power*" na dola za kimarekani (USD) 6.64 mmBTU kwa ajili ya "*Heating*" na kiwanda cha Dangote kinauziwa kwa dola za kimarekani (USD) 4.2 mmBTU. Licha ya kigezo cha umbali kuchangia katika upangaji huu wa bei, **Kamati inaona kuwa mkakati wa kuwa na bei zinazovutia watumiaji wengi kutumia gesi ungewezesha matumizi ya gesi kuongezeka kwenye sekta ya uzalishaji na hivyo kupanua**

**wigo wa mapato ya kikodi kwa Serikali kupitia sekta nyingine kukuza ajira.**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali hiyo huenda viwanda vingine vinavyotumia Gesi Asilia vikasimamisha uzalishaji hivyo, Kamati inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha inaweka mikakati madhubuti ya kufanya majadiliano na wadau mbalimbali, wamiliki wa viwanda, TRA, EWURA na wazalishaji wa Gesi Asilia katika mkondo wa juu na kuhakikisha bei ya Gesi Asilia inapungua na kuleta tija kwa pande zote ili kuvutia uwekezaji katika sekta ya viwanda nchini.

### 1.4.5 **Umuhimu wa kufanya marejeo ya Mikataba (PSAs)**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa sasa nchi yetu ina Mikataba hai 11 ya utafutaji na uendelezaji wa shughuli za Gesi Asilia ambapo kati ya hiyo mikataba mitatu (3) ipo kwenye hatua za uzalishaji na mikataba 8 ipo katika hatua ya utafutaji na ugunduzi. Mikataba yote hii iliingiwa kwa Sheria ya zamani na kwa msingi huo inakinzana na Sheria zilizopo sasa **(Sheria ya Petroli Sura ya 392, Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Maliasili za Nchi ya mwaka 2017 na Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Umiliki wa Maliasili ya mwaka 2017)**. Mikataba hii imeinyima nchi fursa ya kunufaika kikamilifu na rasilimali zake. Aidha, mara ya mwisho utangazaji wa vitalu ulifanyika mwaka 2013. Hivyo kuchelewa kufanya mapitio kunalikosesha Taifa fursa ya upatikanaji wa wawekezaji wapya katika mkondo wa juu.

**Mheshimiwa Spika,** Kuendelea kuwepo kwa mikataba yenye masharti hasi ambayo haina tija ni jambo ambalo halipaswi kuvumiliwa hata kidogo. Mathalani, mikataba mibovu ya mauziano ya Gesi Asilia na umeme utokanao na Gesi Asilia imesababisha TANESCO kuelemewa na mzigo wa madeni makubwa ambayo hadi kufikia Januari 2018 TANESCO ilikuwa ina deni la takriban **shilingi bilioni 630.8** inazodaiwa na SONGAS, PAET, na TPDC. Aidha kwa TANESCO kushindwa kulipia ankara za Gesi Asilia kwa TPDC kwa muda mrefu kumeisababishia TPDC kushindwa kujiendesha kibiashara na kuendeleza uwekezaji katika sekta ndogo ya Gesi Asilia na

vilevile TPDC inashindwa kulipa Ankara za ununuzi wa Gesi Asilia kwa wakati kwa makampuni ya mkondo wa juu hali ambayo imesababisha wakati mwingine Makampuni ya Mkondo wa Juu kusitisha kuuza Gesi Asilia kwa TPDC kutokana na deni kuwa kubwa.

## 1.5 Hali ya Upatikanaji wa Mafuta Nchini

**Mheshimiwa Spika**, Mfumo wa uingizaji wa mafuta nchini unasimamiwa na Wakala wa Serikali wa Uagizaji Mafuta kwa pamoja *(The Petroleum Bulk Procurement Agency – PBPA)*.
**Mheshimiwa Spika,** kuanzia mwezi Julai, 2018 hadi Februari, 2019, Wakala wa PBPA umeendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ambapo hakuna uhaba wowote wa mafuta uliojitokeza nchini kwa kipindi hicho. Aidha, katika kipindi hiki bei za mafuta nchini zimekuwa zikipanda na kushuka kulingana na bei za mafuta hayo katika soko la Dunia. Jumla ya **lita bilioni 3.243** za mafuta ya dizeli, petroli, mafuta ya ndege na mafuta ya taa yaliingizwa nchini kwa ajili ya matumizi ya ndani **(*local use*)** na kwenda nje ya nchi **(*transit*).** Kati ya kiasi hicho cha mafuta kilichoingizwa nchini, jumla ya **lita bilioni 1.717** sawa na **asilimia 53** zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya ndani, na **lita bilioni 1.526** sawa na **asilimia 47** kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi jirani.

Jedwali lifuatalo linaonesha mchanganuo wa kiasi, uwiano, aina ya mafuta na ongezeko au upungufu uliojitokeza ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa Mwaka 2017/2018. Kupungua kwa kiwango cha mafuta yaliyoingizwa nchini kwa miezi nane (8) (Julai, 2018 hadi Februari, 2019) ya mwaka 2018/2019 kumetokana na kuwepo kwa kiwango kikubwa cha mafuta mwishoni mwa mwaka 2017/2018; kuongezeka kwa matumizi ya Gesi Asilia katika baadhi ya viwanda vikubwa nchini na kusitisha uzalishaji wa umeme unaotokana na dizeli na mafuta mazito (HFO) kwa baadhi ya mitambo mikubwa ya kuzalisha nishati hiyo.

**Aina na Kiasi cha Mafuta kilichoingizwa nchini kwa Matumizi ya Ndani (*Local*) kuanzia mwezi Julai, 2018 hadi Februari, 2019 kwa Ujazo wa Lita**

| Mwezi /kipindi | Aina ya Mafuta | | | Jumla kwa Mwezi |
|---|---|---|---|---|
| | Dizeli | Petroli | Mafuta ya Ndege/Taa | |
| Jul - 2018 | 83,748,011 | 57,276,137 | 22,146,229 | 163,170,377 |
| Aug - 2018 | 156,788,032 | 82,991,592 | 20,146,995 | 259,926,619 |
| Sep - 2018 | 111,065,363 | 62,431,044 | 26,544,314 | 200,040,722 |
| Okt - 2018 | 109,781,055 | 70,122,491 | 28,386,745 | 208,290,292 |
| Nov - 2018 | 106,334,404 | 85,708,791 | 22,550,332 | 214,593,527 |
| Des - 2018 | 150,849,541 | 52,873,371 | 22,499,053 | 226,221,965 |
| Jan - 2019 | 157,155,720 | 105,287,914 | 15,765,547 | 278,209,181 |
| Feb - 2019 | 186,880,369 | 65,630,408 | 15,662,584 | 268,173,361 |
| **Jumla kwa Kipindi cha mwezi Jul, 2018 –Feb, 2019** | **1,047,102,203** | **574,457,226** | **155,938,604** | **1,777,498,032** |
| **Jumla kwa Kipindi cha mwezi Jul, 2017 –Feb, 2018** | **1,462,716,545** | **818,494,071** | **172,818,923** | **2,454,029,538** |
| **Asilimia ya Mabadiliko** | **(0.28)** | **(0.30)** | **(0.10)** | **(0.28)** |

**Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya PBPA kwa mwaka wa fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na hali ya upatikanaji wa mafuta nchini pamoja na usimamizi mzuri wa uagizaji wa mafuta unaofanywa na Wakala wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja (PBPA) hivyo ni imani ya Kamati kuwa Serikali na PBPA zitaendelea kusimamia sekta ya mafuta kwa ufanisi na kwa manufaa ya uchumi wa nchi yetu sambamba na kuandaa mkakati mahsusi wa muda mrefu utakaoziwezesha kampuni za ndani kushiriki na kushinda zabuni za uagizaji mafuta.**

## 1.6 Hali ya Upatikanaji wa Umeme Nchini

**Mheshimiwa Spika**, Serikali imekusudia kuzalisha umeme MW 10,000 ifikapo mwaka 2025. Lengo ni kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa nchi ya uchumi wa kati unaochochewa na ukuaji wa viwanda ifikapo mwaka 2025. Katika kipindi cha

kuanzia mwezi Julai, 2018 hadi sasa hali ya upatikanaji umeme nchini imeendelea kuimarika. Hali hiyo imetokana na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali za kuhakikisha kuwa miundombinu ya kuzalisha umeme nchini inaimarishwa ili izalishe umeme kwa wastani wake wa juu. Mitambo hiyo ni pamoja na Kidatu yenye uwezo wa kuzalisha MW 204, Kihansi MW 180, Mtera MW 80 na New Pangani MW 68.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Februari, 2019 uwezo wa jumla wa mitambo ya kuzalisha umeme *(installed capacity*) nchini umeongezeka hadi kufikia **MW 1,601.896** kutoka **MW 1,204.52** ya Mwaka 2015. Ongezeko hilo limewezesha kuwa na umeme wa ziada wa wastani wa zaidi ya MW 300 ambapo matumizi ya juu ya umeme kwa sasa katika Gridi ya Taifa yalifikia **MW 1,116.58** tarehe 30 Novemba, 2018. Umeme unaozalishwa unatokana na vyanzo mbalimbali *(Energy Mix)* ambapo Maji (**asilimia 35.81**), Gesi Asilia (**asilimia 55.73**), Mafuta Mazito (**asilimia 7.80**) na Tungamotaka (**asilimia 0.66**). Aidha, kati ya MW 1,601.896 zinazozalishwa MW 1565.72 zimeunganishwa kwenye Gridi ya Taifa na MW 36.176 zipo nje ya Gridi. Kati ya maeneo yaliyo nje ya Gridi ya Taifa yamepungua na kubaki MW 36.176 ikilinganishwa na MW 74.4 zilizokuwepo Mwaka, 2015 kutokana na jitihada za Serikali za kuyaunganisha maeneo hayo katika Gridi. Maeneo yaliyounganishwa ni pamoja na Mkoa wa Ruvuma, Mtwara, Lindi na Kagera katika Wilaya za Ngara na Biharamulo.

**Mheshimiwa Spika**, nchi yetu imejiwekea lengo la kuzalisha umeme kiasi cha **MW 5000** ifikapo mwaka 2020 na **MW 10,000** ifikapo mwaka 2025. Hata hivyo, kwa mujibu wa taarifa ya Wizara iliyowasilishwa kwenye Kamati, upo uwezekano mkubwa wa kutofikisha **MW 5000** ifikapo mwaka 2020. Taarifa zinaonesha kuwa uwezekano uliopo ni kufikia uzalishaji wa **MW 2780**, na hii itategemea kukamilika kwa wakati kwa zoezi la uchambuzi wa zabuni unaoendelea sasa kupata Kampuni za wawekezaji binafsi zenye sifa ya kutekeleza miradi ya kuzalisha umeme yenye jumla ya **MW 950** (Makaa ya mawe **MW 600**, Umeme wa Jua **MW 150**, Umeme wa upepo **MW**

**200**); ili uzalishaji huo uweze kuanza mwaka 2019 kama inavyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika, ili kuendana na kasi ya ujenzi wa uchumi wa Viwanda, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha Mradi wa kuzalisha Umeme kwa kutumia Maji ya Mto Rufiji unapelekewa fedha za kutosha na kusimamiwa kikamilifu ili ukamilike kwa wakati.** Sambamba na hilo, TANESCO ihakikishe inaimarisha miundombinu ya kusambaza umeme nchini kwa kubuni na kujenga miundombinu imara inayodumu kwa muda mrefu na kuongeza ufanisi wa Shirika ili kupunguza kero kwa wateja. Aidha, katika kuendelea kupata nishati ya uhakika nchini, TANESCO inapaswa kujikita katika kuzalisha umeme kwa kutumia vyanzo vingine vya Nishati kama vile umeme wa Upepo ambao kwa takwimu imebainika kuwa zaidi ya **MW 850** zinaweza kuzalishwa kutoka katika chanzo cha nishati ya upepo katika maeneo mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuwa na wawekezaji wengi wenye nia ya kuwekeza katika nishati jadidifu bado kumekuwa na urasimu mkubwa katika makubaliano na wawekezaji kuhusu bei ya kuuza umeme baada ya wazalishaji binafsi kuzalisha umeme huo. Kwakuwa TANESCO ndio mnunuzi pekee nchini wa umeme, wawekezaji binafsi wamekuwa wakishindwa kukubaliana bei za mauziano na TANESCO na wakati mwingine majadiliano ya makubaliano yanachukua muda mrefu kuliko ilivyokusudiwa hivyo kuchangia kwa kiasi kikubwa kuwakatisha tamaa wawekezaji binafsi wenye nia ya kuwekeza na kuendeleza uzalishaji nishati hii ya umeme.

**Mheshimiwa Spika, Ni rai ya Kamati kwa TANESCO kuhakikisha inaweka mazingira rafiki kwa wawekezaji wenye nia ya kuwekeza na kuzalisha nishati ya umeme nchini.** Aidha, TANESCO ihakikishe unakuwepo mfumo madhubuti na unaoeleweka ambao utawezesha wawekezaji kufanya maamuzi ya kuwekeza nchini kwa kuzingatia matakwa yetu bila kuiingiza TANESCO kwenye mzigo wa kununua umeme kwa gharama kubwa. Vilevile, Shirika linapaswa kujikita katika

kujiendesha kibiashara pamoja na kuleta ushindani wenye tija ili Taifa linufaike na uwepo wa umeme wa uhakika nchini.

### 1.6.1 Utekelezaji wa miradi ya Jotoardhi kupitia TGDC

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye rasilimali ya Jotoardhi ambayo inaweza kutumika kama chanzo cha nishati ya umeme. Hapa nchini mikoa yenye rasilimali Jotoardhi ni Arusha, Dodoma, Kagera, Katavi, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Pwani, Rukwa, Shinyanga, Singida, Songwe na Tanga. Baada ya Serikali kubaini uwepo wa maeneo yenye Jotoardhi mwaka 2014 ilianzisha kampuni tanzu ya uendelezaji wa miradi ya jotoardhi TGDC na kuipa lengo la kuzalisha MW 200 za umeme wa Jotoardhi kufikia mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa gharama za uendelezaji wa umeme wa jotoardhi ni kubwa lakini gharama za uzalishaji ni nafuu sana kuliko vyanzo vingine vya nishati ya umeme na vilevile umeme wake ni wa uhakika na endelevu. Mathalani, Umeme wa jotoardhi huweza kuuzwa kwa **senti 0.04 hadi 0.08** ya dola ya kimarekani kwa "*unit*" moja. Hatahivyo, tangu mwaka 2014 ilipoanzishwa TGDC hadi sasa hakuna uchorongaji wa kisima hata kimoja licha ya uwepo wa maeneo yenye jotoardhi linalofikia hadi nyuzi joto 230-250. Hivyo ni wazi kuwa TGDC imeshindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo kutokana na changamoto zifuatazo:-

(i) Kukosekana kwa Sheria mahsusi ya Jotoardhi nchini;

(ii) Gharama kubwa za leseni za utafiti ambazo zinalipwa kwa dola;

(iii) Gharama kubwa za utekelezaji wa miradi ya jotoardhi hasa katika hatua ya utafiti na uhakiki; na

(iv) Uhaba wa wataalam na vitendea kazi kwa ajili ya uendelezaji wa Jotoardhi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwakuwa Serikali imedhamiria kuwa na umeme wa uhakika kufikia MW 10,000 ifikapo mwaka 2025. Ili kufikia dhamira hiyo ni muhimu kuwa na vyanzo mchanganyiko na vyenye uhakika na endelevu. Jotoardhi ni chanzo cha uhakika, endelevu na cha bei nafuu hivyo ni ushauri wa Kamati kwamba Serikali iipitie upya Sheria ya Madini Sura ya 123 ili ikidhi mahitaji ya masuala ya Jotoardhi na kuitengea TGDC fedha za kutosha ili kuweza kuendeleza maeneo ya Jotoardhi kwa kuzalisha umeme na vilevile TGDC iwezeshwe kuajiri watumishi wenye weledi wa hali ya juu katika masuala ya Jotoardhi.

## 1.7 Tathmini ya Miradi ya Umeme Vijijini (REA III) Mzunguko wa Kwanza

**Mheshimiwa Spika**, Tathmini ya utekelezaji wa Mradi wa kusambaza umeme vijijini (REA III mzunguko wa kwanza) inaonesha kuwa mikataba ya kutekeleza miradi hii ilisainiwa Julai 3, 2017 na malipo ya awali (Advance Payment) kwa wakandarasi yalilipwa Oktoba 31, 2017 hivyo kuna ucheleweshwaji wa takriban miezi minne. Aidha, ufunguaji wa hati za mwamana (Letter of Credit) ulifanyika mwezi Mei 2018 hali iliyosababisha utekelezaji kuchelewa kwa miezi takriban 10 baada ya mikataba kusainiwa mnamo mwezi Julai 2017 na hivyo kusababisha muda wa kuanza miradi kusogea mbele kwa takribani mwaka mmoja. Kwa msingi huu inatarajiwa kuwa mikataba itakamilika katika kipindi cha kati ya mwezi Aprili na Julai 2020 badala ya Juni 2019. Ili kuiepusha Serikali na hatari ya madai ya fidia kutoka kwa wakandarasi kutokana na Serikali kuchelewesha utekelezaji wa mikataba, **Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa hali iliyojitokeza kwenye mradi wa REA III mzunguko wa kwanza haijirudii wakati wa kuanza utekelezaji wa mradi wa REA III mzunguko wa pili.**

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya Wizara kuhusiana na tathmini iliyofanyika mwezi Aprili 2019 inaonesha kuwa kati ya kampuni 29 zilizopewa kandarasi ya kusambaza umeme vijijini ni kampuni 15 tu ndizo ambazo utekelezaji wa mikataba yao upo juu ya malengo.

Aidha, taarifa hiyo inabainisha kuwa kumekuwa na changamoto ya kasi ndogo ya utekelezaji kwa baadhi ya wakandarasi. Mathalani, katika kipindi cha takribani miezi 9 kati ya miezi 24 ya mikataba ambayo ni sawa na asilimia 38 ya muda wa mkataba zipo jumla ya kampuni 7 ambazo utekelezaji wa mikataba yao hauridhishi kabisa. Kampuni hizo ni *M/s CCC - Etern Consortium – Kigoma* - utekelezaji wa jumla umefikia asilimia **7.4*,*** Singida - utekelezaji wa jumla umefikia asilimia **22.9,** *JV Radi Service Ltd, Njarita Contractor Ltd & Aguila Contractor Ltd – Mtwara - utekelezaji wa* jumla umefikia asilimia **28.4,** *Urban & Rural Engineering Ltd - Kilimanjaro-* utekelezaji wa jumla umefikia asilimia **32.84,** *JV Pomy Engineering Co. Ltd, Intercity Builders Ltd & Octopus Ltd. –* Tabora - utekelezaji wa jumla umefikia asilimia **38*,*** *State Grid Electrical & Technical Work Ltd* – Morogoro - utekelezaji wa jumla umefikia asilimia **31*,*** *Urban & Rural Engineering Ltd –* Kigoma - utekelezaji wa jumla umefikia asilimia **31.0.**

**Mheshimiwa Spika**, Tathmini zaidi inaonesha kuwa Kampuni 7 zilizosalia utekelezaji wa mikataba yao upo chini kidogo ya malengo. Kampuni hizo ni *JV White City and Guangdong Ltd - Geita* - utekelezaji wa jumla umefikia asilimia **48.0,** *A2Z Infra Engineering Ltd* - Dodoma - utekelezaji wa jumla umefikia asilimia **33.9,** *JV Pomy Ltd, Intercity Ltd & Octopus Ltd* - Tabora - utekelezaji wa jumla umefikia asilimia **36.7,** *State Grid Electrical & Technical Work Ltd* - Lindi - utekelezaji wa jumla umefikia asilimia **38.9,** *NIPO Group Ltd* - Arusha - utekelezaji wa jumla umefikia asilimia **42.0,** *Angelique International Limited* - Shinyanga - utekelezaji wa jumla umefikia asilimia **43** na Manyara - utekelezaji wa jumla umefikia asilimia **45.0.**

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaona ipo haja ya wakandarasi kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi hii, hatahivyo, Serikali inapaswa kuongeza nguvu ya usimamizi na ufuatiliaji wa utendaji wa Kampuni hizo ili kuhakikisha kuwa miradi hii inakamilika kwa wakati na kwa ubora uliokusudiwa kulingana na matakwa ya mikataba. Aidha, endapo jitihada za ufuatiliaji zitashindwa kuzaa matunda yanayotarajiwa, Kamati inaishauri Serikali kutosita kuzichukulia kampuni husika hatua stahiki na za haraka kulingana na matakwa ya mikataba yao**

**na kazi ambazo hazijamalizika zikabidhiwe kwa TANESCO ili iweze kukamilisha sehemu ya kazi zilizobaki.**

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti kwa kuzingatia mambo makuu matatu ambayo ni:-

a) Makusanyo ya Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2018/2019;

b) Hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina na;

c) Uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ya Nishati na Madini wakati huo.

### 2.1 **Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

a) **Makusanyo ya Maduhuli kwa mwaka wa fedha 2018/2019;**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Nishati katika Mwaka 2018/19 ilipanga kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 394.45**. Kati ya makusanyo hayo, jumla ya **Shilingi bilioni 394.44** zilitarajiwa kukusanywa kupitia shughuli za Mafuta na Gesi Asilia na **Shilingi milioni 10.0** kukusanywa kupitia shughuli za utawala. Mapato hayo yanatokana na vyanzo mbalimbali vikiwemo; Shughuli za TPDC za utafiti wa mafuta, Mauzo ya Gesi Asilia na Mauzo ya Nyaraka za Zabuni.

Hadi kufikia Februari 28, 2019, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi bilioni 291.84**. Makusanyo hayo yalitokana na shughuli za Mafuta na Gesi Asilia nchini zinazoratibiwa na TPDC. Makusanyo hayo ni sawa na **asilimia 131.7** ya lengo la hadi mwezi Februari, 2019 la makusanyo ya **Shilingi bilioni 221.61.** Ongezeko la kiasi cha makusanyo ya maduhuli katika kipindi hiki kunatokana na malipo ya gawio la faida katika

shughuli za mkondo wa juu ikiwemo kampuni ya PAET ambayo imeanza kulipa baada ya kutofanya hivyo kwa miaka mingi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa usimamizi mzuri wa makusanyo ya maduhuli na hivyo kuvuka malengo ya makusanyo.

b) **Hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina;**

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 28 Februari, 2019 Wizara ya Nishati (Fungu 58) ilikuwa imepokea kutoka Hazina jumla ya **Shilingi bilioni 345.22.** Pamoja na mapokezi hayo, Hazina pia ilitenga jumla ya **Shilingi bilioni 688.65** ambazo zililipwa kwa Mkandarasi wa Mradi wa Rufiji tarehe 24 April, 2019 kama malipo ya awali *(advance payment)* katika mradi huo. Kutolewa kwa fedha hizo kumefanya Wizara kupewa jumla ya **Shilingi trilioni 1.03**, sawa na **asilimia 92.1** ya fedha zote zilizotarajiwa kupokelewa kwa kipindi husika ambazo zilikuwa **Shilingi trilioni 1.43**. Kati ya **Shilingi trilioni 1.03** zilizopokelewa na kutengwa, **Shilingi trilioni 1.31** ni fedha za miradi ya maendeleo, sawa na **asilimia 93.2** ya fedha za maendeleo zilizotakiwa kupokelewa (**Jedwali Na. 1**). Fedha hizo za maendeleo zilielekezwa katika miradi minne (4) ambayo ni: Mradi wa kupeleka umeme vijijini kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) **Shilingi bilioni 302.61** ambapo **fedha hizi zinajumuisha shilingi bilioni 87.75** ambazo zilipokelewa na REA moja kwa moja kutoka kwa wafadhili (*Direct Funding*); Mradi wa *Resource Mobilization* (unaoratibiwa na TPDC) **Shilingi milioni 994.78;** Mradi wa Makambako – Songea **Shilingi bilioni 5.61** ambazo ni fedha za nje; na Mradi wa Kuzalisha Umeme katika Mto Rufiji (MW 2,115) **Shilingi trilioni 1.004** ambapo **Shilingi bilioni 20.41** zimetumika kwa ajili ya miundombinu wezeshi na **Shilingi bilioni 688.65** tayari zimelipwa kama malipo ya awali kwa mkandarasi wa mradi wa umeme katika Mto Rufiji.

Kwa upande wa Fedha za Matumizi ya Kawaida, Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi bilioni 15.59**, ambazo ni sawa na **asilimia 86.2** ya fedha zilizotakiwa kupokelewa katika kipindi hiki.

**Jedwali Na. 1:** Muhtasari wa fedha zilizopokelewa na kutengwa katika kipindi cha mwezi Julai, 2018 hadi Februari, 2019

| FEDHA ZILIZOTENGWA NA KUPOKELEWA KWA MWAKA 2018/19 HADI KUFIKIA MWEZI FEBRUARI, 2019 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Na** | **Matumizi** | **Bajeti iliyopitishwa kwa Mwaka 2018/19** | **Fedha zilizotakiwa kutolewa hadi kufikia Februari, 2019** | **Fedha zilizopokelewa/ zilizotengwa hadi Februari, 2019** | **Asilimia ya mapokezi** |
| 1 | Matumizi Mengineyo (OC) | 15,025,821,000 | 10,017,214,000 | 8,703,618,200 | 86.9% |
| 2 | Mshahaara (P.E) | 12,119,193,000 | 8,079,462,000 | 6,888,262,300 | 85.3% |
| | **Jumla Ndogo** | **27,145,014,000** | **18,096,676,000** | **15,591,880,500** | **86.2%** |
| 3 | Fedha za Ndani | 1,489,741,000,000 | 1,293,168,666,700 | 236,272,683,550 | 94.0% |
| | Fedha zilizotengwa | | | 984,000,000,000 | |
| 4 | Fedha za Nje | 175,400,000,000 | 116,933,333,300 | 93,359,915,500 | 79.8% |
| | **Jumla Ndogo** | **1,665,141,000,000** | **1,410,102,000,000** | **1,313,632,599,050** | **93.2%** |
| | **JUMLA KUU** | **1,692,286,014,000** | **1,428,198,676,000** | **1,329,224,479,550** | **93.1%** |

***Chanzo; Taarifa ya Wizara ya Nishati Fungu 58 kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/19.***


Ufafanuzi zaidi kuhusu uwiano kati ya Bajeti iliyoidhinishwa na fedha zilizopatikana hadi Februari, 2019 ni kama unavyoonekana kupitia Jedwali Na. 2 katika taarifa hii.

**Kielelezo Na. 2**

| **BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2018/2019** | | | **FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI Februari, 2019** | |
|---|---|---|---|---|
| **UFAFANUZI** | **KIASI** | **ASILIMIA** | **KIASI** | **ASILIMIA** |
| **JUMLA KUU** | **Tril. 1. 692** | 100 | Tril 1.329 | 93.1 |
| **FEDHA ZA MAENDELEO** | Tril 1.665 | 98.4 | Tril 1.313 | 93.2 |
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | Bil 27.145 | 1.6 | Bil 15.591 | 86.2 |

***CHANZO: Taarifa ya Wizara ya Nishati Fungu 58 kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/19.***

**HALI YA UPATIKANAJI WA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2018/2019**




**Mheshimiwa Spika,** hadi wakati Kamati inaandaa tarifa hii Wizara ilikuwa imepokea fedha kwa kiwango cha zaidi ya asilimia 70 kwa miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida. Hivyo Kamati imeridhishwa na utoaji wa fedha kwa ajili ya Wizara kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa Fedha 2018/2019.

c) **Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa Bajeti ya Mwaka 2018/19 Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Toleo la Januari, 2016 iliyoelezea majukumu ya Kamati ya kusimamia na kufuatilia utendaji kazi wa shughuli za Wizara. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa, sehemu kubwa ya ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa na baadhi bado haujafanyiwa kazi na Serikali. Maoni ambayo kamati inaamini ni muhimu lakini hayajafanyiwa kazi ni yafuatayo:-

a) Serikali iendelee kuwekeza katika vyanzo vingine vya nishati jadidifu *(renewable energy)* ambayo uzalishaji wake ni nafuu na rafiki kwa mazingira kwa mfano uzalishaji wa

umeme wa upepo katika maeneo ya Singida, Makambako na Same yenye upepo wa kutosha.

b) Serikali inapaswa kuharakisha mchakato wa majadiliano ya uwekezaji wa mradi wa *Liquefied Natural Gas (LNG)* ili kukwepa tishio la kutekwa kwa soko la biashara ya gesi na nchi nyingine.

c) Serikali iendelee kushirikisha wananchi pamoja na viongozi wao wakati wa kuainisha maeneo ya kutekeleza miradi ya REA. Kwa kufanya hivyo, maeneo mengi ya Vijiji na Vitongoji hasa yale ya kijamii yatapata huduma ya nishati hii muhimu.

d) Serikali ilipe fidia kwa wakati kwa wananchi wote wanaotoa maeneo yao kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo mfano miradi ya Gesi Asilia ya LNG mkoani Lindi, pamoja na wananchi wa Igunga waliopisha mradi wa ujenzi wa kusafirisha umeme wa kV 400 wa Singida – Arusha.

e) Serikali ihakikishe inaiendeleza kampuni yake ya *Tanzania Concrete Poles Manufacturing Company Limited (TCPM)* katika utengenezaji wa nguzo za zege kwa kuipatia mtaji. Vilevile kutoa fursa kwa kampuni ambazo zinazalisha nguzo hapa nchini ili kuharakisha matumizi ya nguzo hizo katika miradi inayoendelea hususan Miradi ya REA.

**Mheshimiwa Spika, Ni Rai ya Kamati kuwa Wizara itaendelea kufanyia kazi maoni na ushauri unaotolewa na Kamati.**

## 2.2 Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa (Fungu 58) Mwaka Wa Fedha 2019/2020

### 2.2.1. Mapitio ya Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Nishati inaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Mpango Mkakati wake. Kulingana na Mpango Mkakati huo Wizara ina malengo makuu sita (6) ambayo ni:

i) Kuongeza uzalishaji na kuboresha mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme;

ii) Kuongeza mchango wa nishati jadidifu katika matumizi mbalimbali ya nishati;

iii) Kuimarisha shughuli za utafiti na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia;

iv) Kuboresha rasilimali za Wizara ili kutoa huduma bora za nishati;

v) Kutekeleza kwa ufanisi Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Kuzuia Rushwa; na

vi) Kupunguza maambukizi ya VVU na UKIMWI sehemu za kazi na kuboresha utoaji wa huduma kwa waathirika.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na malengo hayo Wizara inapaswa kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara na Taasisi zake katika kusimamia Sekta ya Nishati, Kuendelea kuboresha mazingira ya ofisi kwa watumishi wa Wizara na Taasisi zake ili kutoa huduma bora zaidi na Kuendelea kuelimisha umma na kuboresha mawasiliano kati ya Wizara na wadau mbalimbali kuhusu masuala ya nishati.

## 2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

### 2.3.1 Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka 2019/2020, Wizara ya Nishati (Fungu 58) inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 2,142,793,309,000** ikilinganishwa na **Shilingi 1,692,286,014,000** zilizotengwa kwa Mwaka 2018/2019 sawa na ongezeko la **asilimia 26.6**. Ongezeko hilo limetokana na kuanza kutekelezwa kwa miradi mikubwa ukiwemo Mradi wa umeme wa Mto Rufiji utakaozalisha **MW 2,115**. Bajeti ya Mradi huo imeongezeka kutoka **Shilingi 700,000,000,000** kwa Mwaka 2018/2019 hadi **Shilingi 1,443,264,000,000** ambalo ni ongezeko la **asilimia 106.2**.

### 2.3.2 Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti iliyotengwa kwa mwaka 2019/20 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ni **Shilingi 2,116,454,000,000** sawa na **asilimia 98.8** ya bajeti yote ya Wizara. Bajeti ya fedha za ndani iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 1,956,372,000,000** sawa na **asilimia 92.4** ya Bajeti yote ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Fedha nyingi za ndani za miradi ya maendeleo zimeelekezwa katika miradi minne (4) ya kimkakati ambapo jumla ya **Shilingi trilioni 1.88** sawa na **asilimia 95.9** ya Bajeti yote ya ndani iliyotengwa. Miradi hiyo ni: Mradi wa Kuzalisha Umeme Mto Rufiji, MW 2,115 (**Shilingi trilioni 1.44**); Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu (**Shilingi bilioni 363.11**); Mradi wa kuzalisha Umeme wa Kinyerezi I *Extension* **MW 185** (**Shilingi bilioni 60**) na Mradi wa Ruhudji wa **MW 358** (**Shilingi bilioni 10**).

### 2.3.3 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyotengwa kwa Mwaka 2019/2020 ni **Shilingi 26,339,309,000** sawa na **asilimia 1.2** ya bajeti yote ya Wizara. Kati ya fedha hizo **Shilingi 15,025,821,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C) na **Shilingi 11,313,488,000** zitatumika kwa ajili ya kulipa mishahara (P.E) ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

**Jedwali Na. 1:** Muhtasari wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2019/2020

| A: FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA | | |
|---|---|---|
| MAELEZO | BAJETI | ASILIMIA (%) YA BAJETI YOTE |
| Mishahara (P.E) | 11,313,488,000 | |
| Matumizi Mengineyo (O.C) | 15,025,821,000 | |
| **Jumla Fedha za Matumizi ya Kawaida** | **26,339,309,000** | **1.2%** |
| **B: FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO** | | |
| Fedha za Ndani | 1,956,372,000,000 | |
| Fedha za Nje | 160,082,000,000 | |
| **Jumla Fedha Za Maendeleo** | **2,116,454,000,000** | **98.8%** |
| **JUMLA KUU** | **2,142,793,309,000** | **100%** |

**Chanzo;** Maelezo ya Randama kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2019/2020

Aidha, Makisio ya makusanyo ya maduhuli kwa Mwaka 2019/2020 ni **Shilingi 602,059,798,000,** ambalo ni ongezeko la **asilimia 52.6** ikilinganishwa na **Shilingi 394,450,860,600** lililokuwa lengo la Mwaka 2018/2019. Kati ya makusanyo hayo, jumla ya **Shilingi 602,047,796,000** zitakusanywa kupitia shughuli za Mafuta na Gesi Asilia na **Shilingi 12,002,000** zitakusanywa kupitia shughuli za utawala.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kutekeleza majukumu yake ya kikanuni ambayo ni ukaguzi wa miradi ya maendeleo na uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa fedha 2018/2019 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa fedha 2019/2020, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao: -

### 1. Utoaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo

Katika kutekeleza miradi mikubwa na ya kimkakati ni muhimu Serikali kuhakikisha kwamba utekelezaji wa miradi hiyo hausimami kwa sababu za ukosefu wa fedha. **Hivyo, kamati inasisitiza na kuishauri Serikali juu ya umuhimu wa kujipanga kikamilifu na kuhakikisha kuwa inapeleka Fedha za ujenzi na uendelezaji wa miradi kwa wakati kama zilivyotengwa na kuidhinishwa na Bunge.**

### 2. Ajira kwa watumishi na Kuthibitishwa Kazini kwa watendaji wanaokaimu nafasi mbalimbali

Watendaji wengi katika Wizara na Taasisi zake wamekuwa wakikaimu nafasi walizonazo kwa muda mrefu sasa hali ambayo inasababisha watendaji hao kutotekeleza majukumu yao ipasavyo kwa kuwa hawana mamlaka kamili. Aidha, baadhi ya Taasisi zimechukua watumishi kutoka Wizarani na kusababisha uhaba wa watumishi katika nafasi mbalimbali. Hivyo ni ushauri wa Kamati kuwa Wizara

iwathibitishe watendaji wanaokaimu ambao wamekidhi vigezo na sifa stahiki ili kuchochea ari kwa watumishi hao na hatimaye kuleta tija na ufanisi katika utendaji wa shughuli zao. Aidha, Serikali iharakishe kuajiri watumishi katika kada mbalimbali za utumishi ili kuongeza kasi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

**3. Utoaji fursa kwa wawekezaji binafsi**

Kama nchi ni muhimu kuwa na vyanzo mchanganyiko na vyenye uhakika vya kuzalisha nishati na vilevile kuwa na mpango mkakati ambao utaweka utaratibu mzuri na rahisi kwa wawekezaji binafsi kuwekeza kwenye baadhi ya vyanzo hivyo. Hivyobasi, Kamati inaishauri Serikali kujipanga kimkakati ili kutoa fursa kwa wawekezaji binafsi kuendeleza sekta ya nishati kwa kuzalisha umeme katika baadhi ya vyanzo.

**4. Upatikanaji wa vifaa vya kutekeleza miradi ya umeme hususan REA na malipo ya wakandarasi**

Vifaa vya usambazaji umeme vimekuwa havipatikani kwa wakati katika baadhi ya maeneo, mfano; nguzo, nyaya na hivyo kusababisha zoezi la usambazaji umeme kusuasua. Kamati inaishauri serikali kuhakikisha kuwa vifaa vya kutekeleza miradi ya REA vinapatikana wakati wote pamoja na kuwalipa wakandarasi fedha kwa wakati ili waweze kukamilisha utekelezaji wa miradi kwa mujibu wa mikataba.

**5. Kasi ya usambazaji wa umeme wa vijijini (REA)**

Kasi ya usambazaji wa umeme iongezeke ili iendane na matarajio ya wananchi na hivyo kufikia malengo yake ili wananchi wengi wanufaike na huduma ya umeme. Kamati inaishauri Serikali kumaliza changamoto zinazosababisha usambazaji wa umeme kusuasua na hatimaye kuongeza kasi na ufanisi katika usambazaji wa umeme ili kuweza kufikia malengo ya miradi ya REA na vilevile kamati inaona ipo haja ya wakandarasi kusimamiwa kwa karibu zaidi.

**6. Miundombinu ya mradi wa umeme wa Mto Rufiji**
Miundombinu wezeshi ya mradi wa umeme wa mto Rufiji hasa barabara, madaraja na makalavati ni vema ikawa imara na ya kudumu na kuweza kupitika wakati wote ili kuhakikisha kuwa ujenzi wa mradi utakapoanza hauchelewi kwa sababu ya miundombinu mibovu.

**7. Wigo wa Utekelezaji wa Miradi ya umeme vijijini (REA)**
Wakandarasi wanaotekeleza miradi ya REA wamekuwa wakipewa maeneo madogo (wigo) kuliko uhalisia kutokana na kutofanyika kwa upembuzi yakinikifu sahihi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia TANESCO ifanye upembuzi yakinifu na kwa usahihi kujua ukubwa wa Kijiji kabla ya kumkabidhi mkandarasi ili kuepuka kumpa mkandarasi eneo dogo kuliko ukubwa halisi wa kijiji au eneo husika.

**8. Bei ya kuunganishwa na huduma ya umeme vijijini**

Kamati inatambua kuwa Serikali kupitia TANESCO imeweka utaratibu wa kuunganisha umeme vijijini kupitia mradi wa REA au TANESCO kwa gharama ya **shilingi 27,000** lakini bado suala hilo limekuwa gumu kutekelezeka kwa baadhi ya watendaji katika maeneo ya Miji na Vijiji. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali isimamie kikamilifu zoezi hili pamoja na kuweka utaratibu mahususi utakaoelezea gharama za kuunganisha umeme vijijini.

**9. Gharama za uunganishwaji umeme Mijini**

Gharama za kuunganisha umeme Mijini bado ni kubwa na hivyo wananchi wengi kushindwa kuunganishwa na huduma ya umeme, Kamati inaona kuwa ni vema sasa TANESCO ikaangalia namna nzuri ya kupunguza gharama hizo ili kupata wateja wengi na kuongeza mapato zaidi.

**10. Uwezeshwaji wa Wakala wa udhibiti wa Mkondo wa juu wa Petroli(PURA)**
PURA ni taasisi muhimu katika udhibiti wa sekta ya Gesi Asilia katika mkondo wa juu. Licha ya kwamba taasisi hiyo ina zaidi ya miaka miwili tangu kuanzishwa kwake lakini hadi sasa

haina rasilimali watu wa kutosha katika maeneo muhimu, haina bajeti ya kutosha wala haina hata uwezo wa kuhifadhi takwimu za masuala ya gesi ingawa inasimamia kampuni za kimataifa zenye teknolojia ya hali juu na rasilimali watu wenye weledi mkubwa. Ili nchi iweze kunufaika ipasavyo na Gesi ni lazima taasisi hii iweze kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa. **Hivyo, kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa inaiwezesha Wakala wa udhibiti wa mkondo wa juu wa Petroli (PURA) kifedha, kiteknolojia na katika rasilimali watu ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.**

**11. Deni la Kampuni ya Mafuta (TPDC)**

Kwa kuwa mkopo wa ujenzi wa bomba la gesi kutoka Mtwara hadi Dar Es Salaam utalipwa na Serikali ingawa bado mkopo huo unasomeka kwenye vitabu vya TPDC na hivyo kufanya TPDC kuonekana na madeni makubwa na kushindwa kukopesheka. Ni ushauri wa Kamati kwamba mkopo huo sasa uondolewe kwenye vitabu vya TPDC ili iweze kukopesheka na kuwekeza katika miradi ya maendeleo na ya kimkakati.

**12. Mfumo wa gawio la mapato yatokanayo na Mafuta na Gesi Asilia**

Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi ya mwaka 2015, imeweka utaratibu wa mfumo wa GDP ili kuweza kuipatia TPDC fedha za kuwekeza katika sekta ya gesi. Kamati inaamini kuwa itachukua muda mrefu kwa sekta ndogo ya Gesi Asilia kuchangia pato la taifa kwa asilimia 3. Pamoja na kuzingatia kifungu cha 16(5) na (6) cha Sheria hiyo kinachoelekeza jinsi ya kufanya marekebisho katika Sheria hii; Kamati inaona upo umuhimu wa Sheria hiyo kuangaliwa upya ili pamoja na mambo mengine ibadili mfumo wa kuigawia TPDC fedha za mfuko wa Gesi Asilia na Mafuta kwa kutegemea uchangiaji wa pato la taifa (GDP) kwa asilimia 3.

**13. Serikali kuzingatia maoni ya Kamati Maalum ya Bunge kuhusu Ushauri katika Sekta ndogo ya Gesi Asilia**

Mbali ya kwamba Sheria ya Petroli, Sura ya 392 ilianza kutumika mwaka 2015 na sasa ni zaidi ya miaka 4 na pia Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika

Mikataba ya Maliasili za Nchi ya mwaka 2017 na Sheria ya Mamlaka ya Nchi kuhusu Umiliki wa Maliasili ya mwaka 2017 zimeanza kutumika tangu mwezi Julai 2017 hadi sasa yapata miaka 2 Serikali ndiyo inafanya mapitio ya mikataba ili kubaini masharti yenye kasoro katika PSAs hizo ili kuendana na masharti na matakwa ya Sheria hizo. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mapitio ya mikataba hiyo. Aidha, ni rai ya Kamati kuwa Serikali itaendelea kutekeleza maoni, ushauri na mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati Maalum ya Bunge iliyoundwa na Mhe. Spika kuhusu sekta ndogo ya gesi.

**14. Utekelezaji wa mradi wa maghala ya kuhifadhia mafuta**

Kwakuwa mradi wa uhifadhi wa mafuta nchini unaratibiwa na Kampuni ya Taifa ya mafuta nchini (TPDC) na jukumu hilo lipo chini ya kifungu cha 182(1) cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392 ambapo Mradi huu unahusisha ujenzi wa maghala ya mafuta katika maeneo ya kimkakati pembezoni mwa Bahari ya Hindi na katikati ya nchi ili kurahisisha upatikanaji wa bidhaa ya mafuta. Ni Rai ya Kamati kuwa Serikali iiwezeshe TPDC kutekeleza mradi huu kwa wakati na kuipatia Fedha kwani mradi wa kuwa na maghala ya kuhifadhia mafuta (Strategic Oil Tank Reserves) una manufaa makubwa kwa Taifa.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge, kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge hili Tukufu. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza wajibu huu mkubwa tuliowakabidhi.

Aidha, Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa Waziri wa Nishati Mhe. Dkt Medard Matogolo Kalemani, (Mb), Mhe. Subira Khamis Mgalu, (Mb)- Naibu Waziri wa Nishati pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo

wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Hamisi Mwinyimvua kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati yetu wakati wote.

Kwa namna ya pekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa weledi na umahiri waliouonesha wakati wote wa kutekeleza majukumu ya kamati. Kwa heshima kubwa naomba majina yao katika orodha ifuatayo yaingizwe kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge:-

1. Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb - **MWENYEKITI**
2. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb – **M/MWENYEKITI**
3. Mhe. Hamida Mohamed Abdallah, Mb
4. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb
5. Mhe. Hamoud Abuu Jumaa, Mb
6. Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb
7. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb
8. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb
9. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb
10. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb
11. Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb
12. Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mb
13. Mhe. Kiza Hussein Mayeye, Mb
14. Mhe. Mohamed Juma Khatib, Mb
15. Mhe. Bahati Ali Abeid, Mb
16. Mhe. Msukuma Joseph Kasheku, Mb
17. Mhe. Ajari Rashid Akbar, Mb
18. Mhe. Yosepher Ferdinandi Komba, Mb
19. Mhe. James Kinyasi Millya, Mb
20. Mhe. Lameck Okambo Airo, Mb
21. Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb
22. Mhe. Zubeda Hassan Sakuru, Mb
23. Mhe Ally Mohamed Keissy, Mb
24. Mhe. John Wegesa Heche, Mb
25. Mhe. Frank George Mwakajoka, Mb
26. Mhe. Abdallah Ally Mtolea, Mb

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi, Ndg.

Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Ndg. Ndg. Felister Mgonja na Ndg. Omary Magwinza kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema haya sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya **Fungu 58** Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ambayo ni **Shilingi 2,142,793,309,000.**

**Mheshimiwa Spika,** naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Dunstan Luka Kitandula, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**
28 Mei, 2019

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dustan Kitandula Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini kwa taarifa hiyo kuhusiana na masuala ya Nishati.

Sasa namkaribisha Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Nishati, Mheshimiwa John Mnyika, karibu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge naomba kuwasilisha hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu mapitio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha katika Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunijalia uhai na kunipa nguvu na uwezo wa kusimama mbele

ya Bunge lako Tukufu ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kuwashukuru na kuwapongeza sana Wabunge wote wa Upinzani na viongozi wote wa CHADEMA kwa ujasiri wao wa kuendelea kuchapa kazi bila woga licha ya mazingira magumu ya kufanya siasa hapa nchini. Aidha, nawatia moyo wote waliokamatwa na kuwekwa kizuizini magerezani; walioumizwa na kujeruhiwa kwa sababu tu ya kutumia haki yao ya kikatiba ya kushiriki shughuli za kisiasa. Napenda kuwaambia wasikate tamaa kwani mateso wanayoyapata ni kielelezo cha ukombozi wa Watanzania walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upekee kabisa napenda kuwashukuru Wabunge na wadau mbalimbali ambao kwa namna moja au nyingine wamenisaidia katika kufanikisha hotuba hii, siwezi kuwataja wote lakini naomba kuwatambua na kuthamini mchango wa HakiRasiliamali, Asasi mbalimbali ndani na nje ya nchi, wadau mbalimbali kwa nafasi zenu pamoja na wanataaluma mbalimbali mlionipatia michango yenu, natambua haya yote ni kwa maslahi mapana ya Taifa na uzalendo wenu kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru Naibu Waziri Kivuli wa Nishati Mheshimiwa Jesca Kishoa kwa ushirikiano wake katika maandalizi ya hotuba hii na majukumu mengine ya Wizara yetu ya Nishati. Kwa wote ambao sitawataja kwa majina lakini nyuma ya pazia mmekuwa nguzo yetu Nasema ahsanteni na Mwenyezi Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni bajeti ya nne ya Serikali hii ya Awamu ya Tano ambapo imebaki bajeti moja tu ya mwaka wa fedha 2020/2021. Hata hivyo katika utaratibu wa mzunguko wa Bajeti za Serikali, Bajeti hii ni ya mwisho kwa Serikali hii ya Awamu ya Tano chini ya Chama cha Mapinduzi kwa kuwa awamu ijayo itakuwa chini ya Vyama Vya Upinzani

vikiongozwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). Hata hivyo, pamoja na kwamba imebaki bajeti ya takriban miaka miwili Serikali hii imalize muhula wake wa miaka mitano madarakani utekelezaji wa bajeti zilizotangulia umekuwa ni wa kusuasua jambo ambalo limeathiri sana Sekta ya Nishati, hadi sasa hakuna mradi wowote mpya uliokamilika kupunguza au kuhakikisha Tanzania kuna umeme wa uhakika katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mara zote Serikali imeonesha kushindwa katika Sera zake, Sera Mbadala za CHADEMA ni kuhakikisha kunakuwepo na uzalishaji wa nishati ya uhakika na endelevu, kuwepo na umakini na weledi katika usambazaji nishati na matumizi endelevu ya nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera za CHADEMA zinatokana na ukweli kwamba CHADEMA tunatambua kuwa nishati ni muhimu kwa ajili ya maisha bora kwa wananchi na kwamba nishati ni nyenzo muhimu ya uzalishaji katika sekta mbalimbali za uchumi. Kwa hiyo, ni muhimu kuhakikisha uwepo wa nishati ya uhakika kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. CHADEMA inatambua kwamba Tanzania imejaliwa vyanzo vingi vya nishati ikiwa ni pamoja na umeme wa biomasi, gesi asilia, makaa ya mawe, nishati jadidifu kama jotoardhi, upepo na jua na vyanzo vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza na sekta ya umeme nitaomba hotuba hii kwa ukamilifu wake iingie katika Kumbukumbu za Bunge; na kwa umuhimu wa pekee naomba nianze na Hitimisho la hotuba hii, kama sehemu ya Utangulizi wa hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima Serikali izingatie mgawanyo wa rasilimali fedha kwa sekta mbalimbali nchini, kwa sababu kulundika rasilimali nyingi kwenye miradi michache kunaweza kusababisha kudumaa kwa miradi mingine ya maendeleo kutakakosababishwa na mgawanyo wa raslimali. Ulundikwaji wa rasilimali fedha kwenye miradi michache kunadhihirika katika makadirio ya bajeti ya mwaka 2019/2020 katika Wizara ya Nishati ikijumlisha na Wizara ya

Ujenzi ambazo kwa Wizara hizi mbili peke yke zinachukua zaidi ya asilimia 50 ya bajeti yote ya maendeleo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali kama hii ya kulundikwa kwa fedha nyingi kwenye Wizara hii, ili Bunge lako Tukufu liweze kuisimamia ipasavyo Serikali, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka mambo matano yafuatayo:-

i. Mikataba yote mikubwa inayohusu ujenzi wa mradi wa umeme wa Rufiji *(Stiegler's Gorge),* iletwe Bungeni na kujadiliwa na Bunge. *(Makofi)*

ii. Tathmini ya kimazingira na upembuzi yakinifu kuhusu mradi tajwa iletwe na kujadiliwa na Bunge. *(Makofi)*

iii. Mikataba yote mikubwa kuhusu ujenzi wa bomba kutoka Mtwara mpaka Dar-es-Salaam iwasilishwe na kupitiwa na Bunge.

iv. Serikali iwasilishe Bungeni Taarifa ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati ya Bunge iliyoundwa na Spika wa wakati huo, Mheshimiwa Anna Makinda, kuchunguza kuhusu mgogoro wa gesi kati ya Serikali na Wananchi wa Mtwara juu ya ujenzi wa bomba la gesi. *(Makofi)*

v. Serikali iwasilishe Bungeni Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Kamati iliyoundwa na Spika wa sasa, Mheshimiwa Job Ndugai, kuhusu kuchunguza mikataba ya utafutaji na uvunaji wa gesi asilia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, naomba utulie kidogo.

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tuongozwe kama ameanza mwisho atusaidie ni *page* gani kutoka huko mwisho? Kwa sababu tumepotea kabisa, tunashindwa kufuatilia kwenye hotuba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika anasoma mwisho kabisa, ameamua kusoma mwisho.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna shida...

**MWENYEKITI:** A'aaa', Mheshimiwa Ester Bulaya sijakuruhusu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA – MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru umemuelimisha Mheshimiwa Waziri kwamba, aende kwenye aya ya 163, Ukurasa wa 52, halafu asipoteze muda wangu wa kusoma hotuba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ndogo ya umeme; Shirika la Umeme Nchini *(TANESCO)* na Mwenendo Usioridhisha wa Kifedha. Kwa miaka kadhaa *TANESCO* imekuwa na mwenendo usioridhisha wa kupata hasara mfululizo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 hasara iliyopatikana ilikuwa shilingi bilioni 346.40 na kwa hesabu za miezi 18 hadi Mwaka wa Fedha ulioishia Juni, 2015 hasara ilikuwa shilingi bilioni 124.446, na hadi kufikia mwaka 2018 hasara ilikuwa shilingi bilioni 346. Mwenendo wa hasara umekuwa ukichangiwa na hali isiyoridhisha ya maji ya kuzalisha nguvu ya umeme pamoja na ongezeko la gharama za uzalishaji. Mfulilizo wa gharama hizi una athari kubwa

kwenye mtaji wa shirika, hivyo kufanya kutokopesheka, ili kukidhi mahitaji yake ya kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hesabu zilizoishia tarehe 30 Juni, 2016 madai yameongezeka kwa asilimia 23 hadi shilingi bilioni 958 kutoka shilingi bilioni 738 zilizoripotiwa kwenye hesabu zilizoishia tarehe 30 Juni, 2015. Kwa upande mwingine thamani ya wadaiwa ilipungua hadi shilingi bilioni 330.55 kwa hesabu zilizoishia...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika unavyosoma uwaambie Wabunge wajue unatoka wapi unakwenda wapi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Si anasoma taarifa, lakini anaenda mbele akirudi nyuma awaambie watu, Mheshimiwa Mnyika naomba uwaelekeze Wabunge.

**MHE. JOHN J. MNYIKA – MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ninayoyasoma yote yako ndani ya kitabu, kama kuna mtu atasema hayapo kwenye ukurasa gani asimame aombe kuhusu utaratibu, lakini naomba niendelee kusoma.

**MWENYEKITI:** Uwe unaelekeza basi tujue kwa sabab, hata na mimi nashindwa kujua unasoma ukurasa gani.

**MHE. JOHN J. MNYIKA – MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hakuwa anatuelekeza kwenye hotuba yake alikuwa anasoma ukurasa gani. Naomba kama ulivyomuachia Waziri uniachie nisome, kama kuna jambo liko nje ya ukurasa useme niseme kwamba, jambo liko nje ya ukurasa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, subiri, subirini.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Subiri, hebu subirini, subirini nizungumze; Mheshimiwa Waziri wakati anasoma alikuwaanakwenda na kuruka. Tulikuwa tunakwenda anaelewa anachosoma, yeye ameanza mwisho anakuja mwanzo kwa hiyo, atuelekeze...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA – MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba muda wangu utunze tafadhali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika naomba utuelekeze unavyosoma kurasa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA – MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu utunzwe. Nakwenda Ukurasa wa 10, Aya ya 26, Uunganishaji wa Umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalmiko makubwa ya gharama za uunganishaji wa huduma za umeme pamoja na mlolongo wa uunganishaji wateja ambao tayari wamekamilisha taratibu za kuunganishiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiachana nagharama za kuunganisha umeme bado kumekuwa na usumbufu wa uunganishaji wa wateja kwa wakati kwa visingizio mbalimbali wakati ambapo wateja wa umeme huwa wameshakamilisha malipo na kufuata taratibu za kuunganisha huduma hiyo. Kutokana na malalamiko hayo kwa mujibu wa ripoti ya Benki ya Dunia kuhusu kufanya biashara Tanzania mwaka 2019 *(Doing Business 2019)* Tanzania imeshika nafasi ya 83 kati ya nchi 190 duniani katika viwango vya wateja kuunganisha umeme *(Getting Electricity).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya mteja kupewa makadirio ya umeme gharama za uunganishaji mteja hutakiwa kufanya malipo kwa awamu iwapo ataomba kwa kuingia mkataba na *TANESCO* kwa kulipa gharama kwa awamu. Na ikiwa *TANESCO* itashindwa kumuunganisha mteja kwa muda uliotakiwa itawajibika kumuarifu mteja mapema; lakini kumekuwa na malalmiko makubwa ya watumiaji wa umeme juu ya kushindwa kwa *TANESCO* kufuata taratibu zilizowekwa. Aidha, kwa maeneo ya vijijini ambapo huduma za uunganishaji wa umeme zinafanywa chini ya *REA* kumekuwa na malalamiko ya mazingira ya uunganishaji wa huduma za umeme ambapo wananchi mbalimbali wamelalamikia kuhusu wenye uwezo na rushwa ndio ambao wanapewa kipaumbele katika kuunganishiwa huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa kushindwa kwa shirika la umeme nchini katika kuwasambazia na kuunganishia wananchi huduma ya umeme ni kutokana na kuelemewa kwa shirika hilo katika utoaji wa huduma hiyo. Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kuwepo kwa soko huria kwa wasambazaji wa huduma ya umeme, ili kupunguza urasimu wa uunganishaji na hivyo kulipa faida shirika hilo ambalo sasa linakosamapato kutokana na kuelemewa kuunganishia wateja wapya huduma ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sehemu yote ya kuhusu kiwango cha kaya zilizounganishiwa umeme iingie kwenye Kumbukumbu za Bunge kwa sababu ya muda ambao umepotezwa. Sasa naelekea kwenye Mradi wa Kuzalisha Umeme; Ujenzi wa Mradi wa Umeme wa *Rufiji Hydro Project.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa za Serikali lengo la kutekeleza mradi huu ni kuzalisha umeme wa jumla ya megawati 2,115 kwa kutumia *Hydro Power* kwa maana ya nguvu ya maji katika Bonde la Mto Rufiji ambapo Serikali inadai utekelezaji wa mradi huu utakuwa ni kichocheo muhimu katika kuiwezesha Tanzania kufikia azma ya kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025. Pamoja na kukubaliana na dhana ya kuzalisha umeme wa megawati

2,100 Kambi Rasmi ya Upinzani haikubaliani na namna utekelezaji wa ujenzi wa Mradi wa *Rufiji Hydro Power Project* unavyofanyika kwenye eneo la mradi lililoteuliwa na Serikali hivi sasa kwa sababu mbalimbali ambazo nitazieleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gharama za Kiuchumi za Ujenzi wa Mradi Huu kwa Wakati Mmoja. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pekee Serikali kupitia Hotuba ya Waziri wa Nishati alieleza mpango wa Serikali wa kujenga mradi huu katika aya ya 22 na aya ya 23 ya hotuba yake. Katika aya ya 23 Mheshimiwa Waziri wa Nishati alisema katika kipindi cha mwaka 2018/2019 Serikali itaendelea kutekeleza mradi huu na shughuli zitakazofanyika ni pamoja na, mosi ujenzi wa kambi na ofisi za wafanyakazi, pili ujenzi wa bwawa *(main dam* na *sleep ways)* na tatu ujenzi wa njia kuu za kupitisha maji *(tunnels).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilisema fedha za ndani shilingi bilioni 700 zimetengwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa kazi hiyo; na kwamba, utekelezaji wa shughuli za ujenzi wa mradi ulitarajiwa kuanza Julai, 2018 na sio Julai, 2019 kama tunavyoelezwa sasa; na kwamba inaelezwa utekelezaji huo ungekamilika katika kipindi cha miezi 36. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma taarifa ya Wizara kuhusu Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Kipindi cha Mwaka 2018/2019 Waziri anasema, na ninamnukuu, *"Wizara ya Fedha na Mipango imetenga cash jumla ya shilingi bilioni 984 ambazo taratibu za malipo zinaendelea, ili zilipwe kwa mkandarasi wa Mradi wa Rufiji kabla ya mwisho wa mwezi Aprili, kama malipo ya* awali *(advance payment) katika mradi huo."* Kwa maneno mengine ni kwamba, sasa Serikali ilipanga kulipa fedha kwa ongzeko la shilingi bilioni 284 bila idhini ya Bunge lako Tukufu kwa kazi zilezile. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuliambia Bunge hili bilioni 284 zinazodaiwa kulipwa mradi hu zimetoka wapi? Zimeongezeka kufanya shughuli gani? Na kwa nini Serikali haikufuata matakwa ya makadirio na matumizi ya nyongeza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pili, Muda na Ongezeko la Gharama Halisi za Ujenzi wa Mradi wa Bonde la Mto Rufiji. Kwa mujibu wa Mkakati wa Muongozo wa Mabadiliko ya Sekta ya Usambazaji wa Umeme Nchini wa Mwaka 2014 Mpaka 2025 *(Electricity Supply Industry Reform Strategy Road Map)* uwezo wa kuzalisha umeme unatakiwa kuongezeka kutoka megawati 1,583 mwaka 2014 mpaka kufikia megawati 10,000 mwaka 2025 ili kuwezesha nchi kufikia uchumi wa kati sambamba na Dira ya Maendeleo ya Taifa *(Vision 2025).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu wa Umeme wa Mto Rufiji tunaambiwa na Serikali kuwa utakamilika ndani ya kipindi cha miezi 36, sawa na miaka mitatu kuanzia sasa, yaani kuanzia mwaka jana, na utaweza kuzalisha megawati 2,100 kiasi ambacho ni asilimia 21 ya lengo la kufikia kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati. Wakati ujenzi unakamilika ndani ya miezi 36, hata kama ukikamilika kama tunavyoaminishwa na Serikali, itakuwa imesalia miaka miwili tu kufikia mwaka 2025, hivyo shabaha ya kufikisha uzalishaji wa megawati elfu 10 ifikapo mwaka 2025 bado ni ndoto za mchana ambazo Serikali hii itaendelea kuota. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo uchanbuzi wa gharama za Mradi wa Maji wa Mto Rufiji zilizofanywa na *ODEBRECHT* mwaka 2012, na iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini mwaka 2016 walikadiria kuwa mradi utajengwa kwa vipindi vya miaka tisa, awamu ya kwanza miaka tisa na miaka mitatu kwa awamu ya pili. Hii inafanya idadi ya muda wa ujenzi kuongezeka kutoka miezi 36 ya awali hadi miaka 12 ambayo ni sawa na miezi 144. Katika uchambuzi huo wa gharama za ujenzi wa Mradi wa Mto Rufiji miwezi 36 ambayo imeripotiwa na Serikali haitawezekana kuumaliza mradi huo, hivyo kuufanya kuwa moja ya miradi mikubwa nchini itakayoigharimu nchi kiwango kikubwa cha fedha za walipa kodi kwa kuwa, gharama za mwisho za mradi huu zitakuwa kubwa kulikoni gharama zilizoainishwa wakati wa mradi kuanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi huo kunakadiriwa kuwa aina ya miradi mikubwa kama huu

gharama za mradi zinakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 30, yaani *cost overruns* tangu hatua za ujenzi kuanza mpaka kumalizika. Mwaka 2016 gharama za awali za mradi zilikadiriwa kufikia dola bilioni 3.738 sawa na shilingi trilioni 7.5. Endapo gharama za ujenzi wa mradi zitaongezeka, *(cost overruns)* kwa asilimia 30 basi gharaa za Mradi wa Umeme wa Mto Rufiji zitaongezeka mpaka kufikia Dola za Marekani bilioni 9.852 ifikapo mwaka 2027, kwa makadirio ya mwaka 2016 kiasi ambacho kama *exchange rate* ya mwaka 2019 ikitumika, yaani shilingi 2,330, basi kiasi hicho kitakuwa sawa na shilingi trilioni 22.95. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchambuzi huu uliofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani basi Mradi huu wa Umeme wa Mto Rufiji utakuwa ni aina nyingine ya maamuzi yanayoenda kuiweka nchi katika hali mbaya ya kifedha, na itakuwa ni hatua kubwa sana ya Serikali ya Awamu ya Tano kuhujumu uchumi wa nchi kwa kuzingatia kuwa mradi unatekelezwa na mkandarasi kutoka nje kwa fedha za ndani na hivyo, sehemu kubwa ya malipo itaondoka kutoka mzunguko wetu wa ndani wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nitoe wito tu kwa Serikali hii ya Awamu ya Tano kufikiria upya na kutupa majibu ya namna gani wanajipanga na ugharamiaji wa gharama zinazokadiriwa kuongezeka katika ujenzi wa mradi huu kwa kuwa umeshaanza kutekelezwa. Hatutaki ije Serikali ya Awamu ya Sita kwa vyovyote itakavyokuwa iwe ni Serikali inayoongozwa na CHADEMA ama chama kingine chochote ilazimike kufanya maamuzi tofauti wakati nchi ikiwa tayari imeshaathirika kufuatia upungufu wa kiutendaji katika Serikali ya Awamu ya Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera za Uchumi za Serikali ya Chama Cha Mapinduzi hazieleweki kabisa. Awali Mradi wa Umeme wa Stiegler's uliasisiwa tangu enzi za Mwalimu Nyerere na haukutekelezwa kutokana na sababu za kimazingira. Na mpango wa *Tanzania Power System Master Plan* wa mwaka 2016, *update,* umeonesha mradi huo kuwa ni chaguo la mwisho endapo miradi mingine mikubwa ikiwa

imeshatekelezwa na mahitaji ya ziada ya umeme bado yangeibuka katika nchi yetu. Katika mpango huo imetajwa miradi mbalimbali ya maji ambayo ingepaswa kuanza kutekelezwa na pia, imetajwa pia miradi ya gesi ambayo ingetekelezwa sanjari na miradi mipya ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu kuingia madarakani kwa Serikali hii ya Awamu ya Tano hakuna anayezungumzia tena kwa kina miradi mingine ya muda mrefu zaidi ya umeme wa maji wala miradi ya umeme wa gesi asilia na sasa tunaambiwa kipaumbele kikuu ni *Stieglers, Stiegler's, Stiegler's.* Tunaomba kufahamu zipi hasa sababu za Serikali kuacha miradi ya kuzalisha umeme ambayo ilikuwa tayari katika mkondo wa utekelezaji na kuanza mradi mmoja mkubwa mpya ambao haina uwezo wa kuutekeleza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya Ufisadi Katika Ujenzi wa Mtandao wa Usambazaji wa Umeme kwa Ajili ya Mradi wa Umeme Mtwara. Kambi Rasmi ya Upinzani ina taarifa ya madai ya ufisadi ambao inaelekezwa kuwa ulifanyika wakati wa ujenzi wa mtandao wa usambazaji wa umeme Mtwara *(MAP)* yaliyosababisha kampuni ya Wentworth *Gas Limited* pamoja na kampuni zake kufanya kazi zake bila kuzingatia masharti ya mikataba ya *Tarrif Equalisation Fund* na *MICRA,* na pia ukafanyika ununuzi wa mitambo ya umeme bila kumshirikisha Mthamini Mkuu wa Serikali. Ilipendekezwa kwamba, Serikali ilipaswa kurejeshewa kutoka kwa Kampuni ya Wentworth *Gas Limited* na Kampuni tanzu ya *Umoja Light Company Limited* kiasi cha Dola za Kimarekani bilioni 8.426 ambazo ni mabilioni ya shilingi za kitanzania, lakini hadi sasa hakuna taarifa kama kiasi hicho cha fedha kimerejeshwa kama ilivyoshauriwa na ni hatua gani za kiuwajibikaji zimechukuliwa kwa wote waliohusika na ufisadi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahamia kwenye Wakala wa Nishati Vijijini – *REA.* Wakala wa Nishati ya Vijijini ulianzishwa kwa Sheria ya Nishati Vijijini Namba 8 ya Mwaka 2005 na kuanza rasmi mwezi Oktoba, 2007 ikiwa ni sehemu ya utekelzaji wa Sera ya Taifa ya Nishati. Lengo la uanzishaji wa

*REA* lilikuwa ni kuwapatia Wananchi waishio vijijini nishati bora. Pamoja na umuhimu wa wakala huu bado Serikali haijaonesha kwa vitendo kuwa ina nia ya kusaidia wakala huyu, ili aweze kutimiza majukumu yake kikamilifu na hasa linapokuja suala la kuupatia fedha kama zilivyoombwa na zilivyopitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa Serikali imekuwa haitimizi wajibu wake wa kuipatia *REA* fedha kama zilivyotengwa na Bunge, hata fedha ambazo zimewekewa wigo na Bunge, yaani kuwa *ring fenced.* Kambi Rasmi ya Upinzai imechambua hayo kwa takwimu, lakini nijielekeze kwenye Aya ya 80 kwamba, pamoja na fedha zinazotolewa, pamoja na kuhakikisha kuwa fedha zinapokelewa kwa kuzingatia bajeti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe maelezo ni baada ya muda gani uwekezaji unaofanywa na *REA* utaanza kurudisha mtaji uliowekezwa huko *(Return On Investiment).* Kwa kuwa yamekuwepo matukio kadhaa ya nchi yetu Serikali kuwekeza kwenye miradi yenye kuingiza hasara, mingine uwekezaji ukifanyika bila hata ya kuwepo kwa mchanganuo wa kibiashara kama ilivyo kwa ununuzi wa ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji wa *REA, (Final Report Mid Term Review of the Capacity Development Project of The Rural Energy Agency Tanzania)* iliyotolewa na *Swidish International Development Cooperation Agency (SIDA),* inaonesha kuwa kati ya miradi yote inayotekelezwa na *REA* miradi 234 sawa na asilimia 72.9 inatekelezwa na *TANESCO* ikiwa na gharama ya shilingi bilioni 289 na miradi 87 sawa na asilimia 27.1 inatekelezwa na wakandarasi wengine. Kati ya fedha hizo *TANESCO* ilipatiwa asilimia 89, wakandarasi wengine walipatiwa asilimia mbili tu ya kile walichotakiwa kupatiwa; hii inaonesha kuwa fedha nyingi zinazotengwa kwa *REA* zinapelekwa kutekeleza miradi inayotekelezwa na *TANESCO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia miradi mingi ya *REA* inayotekelezwa na *TANESCO* ni ile ya *grid electrification* ya kutekeleza Mpango Kabambe wa Usambazaji Umeme

Vijijini *(Turnkey Operation Projects).* Miradi mingine inayohusu nishati ya umeme inayotokana na jua, upepo, maji katika maporomoko madogo madogo na na kadhalika *(solar, wind, biogas, small hydro projects)* bado miradi hiyo upatikanaji fedha kutoka *REA* unasuasua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba miradi hiyo ya nishati jadidifu *(renewable energy)* ndio inaweza kuwa mkombozi kwa mazingira yetu halisia badala ya kutegemea umeme unaozalishwa na kusambazwa na *TANESCO* peke yake.Hivyo basi ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa *REA* kuhakikisha kipaumbele wanapewa wakandarasi ambao wanahusika na uzalishaji umeme kutokana na nishati jadidifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa hiyo ni kwamba *REA* ndiyo inaiendesha *TANESCO*, fedha zote zinazokatwa kwenye mafuta na gharama za kununua umeme ili zipelekwe *REA* kwa lengo la kusambaza umeme vijijini ambapo *TANESCO* haijafika, kwa mlango wa nyuma fedha hizo zinarudishwa *TANESCO* kupitia njia ya kuwapatia kandarasi *TANESCO* ili watimize wajibu wao wa kuwapatia wananchi umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ukweli huo ni vyema *REA* ikafanyiwa tathmini upya na kuangalia inatakiwa ishughulikie miradi ya aina gani katika kutimiza majukumu yake kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wizi wa fedha za *REA* kupitia malipo ya ziada ya bilioni 97.9 yaani dola elfu 44.7.; mapitio ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali *(CAG),* taarifa ya Machi, 2017 inaonesha kwamba Wakala wa Nishati ya Umeme Vijijini *(REA)* ilifanya malipo ya ziada ya dola za Marekani 91.1 kwa *HIFAB* badala ya kulipa Dola za Marekani elfu 9.2 na hivyo kufanya malipo ya ziada ya jumla ya Dola za Marekani 81,950. Taarifa ya mwisho inaonesha kwamba jumla ya Dola za Marekani 44,725.53 hazijarejeshwa *REA. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha REA kulipa *HIFAB* fedha nyingi na za ziada kuliko kiasi kilichopaswa kulipwa ni wizi kama ulivyo wizi mwingine na ni vitendo ambavyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekuwa ikivikumbatia. Hadi sasa ulipaji huo ambao ni uhujumu wa miradi ya Taifa na uhujumu uchumi, bado fedha hizo hazijarejeshwa *REA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa dhidi ya wahujumu uchumi hawa pamoja na tambo za Serikali kuanzisha Mahakama ya Uhujumu Uchumi Nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwaambia walipakodi wa Tanzania sababu zilizosababisha *REA* wakawalipa *HIFAB* zaidi ya Dola za Marekani 81,950, wahusika ni akina nani kama siyo wizi unaofanywa na vigogo ni hatua zilizochukuliwa dhidi ya waliohusika na uhujumu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahamia ukiukwaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma na Taasisi ya *REA*. Mheshimiwa Mwenyekiti, uchunguzi uliofanywa kwenye mikataba mitatu yenye thamani ya bilioni 984.3 ulibaini kwamba, *REA* iliingia mkataba na Kampuni ya *SMEC* ambayo haikusajiliwa na Bodi ya Wakandarasi na hivyo kuleta mashaka kwa mkataba husika, pia zabuni ya kupata wakandarasi ilitangazwa kabla ya maandalizi ya nyaraka za usanifu wa mradi kukamilishwa na mshauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchunguzi huo pia ilibainika kwamba majadiliano na mapendekezo ya wazabuni kupewa kandarasi hayakufanyika vizuri. Aidha, makisio ya vifaa vilivyohitajika kutokana na *BOQ* ni vichache kuliko vilivyoorodheshwa katika mikataba yote sita iliyosainiwa na wakandarasi na jumla ya tofauti ya shilingi bilioni 99 ilikuwepo kwa mikataba yote. Aidha, vijiji 55 ambavyo vilikuwa vimeshapata umeme viliingizwa tena kwenye mikataba ili wakandarasi waitekeleze katika Mikoa ya Tanga, Mwanza, Arusha, Shinyanga na Manyara, pamoja na hayo mikataba ilikuwa na utata nani anawajibika kulipia gharama za kuingiza vifaa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiukwaji huu unafanywa katika kipindi ambacho Watanzania ambao ni walipakodi wakiaminishwa na Serikali kwamba Serikali yenyewe ni safi na kwamba iko kwa ajili ya kutetea wanyonge. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa kufahamu hatua stahiki zilizochukuliwa dhidi ya matumizi haya mabaya ya fedha za umma na madai ya ufisadi katika mikataba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda naomba niruke kuhusu takwimu za usambazaji wa umeme na mambo mengine, nihamie kwenye Sekta ndogo ya Gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inaipa *TPDC* jukumu la kuhakikisha inaendesha kibiashara shughuli za mtandao wa juu yaani utafutaji wa mafuta na gesi, mkondo wa kati, uchakataji na usafirishaji wa mafuta na gesi pamoja na mkondo wa chini yaani usambazaji wa gesi na mafuta kwa watumiaji. Kwa maana hiyo, kazi za *TPDC* ni pamoja na kusimamia shughuli za utafutaji, uendelezaji na usambazaji wa mafuta na gesi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu wa mamlaka ya *TPDC* bado inakabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo changamoto za madeni na ukusanyaji usioridhisha wa wadaiwa. Kwa taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo zinaonesha kuwa hadi kufikia Juni 30, 2018, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)* ilipata hasara ya shilingi 64,543,000,000 huku ikiwa na madeni yanayofikia shilingi 3,544,892,000,000 hivyo kuwa katika moja ya mashirika yenye hali mbaya sana ya kifedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, deni hilo limesababisha makampuni yenye mkondo wa juu kutishia kuzuia kuuza gesi asilia kwa *TPDC* kwa sababu ya kushindwa kulipia ankara zake kwa wakati hali ambayo inahatarisha upatikanaji wa umeme nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani pamoja na kusikitika juu ya hasara inayoendelea kupata shirika, inapenda kufahamu mkakati wa Serikali wa kulifanya shirika hili lisijiendeshe kwa hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati *TPDC* ikipata hasara hiyo, taarifa zinaonesha kuwa, hadi kufikia Disemba, 2018, *TPDC* ilikuwa inadai jumla ya shilingi bilioni 527. Wadaiwa sugu wakiwa ni Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO),* Kampuni ya Kuzalisha Umeme ya *SONGAS*, Kampuni ya *Ndovu Resources Limited* na Kampuni ya *Kilimanjaro Oil Limited* na wadaiwa wengine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupata majibu kutoka kwa Serikali, kuhusu mkakati wa makusudi wa kuhakikisha wadaiwa hawa sugu wanalipa madeni yake ili kuliwezesha Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kufanya shughuli zake kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji mdogo wa *TPDC* katika shughuli za maendeleo; uwekezaji kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya shirika nao unapata changamoto ya ufinyu wa bajeti, uwekezaji mdogo *TPDC* na utashi wa kisiasa. Changamoto hizi ni miongoni mwa sababu zinazokwamisha ufanisi katika kutekeleza wa mikakati inayojiwekea. Kwa mfano, mwaka 2016, Shirika la Maendeleo ya Petroli Nchini *(TPDC)* iliandaa Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asilia *(Natural Gas Utilization Master Plan).* Mpango huu uliainisha kwa kina usambazaji wa gesi asilia nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, mpango huu umekuwa ukisuasua kutekelezeka hadi leo kwa sababu ya ukosefu wa rasilimali fedha, kutokana na ukosefu wa utashi wa kisiasa, sasa usambazaji wa gesi asilia unakumbwa na changamoto wakati Taifa linaonekana linaelekeza nguvu zake katika maeneo mengine kama Mradi wa *Stiegler's* na miradi mingine. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha Mpango wa Matumizi ya Gesi Asilia nchini unatekelezwa kwa ukamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majadiliano yasiyo na kikomo; kwa kipindi kirefu sana, kupitia taarifa zinazotolewa na Wizara ya Nishati, kumekuwepo kwa majadiliano yasiyo na kikomo kwa Serikali na Wawekezaji. Hii inaathiri utekelezaji

wa mikakati ya baadhi ya shughuli za gesi asilia iliyopo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Mathalani Utekelezaji wa Mradi wa Kusindika Gesi Asilia kwenye Hali ya Kimiminika *(Liquefied Natural Gas Plant-LNG).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo majadiliano haya yasiyo na kikomo, yanasababisha ucheleweshwaji wa uwekezaji wa mitaji ya kigeni *(FDI)* ambayo ni kichocheo cha uchumi na maendeleo ya miradi mbalimbali nchini. Pia upatikanji wa *FDI* ungeisaidia Serikali kuelekeza rasilimali zaidi katika sekta zilizo na ufinyu wa bajeti hasa katika maeneo ya kimkakati ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba, Serikali ilipatie Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)* kipaumbele katika uwekezaji ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kisheria kama inavyotakiwa, ufinyu wa bajeti na uhaba katika uwekezaji kunalifanya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)* kuwa tegemezi na kushindwa kuhimili ushindani kwa kasi inayohitajika katika biashara. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Malizia, hitimisha.

**MHE. JOHN. J. MNYIKA – MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bomba la gesi kutoka Mtwara - Dar es Salaam – Tanga-Mwanza-Kagera mpaka Uganda. Bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam lilijengwa na Kampuni ya China *Petroleum and Technology Development Company (CPTDC)* kwa gharama ya takriban Dola za Kimarekani takriban bilioni 1.283 ambapo kati ya hizo, dola za Kimarekani bilioni 1.225 ni mkopo kutoka Benki ya *Exim* ya China.

Mheshimwa Mwenyekiti, kwa sasa Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* ndilo mteja mkuu wa gesi asilia; ambapo anatumia wastani wa futi za ujazo milioni 46.61 kwa siku, sawa

na 6% tu ya ujazo wa bomba; ambapo, kiasi hicho ni pungufu futi za ujazo milioni 737.89 kwa siku kulijaza bomba. Matumizi haya ni tofauti na makubaliano ya awali ambayo ilikua *TANESCO* liweze kutumia takribani futi za ujazo milioni 80 kwa siku kama ilivyokuwa kwenye makubaliano ya mkataba wa mauziano ya gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bunge inaitaka Serikali kutoa ufafanuzi ni kwa vipi bomba lililojengwa kwa gharama kubwa na Serikali linatumika kwa asilimia sita tofauti pekee na mikataba yote iliyohusiana na ujenzi wa bomba hili iweze kuwasilishwa Bungeni ili Bunge lipitie liweze kuona hasara ambayo Taifa inaipata na hatua ambayo Serikali inachukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo hayo kwa sababu umeniambia nihitimishe, nihitimishe tu kwamba kwa mazingira yote haya ndiyo maana tunaitaka Serikali izingatie mgawanyo wa rasilimali fedha kwa sekta mbalimbali nchini kwa sababu kurundika rasilimali nyingi kwenye miradi michache kunaweza kusababisha kudumaa kwa miradi mingine ya maendeleo itakayosababishwa na ufinyu wa mgawanyo wa rasilimali fedha, urundikaji wa rasilimali fedha kwenye miradi michache kunaathirika kwa makadirio ya bajeti ya mwaka 2019/2020 katika Wizara ya Nishati ikijumlisha na ujenzi zinazochukua zaidi ya asilimia 50 ya bajeti ya nchi yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, nihitimishe kwa kutaka Serikali kutekeleza mambo matano:-

Mosi; mikataba yote mikubwa inayohusu Ujenzi wa Mradi wa Umeme wa Rufiji *(Stiegler's Gorge)* iletwe na kujadiliwa na Bunge.

Pili, tathmini ya kimazingira na upembuzi yakinifu kuhusu mradi tajwa iletwe na kujadiliwa na Bunge ili kuepusha hasara kwa Taifa.

Tatu, mikataba yote mikubwa kuhusu ujenzi wa bomba kutoka Mtwara Mpaka Dar es Salaam iwasilishwe na ule ujenzi wa bomba kwenda Uganda na kupitiwa na Bunge.

Nne, Serikali iwasilishe Bungeni Taarifa ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati ya Bunge iliyoundwa na Spika wakati huo MheshimiwaAnna Makinda kuchunguza kuhusu mgogoro kati ya wananchi na Serikali Mtwara juu ya ujenzi wa bomba la gesi.

Tano, Serikali iwasilishe Bungeni Taarifa ya Utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati iliyoundwa na Spika Mheshimiwa Job Ndugai kuchunguza mikataba na utafutaji na uvunaji wa gesi asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA NISHATI, MHESHIMIWA JOHN JOHN MNYIKA (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU MAPITIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA WIZARA HIYO, KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 - KAMA ILIVYOWASILSIHWA MEZANI**

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016*

---

## A. UTANGULIZI

**1. Mheshimiwa Spika**, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunijalia uhaina kunipa nguvu na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako tukufu ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

2. **Mheshimiwa Spika,** pili napenda kuwashukuru na kuwapongeza sana Wabunge wote wa Upinzani na viongozi wote wa CHADEMA kwa ujasiri wao wa kuendelea kuchapa kazi bila woga licha ya mazingira magumu ya kufanya siasa hapa nchini. Aidha, nawatia moyo wale wote waliokamatwa na kuwekwa kizuizini magerezani; walioumizwa na kujeruhiwa kwa sababu tu ya kutumia haki yao ya kikatiba ya kushiriki shughuli za kisiasa. Napenda kuwaambia wasikate tamaa kwani mateso wanayoyapata ni kielelezo cha ukombozi wa watanzania walio wengi.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa upekee kabisa napenda kuwashukuru Wabunge na wadau mbalimbali ambao kwa namna moja au nyingine wamenisaidia katika kufanikisha hotuba hii, siwezi kuwataja wote lakini naomba kuwatambua na kuthamini mchango wa **HakiRasiliamali**, Asasi mbalimbali ndani na nje ya nchi, wadau mbalimbali kwa nafasi zenu pamoja na wanataaluma mbalimbali mlionipatia michango yenu, natambua haya yote ni kwa maslahi mapana ya Taifa na uzalendo wenu kwa nchi yetu! Namshukuru Naibu Waziri Kivuli wa Nishati Mheshimiwa Jesca Kishoa (Mb) kwa ushirikiano wake katika maandalizi ya hotuba hii na majukumu mengine ya Wizara yetu ya Nishati. Kwa wote ambao sijawataja kwa majina lakini nyuma ya pazia mmekuwa nguzo yetu Nasema Asanteni na Mwenyezi Mungu awabariki!

4. **Mheshimiwa Spika,** hii ni bajeti ya nne ya Serikali hii ya awamu ya tano ambapo imebaki bajeti moja tu ya mwaka wa fedha 2020/2021. Hata hivyo katika utaratibu wa mzunguko wa Bajeti za Serikali, Bajeti hii ni ya mwisho kwa Serikali hii ya Awamu ya Tano chini ya Chama Cha Mapinduzi kwa kuwa awamu ijayo itakuwa chini ya Chama Cha Demokrasia na Maendeleo – CHADEMA. Hata hivyo, pamoja na kwamba imebaki bajeti ya takriban miaka miwili Serikali hii imalize muhula wake wa miaka mitano madarakani utekelezaji wa bajeti zilizotangulia umekuwa ni wa kusuasua jambo ambalo limeathiri sana Sekta ya Nishati, hadi sasa hakuna mradi wowote uliokamilika kupunguza au kuhakikisha Tanzania kuna umeme wa uhakika.

**5. Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa mara zote Serikali imeonesha kushindwa katika Sera zake, Sera Mbadala za CHADEMA ni kuhakikisha kunakuwepo na uzalishaji wa Nishati ya Uhakika na Endelevu, kuwepo na umakini na weledi katika usambazaji Nishati na Matumizi Endelevu ya Nishati.

**6. Mheshimiwa Spika,** Sera za CHADEMA zinatokana na ukweli kwamba CHADEMA tunatambua kuwa nishati ni muhimu kwa ajili ya maisha bora kwa wananchi na kwamba nishati ni nyenzo muhimu ya uzalishaji katika sekta mbalimbali za uchumi. Kwa hiyo, ni muhimu kuhakikisha uwepo wa nishati ya uhakika kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. CHADEMA inatambua kwamba Tanzania imejaliwa vyanzo vingi vya nishati ikiwa ni pamoja na umeme wa biomasi, gesi asilia, umeme wa nguvu za maji, Makaa ya Mawe na vyanzo vya nishati jadidifu kama umeme unaotokana na jotoardhi (Geothermal), umeme wa nguvu ya upepo na umeme wa nguvu ya jua. Lakini pamoja na uwepo wa vyanzo vingi vya nishati ni sehemu ndogo sana ya vyanzo hivyo ambayo imekuwa inatumiwa na kuendelezwa ipasavyo kutokana na sera mbovu za Serikali ya Chama Cha Mapinduzi**.**

**7. Mheshimiwa Spika,** ni kutokana na kupwaya huko kwa sera za Chama Cha Mapinduzi, ambazo hazitoi uhakika wa nishati hapa nchini tangu uhuru hadi sasa, CHADEMA tunakuja na sera mbadala ambapo tutahakikisha kuwa nchi inakuwa na nishati ya uhakika, yenye gharama nafuu na endelevu na itakayokuwa inapatikana kwa urahisi katika sekta zote za uchumi. Kufikia lengo hili, CHADEMA tutahakikisha unafanyika utafiti wa kina kuhusu vyanzo mbalimbali vya nishati na hatimaye kutunga Sera ya Taifa ya Nishati itakayoendana na Sera nyingine za kiuchumi na kijamii. Aidha ili kuhakikisha umeme unaozalishwa unatumika kwa tija na ufanisi, CHADEMA tutaweka mfumo wa ugatuaji katika uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme kwa kushirikiana na Sekta Binafsi.

**8. Mheshimiwa Spika,** kutokana na sera hii, wananchi watanufaika kutokana na uwepo wa teknolojia mpya na nishati jadidifu gharama za matumizi ya nishati hiyo

zitapungua na hivyo kuifanya jamii ya watu wengi hasa wanaoishi mbali na gridi ya Taifa au mbali na miji kunufaika. Wananchi watanufaika pia kwa kuwa na umeme wa uhakika kwa matumizi ya majumbani na viwandani, kutokana na vyanzo vingi vya nishati vilivyopo nchini na hivyo kuipelekea Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati. Kwa utangulizi huo, Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni yamezingatia matakwa ya sera mbadala baada ya Sera za Chama Cha Mapinduzi na Serikali yake kushindwa kutatua kero za nishati kwa watanzania kwa zaidi ya miaka hamsini ya uhuru sasa. Aidha madhaifu, upungufu, ufisadi na uwezo mdogo wa Serikali kutekeleza miradi ambayo ingeondoa kero ya nishati kwa watanzania ni dalili tosha kuonesha kwamba Sera za Serikali ya Chama Cha Mapinduzi zimefikia kikomo na hivyo watanzania wamejiandaa na wako tayari kwa Sera Mbadala.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019.

**9. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara ya Nishati ilikadiria kukusanya na kutumia shilingi 1,692,286,014,000 kati ya fedha hizo, fedha zilizopitishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni shilingi 1,665,141,000,000 na shilingi 27,145,014,000 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia mwezi Disemba, 2018 Serikali ilitoa jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 275.40 kwa ajili ya shughuli za Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika;** Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kwamba uwezo wa Serikali kutoa fedha za Miradi ya Maendeleo hauridhishi kutokana na Sera zilizopitwa na wakati za Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, kwa Bajeti hii matatizo ya nishati Tanzania yataishaje na wakati Serikali iko taabani kifedha?

**10. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara inakadiria kutumia shilingi **2,142,793,309,000** ambapo kati ya makadirio hayo shilingi **2,116,454,000,000** ni kwa ajili ya fedha za maendeleo na shilingi **26,339,309,000** ni fedha

kwa ajili ya matumizi ya kawaida kutokana na vyanzo vya ndani na nje ya nchi. Aidha Wizara inatarajia kukusanya shilingi, **1,956,372,000,000** kutoka vyanzo vya ndani na shilingi **160,082,000,000** kutoka nje ya nchi. Hata hivyo takwimu za Wizara zinaonesha kwamba makusanyo ya maduhuli yanayotarajiwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2019/ 2020 ni bilioni **612,370,725,000** sawa na ongezeko la 55.5% kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

## C. SEKTA NDOGO YA UMEME.

**11. Mheshimiwa Spika,** Sekta ndogo ya umeme nchini inasimamiwa na Shirika la Umeme Nchini - TANESCO. Kama inavyofahamika Serikali kupitia TANESCO imekuwa kwa kipindi kirefu sasa ikitekeleza miradi mbalimbali ya kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme. Majukumu makubwa ya TANESCO ni kuzalisha/kununua, kusafirisha, kusambaza na kuuza umeme na ili kutekeleza majukumu haya TANESCO inapaswa kuwekeza katika miradi mipya ya uzalishaji, usafirishaji, usambazaji na kufanya tafiti za vyanzo mbalimbali vya nishati ya umeme ikiwemo nguvu za maji, gesi asilia, makaa ya mawe, nishati jadidifu, kuendeleza na kuimarisha miundombinu ya usafirishaji wa umeme, kuendeleza na kuimarisha miundombinu ya usambazaji, uuzaji umeme na huduma kwa wateja, kufua na kuimarisha mitambo ya umeme inayomilikiwa na Shirika na kununua umeme kutoka kwa wazalishaji binafsi na nchi jirani.

**12. Mheshimiwa Spika**, kutokana na majukumu hayo ya Shirika la Umeme Nchini, ni dhahiri kwamba kuzalisha ama kununua, kusafirisha, kusambaza na kuuza umeme ni majukumu ambayo shirika hili linayatekeleza na hivyo limezidiwa na mzigo huo. Kutokana na muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatachambua upungufu katika ufanisi wa kiutendaji na changamoto za Tanesco katika sekta hii ndogo ya umeme.

### i. Shirika la umeme nchini TANESCO na mwenendo usioridhisha kifedha

**13. Mheshimiwa Spika,** Kwa miaka kadhaa TANESCO imekuwa na mwenendo usioridhisha kwa kupata hasara

mfululizo. Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 hasara iliyopatikana ilikuwa Shilingi bilioni 346.40; na kwa hesabu za miezi 18 hadi mwaka wa fedha ulioishia Juni 2015, hasara ilikuwa Shilingi bilioni 124.46 na hadi kufikia mwaka 2018 hasara ilikuwa imefikia shilingi bilioni 346. Mwenendo wa hasara umekuwa ukichangiwa na hali isiyoridhisha ya maji ya kuzalisha nguvu ya umeme pamoja na ongezeko la gharama za uzalishaji. Mfululizo wa hasara hizo una athari kubwa kwenye Mtaji wa Shirika, hivyo kulifanya kutokopesheka ili kukidhi mahitaji yake ya kifedha.

**14. Mheshimiwa Spika**, Kwa hesabu zilizoishia tarehe 30 Juni, 2016 madai yameongezeka kwa asilimia 23 hadi Shilingi bilioni 958 kutoka Shilingi bilioni 738 zilizoripotiwa kwenye hesabu zilizoishia tarehe 30 Juni, 2015. Kwa upande mwingine thamani ya wadaiwa ilipungua hadi Shilingi bilioni 330.55 kwa hesabu zilizoishia tarehe 30 Juni, 2016 kutoka Shilingi bilioni 440.66 zilizoripotiwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2015.

**ii. Usimamizi wa kampuni binafsi za uzalishaji umeme na gharama za kuiuzia TANESCO**

**15. Mheshimiwa Spika,** Shirika la umeme Tanzania - TANESCO katika jitihada za kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa uhakika wa umeme nchini, shirika liliingia mikataba na makampuni binafsi yanayozalisha umeme kwa lengo la kuiuzia TANESCO. Aidha taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo ni kwamba TANESCO inanunua umeme kwa bei ya wastani wa shilingi 544.65 kwa kila “unit” na kuuza kwa shilingi 279.35 na hivyo kulifanya shirika kupata hasara ya shilingi 265.3 kwa kila *unit*.

**16. Mheshimiwa Spika,** kabla ya kusitishwa kwa mkataba na Kampuni ya Symbion, TANESCO ilikuwa inalipa jumla ya dola za Marekani milioni 16.36 kama capacity charge kwa makampuni yanayozalisha umeme wa dharura. Taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Bunge lako Tukufu inazo zinaonesha kwamba kwa sasa, Shirika linatumia Dola za Marekani milioni 9.75 kwa mwezi kununua umeme kutoka Aggreko, Songas na IPTL.

**17. Mheshimiwa Spika**, Bei za nishati ya umeme inayotozwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) zinadhibitiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) kila robo mwaka baada ya mapitio ya gharama halisi za uzalishaji. Aidha kwa mujibu wa taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo ni kuwa mapitio ya kila robo mwaka ya bei ya nishati ya umeme hayahusishi madeni yaliyojitokeza kabla ya kuanzishwa kwa utaratibu wa mapitio ya bei ya umeme ya robo mwaka. Hivyo, utaratibu huu Mheshimiwa Spika, hauiwezeshi TANESCO kulipa madeni yote inayodaiwa.

**18. Mheshimiwa Spika**, bei ya umeme inayopitishwa na EWURA haionyeshi gharama halisi zilizotumiwa na TANESCO jambo linaloathiri uwezo wa TANESCO katika kulipa madeni yanayolikabili Shirika.

**Mheshimiwa Spika;** Kambi Rasmi ya Bunge lako Tukufu inaishauri Serikali kupitia EWURA kuzipitia kwa umakini gharama za umeme ili kuhakikisha kuwa gharama zote za uzalishaji wa umeme zinahusishwa, ili hatimaye, kusaidia upatikanaji wa faida baada ya uwekezaji wenye lengo la kuboresha huduma na kuongeza matokeo chanya kwa TANESCO.

**19. Mheshimiwa Spika,** Kwenye Kampuni ya Umeme Tanzania (TANESCO) CAG alibaini kuwa eneo la Ubungo Complex lilipewa Songas mwaka 2004 wakati Songas ilipoanza shughuli zake nchini Tanzania. TANESCO ilipatiwa hisa 10,000 katika kampuni ya Songas kama malipo kwa ajili ya Ubungo Complex; pia Songas ilichukua yaliyokuwa madeni ya TANESCO yaliyotokana na ununuzi wa mitambo ya kuzalisha umeme kwa gesi pamoja na mitambo husika iliyopo Ubungo Complex. Hata hivyo, hakuna ushahidi unaoonesha kuwa Ubungo Complex pamoja na mali nyingine ilizopewa Songas Limited zilithaminishwa kabla uhamishaji haujafanyika.

### iii. Madeni ya Shirika la Umeme nchini TANESCO

**20. Mheshimiwa Spika,** TANESCO inashindwa kukusanya madeni ambayo inapaswa kulipwa na hivyo kuzua maswali

mengi ambayo hayana majibu. Taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani inazo zinaonesha kwamba TANESCO inaidai Hospitali ya Tumaini jumla ya Dola za Marekani Milioni 9.4 sawa zaidi ya shilingi bilioni 18 zilizotokana na madai ya kodi ya pango tangu mwaka 1998. Pamoja na kwamba mwaka 2016 TANESCO ilishinda kesi na mahakama ikaamua Hospitali ya Tumaini kulipa fedha hizo na kuondoka kwenye Jengo la TANESCO lakini hadi mwaka jana TANESCO wenyewe walikuwa hawajachukua hatua zozote. Kutokana na taarifa hizo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka majibu ya Serikali iwapo TANESCO wameshalipwa fedha hizo na kama bado ni kwa nini wameshindwa kulipwa hizo fedha wakati wanajiendesha kwa hasara mwaka hadi mwaka.

**iv. Fidia ya ucheleweshaji wa malipo ya kampuni ya Pan African Energy yenye thamani ya dola za kimarekani milioni 10.43**

**21. Mheshimiwa Spika,** Mkataba wa Usambazaji wa Gesi (Gas Supply Agreement) baina ya TANESCO na Kampuni ya Uzalishaji Gesi ya Pan African (PAET), unaeleza kuwa endapo kutatokea mgogoro wa kiasi chochote cha malipo, kiasi hicho kinatakiwa kuwekwa kwenye Akaunti ya Pamoja (Escrow Account) hadi pale mgogoro utakapotatuliwa.

**22. Mheshimiwa Spika,** Kinyume na hapo, fidia ya ucheleweshaji wa malipo itatozwa. Kutoka mwaka 2011 hadi 2016 TANESCO imekuwa na mgogoro dhidi ya baadhi ya malipo ya usambazaji wa gesi ya PAET yenye thamani ya dola za kimarekani milioni 6.48. Hadi tarehe 30 Juni 2016, TANESCO ilikuwa inadaiwa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 71.38 na PAET; Kuchelewa kulipa deni hilo kwa wakati kutapelekea TANESCO kulipa fidia ya ucheleweshaji kwa PAET yenye thamani ya Dola za Kimarekani Milioni 10.43.

**v. Kesi zinazoliandama Shirika la Umeme Nchini-TANESCO**

**23. Mheshimiwa Spika**, Mnamo mwezi Septemba 2010, TANESCO ilishtakiwa na Benki ya Standard Chartered ya Hong

Kong (SCBHK) kulipa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 258.7 kilichotokana na madai ya malipo ya uzalishaji wa umeme pamoja na fidia ya kutolipa madai ya uzalishaji umeme na uharibifu uliosababishwa na TANESCO kutoilipa IPTL kwa wakati.

**24. Mheshimiwa Spika,** maamuzi ya mwisho yaliyotolewa tarehe 12 Septemba, 2016 yaliitaka TANESCO kuilipa SCBHK, ikijumuisha fidia ya kiasi cha Dola za Kimarekani 148.4, baada ya hukumu hiyo, TANESCO ilipinga maamuzi hayo kwa kukata rufaa Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhishi wa Migogoro ya Kibiashara (ICSID) kisha kuwasilisha utetezi wake tarehe 21 Agosti, 2017 ambapo baadaye SCBHK iliwasilisha pingamizi juu ya utetezi huo wa TANESCO.

**25. Mheshimiwa Spika,** tangu kipindi hicho, TANESCO imekuwa ikitumia gharama kubwa za uendeshaji wa kesi hiyo, Shilingi bilioni 3.65 kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na Shilingi bilioni 3.93 kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Hata hivyo, suala hili litarejeshwa kwa mamlaka za kisheria za ndani ambapo utekelezaji wake kisheria utazingatia uwezo wa kulipa wa TANESCO. Licha ya kiasi kikubwa cha fedha zinazotumika kwenye kesi hiyo, hakuna uhakika wa kushinda.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kutoa taarifa hapa Bungeni kuhusu kesi zote ambazo zinaendelea na zilizokamilika dhidi ya TANESCO na gharama ambazo shirika limeingia ikihusisha gharama ambazo zinatarajiwa kulipwa katika kesi ambazo TANESCO imeshindwa kama zipo ili umma wa watanzania wajue kwa kuwa zitalipwa kwa fedha za walipa kodi wa Tanzania.

### vi. Uunganishaji wa Huduma za Umeme

**26. Mheshimiwa Spika,** kumekua na malalamiko makubwa ya gharama za uunganishaji wa huduma za umeme pamoja na mlolongo wa uunganishaji kwa wateja ambao tayari wameshakamilisha taratibu za kuunganishiwa umeme. Ukiachana na gharama za uunganishaji wa umeme, bado kumekua na usumbufu wa uunganishaji wa wateja kwa

wakati kwa visingizio mbalimbali wakati ambao wateja wa umeme huwa wameshakamilisha malipo na kufuata taratibu za uunganishaji wa huduma hiyo.

**Mheshimiwa Spika, kutokana na malalamiko hayo;** kwa mujibu wa ripoti ya Benki ya Dunia kuhusu Kufanya Biashara Tanzania mwaka 2019 (Doing Business 2019), Tanzania imeshika nafasi ya 83 kati ya nchi 190 duniani katika viwango vya wateja kuunganishiwa umeme (Getting Electricity).

**27. Mheshimiwa Spika**, mara baada ya mteja kupewa makadirio ya gharama za uunganishaji, mteja hutakiwa kufanya malipo kwa awamu iwapo ataomba kwa kuingia mkataba na TANESCO kwa kulipia gharama hizo kwa awamu. Na ikiwa TANESCO itashindwa kumuunganisha mteja kwa muda uliotakiwa, itawajibika kumtaarifu mteja mapema. Lakini kumekuwa na malalamiko makubwa ya watumiaji wa umeme juu ya kushindwa kwa TANESCO kufuata taratibu zilizowekwa. Aidha, kwa maeneo ya vijijini ambapo huduma za uunganishaji wa umeme zinafanywa chini ya REA kumekua na malalamiko ya mazingira ya uunganishaji wa huduma za umeme ambapo wananchi mbalimbali wamelalamikia kuwa wenye uwezo wa kutoa rushwa ndio ambao wanapewa kipaumbele cha kuunganishwa huduma hiyo.

**28. Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kuwa kushindwa kwa shirika la umeme nchini katika kusambazia na kuwaunganishia wananchi huduma ya umeme ni kutokana na kuelemewa kwa shirika hilo katika utoaji wa huduma hiyo. Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwepo kwa soko huria kwa wasambazaji wa huduma ya umeme ili kupunguza urasimu wa uunganishaji na hivyo kulipatia faida shirika hilo ambalo sasa linakosa mapato kutokana na kuelemewa katika kuunganishia wateja wapya huduma ya umeme.

### vii. Kiwango kidogo cha kaya zilizounganishwa kwenye huduma ya umeme

**29. Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa ripoti ya utafiti wa hali ya upatikanaji wa umeme nchini, uliofanywa na Shirika la

Umeme TANESCO kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS, 2016), idadi ya kaya zilizounganishiwa huduma ya umeme ni asilimia 32.8 pekee kwa upande wa Tanzania bara.

**30. Mheshimiwa Spika,** kati ya asilimia hizo 32.8 ya kaya zilizounganishwa na huduma ya umeme, asilimia 65.3 ya kaya ni za mjini na asilimia 16.9 ya kaya ni za vijijini. Hii maana yake ni kuwa asilimia 83.1 ya kaya za vijijini hawana umeme wa kawaida. Wakati huo huo maeneo ya mijini ni asilimia 34.7 ya kaya ambazo hazijunganishwa na huduma ya umeme.

**31. Mheshimiwa Spika;** kuzalisha umeme mwingi sio kigezo cha kuunganisha kaya zote na huduma ya umeme. Endapo asilimia 34.7 ya kaya katika maeneo ya mijini hawana huduma ya umeme, maana yake ni kuwa hawawezi kumudu gharama za kuunganishiwa umeme kwa kuwa na kipato duni au kutokuwa na kipato kabisa cha kumudu gharama hizo.

**32. Mheshimiwa Spika;** mwaka 2016 kwa kati ya kaya zote zilizounganishwa na huduma ya umeme, asilimia 31.5 ya kaya zililipia chini ya shilingi 100,000 ili kuunganishwa na huduma ya umeme, wakati asilimia 23.8 ya kaya zililipa kati ya shilingi 100,000 na 299,999 na asilimia 31.4 walilipa kati ya shilingi 300,000 na 499,999 kuunganishiwa umeme. Ukweli mchungu ni kuwa chini ya asilimia moja tu ndio walimudu kulipia zaidi ya shilingi milioni moja.

**33. Mheshimiwa Spika;** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali, kufikiria tena gharama zake za kuunganisha umeme kwa kaya ambazo zina kipato duni au zisizo na kipato kabisa ili kaya hizo ziweze kumudu gharama za kuunganishiwa umeme kulingana na uwezo wa kaya husika.

### viii. Mikoa iliyoshika mkia kwa kaya zake kuunganishwa na umeme

**34. Mheshimiwa Spika;** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuanzisha operation maalumu kuhakikisha kuwa mikoa ambayo haikufanya vizuri katika kaya

zilizounganishwa na huduma ya umeme zinaongeza juhudi katika hatua za makusudi kusaidia wananchi wa maeneo hayo kuunganishwa na huduma ya umeme.

**35. Mheshimiwa Spika;** Katika utafiti wa hali ya umeme (2016), mkoa wa Rukwa ndio ulishika mkia katika kaya zilizounganishwa na huduma ya umeme kwa kaya asilimia 8.7 pekee zilizounganishwa na umeme. Mikoa mingine ni pamoja na Simiyu (11.5%), Shinyanga (12.8%), Geita (14.0%), Songwe (15.9%) na Kigoma (16.2%).

**36. Mheshimiwa Spika;** mikoa iliyoongoza kwa kuwa na kaya nyingi zilizounganishwa na huduma ya umeme ni pamoja na Dar es Salaam (75.2%), Njombe (50.5) na ilimanjaro (42.6%).

**ix. Ufanisi mdogo wa TANESCO kufanya matengenezo ya mitambo ya kufua umeme**

**37. Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi wa ufanisi kwa Shirika la TANESCO umefanyika na imebainika kuwa Shirika lina ufanisi duni wa kufanya matengenezo ya mitambo ya kuzalishia umeme. Matokeo ya ukaguzi huo yalichapishwa mwezi Machi, 2019.

**38. Mheshimiwa Spika,** ukaguzi huo ulitokana na ukweli kuwa kumekuweko mwenendo usioridhisha wa upatikanaji wa umeme nchini, kutokana na kukatika mara kwa mara kwa umeme katika mikoa yote iliyounganishwa kwenye gridi ya Taifa, kuwepo kwa mitambo na miundombinu ya umeme wa maji iliyopitwa na wakati, na msukumo mdogo wa kutoa kiapumbele kwenye matengenezo ya mitambo ya kuzalisha umeme.

**39. Mheshimiwa Spika,** ilibainika kuwa kwa mujibu wa mpango kazi wa TANESCO wa mwaka (2017/18-2020/21) katika kifungu cha 1.3.1.1(a) TANESCO inapaswa kufanya marekebisho na matengenezo ya mitambo yote ya kuzalisha umeme ili kuhakikisha kuwa muda wote mitambo inafanya kazi ya kuzalisha umeme na kuhakikisha kuwa vipuri vya matengenezo vinapatikana kila vinapohitajika.

**40. Mheshimiwa Spika,** katika ukaguzi ule ilibainika kuwa TANESCO haitekelezi ipasavyo mpango kazi wake kwenye eneo la matengenezo ya mitambo ya kufua umeme. Mfumo wa manunuzi kule ambako TANESCO inaendesha mitambo ya kufua umeme haukutekelezwa na TANESCO yenyewe haikujisumbua kufanya utafiti wa bei za soko la manunuzi ya vipuri.

**41. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge ni kwa nini TANESCO imeshindwa kutekeleza mpango kazi wake iliyojiwekea yenyewe?

**42. Mheshimiwa Spika,** Pia Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali iwaeleze Watanzania imejipanga kiwango gani kuhakikisha kuwa manunuzi ya vipuri vya mitambo ya kufua umeme yanafanyika kwa wakati ili kuwaondolea Watanzania mateso na adha ya kukatika umeme mara kwa mara kwenye mikoa yote iliyounganishwa na gridi ya Taifa.

**x. Zabuni 7 za matengenezo ya mitambo ya kufua umeme ambazo hazikutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2017/18 kwa kukosa fedha**

**43. Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa CAG, zipo zabuni takribani 7 zenye thamani ya shilingi bilioni 2.308 ambazo hazikutekelezwa na TANESCO kutokana na ufinyu wa Bajeti.

**44. Mheshimiwa Spika,** zabuni hizo ni pamoja na zabuni ya manunuzi ya vipuri na huduma ya gesi na mita za vituo ya "Tender No. PA/001/17-18/HQ/G/29 for supply of spare parts and services of gas pressure reduction and metering station" yenye thamani ya Shilingi Milioni 80; Zabuni ya vipuri vya mtambo wa kufua umeme yaani "Tender No. PA/001/17-18/HQ/G/53 for supply of spare parts for caterpillar Generators" yenye thamani ya shilingi milioni 420"

**45. Mheshimiwa Spika,** zabuni nyingine zilizokwama kutokana na ukata wa TANESCO ni pamoja na zabuni ya kupata vifaa vya uendeshaji na matengenezo ya mitambo yaani *"Tender*

*No. PA/001/17-18/HQ/G/55 for Supply of tools for operation & maintenance of caterpillar power plants"* yenye thamani ya shilingi milioni 600; zabuni *"Tender No. PA/001/17-18/HQ/ G/56 for supply of tools for Mirrlees Blackstone generators"* yenye thamani ya shilingi milioni 100. Zabuni nyinginezo zilizokwama ni pamoja na zabuni ya vifaa vya uendeshaji na matengenezo *"Tender No. PA/001/17-18/HQ/G/57 for supply of tools for operation &maintenance"* yenye thamani ya shilinigi bilioni 1, na zabuni ya *"Tender No. PA/001/17-18/HQ/ G/61 for supply of steam cleaners for use in service of isolated stations"* yenye thamani ya shilingi milioni 80 na zabuni ya saba ni yenye thamani ya shilingi milioni 28 *"Tender No. PA/ 001/2017-18/HQ/N/19 for Hiring of scaffolding and canvas covering of Gas Turbine No. 1 for Level B Maintenance"*

**46. Mheshimiwa Spika,** shughuli zote za matengenezo ya mitambo ya kufua umeme kwa mwaka wa fedha 2017/18 hazikufanyika kutokana ha zabuni hizo kutotekelezwa.

**47. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Watanzania wajue kuwa hali ya kifedha ya Shirika lao la umeme ni hoi bin taaban, na hivyo hali ya kukatika mara kwa mara kwa umeme itaendelea inatokana na sera mbovu za Serikali ya CCM kushindwa kusimamia uendeshwaji wa faida wa Shirika la umeme nchini kwa zaidi ya miaka 50 tangu nchi yetu ipate uhuru.

**SHIRIKA LA UMEME NCHINI - TANESCO LIGAWANYWE**

**48. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi kirefu sasa TANESCO inajiendesha kwa hasara kutoka Serikali ya awamu ya nne ambapo TANESCO ilikuwa ikipata hasara ya shilingi 124. Takwimu zinaonesha kwamba baada ya kuingia madarakani kwa Serikali ya Awamu ya Tano, shirika hili limekuwa likipata hasara kubwa zaidi ambapo hadi mwaka 2017 TANESCO ilipata hasara ya shilingi 346 sawa na ongezeko la bilioni 122.

**49. Mheshimiwa Spika,** hasara hiyo inatokana na upungufu wa maji ya uzalishaji umeme pamoja na gharama za uendeshaji wa Shirika la Umeme Nchini. Pamoja na hayo

madeni ya TANESCO yameongezeka kwa zaidi ya 23% kutoka shilingi bilioni 738 katika kipindi cha Serikali ya awamu ya nne hadi kufikia shilingi bilioni 958 katika utawala wa Serikali ya Awamu ya Tano.

**50. Mheshimiwa Spika,** kwa nyakati mbalimbali Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni pamoja na wadau wengine tumependekeza mikakati mingi ya kulinusuru Shirika la Umeme Nchini, kama ambavyo nchi nyingine duniani zinafanya na moja ya mapendekezo ambayo hadi sasa tunapendekeza ni kuligawa Shirika la Umeme Nchini na kupata mashirika mawili.

**51. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba Shirika la Umeme Nchini - TANESCO ligawanywe na yapatikane mashirika mawili. Shirika moja lishughulikie masuala ya uzalishaji wa umeme nchini wakati jukumu la kusambaza umeme nchini likiwa chini ya usimamizi wa shirika lingine. Mapendekezo haya Mheshimiwa Spika yatapunguza mzigo kwa TANESCO ambayo inahusika na majukumu ya kuzalisha/kununua, kusafirisha kusambaza na kuuza umeme na kupelekea mzigo wa changamoto lukuki katika kuyatekeleza majukumu hayo.

**MIRADI YA KUZALISHA UMEME**
**a) Ujenzi wa Mradi wa Rufiji (Rufiji Hydro Power Project)**

**52. Mheshimiwa spika,** kwa mujibu wa taarifa za Serikali, lengo la kutekeleza mradi huu ni kuzalisha umeme wa jumla ya MW 2100 kwa kutumia maji (Hydro Power Plant) katika Bonde la Mto Rufiji ambako Serikali inadai utekelezwaji wa mradi huu utakuwa ni kichocheo muhimu katika kuiwezesha Tanzania kufikia azma yake ya kuwa nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

**Msimamo wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Mradi wa Rufiji (Rufiji Hydro Power Project)**

**53. Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kukubaliana na dhana ya kuzalisha umeme wa MW 2100 Kambi Rasmi Bungeni

haikubaliani na namna utekelezwaji wa Ujenzi wa Mradi wa Rufiji Hydro Power Project unavyofanyika kwenye eneo la mradi lililoteuliwa na Serikali hivi sasa kwa sababu mbalimbali ambazo nitazieleza hapa chini.

**1) Gharama za kiuchumi za ujenzi wa Mradi huo kwa wakati mmoja**

**54. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pekee, Serikali kupitia hotuba ya Waziri wa Nishati alieleza mpango wa Serikali wa kujenga mradi huu katika aya ya 22 na 23 ya hotuba yake. Katika aya ya 23 Mheshimiwa Waziri wa Nishati alisema katika kipindi cha mwaka 2018/2019 Serikali itaendelea kutekeleza mradi huu na shughuli zitakazofanyika ni pamoja na mosi, ujenzi wa kambi na Ofisi za wafanyakazi, pili, ujenzi wa bwawa yaani main dam and spillways na tatu, ujenzi wa njia kuu za kupitishia maji (tunnels). Serikali ilisema fedha za ndani shilingi **bilioni 700** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa kazi hizo na kwamba utekelezaji wa shughuli za ujenzi wa mradi ulitarajiwa kuanza mwezi Julai, 2018 kwa mkandarasi kuanza kazi za awali kwa miezi mitatu na kufuatiwa na ujenzi wa miundombinu ya mradi unaotarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi 36.

**55. Mheshimiwa spika,** ukisoma taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara ya Nishati kwa kipindi cha mwaka 2018/2019 Waziri anasema "Wizara ya Fedha na Mipango imetenga "cash" jumla ya **shilingi bilioni 984** ambazo taratibu za malipo zinaendelea ili zilipwe kwa mkandarasi wa Mradi wa Rufiji kabla ya mwishoni mwa mwezi Aprili, 2019 kama malipo ya awali (advance payment) katika mradi huo"

**56. Mheshimiwa Spika,** kwa maneno mengine ni kwamba sasa Serikali ilipanga kulipa fedha kwa ongezeko la shilingi **bilioni 284** bila idhini ya Bunge lako tukufu kwa kazi zile zile za ujenzi wa kambi na Ofisi za wafanyakazi, ujenzi wa bwawa (main dam and spillways) na ujenzi wa njia kuu za kupitishia maji (tunnels) ambazo Serikali ilisema Mkandarasi atatekeleza kwa miezi 36.

**57. Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Awamu ya Tano inaongoza kwa kukiuka taratibu na sheria za nchi. Kwenye mradi huu Serikali imetoa wapi nyongeza ya Bilioni 284 ambazo hazikupitishwa na Bunge hili? Kwamba Serikali sasa haizingatii matakwa ya Ibara ya 99 ya Katiba na Kanuni ya 110 ya Kanuni za Bunge kuhusu makadirio ya matumizi ya nyongeza. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuliambia Bunge hili, Bilioni 284 zinazodaiwa kulipwa kwenye mradi zimetoka wapi, zimeongezeka kufanya shughuli gani na kwa nini Serikali haikufuata matakwa ya makadirio ya matumizi ya nyongeza?

**2) Muda na ongezeko la gharama halisi za Ujenzi wa Mradi wa umeme wa Bonde la Mto Rufiji**

**58. Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Mkakati wa Mwongozo wa Mabadiliko ya Sekta ya Usambazaji wa Umeme Nchini wa mwaka 2014 mpaka 2025 (Electricity Supply Industry Reform Strategy Roadmap), uwezo wa kuzalisha umeme unatakiwa kuongezeka kutoka Megawati 1,583 mwaka 2014 mpaka kufikia Megawati 10,000 mwaka 2025, ili kuiwezesha nchi kufikia uchumi wa kati sambamba na dira ya Maendeleo ya Taifa (Vision 2025).

**59. Mheshimiwa Spika**, mradi huu wa umeme wa Mto Rufiji tunaambiwa na Serikali kuwa utakamilika ndani ya kipindi cha miezi 36 (sawa na miaka mitatu kuanzia sasa) na utaweza kuzalisha Megawiti 2100 kiasi ambacho ni asilimia 21.0 ya lengo la kufika kuwa nchi ya uchumi wa kipato cha kati. Wakati ujenzi unakamilika ndani ya miezi 36 kama tulivyoaminishwa na Serikali, itakuwa imesalia miaka miwili tu kufikia mwaka 2025, hivyo shabaha ya kufikisha uzalishaji wa megawati 10,000 ifikapo mwaka 2025 bado ni ndoto za mchana ambazo Serikali yetu inaendelea kuota.

**60. Mheshimiwa Spika**, hata hivyo uchambuzi wa gharama za mradi wa umeme wa maji wa Mto Rufiji, zilizofanywa na ***Odebrecht (2012) na iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini (2016)***, walikadiria kuwa mradi utajengwa kwa vipindi vya miaka tisa awamu ya kwanza na miaka mitatu kwa awamu ya pili, hii inafanya idadi ya muda wa ujenzi kuongezeka

kutoka miezi 36 ya awali hadi miaka 12 ambayo ni sawa na miezi 144.

**61. Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi huo wa gharama za ujenzi wa mradi wa umeme wa Mto Rufiji, miezi 36 ambayo imeripotiwa na Serikali, haitawezekana kuumaliza huu mradi hivyo kuufanya kuwa moja ya miradi mikubwa nchini itakayoigharimu nchi kiwango kikubwa cha fedha za walipa kodi kwa kuwa gharama za mwisho wa mradi zitakuwa kubwa kulikoni gharama ziliziainishwa wakati mradi unaanza!

**62. Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi huo, kunakadiriwa kuwa kwa aina ya miradi mikubwa kama huu, gharama za mradi zinakaridiwa kuongezeka kwa asilimia 30 (cost overruns) tangu hatua za ujenzi kuanza mpaka kuja kumalizika.

**63. Mheshimiwa Spika**, mwaka 2016 gharama za awali za mradi zilikadiriwa kufikia dola bilioni 3.738 sawa na Shilingi Trilioni 7.5. Endapo gharama za ujenzi wa mradi zitaongezeka (cost overruns) kwa asilimia 30% basi gharama za Mradi wa Umeme wa Mto Rufiji zitaongezeka mpaka kufikia Dola za Marekani bilioni 9.852 ifikapo mwaka 2027, kiasi ambacho kama (exchange rate ya mwaka 2019 ikitumika, Shilingi 2330) basi kiasi hicho kitakuwa ni sawa na Shilingi Trilioni 22.95.

**64. Mheshimiwa Spika**, kupanga ni kuchangua, Shilingi Trilioni 22.95 ni sawa na asilimia 69.3 ya Bajeti nzima ya mwaka wa fedha 2019/20 inayopendekezwa na Serikali ya CCM. Kama bajeti kila mwaka wa fedha itaongezeka kwa asilimia 1.9 (maana mwaka wa fedha 2018/19, bajeti ilikuwa ni Shilingi Trilioni 32.48) na mwaka 2019/20 bajeti inayopendekezwa ni Shilingi Trilioni 33.10; basi gharama za ujenzi wa mradi wa umeme wa Mto Rufiji zikiwa Trilioni 22.95 ifakapo mwaka 2027 basi itakuwa ni sawa na asilimia 60 ya bajeti tarajiwa kwa mwaka wa fedha 2027/28, ambayo itakuwa ni Shilingi Trilioni 38.071

**65. Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huu uliofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, basi mradi huu wa umeme wa Mto Rufiji utakuwa ni aina nyingine za maamuzi

yanayoenda kuiweka nchi katika hali mbaya ya kifedha na itakuwa ni hatua kubwa sana ya Serikali ya awamu ya tano, kuhujumu uchumi wa nchi kwa kuzingatia kuwa mradi unatekelezwa na mkandarasi kutoka nje na hivyo sehemu kubwa ya malipo itaondoka kutoka mzunguko wetu wa ndani wa kifedha.

**66. Mheshimiwa Spika**, nitoe wito tu kwa Serikali hii ya awamu ya tano; kufikiria upya na kutupa majibu ya namna gani wanajipanga na ugharimiaji wa gharama zinazokadiriwa kuongezeka katika ujenzi wa mradi huu kwa kuwa umekwishaanza kutekelezwa. Hatutaki ije Serikali ya Awamu ya Sita, kwa vyoyote itakavyokuwa iwe ni Serikali itakayoongozwa na CHADEMA ama chama kingine chochote ilazimike kufanya maamuzi tofauti wakati nchi ikiwa tayari imeshaathirika kufuatia upungufu wa kiutendaji katika Serikali ya awamu ya tano.

**3) Sababu za kimazingira**

**67. Mheshimiwa Spika**, imesemwa mara nyingi na watalamu mbalimbali kwamba Mradi huu utaathiri Selous Game Reserve ambayo ni moja ya World Heritage Sites na hivyo ujenzi katika eneo hili utaathiri ecology ya Selous kwa kuathiri mazingira hatimaye yataathiri uchumi na maisha ya watu. Mradi huo utazuia tani milioni 16.6 za virutubisho vya ardhi kwa mwaka, hivyo kusababisha mmomonyoko wa Ardhi kwenye delta ya Rufiji.

**68. Mheshimiwa Spika,** ipo pia hoja ya eneo ambalo mradi husika utatekelezwa ambalo ni kilomita za mraba 1,200. Eneo hili ni kubwa na litaufanya mradi kuwa ni bwawa kubwa kuliko yote Afrika Mashariki na kuzua hofu ya kukausha maziwa madogo madogo yote ya eneo la jirani, litaathiri utalii, kukomba rutuba yote ya ardhi ya eneo hilo hadi kwenye Delta ya Rufiji na hivyo kuua samaki na kuathiri uvuvi wa samaki kamba na kamba koche wanaotegemewa na watu zaidi ya laki mbili wa eneo hili.

**69. Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unaotekelezwa, unatekelezwa kinyume cha mikataba ya kulinda urithi wa

asili (World Heritage) ambayo Tanzania tumesaini. Kwa kutekeleza mradi huu tunaingia katika ongezeko la matumio mbalimbali ambayo Tanzania tunafanya yanayokiuka mikataba mbalimbali pamoja na sheria pia zikiwemo ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu, Lakini haishangazi kuona Serikali ikikasirika iambiwapo kwamba wanaongoza kuvunja sheria na mikataba ambayo kama Taifa tulikubali kushirikiana na Dunia.

**70. Mheshimiwa Spika**, Sera za uchumi za Serikali ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) hazieleweki kabisa, awali mradi wa umeme wa Stiglers Gorge uliasisiwa tangu enzi za Nyerere na haukutekelezwa kutokana na sababu za kimazingira na mpango wa Tanzania Power System Master Plan (2016 update) umeonesha mradi huo kuwa ni chaguo la mwisho endapo miradi mingine mikubwa ikiwa imeshatekelezwa na mahitaji ya ziada ya umeme yangeibuka. Katika mpango huo imetajwa miradi mbalimbali ya maji ambayo ingepaswa kuanza kutekelezwa na pia imetajwa pia miradi ya gesi ambayo ingetekelezwa sanjari na miradi mipya ya maji. Tangu kuingia madarakani kwa Serikali hii ya Awamu ya Tano hakuna anayezungumzia tena miradi mingine ya muda mrefu zaidi ya umeme wa maji wala miradi ya umeme wa gesi na sasa tunaambiwa kipaumbele kikuu ni umeme wa Stieglers, Tunaomba kufahamu zipi hasa sababu za Serikali kuacha miradi ya kuzalisha umeme ambayo ilikuwa tayari katika mkondo wa utekelezaji na kuanza mradi mmoja mkubwa mpya ?

### xi. Madai ya ufisadi katika ujenzi wa Mtandao wa usambazaji umeme kwa ajili ya Mradi wa Umeme Mtwara

**71. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani ina taarifa ya madai ya ufisadi ambao inaelezwa kuwa ulifanywa wakati wa ujenzi wa mtandao wa usambazaji wa umeme Mtwara (MEP) yaliyopelekea Kampuni ya M/S Wentworth Gas Limited pamoja na kampuni zake kufanya kazi zake bila kuzingatia masharti ya mikataba ya Tariff Equalisation Fund na MICRA, na pia ukafanyika ununuzi wa mitambo ya umeme bila kumshirikisha Mthamaini Mkuu wa Serikali. Ilipendekezwa

kwamba Serikali ilipaswa kurejeshewa kutoka kwa Kampuni ya Wentworth Gas Limited (Umoja Light Co. Ltd) kiasi cha Dola za Kimarekani 8,426,819.33. Hadi sasa hakuna taarifa kama kiasi hicho cha fedha kimesharejeshwa kama ilivyoshauriwa na ni hatua gani za kiuwajibikaji zimechukuliwa.

**xii. WAKALA WA NISHATI VIJIJINI- (REA)**

**72. Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Nishati Vijijini ulianzishwa kwa sheria ya Nishati Vijijini Na.8 ya mwaka 2005 na kuanza rasmi mwezi Oktaba 2007, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Nishati. Lengo la uanzishwaji wa REA lilikuwa ni kuwapatia wananchi waishio vijijini nishati bora. Pamoja na umuhimu wa wakala huyu bado Serikali haijaonesha kwa vitendo kuwa ina nia ya kusaidia wakala huyu ili aweze kuhimiza majukumu yake kikamilifu na hasa linapokuja suala la kuupatia fedha kama zinavyoombwa na zinavyopitishwa na Bunge lako tukufu.

**73. Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kuwa Serikali imekuwa haitimizi wajibu wake wa kuipatia REA fedha kama zinavyotengwa na kuidhinishwa na Bunge hili, kwa mfano mwaka 2009/2010, fedha zilizopitishwa zilikuwa ni shilingi bilioni 39.55 na kiwango cha fedha zilizotolewa ni shilingi bilioni 22.14 sawa na 56%. Mwaka 2010/2011 kiasi cha fedha kilichotengwa ni shilingi bilioni 58.883 na kiasi cha fedha kilichotolewa ni shilingi bilioni 14.652 sawa na 25%, mwaka 2011/2012 kiasi kilichotengwa ni shilingi bilioni 71.044 na kiasi cha fedha kilichotolewa ni shilingi bilioni 56.748 sawa na 80%, mwaka 2012/2013 kiasi cha fedha kilichotengwa ni shilingi bilioni 53.158 na kiasi cha fedha kilichotolewa ni shilingi bilioni 6.757 sawa na 13%.

**74. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2015/2016 wakala alitengewa jumla ya **shilingi 420,492,701,200/-** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Lakini kwa mujibu wa taarifa ya utendaji ya Wakala ni kwamba hadi Desemba 2015 zilikuwa zimepokelewa jumla ya **shilingi 141,163,133,226/-** tu ambazo ni sawa na **asilimia 34.**

**75. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2016/17 wakala ulipitishiwa fedha za maendeleo jumla ya shilingi 382,840,122,792/-, taarifa ya wakala iliyotolewa Januari, 2017 takwimu zake zinaonyesha kuwa jumla ya miradi 13 inayoendelea kutekelezwa yenye thamani ya shilingi 1,210,050,878,902 kama mikataba yake ilivyosainiwa, hadi sasa fedha zilizotolewa na Serikali ni shilingi 1,019,957,110,048.20 na kiasi kilichobaki ni shilingi 190,093,768,854. Hiki ni kiasi kikubwa cha fedha, na ni miradi iliyoingiwa mikataba tu, lakini REA ina miradi mingi kwa kulingana na bajeti zilizopitishwa na Bunge pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

**76. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2017/18 hadi kufikia Februari 2018 jumla ya shilingi bilioni 249.33 zilikuwa zimepokelewa sawa na asilimia 49.9 ya shilingi 499,090,426,000/- ambazo kati ya hizo shilingi 469,090,426,000/- zilikuwa ni fedha za ndani na shilingi 30,000,000,000/- fedha za nje kama zilivyopitishwa na Bunge.

**77. Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka 2018/19 Bunge liliidhinisha jumla ya shilingi bilioni 412.08 kwa ajili ya Mfuko wa Nishati Vijijini ili kugharamia miradi ya maendeleo na uendeshwaji wa Wakala wa Nishati Vijijini. Katika fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni 395.61 sawa na 96% zilitengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Aidha hadi kufikia mwezi Februari 2019 Wakala wa Nishati ulikuwa umepokea jumla ya shilingi bilioni 302.61 sawa na 126%. Sababu inayotolewa ni kwamba fedha zilitolewa zaidi kuzidi matarajio kutokana na washirika wa maendeleo kutoa fedha zaidi ikilinganishwa na ukomo wa bajeti ya fedha za nje iliyotengewa Mfuko wa Nishati Vijijini na kwamba wafadhili walitoa kutokana na ahadi (commitment) ambazo walishaingia na Serikali katika kufadhili miradi ya BTIP – VEI, Ujazilizi, Makambako – Songea, REA III Mzunguko wa kwanza na ile ya nje ya gridi. Kinachozua maswali ni kwa nini Wizara haikuwa na makadirio ya fedha hizi wakati ilikuwa tayari na ahadi hizo (commitment) kutoka kwa wahisani hao wakati bajeti husika haikuwa na makadirio hayo.

**78. Mheshimiwa Spika,** Mwaka 2019/2020 wakala unaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 423.1 ikiwa ni ongezeko la bilioni 10.3.

**79. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Usambazaji Umeme Vijijini Awamu ya Tatu ambao umegwanywa katika vipengele vinne(4) ambavyo ni sehemu ya REA III, inaonesha kuwa Miradi ya Usambazaji Umeme kwenye maeneo ambayo yameshafikiwa na Miundombinu ya Umeme (DENSIFICATION) unakadiriwa kuwa utatumia jumla ya shilingi bilioni 2,000 na utatekelezwa kwa kipindi cha miaka 5 ya fedha. Na vijiji vitakavyonufaika ni 4,395 Mheshimiwa Spika, hizi densification zimegawanywa katika awamu II kulingana na idadi ya vijiji vinavyohitajika kupatiwa umeme.

**80. Mheshimiwa Spika,** ni ukweli kuwa REA inatumia fedha nyingi sana katika kutekeleza wajibu wake. Kwa kuwa kila mradi ili utekelezeke ni lazima kuwepo na andiko la kuonesha "costs benefits analysis". Kwa kuwa fedha za walipa kodi wa ndani na wengine ambao wanasaidia katika kutekeleza miradi hii fedha zinatumika, kwa mahesabu ya haraka haraka kwa kuanzia mwaka wa fedha 2008/09 hadi 2018/19 takriban zimekwishatengwa jumla ya shilingi **2,199,772,249,992/-** ambazo ni fedha nyingi sana. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali itoe maelezo ni baada ya muda gani uwekezaji unaofanywa na REA utaanza kurudisha mtaji uliowekezwa huko (return on investment) kwa kuwa yamekuwepo matukio katika nchi yetu ya Serikali kuwekeza kwenye miradi yenye kuingiza hasara mingine uwekezaji ukifanyika bila hata ya kuwepo kwa mchanganuo wa kibiashara.

**81. Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji wa REA ***(Final Report- Mid-term Review of the Capacity Development Project of the Rural Energy Agency, Tanzania)*** iliyotolewa na **Swedish International Development Cooperation Agency (SIDA)** inaonesha kuwa kati ya miradi yote inayotekelezwa na REA, miradi 234 sawa na asilimia (72.9%) inatekelezwa na TANESCO ikiwa na gharama ya

shilingi bilioni 289 na miradi 87 sawa na 27.1% ilitekelezwa na wakandarasi wengine. Kati ya fedha hizo Tanesco ilipatiwa asilimia 89 na wakandarasi wengine walipatiwa 2% ya kile walichotakiwa kupatiwa. Hii inaonesha kuwa fedha nyingi zinazotengwa na REA zinapelekwa kutekelezwa miradi inayotekelezwa na TANESCO.

**82. Mheshimiwa Spika**, ukiangalia miradi mingi ya REA inayotekelezwa na TANESCO ni ile ya "grid electrification" ya kutekeleza Mpango Kabambe wa Usambazaji Umeme Vijijini (Turnkey Operation Projects).Miradi mingine inayohusu nishati ya umeme inayotokana na Jua, Upepo, maji katika maporomoko madogo madogo na n.k (solar, wind, biogas, hydro etc) bado miradi hiyo upatikanaji fedha kutoka REA unasuasua sana.

**83. Mheshimiwa Spika**, Ukweli ni kwamba miradi hiyo ya nishati Jadidifu ***(renewable energ*y)** ndio inaweza kuwa mkombozi kwa mazingira yetu halisia badala ya kutegemea umeme unaozalishwa na kusambazwa na TANESCO.Hivyo basi ni Rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa REA kuhakikisha kipaumbele wanapewa wakandarasi ambao wanahusika na uzalishaji umeme kutokana na nishati Jadidifu.

**84. Mheshimiwa Spika,** kutokana na taarifa hiyo ni kwamba REA ndiyo inaiendesha TANESCO, fedha zote zinazokatwa kwenye mafuta na gharama za kununua umeme ili zipelekwe REA kwa lengo la kusambaza umeme vijijini ambapo TANESCO haijafika, kwa mlango wa nyuma fedha hizo zinarudishwa TANESCO kupitia njia ya kuwapatia kandarasi TANESCO ili watimize wajibu wao wa kuwapatia wananchi umeme.

**85. Mheshimiwa Spika,** kwa ukweli huo ni vyema REA ikafanyiwa tathmini upya na kuangalia inatakiwa ishughulikie miradi ya aina gani katika kutimiza majukumu yake kwa mujibu wa sheria.

**WIZI WA FEDHA ZA REA KUPITIA MALIPO YA ZIADA TZS BIL.97, 935,493.04 (USD 44,725.53)**

**86.** **Mheshimiwa Spika**, Mapitio ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali CAG, taarifa ya Machi, 2017 inaonesha kwamba Wakala wa Nishati ya Umeme Vijijini - REA ilifanya malipo ya ziada ya dola za Marekani **USD 91,168.48** kwa HIFAB badala ya kulipa Dola za Marekani USD 9,218.48 na hivyo kufanya malipo ya ziada ya jumla ya dola za Marekani USD 81,950. Taarifa ya mwisho inaonesha kwamba jumla ya Dola za Marekani 44,725.53 hazijarejeshwa REA.

**87. Mheshimiwa Spika**, kitendo cha REA kulipa HIFAB fedha nyingi na za ziada kuliko kiasi kilichopaswa kulipwa ni wizi kama ulivyo wizi mwingine na ni vitendo ambavyo Serikali ya Chama Cha Mapinduzi imekuwa ikivikumbatia, hadi sasa ulipaji huo ambao ni uhujumu wa Miradi ya Taifa na Uhujumu Uchumi lakini hadi sasa bado fedha hizo hazijarejeshwa REA, Pili, hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa dhidi ya wahujumu uchumi hawa pamoja na tambo za Serikali kuanzisha mahakama ya uhujumu uchumi nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani Nchini inaitaka Serikali kuwaambia walipa kodi wa Tanzania sababu zilizosababisha REA wakawalipa HIFAB zaidi ya Dola za Marekani 81,950, wahusika ni akina nani kama siyo wizi unaofanywa na vigogo na hatua zilizochukuliwa dhidi ya waliohusika na uhujumu huo.

**REA IMESHINDWA KUKUSANYA JUMLA YA TZS 7,433,600,000 KUTOKA TANESCO:**

**88. Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na.147 la tarehe 22 Aprili 2011, TANESCO walitakiwa kutuma 3% ya gharama za mauzo ya umeme ya LUKU kwa kila mwezi REA na malipo ya 5% kwa adhabu ikiwa TANESCO watashindwa kufanya malipo hayo kwa muda. Hata hivyo REA ilishindwa kukusanya kiasi cha shilingi 7,433,600,000 kutoka TANESCO pamoja na jitihada mbalimbali ambazo zimefanywa.

**REA KUSHINDWA IMESHINDWA KUSIMAMIA MRADI WA UMEME KATIKA MKOA WA KAGERA (REA Phase II)**

**89. Mheshimiwa Spika**, mwezi wa Februari mwaka 2014, REA iliingia mkataba na M/S Urban & Rular Engineering Service wa Thamani ya shilingi bilioni 110.8 kwa mradi wa usambazaji na kuunganisha umeme kwa wateja katika Wilaya za Muleba, Karagwe, Kyerwa, Biharamulo, Ngara, Misenyi na Bukoba. Muda wa kukamilisha mradi huo ilikuwa tarehe 27/8/2015, lakini muda ulisogezwa mbele hadi tarehe 28/08/2016. Hata hivyo ilibainika kwama mpaka Oktoba 2018 vijiji 65 vilikuwa havijaunganishwa umeme. Aidha vijiji 50 vilivyounganishwa havikuwa kwenye makubaliano ya mkataba na jumla ya wateja 1317 waliokuwa wamelipa gharama za umeme ila bado hawajaunganishwa.

**90. Mheshimiwa Spika**, toka mwaka 2014 hadi mwaka 2018 ni kipindi cha miaka minne, bado mkandarasi hajamaliza kazi aliyokusudia kukamilisha mwaka 2015 na Serikali ipo na inafahamu jambo hili, haya ndiyo mazingira yanayopelekea Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kusema miradi hii inagubikwa na mazingira ya ufisadi na Serikali haina uwezo wa kutosha wa kusimamia shughuli za maendeleo kwa maslahi ya nchi hii.

**UKIUKWAJI WA SHERIA YA MANUNUZI YA UMMA NA TAASISI YA REA**

**91. Mheshimiwa Spika,** uchunguzi uliofanywa kwenye mikataba mitatu yenye thamani ya bilioni 984.3 ulibaini kwamba, REA iliingia mkataba na Kampuni ya SMEC ambayo haikusajiliwa na Bodi ya Wakandarasi na hivyo kuleta mashaka kwa mkataba husika, pia zabuni ya kupata wakandarasi ilitangazwa kabla ya maandalizi ya nyaraka na usanifu wa mradi kukamilishwa na mshauri.

**92. Mheshimiwa Spika,** katika uchunguzi huo pia ilibainika kwamba majadiliano na mapendekezo ya wazabuni kupewa kandarasi hayakufanyika vizuri. Aidha makisio ya vifaa vilivyohitajika kutokana na BOQ ni vichache kuliko

vilivyoorodheshwa katika mikataba yote sita iliyosainiwa na wakandarasi na jumla ya tofauti ya shilingi bilioni 99 kwa mikataba yote sita. Vijiji 55 ambavyo vilikuwa vimeshapata umeme viliingizwa tena kwenye mikataba ili wakandarasi waitekeleze katika mikoa ya Tanga, Mwanza, Arusha, Shinyanga na Manyara, pamoja na hayo mikataba ilikuwa na utata nani anawajibika kulipia gharama za kuingiza vifaa nchini. Ukiukwaji huu unafanywa katika kipindi ambacho watanzania ambao ni walipa kodi wakiaminishwa na Serikali kwamba Serikali yenyewe ni safi na kwamba iko kwa ajili ya kutetea wanyonge, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa kufahamu hatua stahiki zilizochukuliwa dhidi ya matumizi haya mabaya ya fedha za umma na madai ya ufisadi katika mikataba hiyo.

## TAKWIMU ZA UPATIKANAJI WA UMEME CHINI YA MRADI WA UMEME VIJIJINI (REA)

**93. Mheshimiwa Spika**, katika kutoa takwimu za upatikanaji wa umeme chini ya Mradi wa Umeme Vijijini (REA) kumekua na upotoshaji mkubwa wa takwimu unaolenga kuonesha mafanikio katika utoaji wa huduma hiyo wakati kwa uhalisia wananchi wengi hawajafikiwa na huduma hizo za REA.

**94. Mheshmiwa Spika**, ni dhahiri kuwa wananchi wa sasa sio wajinga kama ambavyo amenukuliwa mara kadhaa Mhe. Rais. Ikumbukwe kuwa miradi hii ya REA ilianzishwa kwa lengo la kuunganisha na kusambaza umeme vijijini Tanzania ambavyo ni zaidi ya vijiji 12000. Lakini katika takwimu zinazotolewa kwa umma juu ya vijiji vilivyounganishwa na umeme haviendani na uhalisia wa kaya ambazo zimeunganishwa ama kufikiwa na huduma za umeme. Kwa mfano; katika uchunguzi uliofanywa na Kambi ya Upinzani na pia kutokana na taarifa za Wabunge wake walio katika Kamati yako ya Nishati na Madini imegundua upikwaji mkubwa wa takwimu unaofanywa chini ya Wizara ya Nishati na kupotosha umma.

**95. Mheshimiwa Spika**; kwa uhalisia Miradi ya REA inapofika katika Vijiji husika, mkandarasi hutakiwa kuunganisha umeme

katika vijiji vilivyo ndani ya'scope' inayotolewa na wataalamu. Aidha, ikiwa katika kata au tarafa moja kuna vijiji 11 na vilivyo ndani ya Scope ya REA ni vijiji vitatu (3) basi TAKWIMU hizo husoma jumla ya vijiji vyote ndani ya kata au tarafa kuwa vimeunganishwa na umeme wakati kiuhalisia ni vijiji 3 tu ndio vyenye umeme. Na ili kuepukana na kuupotosha umma kwa kutoa takwimu ambazo hazina uhalisia, Kambi ya Upinzani kwa nyakati tofauti imeendelea kupendekeza kwa michango ya Wabunge wake na maoni yake kuwa takwimu za uunganishwaji wa umeme vijijini ufanywe kwa kutumia kaya zilizofikiwa na si kwa kutumia vijiji ambavyo havitoi uhalisia wa kitakwimu.

**Mradi wa Usambazaji Umeme katika maeneo ambayo yameshafikiwa na Miundombinu ya UMEME (Densification)**

**96. Mheshimiwa Spika,** mradi huu unahusisha kuongeza wigo wa usambazaji wa umeme katika vijiji, vitongoji na maeneo ambayo tayari yana miundombinu ya umeme. Mradi huu umetekelezwa kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza (Densification Round I) ilianza mwaka 2017 na (Densification Round II )ilianza Julai 2018 na ulikadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi Bilioni 62 1 . Mradi huu ulilenga kuunganisha vitongoji vilivyomo katika vijiji 4090. Lakini katika Randama ya Bajeti ya Wizara haijawekwa wazi utekelezaji wa mradi huu na iwapo umetengewa tena bajeti kwa mwaka 2019/2020.

## xiii. SEKTA NDOGO YA NISHATI JADIDIFU

### i. HEKAYA JUU YA UZALISHAJI WA UMEME WA UPEPO

**97. Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kuwa kuendelea kuwa na vyanzo vichache vya nishati hakuwezi kutimiza azma ya Serikali ya viwanda hasa ukizingatia kuwa maeneo mbalimbali nchini yana jiografia tofauti lakini pia uwezekano wa kuzalisha umeme kwa kupitia vyanzo vingine tofauti na maji (hydropower energy generation) na jua (solar enegy generation). Mikoa kama ya Singida, Iringa, Kilimanjaro ni mojawapo ya maeneo yenye upepo mkali ambao unaweza kuzalisha umeme na ukatumika kama nishati mbadala na

hivyo kupunguza msongamano wa watumiaji wa umeme wa maji.

**98. Mheshimiwa Spika**, tangu kuingia kwa awamu ya tano tumesikia simulizi kutoka kwa Mawaziri na Manaibu Waziri wanaotumikia Wizara ya Nishati juu ya utekelezaji wa umeme wa upepo kwa maeneo yaliyotajwa awali. Ikumbukwe kuwa Novemba 2016, aliyekuwa Naibu Waziri wa iliyokuwa Wizara ya Nishati na Madini ambaye sasa ni Waziri wa Wizara ya Nishati Dr. Medard Kalemani akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum kutoka Singida Mhe. Jesca Kishoa (CHADEMA) alinukuliwa kuwa ujenzi wa mradi wa uzalishaji wa umeme wa upepo utaanza ifikapo Aprili 2017 na kukamika mwaka 2019 baada ya majadiliano kati ya TANESCO na kampuni ya Wind East Africa Limited kukamilika mwezi Desemba 2016 na kuwa mradi huo ungefanyika kwa ubia wa Wind East Africa Ltd na wabia wengine watatu ambao ni Six Telecoms (Tanzania), Kampuni ya Kimataifa ya Aldwych ya nchini Uingereza pamoja na moja ya wajumbe wa Benki ya Kimataifa (IFC) na ungegharimu jumla ya kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 264.77.

**99. Mheshimiwa Spika**, Sasa ni Mei 2019 ikiwa ni miezi takribani 30 baada ya ahadi ya Mhe. Kalemani mbele ya Bunge lako tukufu, Kambi ya Upinzani Bungeni inahoji je mradi huu wa umeme wa upepo umekamilika na kuzinduliwa lini? Serikali inajinasibu kuwa ‘Hapa Kazi Tu’’huku ikishindwa kutekeleza ahadi zake na kuendela kusema uongo ndani ya Bunge lako. Ni hekaya gani mpya Serikali itatoa hivi sasa kuhusu mradi huu na mingine ya upepo hapa nchini?

**UCHAKAVU WA MIUNDOMBINU YA UMEME**

**100. Mheshimiwa Spika**, pamoja na huduma za umeme kuendelea kutekelezwa bado kuna changamoto kubwa ya uchakavu wa miundombinu ya umeme na hivyo kusababisha athari kubwa kwa watumiaji. Uchakavu wa miundombinu ya umeme hupelekea kukosekana kwa huduma za umeme kwa maeneo mbalimbali na hivyo kukwamisha huduma nyingine za kiuchumi na kijamii.

**101. Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwepo kwa Mradi wa TEDAP wa kuboresha njia za usambazaji umeme (Tanzania Energy Development and Access Project) katika mikoa ya Arusha, Dar Es Salaam na Kilimanjaro ambayo imelenga kufanya marekebisho katika vituo vya kupozea umeme kwa kuboresha miundombinu na mitambo; ipo haja ya Serikali kuwekeza katika kubadilisha nguzo za mbao ambazo ndio kero kubwa sana na kusababisha usumbufu kwa watumiaji wa umeme. Kwa nyakati tofauti, ndani ya Bunge lako tumejaribu kushauri na kutoa maoni ya umuhimu wa kubadilisha matumizi ya nguzo za mbao kupeleka kwenye nguzo za zege ili kuzuia uchakavu wa mara kwa mara na gharama, lakini bado tunaona kiasi kikubwa cha nguzo za mbao zikiwa zinaendelea kuwepo kama njia ya usafirishaji wa umeme.

**102. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalitaka Bunge lako kuiagiza Wizara ya Nishati kusitisha mara moja uagizaji wa mbao za umeme na kuendelea kuunganisha umeme kwa mbao hizo na badala yake kuwekeza katika miundombinu imara ya nguzo za zege ambazo zinatatua changamoto ya uchakavu kwa maeneo mengi ya nchini hasa maeneo ambayo yanasumbuliwa na mvua kubwa na mmomonyoko wa udongo.

**ii. Programu ya Nishati Endelevu kwa Wote (Sustainable Energy for All-SE4ALL)**

**103. Mheshimiwa Spika**, malengo ya Programu hii ni kuhakikisha kuwa watanzania wote wanafikiwa na huduma za nishati hususan umeme ifipako mwaka 2030 kama ilivyoelezwa katika Randama ya Wizara ya Nishati. Jambo la kushangaza katika Randama hii ni Wizara kurudia maneno na Bajeti kama ambavyo iliwasilisha kwa mwaka 2018/19. Ukiangalia kiasi kilichotengwa kwa mwaka huu wa 2019/20 cha jumla ya shilingi Bilioni 3 (ambapo fedha za ni ni Bilioni 2.5 na fedha za ndani ni Milioni 500) kiasi ambacho ni sawa na kilichotengwa kwa mwaka huu unaoisha wa fedha.

**104. Mheshimiwa Spika**, Kambi ya Upinzani inahoji iwapo wataalamu wa Wizara wanazingatia weledi katika uwasilishaji wa makadirio ya bajeti na utekelezaji wa shughuli zake au inaweka tu kiwango cha fedha ili Serikali ionekane kuwa na miradi ya utekelezaji na kuongezeka kwa bajeti za Wizara?

**xiv. SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA**

**1. Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)**

**105. Mheshimiwa Spika**, Wataalamu wawili wa Shirika la Petroli Tanzania (TPDC) wakati wakiwasilisha mada kwenye semina ya wahariri iliyofanyika Bagamoyo walisema kwa nyakati tofauti kuwa "Tathmini za kitaalamu na uzoefu wa masuala ya uziduaji na mapato ya rasilimali ya mafuta na gesi, yanaonesha pasipo shaka kuwa nchi za Afrika mapato yake hayawezi kuwa zaidi ya asilimia 25 ya pato la Taifa na hivyo ni makosa kufikiri kuwa nchi itaenda mbele sana kwa kutegemea gesi na mafuta pekee, ila kwa kuchechemua sekta nyingine za uchumi". Wakiwasilisha mada mbili ya 'Mapitio ya Sekta Rasilimali Gesi Asilia Historia yake, Hali ya Sasa na Mipango ya Baadaye' na ya 'Mapitio ya Matumizi, na Mkondo wa Chini wa Gesi Asilia' wameonesha wazi tatizo kubwa limezuka nchini la 'kutawala matarajio yaliyokithiri'.

**106. Mheshimiwa Spika**, Wataalamu hao wanasema kulifanyika makosa kutoa kauli zilizokithiri wakati mambo bado yako mbali na hali ya uchumi hairuhusu kirahisi kuwekeza kutokana na mdororo wa uchumi duniani kufuatia sababu hasi lukuki zinazoendelea kudumaza mahitaji ya mafuta duniani, ikiwemo kuongezeka uzalishaji mafuta Marekani na kuanza kuuza mafuta yake katika soko la dunia na hivyo kupunguza mahitaji katika soko la dunia kwa asilimia 25.

**107. Mheshimiwa Spika,** Sababu nyingine ni kwamba, wakati huu dunia imeshuhudia matumizi makubwa ya teknolojia kule Marekani na Canada kufanya mabanzi ya mchanga (shale) kutengeneza mafuta, hivyo kuleta tafrani na utata kwa wawekezaji na kudhuru maendeleo ya miradi ghali ya gesi

kama hiyo ya Tanzania ambayo gesi yake nyingi iko ndani baharini tcf 47.08 kilomita 120 toka nchi kavu kwenye kina cha mita 4000 na ile iliyoko nchi kavu ni tcf 8.04 na hivyo uendelezaji wake ni tatizo.

**108. Mheshimiwa Spika,** wataalam walifafanua kuwa mafuta ndio yanayofanyika kibiashara duniani kote, huku gesi asilia bado ikifanyika kieneo kidogo na hivyo bei ya mafuta ndio inayoamua uwekezaji katika sekta ya nishati. Matokeo yake ni kuanguka kutoka zaidi ya dola 100 miaka miwili iliyopita na kuwa chini ya dola 40 kwa pipa la mafuta mwaka huu. Hivyo kuuathiri uwekezaji wa Lindi kwani Msumbiji nayo imegundua gesi nyingi ya kiasi cha zaidi ya tcf 200 ukifananisha na tcf 57.2 ya Tanzania na hivyo kuwa mshindani mkubwa kwenye uwekezaji.

**109. Mheshimiwa Spika**, kuongeza kuwa ushindani wa kupata mitaji na kuvutia wawekezaji katika Bara la Afrika, ni jambo gumu linalohitaji ushawishi mkubwa na hivyo kufanya watawala kuwa na wakati mgumu kufanya maamuzi sahihi kwa kuvutwa na kushawishiwa na matumizi ya mbinu mbalimbali kuweza kushawishi (lobby) na kuondokana na hali ya mkwamo mbele ya wananchi wao. Pamoja na hali hiyo bado Serikali iliyoko madarakani imeendelea kuwa na baadhi ya wanasiasa wenye kuwaita wawekezaji kuwa ni mabeberu na wanyonyaji wa rasilimali ya nchi badala ya kutafuta namna bora ya kufanya nchi na wananchi kunufaika na rasilimali ambazo Mwenyezi Mungu ameijalia nchi yetu.

**110. Mheshimiwa Spika**,Statoil na mshirika wake ExxonMobil walifanya ugunduzi mkubwa wa gesi asilia katika visima vya Zafarani, Lavani, Tangawizi, Piri, Giligilani na Mronge katika Kitalu namba 2, chenye eneo la takriban kilometa za mraba 5,500, ambalo lipo umbali wa zaidi ya kilometa 100 kutoka ufukweni katika kina cha maji kati ya meta 1,500 hadi 3,000.

**111. Mheshimiwa Spika**, kwa sasa Tanzania imeshagundua akiba ya gesi yenye futi za ujazo zaidi ya trilioni 57 imegundulika.

**112. Mheshimiwa Spika**, si rahisi kusafirisha gesi katika hali yake ya kawaida, ni lazima kuisindika kwa kuibadili kuwa katika hali ya kimiminika (Liquefied Natural Gas – LNG), hivyo mtambo wa LNG una umuhimu mkubwa kwa biashara ya gesi kwa kusafirisha kwenye soko la kimataifa pamoja na matumizi ya ndani. Ni ukweli kwamba, katika ujenzi wa mtambo wa LNG, gharama zote zitalipwa na wawekezaji wakati Serikali jukumu lake ni kutoa ardhi mahali mtambo huo utakapojengwa inaonekana jambo hilo kwa mwaka huu 2018/19, Serikali imetenga jumla ya shilingi 6,500,000,000/- ikiwa ni fedha za kulipa fidia kwa waathirika wa makazi katika eneo la mradi na pia zikiwa ni fedha za kufanya tafiti ili kusaidia timu ya Majadiliano (GNT). Suala hilo halikuanza mwaka ambao tunamaliza utekelezaji wake na katika mwaka mpya wa fedha Serikali imerudia tena kuja na mapendekezo hayo hayo. Hoja ya msingi hasa ni je, wawekezaji ambao fedha za majadiliano tayari zimetengwa wapo tayari?

**113. Mheshimiwa Spika**, tulikwisha oneshwa manufaa faida katika kutumia gesi asilia katika kuendeshea magari badala ya kutumia mafuta ya petroli, kwamba unafuu katika bei ya kununulia nishati hii ni rahisi zaidi ya asilimia 45 kulinganisha na bei ya mafuta ya petroli. Ulinganifu wa gesi asilia na petroli. Kilo 1 ya gesi asilia iliyoshindiliwa ni sawa na lita 1.54 ya petroli, bei ya kilo moja ya gesi asilia ni ndogo kuliko lita moja ya petroli. Pia gharama za ukarabati (service) wa magari zinapungua endapo utatumia gesi asilia badala ya mafuta ya petroli. Hii ni kwa sababu gesi asilia ni safi, muwako wake hauna masizi (carbon) kulinganisha na mafuta, hivyo itachukua muda mrefu kufanya ukarabati wa gari linalotumia gesi asilia (kilomita 5000) ukilinganisha na gari linalotumia mafuta (kilomita 3000).

**114. Mheshimiwa Spika,** TPDC walikwishaanza kuleta vifaa vya kuwezesha magari kutumia gesi asilia badala la Petroli au Dizeli na tukapewa matumaini kuwa kituo cha kujazia gesi kwenye magari kimejengwa Ubungo. Lakini hadi sasa Bunge halifahamu chochote kuhusu mradi huo mkubwa wa matumizi ya gesi asilia kwenye vyombo vya usafiri na

majumbani. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa ufafanuzi wa Mradi huo ambao ulikuwa ni mkombozi kwa wamiliki wa vyombo vya usafiri na watumiaji wa gesi majumbani.

**Changamoto za Madeni na Ukusanyaji usioridhisha**

**115. Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Petroli ya mwaka 2015, inatoa madaraka kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Nchini - TPDC kusimamia na kuendeleza sekta ya mafuta na gesi asilia kwa niaba ya Serikali. Katika kutekeleza hayo, sheria tajwa hapo juu, imeipa TPDC jukumu la kuhakikisha inaendesha kibiashara shughuli za Mkondo wa Juu, yaani utafutaji mafuta na gesi, Mkondo wa Kati (uchakataji na usafirishaji mafuta na gesi) pamoja na Mkondo wa Chini (usambazaji gesi na mafuta kwa watumiaji). Kwa maana hiyo, kazi za TPDC ni pamoja na kusimamia shughuli za utafutaji, uendelezaji na usambazaji wa mafuta na gesi asilia nchini.

**116. Mheshimiwa Spika**, Pamoja na umuhimu wa mamlaka ya TPDC bado inakabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo changamoto za Madeni na Ukusanyaji usioridhisha wa wadaiwa. Kwa taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo zinaonesha kuwa hadi kufikia Juni 30, 2018, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) ilipata hasara ya shilingi bilioni sitini na nne na milioni mia tano arobaini na tatu **(64,543,000,000**) huku ikiwa na madeni yanayofikia shilingi trilioni tatu, bilioni mia tano na arobaini na nne, milioni mia nane tisini na mbili **(3,544,892,000,000**) hivyo kuwa katika moja ya mashirika yenye hali mbaya ya kifedha. Aidha deni hilo limesababisha makampuni yenye mkondo wa juu kutishia kuzuia kuuza gesi asilia kwa TPDC kwa sababu ya kushindwa kulipia ankara zake kwa wakati. Kambi Rasmi ya Upinzani pamoja na kusikitika juu ya hasara inayoendelea kupata shirika, inapenda kufahamu mkakati wa Serikali wa kulifanya shirika hili lisijiendeshe kwa hasara.

**117. Mheshimiwa Spika**, wakati TPDC ikipata hasara hiyo, taarifa zinaonesha kuwa, hadi kufikia Disemba 2018, TPDC ilikuwa inadai jumla ya shilingi bilioni 527.096. Wadaiwa sugu

wakiwa ni Shirila la Umeme Tanzania, TANESCO, Kampuni ya kuzalisha umeme ya SONGAS, Kampuni ya Ndovu Resources Ltd na Kampuni ya Kilimanjaro Oil Ltd na wadaiwa wengine. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupata majibu kutoka kwa Serikali, kuhusu mkakati wa makusudi wa kuhakikisha wadaiwa hawa sugu wanalipa madeni yake ili kuliwezesha Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kufanya shughuli zake kwa mujibu wa sheria.

## Uwekezaji Mdogo TPDC katika Shughuli za Maendeleo

**118. Mheshimiwa Spika**, Uwekezaji kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya shirika nao unapata changamoto ya ufinyu wa bajeti, uwekezaji mdogo TPDC na utashi wa kisiasa. Changamoto hizi ni miongoni mwa sababu zinazokwamisha ufanisi katika utekelezaji wa mikakati inayojiwekea. Kwa mfano, mwaka 2016, Shirika la Maendeleo ya Petroli Nchini (TPDC) iliandaa Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asilia (NGUMP 2016 – Natural Gas Utilization Master Plan). Mpango huu uliainisha kwa kina usambazaji wa Gesi Asilia Nchini. Hata hivyo, mpango huu umekua ukisuasua kutekelezeka hadi leo kwa sababu ya ukosefu wa rasilimali fedha, kutokana na ukosefu wa utashi wa kisiasa, sasa usambazaji wa Gesi Asilia inakumbwa na changamoto wakati Taifa linaonekana linaelekeza nguvu zake katika maeneo mengine, wakati mradi huu haukukamilika kwa ukamilifu wake. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha Mpango wa Matumizi ya Gesi Asilia nchini unatekelezwa kwa ukamilifu.

## Majadiliano yasiyo na kikomo

**119. Mheshimiwa Spika**, Kwa kipindi kirefu sana, kupitia taarifa zinazotolewa na Wizara ya Nishati, kumekuwepo kwa majadiliano yasiyo na kikomo kwa Serikali na Wawekezaji. Hii inaathiri utekelezaji wa mikakati ya baadhi ya shughuli za gesi asilia iliyopo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Mathalani Utelezaji wa Mradi wa Kusindika Gesi Asilia kwenye Hali ya Kimiminika (Liquefied Natural Gas Plant-LNG). Vivyo hivyo majadiliano haya yasiyo na kikomo, yanasababisha ucheleweshwaji wa uwekezaji wa mitaji ya kigeni (FDI)

ambayo ni kichocheo cha uchumi na maendeleo ya miradi mbalimbali nchini. Lakini pia upatikanji wa FDIs ungeisaidia Serikali kuelekeza rasilimali zaidi katika sekta zilizo na ufinyu wa Bajeti hasa katika maeneo ya kimkakati ya kijamii. Ni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba, Serikali ilipatie shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kipaumbele katika uwekezaji ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kisheria kama inavyotakiwa, ufinyu wa bajeti na uhaba katika uwekezaji kunalifanya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kuwa tegemezi na kushindwa kuhimili ushindani kwa kasi inayohitajika katika biashara.

**120. Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 2 Desemba, 2013, aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini wakati huo Prof. Sospeter Muhongo na ujumbe wake nchini Algeria, alisema kuwa makubaliano yamefikiwa baina ya Tanzania na Algeria ya kuanzisha Kampuni ya Ubia itakayohusika na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme na Kampuni ya Ubia ya kujenga mtambo wa kusindika gesi ya "Liquefied Natural Gas" (LNG) na kuiuza gesi kwa wananchi kwa kutumia mitungi.

**121. Mheshimiwa Spika**, Katika hatua nyingine, tuliambiwa kuwa Mawaziri hao waliziagiza Kampuni za Mafuta na Gesi likiwemo Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na kampuni za mafuta na gesi za Algeria za NAFTAL na SONATRAC kukamilisha majadiliano ya kuanzisha kampuni ya ubia ya kujenga mtambo wa LPG na kuuza gesi hiyo kwa wananchi kwa kutumia mitungi, ambapo kampuni zote za ubia zimetakiwa kuanza kazi ifikapo Januari, 2015[1].

**122. Mheshimiwa Spika,** ni muda mwafaka sasa Bunge hili kupewa mrejesho wa makubaliano yaliyofikiwa baina ya nchi zetu hizi yamefikiwa hatua gani ya utekelezaji?

**123. Mheshimiwa Spika,** wakati huohuo Waziri wakati huo, Profesa Sospeter Muhongo alizindua ofisi za "Liquefied Natural Gas" LNG – Tanzania jijini Dar es Salaam. LNG ni muunganiko

[1] MEM News Bulletin, toleo No. 24, Julai 11-17,2014

wa makampuni matano ya BG Group, Statoil, Exxon-Mobil, Ophir na Pavilion kwa ajili ya kufanikisha mi-pango itakayopelekea ujenzi wa kiwanda cha kuchakata gesi. Makampuni hayo yanayounda LNG yatashirikiana na Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Nchini (TPDC) na Wizara ya Nishati.

**124. Mheshimiwa Spika,** hizo hadithi kwa kiasi kikubwa zimepelekea kuaminisha wananchi kuwa tunakwenda kwenye uchumi wa gesi na wimbo huo unaendelea kuimbwa na Serikali iliyopo madarakani wakati uhalisia wa jambo hilo haupo.

**Malipo yasiyostahili kwa kampuni ya Maurel & Prom ya dola za kimarekani milioni 27.18**

**125. Mheshimiwa Spika,** Maurel & Prom (Operator, 48.06% interest) ni kampuni inayoendesha visima viwili vya gesi vilivyopo Mnazi Bay vinavyopeleka gesi pale kituo cha Madimba Mtwara ***(processing centre -operated by GASCO, a subsidiary of TPDC)*** linapoanzia bomba la gesi asilia kati ya Mtwara na Dar es Salaam.

**126. Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 15.1 cha Makubaliano ya Mauziano ya Gesi (GSA) uliosainiwa Septemba 12, 2014, kati ya TPDC na Maurel & Prom (M&P) kinataka TPDC kuweka dhamana ya fedha kwa kuweka kiasi cha fedha kwenye akaunti ya pamoja (Escrow) au kwa Barua ya Mkopo kutoka Benki (letter of credit) au kwa mkataba wa dhamana ya malipo (payment guarantee agreement).

**127. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa ukaguzi wa CAG umebaini kuwa, TPDC ilitoa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 27.18 (sawa na Shilingi bilioni 56.70) kwa kulipa akaunti ya M & P kinyume na masharti tajwa hapo juu huku ikichukulia fedha hizo kama malipo ya awali (prepayment). Pia, ilibainika kuwa fedha zilizolipwa kwa M&P zilikopwa kutoka Benki ya Maendeleo ya TIB.

**128. Mheshimiwa Spika,** Ukosefu wa makubaliano rasmi juu ya namna fedha za dhamana zinavyotakiwa kuhifadhiwa

unaiweka TPDC kwenye nafasi mbaya endapo kutatokea mgogoro wowote. Pia, kukopa fedha kwa lengo la kuweka dhamana kunaongeza gharama kwa taasisi kwa sababu ya riba. Mtindo huu wa kuendesha taasisi zetu ndio umekuwa ukisababisha taasisi zetu kutokupiga hatua za kwenda mbele. Kambi Rasmi ya Upinzani inaadharisha uwepo mwingine wa IPTL kutokana na mkataba huo kuingiwa kwenye mazingira yenye kuacha mashaka baina ya Serikali na Kampuni hiyo ya Kifaransa.

**Masuala ya ujumla kuhusu matumizi ya gesi asili nchini:**

**129. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Nishati kutekeleza mpango kabambe wa TPDC (NGUMP 2016) ili kuwezesha miundombinu ya gesi asilia kujengwa na kuharakisha matumizi ya gesi asilia katika kaya na pia kupunguza mahitaji ya matumizi ya mkaa na kuni hasa kwa mikoa mikubwa ambapo mahitaji huongezeka kila siku kwa ajili ya shughuli za kiuchumi.

**130. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kutoa kipaumbele katika uwekezaji wa vitalu vya kimkakati vya asilia vilivyopo chini ya mamlaka ya TPDC kwa kuharakisha mazungumzo na wawekezaji ili kufikia muafaka wa kupata uwekezaji wenye manufaa na pia kujali muda kwa kutumia fursa ipasavyo, kwa kuwa Kambi Rasmi inaamini kwamba kuendelea kuchelewa kuwekeza kunaweza kutoa fursa kwa nchi nyingine zenye gesi kama nchi ya Msumbiji na kulikosesha taifa faida nono**.**

**131. Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Shirika la Maendeleo ya Petroli Nchini liweke juhudi za kutosha katika utafutaji wa masoko ya uhakika kwa ajili ya usambazaji wa gesi asilia. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali ilikuwa inakusudia kuunganisha viwanda takribani kumi pamoja na kaya zaidi ya 2000 katika miundombinu ya gesi asilia. Kwa vyovyote vile shabaha hizo haziridhishi kwa kuzingatia idadi ya viwanda ambavyo Serikali kwa nyakati mbalimbali imetoa takwimu zake na idadi ya kaya za

watanzania, ni wajibu wa Serikali kupitia TPDC kuhakikisha malengo yanatimia.

**a) Miradi ya Gesi Asilia Nchini**

**i. Utekelezaji wa miradi ya gesi asilia na makadirio yake 2018/ 2019/2020**

**132. Mheshimiwa Spika**, Mradi wa kusindika gesi asilia kwenye hali ya kimiminika unaofahamika kwa lugha ya kigeni kama, Liquefied Natural Gas (LNG) ni miongoni mwa miradi iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2019/20. Ili kutekeleza mradi huu, Serikali imetenga bajeti ya Shilingi bilioni 6.5 kwa ajili ya kutekeleza zoezi la ulipaji fidia, kufanya tafiti mbalimbali za kiuchumi ili kusaidia timu ya Serikali katika majadiliano na wawekezaji. Katika hali ya kushangaza, Mradi huu ulipendekezwa kama ulivyo kwa mwaka wa fedha 2018/ 19 kwa bajeti ya kiwango cha Shilingi bilioni 6.5. Mradi huu umekuwa katika majadiliano tangu miaka 2 iliyopita na hakuna taarifa za kutosha kuhusu maafikiano na hatua zilizofikiwa katika majadiliano baina ya Serikali na wawekezaji. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina maoni kwamba Serikali lazima itambue na kuzingatia muda katika utekelezwaji wa miradi ya maendeleo, aidha Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tunaitaka Serikali kutolea ufafanuzi wa bajeti inayopangwa kila mwaka na ufanisi wake kwa kuwa hakuna taarifa za kina zinatolewa kuhusu miradi mbalimbali, ukiwemo huu.

**ii. Ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia katika Jiji la Dar es Salaam**

**133. Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unalenga kujenga miundombinu ya kusambaza gesi asilia katika jiji la Dar es Salaam na ili kutekeleza mradi huu, Bajeti ya Shilingi bilioni moja na milioni mia moja (1,100,000,000) zimetengwa kwa mwaka wa fedha 2019/20. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 mradi kama huu uliwekwa pia kwa bajeti ya Shilingi Bilioni 2 zilizotengwa. Kwa kuwa Miradi hii ni ya watanzania, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaungana na watanzania na wadau mbalimbali na kupendekeza kwamba Serikali itoe maelezo na taarifa kuhusu hatua za usambazaji wa gesi asilia

katika maeneo husika, kuliko kuandika tu, majina ya miradi kwa kujirudia kutoka mwaka mmoja wa fedha kwenda mwaka mwingine wa fedha.

**iii. Bomba la gesi kutoka Mtwara - Dar es salaam – Tanga-Mwanza-Kagera- Uganda**

**134. Mheshimiwa Spika**, Bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam lilijengwa na Kampuni ya China Petroleum and Technology Development Company (CPTDC) kwa gharama ya takriban Dola za Kimarekani takriban bilioni 1.283 ambapo kati ya hizo, dola za Kimarekani bilioni 1.225 zilipatikana kama mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Exim ya China. Marejesho ya mkopo huo yalitegemea kupatikana kwenye mauzo ya gesi asilia baada ya kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa bomba na kuanza kutumika kibiashara.

**135. Mheshimwa Spika**, kwa sasa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ndilo mteja mkuu wa gesi asilia; ambapo anatumia wastani wa futi za ujazo milioni 46.61 kwa siku, sawa na asilimia sita (6%) tu ya ujazo wa bomba; ambapo, kiasi hicho ni pungufu futi za ujazo milioni 737.39 kwa siku ili kujaza bomba. Matumizi haya ni tofauti na makubaliano ya awali ambayo ilikua TANESCO liweze kutumia takribani futi za ujazo milioni 80 kwa siku kama ilivyokuwa kwenye makubaliano ya mkataba wa mauziano ya gesi asilia (GA).

**136. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Bunge lako tukufu inapenda kupata ufafanuzi kutoka Serikali kuhusu jitihada ambazo Serikali imechukua ili kuhakikisha wateja zaidi wa gesi asilia wanapatikana ili mkopo uweze kulipwa kabla ya marekebisho ya ulipaji ambayo yataongeza gharama kubwa kwa Serikali.

**137. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inafahamu kwamba mkataba wa mauziano ya gesi asilia kati ya TPDC na TANESCO uko wazi kwamba TANESCO itatumia gesi asilia kwenye mitambo yake sita (6) ya kuzalisha umeme ya Kinyerezi I, Kinyerezi II, Ubungo I, Ubungo II, Tegeta kwa kima cha chini cha matumizi cha futi za ujazo milioni 80 kwa

siku na futi za ujazo milioni 138.8 kwa siku kama kiwango cha juu. Hata hivyo, hadi sasa kiwango cha matumizi ya gesi asilia kuzalisha umeme hakilingani na kilichokubaliwa katika mkataba; kwa sasa matumizi ni kiwango cha asilimia thelathini na nne (34%) ya kiasi cha gesi yote iliyolengwa kutumiwa na TANESCO.

**138. Mheshimiwa Spika**, Mitambo mingine iliyokuwa imekadiriwa kutumia kiasi cha 66% bado haijaanza kutumika; na haijulikani ni lini mitambo hiyo itaanza kutumia gesi asilia.

**139. Mheshimiwa Spika,** tukumbuke kwamba gharama za ujenzi wa bomba hilo toka Mtwara hadi Dar es Salaam ulikuwa ni mkopo toka Exim Bank ya China na mkopo huo unatakiwa kulipwa, hoja ya msingi ni kwamba matumizi ya gesi hiyo bado ni kidogo kulinganisha na mahitaji yake.

**140. Mheshimiwa Spika**, ukianangalia Randama uk. 68 inaonesha kuwa mradi huu unahusu ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Dar es Salaam kwenda Uganda kupitia Tanga, bomba hilo linatakiwa kutumia mkuza uliopo wa Bomba la mafuta ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania.

**141. Mheshimiwa Spika,** kwa maana rahisi ni kuwa bomba jipya linalojengwa ni kutoka Dar es Salaam hadi Tanga, na gesi asilia iliyopo ni kwamba matumizi yake hapa kwetu yameshatosheleza na zaida ndiyo inatakiwa ipelekwe Uganda.

**142. Mheshimiwa Spika**, katika mradi huo zimetengwa jumla ya shilingi 1,500,000,000/- kwa ajili ya upembuzi yakinifu utakaoonesha gharama halisi za mradi na namna bora ya kutekeleza mradi huo.

**iv. Mradi wa kusafirisha Gesi Asilia kutoka Dar Es Salaam Tanzania hadi Uganda**

**143. Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unahusisha ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kwenda nchini Uganda kutokea Dar es Salaam, bomba hilo litakwenda sambamba na bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki linalotoka Hoima

Uganda hadi Chongoleani-Tanga (Tanzania) na Serikali imetenga Bajeti ya Shilingi 800,000,000 mwaka 2019/20. Hata hivyo, mradi huu pia ulitengewa Shilingi Bilioni 1.5 katika mwaka 2018/19 kwa ajili ya upembuzi yakinifu. Tunashauri Serikali kufafanua bajeti nzima kwa ajili ya mradi huu na pia kutoa ufafanuzi wa hatua za utekelezaji wa bajeti zinazopangwa kila mwaka.

**MATUMIZI YA GESI ASILIA KWENYE MAGARI**

**144. Mheshimiwa Spika**, taarifa zilizopo ni kwamba upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuweka mtandao wa mabomba ya kusambaza gesi na vituo vya kujazia gesi magari ulifanyika toka mwaka 2006/2007 na kuhusisha magari 8,000 na makazi yapatayo 30,000. Ujenzi wa mradi huo ulitarajiwa kuanza Julai 2015 ambapo zoezi la kumtafuta Mkandarasi pamoja na fedha za ujenzi takribani Dola za Marekani milioni 76 zilikuwa zikihitajika.

**145. Mheshimiwa Spika,** Randama uk. 27 inaonesha kuwa kwa mwaka 2017/18 TPDC imeedelea na juhudi za kutafuta wateja zaidi wa gesi asilia kwa ajili ya matumizi ya viwandani pamoja na ujenzi wa miundombinu ya kusambazia gesi hiyo kwa wateja. Usambazaji wa gesi asilia kwenye viwanda vya Mkuranga ulitengewa shilingi 6,274,252,000/- lakini hadi mwezi Machi, 2018 hakuna hata shilingi iliyokuwa imetolewa.

**146. Mheshimiwa Spika,** aidha, bomba hilo linalosambaza gesi limehusisha uunganishaji wa nyumba 70 tu katika mtandao wa gesi asilia. Kwa mwaka huu wa bajeti 2018/19 jumla ya nyumba 60 zilipangwa kuunganishwa katika maeneo ya Mikocheni na Mwenge, na imetengwa jumla ya shilingi 1,500,000,000/-.

**147. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupatiwa ufafanuzi kuhusu uwekezaji wa shilingi bilioni 1.5 katika usambazaji wa gesi kwa nyumba 60 tu kwa mwaka. Hili la kusambaza miundombinu ya matumizi ya gesi asilia majumbani katika Jiji la Dar Es Salaam, mikoa ya Mtwara na Lindi ambako gesi asilia inaanzia lazima lionekane likifanyika kwa haraka ili baadae ifuatie mikoa mingine.

**b) Miradi ya Usafirishaji wa Mafuta.**

**i. Mradi wa bomba la Mafuta kutoka Hoima – Chongoleani**

**148. Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi ni Mradi wa Sekta binafsi unatekelezwa katika nchi mbili (Uganda na Tanzania). Mradi huo uliokadiriwa kugharimu **Dola za Marekani 3.55 bilioni** na kuleta **ajira za kati ya watu 6,000 na 10,000** ndani ya **miaka mitatu (3).** Mafuta Ghafi ya Hoima (ya aina yake), yatasafirishwa kutoka Uganda kwenda sokoni nchi za nje,kupitia Tanzania. Mradi wa Bomba umbali wake ni **kilometa 1,445** ambapo **kilometa 298** zitakuwa nchini Uganda, na **kilometa 1,147** zitakuwa nchini Tanzania.

**149. Mheshimiwa Spika,** taarifa zinasema kuwa katika mchakato huo wa mradi ni dhahiri kuwa shughuli kadhaa za uchumi katika sehemu litakapoptia bomba hilo na mwisho wake zitaimarika zaidi.

**150. Mheshimiwa Spika,** kutokana na ukweli kwamba kilometa za urefu za bomba hilo zipo nchini Tanzani, na kati ya fedha Dola za Kimarekani 3.55 zilizotarajiwa kutumika ili kukamilisha mradi huo, kwa kuwa sekta binafsi inatarajiwa **kushiriki kikamilifu**, sekta hiyo itaunganishwa na TPSF. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza, Serikali inachangia kiasi gani katika fedha tajwa hapo juu na sekta binafsi inatakiwa kuchangia kiasi gani? Kwani kwa mujibu wa Randama inaonesha kuwa mwaka huu wa fedha zimetengwa jumla ya shilingi 54,200,000,000/- kwa ajili ya ujenzi wa bomba la mafuta toka Uganda hadi Tanga. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani imedokezwa kwamba mazungumzo juu ya mradi huu yameanza kukwama kutokana na sababu mbalimbali, hivyo inataka maelezo iwapo taarifa hizi ni sahihi na ni upi ufumbuzi wa mkwamo huo?

**ii. Mradi wa bomba la kusafirisha Mafuta ghafi la Africa Mashariki kutoka Uganda hadi Tanga Tanzania (EACOP):**

**151. Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ni mwendelezo wa ujenzi wa bomba la mafuta ghafi kutoka nchini Uganda hadi

Tanzania, ambapo, bajeti ya Shilingi 7,000,000,000 zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha majadiliano ya kimkataba kati ya nchi washirika Uganda na Tanzania) na makampuni yaliyowekeza kwenye mradi huu (Total SA na Tullow Plc).

**152. Mheshimiwa Spika,** katika hali inayozua maswali mengi taarifa za Serikali zinaonesha kwamba, katika bajeti ya mwaka 2018/19, Shilingi bilioni 54 zilitengwa kwa ajili ya kazi na majukumu yanayofanana na majukumu yanayotarajiwa kutekelezwa mwaka huu. Pamoja na jitihada za Serikali katika mradi huu, ili kukuza uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wa mradi huu, tunafahamu majadiliano haya yamechukua sura mpya na hivyo basi tunashauri Serikali iweke wazi hatua za makubaliano zilizofikiwa hadi sasa, na kipi kinakusudiwa kwenye majadiliano haya mapya. Pia ijulikane jumla ya fidia zitakazolipwa na mchango wa kila nchi wabia katika utekelezaji wa mradi.

**Mheshimiwa Spika;** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa za kuanza kwa utekelezaji wa mradi huo katika hatua za awali yaani Surveys (Geological Survey, Geophyisical Survey, na GeoTechnical Survey); tunaiomba Serikali ilipatie Bunge lako tukufu hali ya mambo ilivyo katika hatua hizi za awali za utekelezaji wa mradi huo wa Bomba la Mafuta kutoka Uganda kuja Chongoleani, Tanga.

**Mheshimiwa Spika;** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako tukufu ni ajira kiasi gani zimeshaanza kutolewa kwa raia wa Tanzania na endapo Serikali imepata mapato yoyote kutoka kwenye makampuni yaliyokuwa yakitekeleza hatua hizo za tafiti za awali kabla ya ujenzi kuanza.

**Mheshimiwa Spika;** pia Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza kwa undani juu ya uzingatiaji wa sera, sheria na kanuni za "local content" katika uwekezaji mkubwa kama huu. Serikali ililèze Bunge lako tukufu ni kwa kiasi gani makampuni ya Kitanzania yameanza kushiriki katika hatua za awali za mradi huu.

**Matumizi ya Gesi inayotokana na Petroli (Liquified Petroleum Gas – LPG)**

**153. Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa gesi ya kupikia (LPG), jumla ya tani 65,522 ziliingizwa nchini kwa ajili ya matumizi ya ndani, mwaka 2014 na kwa mwaka wa fedha 2015 ziliagizwa tani 70,063 sawa na ongezeko la asilimia 7 kwa kulinganisha na uagizaji wa mwaka 2014 na mwaka 2016 ziliagizwa tani 90,296 sawa na ongezeko la asilimia 29 kwa kulinganisha na uagizaji wa mwaka 2015[2].

**154. Mheshimiwa Spika,** ni ukweli kwamba sasa hivi wafanyabiashara wanazidi kuwekeza mitaji katika biashara hii ya gesi itokanayo na mafuta (LPG) ili kuhakikisha kuwa wanakwenda kutosheleza soko ambalo bado ni kubwa sana hapa nchini. Kwa hili Kambi Rasmi ya Upinzani inaona lingekuwa jambo la msingi kama mitaji ya hawa wafanyabiashara ingekuwa-mobilized pamoja kuweza kuwa na uagizaji wa pamoja (Bulk Procurement) wakati huu ambapo bado taifa linasubiria kujengwa kwa mtambo wa kuchakata gesi (LNG) ili nchi yetu kuanza kutumia mitungi ya gesi ya hapa nchini sanjari na mitungi ya gesi itokanayo na mafuta (LPG) kutoka nje.

**155. Mheshimiwa Spika,** inaonesha kuwa matumizi ya LPG kwa nchi yetu ni kidogo sana kwa kulinganisha na majirani zetu wa Kenya, ambao matumizi ni mara nne ya matumizi yetu. Matumizi ya gesi kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ni wastani wa 2.3Kg kwa mwaka, kwa mujibu wa taarifa ya of World LPG Association (WLPGA),kwa kulinganisha na wastani wa matumizi ya 55Kg kwa mwaka kwa nchi za Afrika ya Kaskazini.

**156. Mheshimiwa Spika,** wakati wastani kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ni matumizi ni 2.3kg kwa mwaka, Tanzania matumizi ni wastani wa 1.4kg kwa mwaka, wastani ambao ni chini na nchi ambazo tuko nazo kundi moja.

---

[2] Ewura- Downstream Petroleum Sub Sector Performance Review Report for Year 2016

**157. Mheshimiwa Spika,** mfano mzuri ni ulinganisho wa gunia moja la mkaa linalouzwa kwa shilingi 40,000/- hadi 60,000/- na mtungi wa gesi ya mafuta (LPG) wa kilo 15 unaouzwa kati ya shilingi 45,000/- hadi 55,000/- kulingana na eneo. Hivyo basi kama tukiwa na mkakati mzuri wa kuhamasisha matumzi ya gesi itokanayo na mafuta (LPG), ikiwemo kuwa na bei elekezi ni dhahiri tutaokoa misitu yetu.

**158. Mheshimiwa Spika,** tumeweka takwimu hizo kuonesha ni jinsi gani matumizi ya nishati kuni ilivyo kubwa kwa nchi yetu na wakati huo hakuna mkakati wote wote wa kuhamasisha matumizi ya nishati gesi kwa matumizi ya nyumbani ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

## xv. MADENI YA WAKANDARASI

**159. Mheshimiwa Spika**, Kwa muda mrefu miradi ya Wizara ya Nishati imeendelea kukwama ama kutokutekelezwa kwa wakati kutokana na kucheleweshwa kwa malipo ya wakandarasi na hivyo kupelekea kuwa na madeni makubwa ya wakandarasi na hivyo kushindwa kuendana na kasi ya miradi hiyo. Kusuasua kwa miradi ya REA kunatokana na changamoto kubwa ya Wizara kutowalipa kwa wakati Wakandarasi kama ambavyo inaelekezwa katika mikataba baina yao. Pamoja na lawama zinazotolewa na Wizara kwa wakandarasi wa miradi ya REA kuwa hawana uwezo wa kutekeleza miradi hiyo; Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji ikiwa shida ni wakandarasi kutokidhi vigezo; ni kwa nini wanashinda zabuni iwapo hawana uwezo wa kukamilisha miradi hiyo? Ikumbukwe kuwa kwa nyakati tofauti tumeshuhudia Rais na Mawaziri wakisitisha mikataba ya wakandarasi wasio na uwezo wa kutekeleza majukumu yao ya kimkataba. Iwapo katika utekelezaji wa miradi ya REA shida ni wakandarasi ni kwa nini wakandarasi hao wasisitishiwe mikataba kwa kushindwa kuitekeleza?

**160. Mheshimiwa Spika**, ikumbukwe kuwa wakati wa ukaguzi wa miundombinu ya awamu ya tatu ya REA mwezi Machi 2018, Mhe. Waziri aliahidi kuwa watasitisha mikataba ya wakandarasi watakaoshindwa kuunganisha umeme kwa vijiji

vilivyo kwenye miradi. Kambi ya Upinzani inahoji; toka atoe tamko hilo je, mpaka sasa ni wakandarasi wangapi wamesitishiwa mikataba? Na je, toka kuanza kwa utekelezaji wa awamu ya tatu REA, Wizara imeweza kulipa kiasi gani cha malimbikizo ya madeni ya miradi iliyopita ya REA?

**161. Mheshimiwa Spika**, katika mjadala wa Bajeti ya Nishati katika Bunge lako kwa Bajeti ya mwaka 2018/19 tulishuhudia kisanga cha Mawaziri wa Nishati na Fedha kwa kutupiana lawama za ucheleweshaji wa Fedha za miradi ya REA huku Wizara ya Fedha ikidai kuwa haijawahi kuchelewesha fedha za miradi na zote hupelekwa kwa Wakala wa Umeme Vijijini (REA) kwa wakati. Naomba nimnukuu Naibu waziri wa Fedha, Mhe. Ashatu Kijaji kuwa kwa mwaka wa fedha wa 2017/18, Julai REA ilipelekewa shilingi Bilioni 21.5, Agosti ikapelekwa shilingi Bilioni 36.7 na Septemba ilipelekwa shilingi Bilioni 35. Na kwa maneno yake, kuanzia Julai hadi Aprili 2018 REA walikuwa wamepewa jumla ya Bilioni 99.9. Kambi ya Upinzani Bungeni inapenda kuhoji, iwapo REA inapelekewa fedha kwa wakati ni kwa nini wakandarasi wanaendelea kuidai?

**162. Mheshimiwa Spika**, Kambi ya Upinzani inalitaka Bunge lako kuweka mkakati wa kukutana na wakandarasi wa miradi ya REA kupitia Kamati ya Kisekta ya Nishati na Madini ili kuweza kuweka bayana mapungufu ya kikandarasi yanasababisha kuwa na utekelezaji hafifu wa miradi ya REA na kuleta ripoti katika Bunge lako kabla ya kuhitimisha Bunge la Bajeti ya mwaka 2019/2020.

## xvi. HITIMISHO

**163. Mheshimiwa Spika,** kutokana na Serikali kutokuwa na utaratibu wa kutekeleza miradi yake ikakamilika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kwamba kwa maeneo ambayo gesi ilishaanza kuvunwa ambako ni Mnazi Bay na SongoSongo, Serikali iwe na mkakati kabambe wa kuuza gesi kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Takwimu zinaonesha kwamba gesi inayotumika kwa mwaka mzima ni kati ya asilimia 4.8 na 6 tu ya uwezo wa bomba. Hii ni hasara kwa

Taifa ikizingatiwa kuwa bomba la gesi limejengwa kwa mkopo wenye riba.

**164. Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hilo, lazima Serikali izingatie mgawanyo wa rasilimali fedha kwa sekta mbalimbali nchini kwa sababu kurundika rasilimali nyingi kwenye miradi michache kunaweza kusababisha kudumaa kwa miradi mingine ya maendeleo utakaosababishwa na ufinyu wa mgawanyo wa rasilimali fedha. Urundikwaji wa rasilimali fedha kwenye miradi michache kunathirika katika makadirio ya bajeti ya 2019/2020 katika Wizara ya Nishati ukijumlisha na ujenzi zinachukua zaidi ya 50% ya bajeti yote ya nchi.

**165.** Hivyo, nihitimishe kwa kutaka Serikali kutekeleza mambo matano: Mosi; mikataba yote mikubwa inayohusu Ujenzi wa Mradi wa Umeme wa Rufiji (Stieglers Gorge) iletwe na kujadiliwa na Bunge. Pili, Tathmini ya Kimazingira na Upembuzi yakinifu kuhusu mradi tajwa iletwe na kujadiliwa na Bunge. Tatu, Mikataba yote mikubwa kuhusu Ujenzi wa Bomba kutoka Mtwara Mpaka Dar Es Salaam iwasilishwe na kupitiwa na Bunge. Nne, Serikali iwasilishe Bungeni Taarifa ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati ya Bunge iliyoundwa na Spika (wakati huo Mhe. Anna Makinda) kuchunguza kuhusu mgogoro kati ya wananchi na Serikali Mtwara juu ya ujenzi wa bomba la gesi. Tano, Serikali iwasilishe Bungeni Taarifa ya Utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati iliyoundwa na Spika (Mheshimiwa Job Ndugai) kuchunguza mikataba na utafutaji na uvunaji wa gesi asili.

**166. Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha.

………………………………………..

John John Mnyika, (Mb)

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI**

**WIZARA YA NISHATI**

28/05/2019

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza uchangiaji wetu wa jumla naomba tutambue uwepo wa wageni 33 wa Mheshimiwa Deo Sanga ambao hawakupata nafasi kuingia asubuhi ambao ni viongozi 33 wa CCM kutoka Kata ya Jimbo la Makambako, karibuni sana wageni kutoka Kata ya huko Jimbo la Makambako kwa Mheshimiwa Deo Sanga. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaanza na uchangiaji wetu, tutaanza na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Lubeleje na Mheshimiwa Balozi Adadi watafuatia, wote wa CCM kwa dakika tano tano.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kuunga mkono hoja hii ya Wizara ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 21, miradi ya kuzalisha umeme; mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji ya Mto Rufiji, *megawatt* 2,115. Kwanza nianze kusema kwamba naunga mkono hoja ya ujenzi wa mradi huu kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kwa kumshukuru Mungu kutupatia maporomoko ya Mto Rufiji kwa sababu siyo kila nchi imepata maporomoko kama yale. Huku duniani kuna mabwawa makubwa 70 tu na ili bwawa liitwe kubwa linatakiwa liwe na sifa ya kuweza kufua umeme wenye zaidi ya *megawatt* 2,000. Bwawa letu hili ambalo linajengwa litakuwa na uwezo wa kufua umeme *megawatt* 2,115 na hivyo kuingia kuwa kwenye sifa ya kuwa mabwawa makubwa 70 duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende katika dunia, katika dunia kama nilivyosema mabwawa makubwa yapo 70, lakini ukienda duniani bwawa la kwanza kubwa liko China; la pili kubwa lipo Brazil na Uruguay na la tatu lipo Brazil. Twende Afrika, mabwawa ni mengi makubwa lakini tuanze bwawa kubwa mpaka sasa hivi linaloonekana ni kubwa ni bwawa

lililopo Msumbiji bwawa la *Cahora Bassa Dam* ambalo linafua umeme kwa *megawatt* 2,075. Ina maana la kwetu linalojengwa litakuwa kubwa kuliko hili ambalo linaongoza sasa hivi. Bwawa lingine ni *Aswan High Dam* ambalo lipo Egypt ambalo linafua umeme *megawatt* 2,100, hili la kwetu ambalo linajengwa Rufiji litakuwa kubwa kuliko hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Ethiopia walianza kujenga bwawa ambalo litakuwa kubwa kuliko yote Afrika, Bwawa la *Grand Ethiopian Renaissance.* Bwawa hili litakuwa na uwezo wa kufua umeme kwa *megawatt* 6,000 na lilianza tangu mwaka 2011 likikamilika litatumia dola bilioni 6.4, bado halijakamilika mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili bwawa linalojengwa hapo katika maporomoko ya Mto Rufiji; ni kweli kelele ni nyingi sana, upinzani ni mkubwa sana katika ujenzi wa bwawa hili lakini naiomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ielewe kwamba hakuna mtu yeyote duniani, hata haya mabwawa yote yaliyojengwa China, Brazil, Uruguay na wapi, si kwamba walijenga bila ya kuwa na changamoto, wote walipata changamoto kubwa sana na wote walipata upinzani, lakini naomba tuelewe kwamba huwezi kufanya jambo kubwa lenye manufaa katika nchi kama manufaa tutakayopata kutoka kwenye bwawa hili tunalojenga usiwe na changamoto, haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yangu kwa unyenyekevu naisihi twendeni bila kusikiliza kelele zozote. Kwanza, ni lazima mwelewe kwamba moja ya tano ya umeme wote unaotumika duniani unatoka kwenye mabwawa haya 70. Sasa sisi tumepata nafasi ya kuwa na bwawa kubwa na sisi tuingie katika kuwa kwenye moja ya tano ya umeme unaozalishwa duniani, tunasikiliza kelele, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasihi sana, changamoto zilizopo tusisikilize kelele kushoto wala kulia, Serikali wasonge mbele kwa sababu kwanza ukiangalia umeme huu wa *hydro* ni rahisi. Pili huu umeme wa *hydro* utatusaidia kwa mambo

makubwa mawili; kwanza; ajira kwa vijana wetu; pili. tayari tutakuwa na uwezo wa kuwa na uwekezaji mkubwa kwenye nchi hii. Sasa iwapo hatutakuwa watu tunaothubutu Serikali ya CCM, tunaogopa kelele za watu, tutakuwa wapumbavu. Naomba uthubutu huu uliooneshwa na Awamu ya Tano tusikatishwe tamaa na kelele zozote zile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anne muda umeisha, ni dakika tano.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, nafikiri Watanzania wamenielewa. *(Makofi/Vigelegele)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kupongeza hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, wajibu wetu ni kuwashauri kama tunavyowashauri kwenye mambo mengine; mkitaka yachukueni, lakini mnapoyaacha na madhara yake yanatokea kama yaliyotokea kwenye kikokotoo na kwenye mambo mengine. Kwa hiyo, Waziri na Naibu Waziri Mheshimiwa Jesca Kishoa ambaye leo ni *birthday* yake wamefanya kazi yao, wamelitendea haki Taifa lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge wa *term* ya pili, na tangu nimeingia kwenye Bunge hili Serikali ya Chama cha Mapinduzi haijawahi kutoa pesa za *REA* zote, mbali ya kwamba pesa zipo kwenye uzio na tunajua pesa zikiwekwa kwenye uzio zinatakiwa ziende zote kwa mujibu wa Katiba na kwa mujibu wa taratibu zetu tulizojiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naanza na awamu ya nne; mwaka 2010/2011 tulitenga bilioni 56.883, zilizotolewa ni bilioni 114; mwaka 2013/2014 zilitengwa bilioni 53.158, zilizotolewa ni bilioni 6.757; 2015/2016 zilitengwa bilioni 420, zilizotolewa ni bilioni 141, sawa na asilimia 34; 2017/2018, awamu ya tano sasa ya majigambo mengi... *(Makofi)*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** ...zilitengwa bilioni 499, zimetolewa bilioni...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester, subiri. Taarifa Mheshimiwa Dkt. Mollel.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Wanataka kuharibu Bunge hawa...

**T A A R I F A**

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kumpa dada yangu mpendwa taarifa kwamba ameanza...

*(Hapa Mheshimiwa John W. Heche alizungumza bila kufuata utaratibu na bila kutumia kipaza sauti)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche, siyo vizuri unavyofanya.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Charles Wegesa, tulia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche, naomba utulie jamani na wenzio. Mheshimiwa Dkt. Mollel, naomba umalizie taarifa yako.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kumpa taarifa dada yangu kwamba ameanza vizuri na ameonesha jinsi ambavyo kwa awamu

ya nne kumekuwa na kwamba inatengwa hela lakini tunahitaji kufikia lengo hatufikii, ndiyo maana tunaweka miradi ya kimkakati, kama ya *Stiegler's* na mingine ambayo itahakikisha tuna-*boost* viwanda na chanzo mapato ya ndani yaweze kuongezeka ili tuweze kubadilisha bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha kusikitisha wanaongea kizalendo wakidai kwamba ni makosa kufanyika hayo ambayo yangetusaidia tuweze kufikia lengo yeye analolitaka. Kwa hiyo, wakati tuna-*address issues* hizo anazolalamikia anapinga kwa hiyo tunafikiri dada yangu ungetusaidia sasa kuunga mkono *Stiegler's* na nyingine ili mwisho wa siku tuweze kufikia lengo ambalo unataka tufikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester, taarifa hiyo.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni uchanga wa kuingia Bungeni unamsumbua, ni njuka siyo *size* yangu, siwezi kumjibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo *trend* ya Serikali…

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Nitaanza vibaya mama.

**MHE. ESTER A. BULAYA** …ya Chama cha Mapinduzi kushindwa…

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Halima Mdee yuko wapi kwanza nikushtaki kwake?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa naomba tutulizane, tusikilizane Waheshimiwa, Mheshimiwa Ester naomba uendelee tafadhali.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema, kwamba pesa zikiwekwa kwenye uzio ni tofauti na pesa zingine anazozisema yeye, hizi zinaenda kwenye

matumizi maalum, lazima ziende zote, ndiyo hoja iliyopo hapa. Ziko kwenye *ring-fenced,* ndicho ninachokisema, na hiyo *trend* ilianza tangu Bunge lililopita mpaka hili la Serikali ya Awamu ya Tano bado hamjafanikiwa kutoa pesa zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu hii imejipambanua inashughulika na ufisadi, imeanza na mishahara hewa...

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu Utaratibu.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 64(f) na (g). Kuwa Mheshimiwa Mbunge ametumia lugha ya kuudhi na inayodhalilisha wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa anayechangia amemwambia Mheshimiwa Dkt. Mollel kuwa ni ushamba wa kuingia Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester, umezungumza maneno ya ushamba? Haya, endelea.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge mnaosema ushamba nitawatoa nje, Mheshimiwa Ester endelea.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee na mchango wangu.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Amenivurugia ndoa yangu huyu unajua, Halima Mdee mke wangu halafu ukaolewa...

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati pesa za *REA...*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuwe na nidhamu jamani, hebu Mheshimiwa Ester naomba umalizie.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati pesa za *REA* Serikali hii inachelewa kupeleka, lakini bado...

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa *Chief Whip* amesimama bado mnapiga kelele ya nini?

Mheshimiwa *Chief Whip* endelea.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba mwongozo wako, kwanza kuhusu aina ya taarifa zinazotolewa hapa Bungeni, lakini pamoja na hayo, Mbunge anachangia lakini Mbunge mwenzake anawasha *microphone* na kutukana. Na bahati mbaya sana inawezekana Kiti chako hakisikii, lakini maneno ambayo yamesemwa ni maneno makubwa sana na yameingia kwenye *microphone. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi naomba mwongozo wako; hivi hii miongozo inayotolewa kwa ajili ya dhihaka tu pamoja na matusi na nini, unairuhusu iendelee kwenye Kiti chako ili vilevile iamshe hasira za watu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini, nimekuelewa.

Waheshimiwa tutulizane. Waheshimiwa tulizaneni, wote Wabunge hapa mnaelewa vizuri Kanuni na mnajua nini mnafanya, kwa hiyo mnafanya makusudi, mnaposema wawili, watatu, wanne mimi huku sisikii kinachozungumzwa na mtu mmoja, siyo ninawaachia, ukiongea wewe na mwingine na mwingine hakuna kinachosikilizika, kwa hiyo, mimi nashindwa kutoa maamuzi. Ila ninyi Wabunge mnaelewa Kanuni na mnafanya makusudi, yeyote ambaye atakwenda sasa hivi kinyume atatoka nje hana ruhusa ya kuchangia, naomba umalizie muda wako.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mbali ya kwamba fedha za *REA* haziendi zote, lakini kumekuwa na ufisadi, kuna malipo hewa. *REA* imeipa Kampuni ya *HIFAB* fedha za ziada, zilizozidi, Dola za Kimarekani 81,000 na ushee wakati ilipaswa kulipa dola 9,000; na hili jambo halijafanyika mwaka 2010, 2011, limefanyika mwaka 2017 kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tano kuingia madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni wizi kama wizi mwingine, wahusika wanatakiwa washughulikiwe na mpaka sasa hivi na kwenye hotuba yetu tumesema bado Dola za Kimarekani 44,000 hazijarudishwa ambapo huko Serikali hii inasema ya wanyonge ndiko pesa za wanyonge zinapigwa. Huko ndiko ambako tunahitaji umeme vijijini, huko ndiko ambako Serikali hii imewapa Wakuu wa Mikoa waanzishe viwanda; wakati kuna uchafu huu hivyo viwanda vitakamilikaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna ukaguzi ulifanywa kwa mikataba mitatu iliyogharimu shilingi bilioni 984 ambapo imegundulika vijiji 55 kwenye Mikoa ya Tanga, Mwanza,

Arusha na Manyara tayari vina umeme lakini wakandarasi wamelipwa tena waende wakaweke umeme. Huu ni wizi, na tunaposema wizi hatuwezi kunyamaza eti tukachagua awamu, huu ni wizi kama wizi uliofanyika awamu zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji ukaguzi maalum ufanywe ili hiyo dhamira sasa ya kuzima vibatari mikoani huko na vijijini itekelezwe. Kwa hiyo tutahitaji majibu sahihi. Sasa kama vijiji 55 hivi, je, kwa nchi nzima tunaingizwa mkenge kiasi gani, huo wizi upo kiasi gani? Kwa hiyo haya lazima yafanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa pia na malalamiko kwenye suala zima la kuunganishiwa umeme vijijini. Wanasema wenye pesa ndio wamekuwa wakipewa kipaumbele katika kuunganishiwa umeme. Wananchi wa kawaida huko majimboni kwetu wanalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninapenda kulizungumzia ni kuhusiana na suala la *TANESCO.* Mpaka sasa hivi Shirikia *TANESCO* linajiendesha kwa hasara kwa bilioni mia tatu na. Kipindi cha awamu ya nne wakati inaondoka madarakani hasara ilikuwa bilioni 124, yaani kuna ongezeko la bilioni 122. Sasa tulitegemea Serikali hii inayokusanya kodi ingeenda kuondoa zile hasara na kuleta faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado madeni; madeni kutoka bilioni 700 mpaka bilioni 958 na *TPDC* peke yake inaidai *TANESCO* bilioni 340. Ndiyo maana Kambi Rasmi ya Upinzani tulisema shirika hili litakufa, sisi siyo wa kwanza, tumeshauri ligawanyeni, kuwe kuna mashirika mawili, limezidiwa uwezo na athari ya madeni, athari ya kujiendesha kwa hasara inakwenda kuathiri kwenye mtaji. Haya ndiyo ambayo tunayasema... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ester Bulaya, tunamalizia na Mheshimiwa Charles Mwijage.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia Bajeti ya Wizara ya Nishati; na ninapoanza, leo tarehe 28 zikiwa zimebaki siku mbili kabla ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kufikisha miaka 50, nichukue fursa hii kuwapongeza Watanzania kwa shirika la Kitanzania kufikisha miaka 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mtumishi wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania kwa miaka 18, lakini ni mtumishi wa sekta ya mafuta kwa miaka 30. Kwa hiyo ninachokizungumza sikukisoma darasani, ninachokizungumza nakijua ndiyo maana wakati mwingine huwa naona mnyukano nashika kichwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaposherehekea miaka 50 ya *TPDC* napenda nichukue fursa hii kuipongeza Serikali na pia nilipongeze Bunge hili. Bunge la Kumi lililopita kupitia Sekta ya Mafuta tuliwahi kufanya mambo makubwa, moja wapo ni kutengeneza tozo, la pili kuzuia uchakachuaji na la tatu *bulk procurement.* Wabunge waliokuwepo watamkumbuka Mheshimiwa January Makamba, Mwenyekiti wetu na Mzee wa *SCOPO***,** Mheshimiwa Mzee Ndassa, haya ni mambo makubwa ambayo tunapaswa kujivunia. Sekta ya mafuta watu wengine wanaweza wasilewe; ni wakala mkubwa wa Serikali kwenye kukusanya kodi; kodi kubwa inakusanywa na *TRA* hupitia kwenye sekta ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine cha kujivunia kwenye sekta ya mafuta, ndiyo sekta nafuu, ndiyo sekta ya kipekee ambako kuna ubia wa sekta binafsi na Serikali. Vituo vya mafuta 1,400 vilivyoko nchini vyote ni vya sekta binafsi, ndipo mahali pa kulea Watanzania ili kuweza kuwaonesha kwamba kumbe sekta binafsi inaweza kufanya kazi. Tanzania tunayo hifadhi ya mafuta ifikayo milioni 1,200 $m^3$, lakini yote hiyo asilimia 89 inamilikiwa na sekta binafsi. Mimi ni muumini wa sekta binafsi nimesimama kuisemea sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kitu kinachoitwa *power mix.* Tunapokwenda kujenga uchumi wa viwanda ifikapo 2025 nchi hii inahitaji gigawati 25 au megawati 25,000. Kwa hiyo mimi mtu anayejadili *Stiegler's Gorge* nashindwa kumuelewa. Mahitaji yetu ni makubwa mno kuliko *Stiegler's Gorge,* tunaihitiaji *Stiegler's Gorge* na... *(Makofi)*

*(Hapa sauti ilikatika)*

**MWENYEKITI:** Sogea kwenye *microphone* nyingine.

**MBUNGE FULANI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hapa.

**MWENYEKITI:** Muda wake bado upo, anaendelea, dakika kumi.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme washindwe na walegee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumza kuhusu *power mix.* Mahitaji ya nchi hii kufika 2025 ni gigawati 25 ambayo mnaita megawati 25,000. Kwa hiyo suala la *Stiegler's Gorge* yenye megawati 2,000 wala si kachumbari, tunaihitaji jana. Lakini ina maana tunahitaji vyanzo vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuwapa uzoefu; niliwahi kwenda huko *SADC*, *Congo DRC* wanatengeneza gigawati au megawati 40,000; *South Africa* ameshaomba 16, Mheshimiwa Waziri ukija hapa uwakumbushe. Ndiyo maana tunatengeneza kitu kinaitwa *interconnector,* tunatengeneza mtandao wa kutoka Kongo, wa kutoka kaskazini, nchi za Ethiopia. Sasa kama baba anakwenda kuhemea usimshangae mama anayelima viazi. Yaani *Stiegler's Gorge* ni kama viazi, chakula bado kinahitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninapenda niwaeleze katika mambo ya nishati kuna vyumba vitatu; chumba cha kwanza kinaitwa *availability,* cha pili *liability* na cha tatu

*affordability.* Wawekezaji tunaowatafuta, kama hawajui kwamba una nishati ya kuaminika kesho hawawezi kuja. Kwa hiyo anayejenga *Stiegler's Gorge* anawavuta wawekezaji waje. Mwekezaji makini haangalii umeme ulionao leo…

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** …anaangalia keshokutwa utakuwa na…

**MWENYEKITI:** Mheshibiwa Mwijage, taratibu; taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimpe taarifa rafiki yangu anayechangia. Amezungumza mambo ya *energy mix;* suala la *energy mix* ni kwamba unakuwa na aina tofautitofauti za umeme, yaani upepo, maji, makaa ya mawe. Sasa hapa anachosema *energy mix* tayari tuna Mtera, tuna Kihansi, sasa kule tena tunaleta tena mambo ya maji tena, sasa hiyo ni *energy mix* ipi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwijage.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema hii sekta siyo mchezo. Huwezi kuisoma umelala, hili si somo la kulala kwenye kitanda ukaanza kusoma. Yaani nimekwambia mwanzo nina miaka 30 kwenye sekta, naweza kuanzia jotoardhi, nikakueleza umeme wa mawimbi, nikakueleza mambo ya mkaa, kwa hiyo watu wengine muwe mnakaa Bungeni mnasikiliza. Mheshimiwa Maige asubuhi ametoa somo la makaa ya mawe na yenyewe nishati tunayo; hiyo taarifa siikubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na katika hiyo niwaeleze dhana isiyo, kuna dhana isiyo; mtu anasimama anasema bomba la kutoka Mtwara linatumika asilimia sita *it's a failure, it is not!* Ukijenga barabara ukamaliza, *traffic* ika-*jam*

umeshindwa; ile bomba ni barabara tunawavutia wawekezaji wachukue gesi zaidi, ile gesi mmesema itakwenda Uganda, bomba halipaswi kujaa na uwepo wa bomba lile ni kivutio cha gesi ya maji marefu ipitie pale ije huku itumike. Lakini gesi ile ni kivutio cha visima vilivyoko kusini vichimbwe vitatumia bomba ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie bomba la Uganda. Wako watu hawajui faida ya bomba la Uganda. Faida ya bomba la Uganda linafungua fursa zetu. Nchini Tanzania tuna kitu kinaitwa *stranded reserve,* sehemu za Kigoma, sehemu za Eyasi, kuna mafuta kule Mungu atatujalia tutayapata, lakini watafutaji hawakuwa na motisha ya kwenda kule. Kwa hiyo kwa kuwepo bomba la kutoka Kabale, Hoima, mpaka Tanga ina maana wawekezaji sasa watavutiwa, watakwenda kuchimba mafuta kule na siku moja nchi yetu itaweza kupata mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali na mwanzo, hili ni somo gumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kumalizia naomba niwaeleze mojawapo ya mambo niliyofundishwa. Wanasema wasafiri wenye busara ni wajibu wao kukumbuka wafikapo safari salama au njiani wakiwa, kukitunza chombo chao vyema na nahodha wao kushikilia. Chombo ni Tanzania na nahodha mtajaza wenyewe. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** *Wakora Buraza wakora!*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwijage, naamini waliokuwa hawajaelewa wameelewa vizuri sasa.

Kabla sijasitisha shughuli za Bunge, kuna tangazo moja hapa; Waheshimiwa Wabunge wote mnatangaziwa kuwa Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na Mwenyekiti wa Klabu ya Kulenga Shabaha, Mheshimiwa Mendrad Kigola, inaratibu zoezi la kulenga shabaha litakalofanyika katika Kambi ya Jeshi Makutupora. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge wote mtakaopenda kushiriki zoezi hilo mnaombwa kujiorodhesha

katika dawati la mapokezi lililopo Lango A katika Ukumbi wa Bunge.

Aidha, tarehe ya kushiriki zoezi hilo mtaarifiwa mara tu idadi kamili ya watakaojiorodhesa itakapojulikana. Kwa hiyo wote mnaotaka kwenda kufanya hilo zoezi mnaombwa mjiorodheshe.

Mheshimiwa Mashimba Ndaki amepotelewa na ufunguo wake wa gari, rangi nyeusi. Kwa hiyo mtu yeyote ambaye ameona ufunguo wa gari rangi nyeusi, naomba tafadhali amkabidhi Mheshimiwa Ndaki au Katibu aweze kumpatia.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi kamili jioni, na wachangiaji watakaowahi ndio watakaoanza.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Wizara ya Nishati**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na uchangiaji, tutaanza na Mheshimiwa George Malima Lubeleje na Mheshimiwa Bahati Ali Abeid ajiandae.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati. Kwanza kabisa naiunga mkono kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono nataka nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu,

Kamishna na watendaji wote wanafanya kazi nzuri sana. Zamani hali ya maisha vijijini tulikuwa tunatumia taa za kawaida vibatari, lakini sasa hivi karibu vijiji vingi Tanzania hapa wananchi wana umeme. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri achape kazi sisi tuko pamoja naye, afanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mpwapwa karibu vijiji vyote vina umeme, Jimbo la Mpwapwa ni vijiji nane tu ambavyo havina umeme lakini zaidi ya vijiji 58 vina huduma ya umeme. Naomba tu kwamba ulivyoahidi pale Kijiji cha Igoji-I kwamba baada ya kusambaza umeme kwenye vijiji sasa wataanza kusambaza umeme kwenye vitongoji. Vitongoji ni vingi na kule ndipo wananchi wengi wanaishi. Kwa hiyo naomba huu mradi wa kusambaza umeme vitongojini nao vilevile uanze.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Waziri Jimbo la Mpwapwa amefika vijiji vine; amefika Tambi kuzindua umeme, Mbori, amefika Igoji-I na kile kijiji kimoja cha Jimbo la Kibakwe. Kwa hiyo tumshukuru sana ni mara chache sana Waziri anafika anafanya ziara katika mwaka mmoja katika vijiji vinne. Kwa hiyo namshukuru sana

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kuhusu kukatika katika kwa umeme. Wilaya ya Mpwapwa *line* ambayo inasambaza umeme inapeleka umeme Mpwapwa, ni *line* ambayo inapeleka umeme vilevile Wilaya ya Chamwino, Wilaya ya Gairo, Wilaya ya Kongwa pamoja na Wilaya ya Mpwapwa. Hivi karibuni wameanzisha tena umeme *line* ile ile ya Mpwapwa, wamechukua Kijiji cha Mpwayungu pamoja na Mwitikila kule Wilaya ya Bahi. Kwa hiyo hii *line* imekuwa *over loaded*, sasa nashauri mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wilaya ya Mpwapwa tujengewe *line* mpya itakayoanza Zuzu, Kikombo *Station*, Kiegea na pale najua umeme ukifika Kiegea hata Kazania watapata umeme *line* hii ikitoka Kiegea iende Mbande na pale Mbande wanajenga *substation* na hii *substation* watajenga *line* moja, moja kwa moja kwenda

mpaka Mpwapwa ambayo itajulikana kwa jina la Mpwapwa *feeder* badala hii *line*. Hii *line* kwanza nguzo zote zinapita kwenye madimbwi ya maji huku kwa hiyo ndiyo maana umeme unakatika katika kila wakati, lakini maeneo mtakayopitisha *line* mpya Mpwapwa hakuna madimbwi ya maji ni eneo kame kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo na nne kuhusu gharama za umeme;gharama ni kubwa. Nashukuru sana alitangaza kwamba gharama ya umeme ni shilingi 27,000 kuvuta umeme kwenye majumba. Sasa umeme kati ya *TANESCO* na *REA* basi ulingane ufanane, maana mwingine Sh.177,000 mwingine Sh.27,000, naomba sana gharama za umeme zipungue ili wananchi wengi waweze kuvuta umeme kwa sababu gharama zikiwa kubwa wananchi watashindwa kuvuta umeme kupeleka kwenye majumba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara hii. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara hii, lakini bila kumsahau Meneja wetu wa Mkoa wa Rukwa ndugu Chambua anafanya kazi vizuri sana anamwakilisha Mheshimiwa Waziri vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa lazima tutambue kwamba pamoja na kusudio la kupeleka umeme vijijini, ili kuchochea maendeleo lakini vilevile lazima tukubali nia ya Serikali ni kufanya matumizi ya umeme yawe makubwa ili *return* irudi Serikalini. Nimeona baadhi ya maeneo kijiji kinapelekewa umeme lakini unakuta vijiji vinne watu wanne ndiyo wamevuta umeme au watano au sita, maeneo mengine yote wananchi wanaangalia umeme. Sasa nasema

hivi lazima waangalie vipaumbele katika maeneo ambayo watu wanahitaji umeme na wanataka kuutumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Jimbo langu la Kwela lina vijiji 115, mpaka sasa hivi ni vijiji 16 tu vilivyopata umeme sawa na asilimia 18.4, vijiji 99 havijapata umeme sawasawa na asilimia 81.6 na Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu kabisa amepita katika eneo lile karibu kila kijiji ni kama mji watu wanataka umeme na kutokana na uwezo walionao walishaweka *solar* ila *solar* wanashindwa matumizi mengine makubwa. Kwa hiyo tunaomba sana waweze kutupelekea umeme katika Jimbo letu la Kwela.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka mwaka 2014, *REA II,* walichukua umeme Sumbawanga wakapitisha kwenye Jimbo langu wakapeleka Katavi, wakaacha karibu vijiji sita bila kuweka umeme jambo ambalo kwa wananchi linawaumiza. Mpaka sasa katika Jimbo langu kuna Kata 16 hazijapata umeme; Kata za Kilangawana, Kaoze, Kapenta, Ilemba, Nankanga, Milepa, Zimba, Kalumbaleza, Mwadui, Mfinga, Msandamuungano, Kaengesa, Kanda, Lyangalile na Mnokola, Kata 16 havijapata umeme hata vijiji vyake. Sasa jamani lazima tufike mahali tuangalie hawa watu wanahitaji umeme na bahati nzuri Jimbo langu wananchi wanataka umeme, wafanyabiashara wameshaanza kufunga viwanda vya mashine za kukoboa mchele, lakini wanasubiria umeme wameshafunga viwanda zaidi ya 20 lakini umeme hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba juhudi ile ile ya Naibu Waziri alipofika kule Mto Wisa alisema lazima umeme uwake. Umeme uliwaka pale Mto Wisa lakini waliruka Vijiji vya Kalakala, Uzia, Kifinga, Mkamba, Mwela, havijapata umeme na kule Kilyamatundu alipohimiza kweli umeme umeshawaka lakini haujasambaa kwenye zile Kata nyingine na Mheshimiwa Waziri alifika kule Nyangalua, akahimiza umeme ukawashwa na alisema vijiji vyote vinavyozunguka maeneo yale lazima vipate umeme, lakini mpaka sasa hivi vile Vijiji vya Tunko, Kamsamba, Kavifuti, Movu, Mkowe, havijapata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wahimize na naomba Meneja wetu wa Mkoa wa Rukwa kama kuna bajeti ameleta ya kuomba pesa ya kujaziliza, wampe bajeti ya kutosha, anatusaidia sana na anaweza akawaokoa sana hata kuchelewa kwa wakandarasi, huyu Meneja ana uwezo mkubwa sana, tena nafikiri wakati mwingine angeweza kupewa fedha huyu angeweza kufanya haraka zaidi kuliko hata mkandarasi. Huyu Meneja wametuletea Meneja kweli kweli, anawajibika, si kwa Jimbo moja kwa mkoa mzima. Pia si kwa umeme huu wa *REA* hata wa *TANESCO,* anatoa majibu kila siku kwamba kuna tatizo hili na analishughulikia. Naomba sana kama amepeleka bajeti, wamsaidie bajeti yake ipite, atatusaidia sana katika kueneza umeme katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nahimiza sana Wizara wanajitahidi, Waziri anajitahidi, Naibu Waziri anajitahidi ila tunaomba sasa waongeze kasi na wanapopeleka umeme waangalie maeneo ya Jimbo la Kwela, wananchi wanahitaji umeme. Lile Jimbo hatuna shida, wanavuta hata umeme wa *TANESCO* kutoka Sumbawanga, itakuwa umeme wa *REA*? Watuletee umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Hamidu Bobali, atafatiwa na Mheshimiwa Hamida Mohammed Abdallah, Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko ajiandae.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kufanya *social cooperate responsibility* yeye akishirikiana na Mkurugenzi wa *TPDC,* namshukuru sana *engineer* Kapulya wamewasaidia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anafanya kazi nzuri. Katika Mkoa wa Lindi tatizo la umeme

sasa hivi katika maeneo mengi limekwisha na nilisema mwaka jana sisi Lindi na Mtwara tulikuwa tuna shida sana ya umeme, lakini walivyotuingiza kwenye grid ya Taifa wamepunguza ile changamoto ya umeme, sasa hivi unaweza kwenda kukaa kijiji kule uka-*relax* kwa kuwa umeme utakuwa unaupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri juzi alikuwepo Lindi na tulizungumza, kuna yule Mkandarasi *State Grid* sasa hivi ameanza kufanya kazi, lakini katika Majimbo manane ya Mkoa wa Lindi Majimbo ya wenzangu yote yamepelekewa nguzo na kazi inafanyika. Jimbo la Mchinga tu ndiko ambako hata nguzo moja haijapelekwa. Sasa Mheshimiwa Waziri hili analiweza walau leo tu amwagize kwamba walau zile nguzo zipelekwe pale tuwe na imani. Viko vijiji vimeingia kwenye *REA* awamu III, *phase one* Vijiji vya Ruvu na Dimba na nimeshampelekea mara nyingi sana Mheshimiwa Waziri na haviko mbali na ulikopita umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba sana Mheshimiwa Waziri hivi vijiji na namshukuru sana Meneja wa *TANESCO* wa Mkoa ndugu yangu Makota, kama tulivyoongea wakati ule mwezi uliopita alikwenda mpaka kwenye vile vijiji akafanya *survey* na baadaye nadhani alileta taarifa kwamba yale maeneo hayahitaji nguzo nyingi ili kupelekwa umeme. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri naomba sana na mimi nione kwamba katika maeneo yale ya Ruvu na Dimba nguzo zinapelekwa ili wananchi wale waweze kupata umeme. Ni vijiji ambavyo viko pembezoni mwa bahari, ni wale wavuvi wamejenga nyumba nzuri, wakiweka na umeme pale mambo yataenda vizuri sana. Kama pale Ruvu pana ile bandari ndogo inatumika, bila umeme kwa kweli ni changamoto kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la mradi wa gesi wa *LNG*, nisipouzungumza huu mimi natoka Lindi, natoka Jimbo la Mchinga ambako ndiyo eneo kabisa mahususi sisi pale na Lindi Mjini mradi huu utatekelezwa. Mradi huu wa

*LNG* kwanza utakuwa na faida kubwa kwa Taifa, utakuwa na faida kubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Lindi na wananchi wa Mkoa wa Mtwara na utakuwa ndiyo mradi mkubwa kabisa kuliko miradi yote katika Afrika Mashariki. Mradi wenye uwekezaji wa dola bilioni 30 siyo mradi mdogo ni zaidi ya trilioni 69.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ukizungumza na wawekezaji, juzi nilikutana nao Lindi, wao wanaonesha kwamba hata kesho wako tayari, Wizara wanaonesha hawana tatizo. Baada ya ku-*study* huu mchezo, maana kila siku ukiuliza huku unaambiwa hivi, nimegundua tatizo lipo kwenye taasisi ama sekta moja inaitwa *Government Negotiation Team,* Timu ya Uatanishi/Mapatano ya Serikali inaonesha kwa sababu hata kwenye kitabu cha Waziri kwenye ukurasa wa 93 alipozungumzia huu mradi amezungumzia kwamba mwaka huu bado utaendelea na majadiliano kati ya Serikali na Wawekezaji. Sasa ninachopata shida ni kwamba, wawekezaji wanaonesha wako tayari Serikali wako tayari, kwa nini kwa miaka minne sasa hii *negotiation team* bado haijamaliza kujadiliana na wawekezaji kujua kwamba Serikali itapata hiki na wao watachukua hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *LNG* sisi hatuanzi huu mradi, siyo kwamba Tanzania tunaanza, ziko nchi ambazo tayari wana hii miradi. Nitatoa mfano, Algeria, wameanzisha mradi wao *LNG* ulianza mwaka 1964. Tangu mwaka 1964 hivi hii *Government Negotiation Team* inashindwa kusafiri kwenda Algeria kwenda kujifunza wenzetu walikubalianaje, Serikali inanufaikaje na sisi Tanzania tutawezaje kuwekeza kwenye huu mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msumbiji wana Mradi wa *LNG*, Angola wana Mradi wa *LNG*, Egypt wana Mradi wa *LNG,* sisi hatuanzi. Kama kuna tatizo wanaona kwamba labda inawezekana Serikali itaingia hasara, twende tukajifunze kwa hawa wenzetu, hawa ni Waafrika wenzetu. Bahati mbaya sana makampuni yenyewe yanayokuja kuwekeza hapa ndiyo hayo hayo ambayo yako Namibia na

Egypt, *Shells Equinor, Camel* ndiyo hayo hayo kwa sababu haya ndiyo makampuni yanaongoza duniani kwa uwekezaji kwenye gesi. Napata ukakasi sana mradi mkubwa kama huu kila mwaka tunauchezea na gesi ipo tu pale baharini katujaalia Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tumegundua gesi sambamba na Msumbiji, wenzetu Msumbiji wameanza kunufaika na gesi wanaumeme wa uhakika, maendeleo yao yanakwenda kwa haraka sana, sasa hivi wameshatuacha. Tuna mfano mzuri wa kuutazama Uingereza na Norway waligundua gesi mwaka mmoja. Norway wamenufaika sana na gesi, Uingereza mpaka sasa hawajanufaika chochote na gesi. Ukisoma kwenye vitabu vyao wanasema hata wao hawajui kwanini hawajanufaika na gesi, lakini wamegundua mwaka mmoja na wako jirani pale Norway wame-*advance* sana, wameendelea kwa kutumia gesi, sasa na sisi tukichelewa wenzetu Mozambique wataendelea watatuacha sisi tutaendelea kukaa kila siku *Government Negotiation Team* haijamaliza kazi, tunaendelea kuwa maskini wakati siyo watu maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo gesi hii ametupa Mwenyezi Mungu ipo pale kwenye visima, Zafarani na maeneo mengine, tuitumie. Kama kuna tatizo wanaliona kwenye makubaliano, basi waende wakajifunze hayo maeneo mengine wenzetu walifanyaje ili huu mradi uweze kuondoka. Sisi tumekaa tunausubiria pale Mchinga, tumejaribu kujipanga ukifika tufanye nini hatuna shida, wananchi tutawapokea hao wawekezaji,watakaa vizuri na eneo wameshaandaa kulipa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalia, mwaka jana kwenye bajeti ya...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja

Mheshimiwa Hamida Mohammed Abdallah atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko na Mheshimiwa Profesa Jumaane Abdallah Maghembe, ajiandae

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia. Kwanza nianze kwa kuwapongeza Wizara, Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na timu nzima ya Wizara yake kwa uwasilishaji wa bajeti katika kipindi hiki kinachokuja cha 2019/ 2020, lakini kwa namna ambavyo wamejipanga katika kuhakikisha kwamba wanaendelea kuleta mapinduzi makubwa ya umeme katika nchi yetu na kuhakikisha kwamba tunajipanga kwa ajili ya uwekezaji na kukuza uchumi lakini kukuza ajira katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuipongeza Serikali kwasababu iko miradi mbalimbali ambayo inaendelea kutekelezwa, lakini mingine iko katika mpango wa utekelezaji na hii yote ina dhamira njema ya kuzalisha umeme katika nchi yetu kwa sababu bado tunahitaji matumizi makubwa ya umeme katika nchi yetu katika kuhakikisha kwamba tunaendelea kujipanga vizuri katika kuleta mapinduzi haya ambayo tunayategemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kusema kwamba katika mradi huu wa *REA* ambao Waheshimiwa Wabunge wengi wameusemea. Nimebahatika kupita katika maeneo mbalimbali tukiwa katika ziara ya Kamati katika kukagua miradi mbalimbali ambayo inaendelea na tumeendelea kuwasha umeme katika vijiji vingi nchini Tanzania. Kwa hiyo bado hali si mbaya sana ya umeme katika maeneo ya vijiji umeme unaendelea kuwekwa, lakini tunaamini kwamba vijiji vinaendelea kukua siku hadi siku, miji pia inatanuka au inaendelea kukua, kwa hiyo mahitaji ya umeme bado ni makubwa. Kwa hiyo niishauri tu Serikali kwamba katika eneo la *REA* basi ni vyema tukaongeza wakandarasi ili kazi zikaenda kwa spidi ambayo tunaitarajia kwa sababu kila mmoja wetu hapa anahitaji katika eneo lake basi vijiji vyote viwe vimefikiwa umeme kwa wakati mmoja jambo si rahisi sana

kwetu, lakini tukijipanga vizuri basi angalau mwaka 2020 basi maeneo mengi yatakuwa yameweza kufikiwa na huu umeme wa *REA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na timu yake; walikuja kupitia shirika la *TPDC* katika Mkoa wetu wa Lindi na walikuja kutuelimisha na kutoa elimu mbalimbali. Tumejionea mambo mbalimbali kupitia mkutano ambao tumeufanya katika Mkoa wetu wa Lindi. Kaimu Mkuu wa Mkoa alimshauri Waziri kwamba makandarasi yule anaonekana hayuko tayari kufanya kazi katika Mkoa wa Lindi. Sasa tuliomba tubadilishiwe mkandarasi yule aweze kuwekwa mkandarasi mwingine ili mambo yaweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala mradi wa *LNG,* kama alivyotangulia kusema mdogo wangu Mheshimiwa Bobali pale, ni mradi mkubwa ambao tunautegemea katika mkoa wetu wa Lindi tuweze kuupokea ingawa tumeupokea tangu mwaka 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kila mwaka tunatenga fedha za kuwalipa fidia wapisha mradi wa *LNG* katika eneo la Likong'o. Miaka minne mfululizo bajeti inakuwa inatengwa lakini fedha haitoki kwa ajili kuwawezesha ndugu zetu ambao wanapisha mradi katika eneo hili la likong'o. Sasa nilikuwa naiomba sana Serikali…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele imekwisha gonga Mheshimiwa muda wako umekwisha. Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko, atafuatiwa na Mheshimiwa Jumanne Abdallah Magembe, Mheshimiwa Jesca David Kishoa ajiandae.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii; nami nitakuwa na mambo matatu tu. Nitazungumzia *grid* ya Taifa kwa mikoa ya Kigoma

na Katavi, nitanzungumizia mradi wa *Stiegler's Gorge* maarufu mradi wa umeme Rufiji halafu nitanzungumzia mradi wa *densification,* ujazilizaji baada ya ufanisi katika mikoa hii minane ambayo imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Mheshimiwa Waziri nikupe hongera sana kwa kazi, wewe na Naibu wako mnafanyakazi nzuri mnazunguka nchi yetu vizuri sana na mnafanya kazi nzuri sana. Kwa hiyo wewe na timu yako *TANESCO, REA, TPDC* mnafanya kazi nzuri sana hongereni sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na mradi huu wa *grid* ya taifa kwa Mkoa ya Kigoma na Mikoa ya Katavi. Katika nchi yetu ni mikoa miwili ambayo haijaunganishwa kwenye grid ya taifa; lakini nashukuru kupitia hotuba yako ya leo umezungumzia juhudi kubwa iliyopo ya kuunganisha Mikoa ya Kigoma na Katavi kwenye *grid* ya taifa. Ombi langu la msisitizo wangu kwako na ushauri kwa Serikali ni mikoa miwili tu imebaki kuunganishwa kwenye *grid* ya taifa.

**TAARIFA**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nsanzugwanko kuna taarifa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika nampa taarifa mzungumzaji anasema mikoa miwili sijui Rukwa ameisahauje? Si mkoa? Ni Wilaya ya Rukwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nsanzugwanko unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina hakika na Rukwa kwa sababu Rukwa wanapata umeme kutoka Zambia sasa sina hakika sana, nami napenda nizungumze vitu nina hakika navyo. Ambayo nina hakika ni Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Katavi, wenzetu wa Rukwa wanapata kidogo kutoka Zambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hoja yangu ni dogo tu, kwa kuwa kuna shughuli mnafanya ya kuunganisha mikoa hii miwili, Mheshimiwa Waziri na timu yako niwaombe muipe *priority* mikoa hii. Bila kunganisha kwenye *grid* ya taifa ni *impossible,* haiwezekani, haiwezeikani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu kwamba umeme ni roho ya uchumi, umeme ni maisha; kwa hiyo nikuombe Mheshimiwa Waziri mikoa hii miwili sasa kwa mujibu wa hotuba yako hapa ipeni *priority,* ipeni kipaumbele iweze kuunganisha na gridi ya taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya yangu ya pili ni Rufiji *Stiegler's Gorge.* Mradi huu wa *Stiegler's Gorge* ni muhimu sana kwa taifa, ni mradi ambao wala hatupaswi kujadiliana; huwezi kuwa na nchi ambayo haina umeme

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimebahatika kwenda kutembelea bwawa la *Aswan Dam* kule Misri. Roho na ujeuri wa nchi ya Misri ni Bwawa la *Aswan,* wanapata umeme mwingi sana. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri tunakuunga mkono kwa nguvu zetu zote, Watanzania tupo nyuma yako, tupate umeme mwingi na wa kutosha. Kwa hiyo mradi muhimu sana, mradi wa kiuchumi, Mheshimiwa Waziri songambele taifa lipo nyuma yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya tatu ni huu mradi wa kujaziliza maeneo ambayo yana umeme. Mheshimiwa Waziri umefika Kigoma mara tatu sasa, tulizindua *REA three* kule Lusesa; tunashukuru sana kwa hotuba yako nzuri uliyoitoa. Baadaye ulikuja mpaka Luhita kule kwangu, umefanya kazi kubwa, hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna huu mradi wa *densification program* au mradi wa kujaziliza maeneo yaliyobaki. Nimesoma kwenye hotuba yako Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 65 unasema kuna mikoa ile minane ambayo imakamilika; sasa nilikuwa naomba hii mikoa miwili ambayo tumechelewa kupata umeme wa *REA II* na *REA III* bado inasuasua. Nikuombe sana katika hii awamu inayokuja

*round two* basi Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Katavi; nasisitiza mikoa hii miwili kwa sababu ni *special* kwa sababu ni mikoa ambayo haiunganishwa na *grid* ya taifa. Nikuombe katika hii pragramu ya *densification* mkoa wa Kigoma na mkoa wa katavi uipe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho; lipo jambo mahususi kabisa. Umeme unaohudumia Wilaya mpya ya Buhigwe unatoka mjini Kasulu. Sasa vipo vijiji na maeneo ambayo watu wanatazama umeme na umepita kwenye maeneo yao. Nikuombe Mheshimiwa Waziri jambo hili nimeshakueleza, nikuombe ulipe kibaumbele. Yale maeneo ambayo umeme umepita katika vijiji vyao wasije wakahujumu miundombinu yetu, nakuomba sana maeneo hayo yaweze kupata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja hii muhimu sana, nasema ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Profesa Jumanne Abdallah Maghembe atafuatiwa na Mheshimiwa Jesca David Kishoa Mheshimiwa Ester Michael Mmasa ajiandae.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii; na kama ilivyoada ningependa kutoka sakafu ya moyo wangu niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na Wizara kwa ujumla kwa kufanya kazi nzuri sana ya kusambaza umeme katika nchi yetu. Kazi mnayofanya inaonekana nasi ni wajibu tuwapongeze.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kazi nzuri na kubwa kila siku lazima kunakuwa na mashimo na madoa ambayo lazima yanyooshwe. Ningependa niende kwenye jimbo langu; niseme mpaka mwisho wa mwaka uliopita wananchi wa vijjini kule Mwanga walikuwa wakinunua umeme wa shilingi 5,000 wanapata unit 43 za umeme. Mwisho wa mwaka jana ukawa ndio mwisho wa furaha. Tangu mwaka huu uanze

shilingi elfu 5 ile ile wananunua *unit* 13 umeme umepanda kwa asilimia 330.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliuliza juu jambo hili wakati wa *briefing* na Mheshimiwa Naibu Waziri akinipa jibu sijui niliite jibu la namna gani; akasema watu wa mwaka wote waliopewa umeme wameanzisha viwanda kule nyumbani. Kwa hiyo kwa sababu wameanzisha viwanda wanapata umeme kwa bei ya watu wenye viwanda. Sasa nimetafuta vile viwanda kule Mwanga sijaviona. Mheshimiwa Waziri ninakuomba kesho ukifanya majumuisho hili jambo la kuwabagua watu wa Mwanga kama wamekuwa watu wa viwanda wote liachwe. Watu wa Mwanga wapate umeme wapate umeme kama wananchi wa Tanzania wanaoishi vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, muda ni mdogo, lakini ningependa nizungumzie kidogo nizungumzie juu ya *REA III.* Nimshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu wake walitembelea kwenye jimbo langu, na kazi kwa kweli kwa *span* imefanya; lakini yapo maeneo ambayo *span* inayotolewa ya kuwafungia watu umeme inatuletea matatizo kule vijiji. Kwa mfano kwenye Kijiji changu cha Kigonigoni wananchi wanaotaka umeme wapo 380. Watu waliopo kwenye *scope* ya kupewa umeme ni watu 38, na kijiji chote watu wanakaa mahali pamoja si kijiji ambacho kimesambaa kwenye eneo kubwa; ukiongeza nguzo hamsini unawapa wote umeme. Sasa ninaelewa mambo ya *span* na mambo ya menejimenti, lakini na ninyi muelewe siasa pia na mtupunguzie malalamiko ya wananchi. Kama kinachotakiwa ni nguzo 50 leteni nguzo ... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kengele imeshangonga ahsante sana. Mheshimiwa Jesca David Kishoa Mheshimiwa Ester Michael Mmasa Mheshimiwa Omar Shaban Shekilindi ajiandae ajiandae.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani. Kabla ya kuendelea na mchango wangu ningependa kuomba kiti chako kutumia kanuni ya 64(1)(a) ambapo ningependa u-*set position,* kwa maana ya kwamba Kanuni hii imekuwa ikitumika kwa upande wa Waheshimiwa Wabunge ambao imekuwa ikisemakana wanatoa taarifa za uongo Bungeni basi iwe *applicable* kwa upande wa Waheshimiwa Mawaziri ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakitoa taarifa za uongo na hakuna hatua yoyote inayochukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Wizara ya Nishati peke yake kuna mambo mbalimbali ambayo yakiahidiwa nami nayahesabia kama ni ya uongo kwa sababu yameshindwa kutekelezeka. Mwaka 2016 mwezi 11 Waziri wa Nishati alipokuwa akijibu swali ndani ya Bunge, swali langu ambalo nilikuwa nina hoji kuhusiana na ujenzi wa miradi ya uzalishaji wa umeme wa upepo aliahidi kwamba kufika mwaka 2017 mwezi wa nne miradi hiyo ujenzi wake utaanza na utakamilika mwaka 2019; lakini mpaka hivi ninavyozungumza Mheshimiwa Naibu Spika hakua taarifa yoyote ambao inaonesha wamekwamba wapi. Ni miezi 30 mpaka sasa hakuna kinachoendelea,

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 25 Mei, 2018 alisimama AG humu ndani akaahidi baada ya hoja yangu ya mikataba mibovu ikiwemo mkataba wa *Songas*; akasema ndani miezi miwili, kuanzia mwezi wa tano, kwa maana ya mwezi wa saba, mikataba yote itakuwa imeshafanyiwa *review,* lakini mpaka kufikia hivi sasa ni takribani mwaka mzima hakuna ambacho kinafanyika. Mwaka 2018 mwezi wa 11 Bunge la mwisho aliyekuwa Waziri wa Madini wakati huo alisimama kutoa taarifa Bungeni kwenye hoja yangu ambayo ilikuwa inahusiana na taarifa kutoka *TEITI,* taarifa ya nane, iliyokuwa inaonyesha kuna upotevu wa fedha bilioni 30.5, akaahidi akasema kwamba ameshapeleka taarifa kwa *CAG* na kufikia mwezi wa 12 taarifa itakuwa tayari. Hata hivyo mpaka sasa hivi ninavyozungumza hata kwenye Kamati taarifa hii haijapelekwa na hapa Bungeni kwenye hotuba sijasikia taarifa ya namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu gani, ni muhimu tukajenga heshima ya Bunge hili na Mawaziri waanavyokuja humu ndani wajue kabisa wanazungumza na *supreme organ of the state*. Pia ni vyema tukajua kwamba moja ya vitu ambavyo vina *taste credibility* ya Bunge hili ni pamoja na masuala kama haya. Kwa sababu hizi ni *sensitive issues* lakini ni mambo ambayo yanakosa majibu kutoka Serikali. Ninajua na tunatambua kwamba kuna kitengo hapa Bungeni ambacho kinahusisha masuala ya kufuatilia ahadi za Serikali, na wanalipwa mshahara mzuri sana, nashindwa kuelewa wanafanya kazi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye hoja nyingine kuhusiana na TEITI. Natamani na ninahitaji kujua kwamba Serikali ina mpango gani na TEITI. Wote tunajua kwamba TEITI ni taasisi ambayo inahusiana na masuala ya uwazi na uwajibikaji; Serikali imeifanya TEITI kama mradi wake na wanasahau kwamba TEITI wana wajibu mkubwa sana katika taifa hili ya kuhakikisha kwamba *public* inakuwa *aware* na masuala yote yanayohusu matumizi ya makubwa ya rasilimali zao. Ni vyema Serikali ikatuambia kama haioni umuhimu wa TEITI ni muhimu mkajiondoa kwenye umoja huu kitamaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa ninavyohamu na ninavyoamini kwa Serikali yoyote ambayo ikijipambanua kwamba yenyewe inayopinga ufisadi kwenye mamlaka au taasisi ambazo zinakuwa zina *influence transparency* zinaunga mkono kwa kiasi kikubwa sana. Nashindwa kuelewa ni kwa nini Serikali inashindwa kuunga mkono suala hili la *TEITI* na kuisaidia *TEITI. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka kufikia Februari, 2019 TEITI hawajapata pesa yoyote. Taatifa ya utekelezaji wa majukumu ya taiti ya mwaka 2016/2017, 2017/2018 zimebaki kwenye droo kwa sababu TEITI haina mratibu. Ni mambo ya aibu kabisa mamlaka kubwa kama hii kukosa mratibu mpaka sasa hivi. Lakini mmewahamisha kutoka Dar es Salaam ambapo walikuwa wanakaa kwenye Ofisi kubwa jengo kubwa mmewahamisha mmewaleta hapa Dodoma

wanakaa kwenye vyumba viwili vidogo viniwafinya kiasi kwamba hata taarifa wanashindwa kuziweka kwenye sehemu husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiona haja ya sisi Wabunge wa Serikali kuhakikisha kwamba tunafanya marekebisho kwenye Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji ya Mwaka 2015 ili kuipa *TEITI* nguvu na mamlaka yakusimama yenyewe kuwa huru kimiundo na kimifumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia nigusie suala la bomba la gesi la kutoka Mtwara kwenda Dar es Salam. Moja ya sababu kubwa ya watu wengi kushindwa kununua gesi ya *TPDC* ni gharama za ujazo wa bomba kuwa kubwa sana. Na kwa sababu mambo hayo mnashindwa kuyaweka wazi kuna taarifa, inasemekana kwamba gharama halisi ya bomba la gesi na gharama tunayolipa kuna ziada ya dola kimarekeni milioni 400.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kulipa gharama zote hizi hii ndio inayopelekea gharama ya gesi hii uwa kubwa. Naomba kupitia Bunge hili Tukufu, na hii nitaishikia shilingi, Serikali iunde timu ya watalamu kwenda kuchunguza gharama halisi ya bomba la gesi, lakini pia wachunguze mkopo ambao tumpewa kutoka China Exim Bank.

Mheshimiwa Naibu Spika, na bahati nzuri sana huu mkataba upo *very clear* mkataba upo clear kwa maana ya kwamba wanasema hivi, ikitokea kwamba Tanzania tumshindwa kulipa hili deni tujue kabisa kwamba gesi yote inayopatika Mtwara inakwenda kuwa *controlled* na China na bomba la gesi lenyewe. Hii haitakuwa maajabu kwa sababu hili suala limefanyika Srilanka, limefanyika Zambia. Kwa hiyo ni muendelezo wa mambo ambayo kama hatuwezi kuwa makini tunaweza tukajikuta tunapotea rasilimali muhimu sana katika taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, bomba la gesi ambalo linafanya kazi kwa 6% tu na tumetumia mkopo mkubwa kiasi hicho kwa sababu ya kulijenga, inaonesha ni namna gani

kama Serikali tunafanya mambo mengi kwa kukurupuka bila kutafakari na kuwa *business plan*. Baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni akushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Ester Michael Mmasi atafutaiwa na Mheshimiwa Shaabani Omari Shekilindi, Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba ajiandae.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Bunge lako Tukufu. Kabla sijaenda mbali napenda kumpongeza sana Waziri mwenye dhamba Dkt. Kalemani pamoja na dada yetu mpendwa dada Subira, kazi zenu zinaonekana. Mimi nimekuwa nikitembea mikoa mbalimbali kuongea na vijana wa vyuo vikuu, wengine wamediriki kuniambia kwamba wazee wao wamefika hata kuwasahau watoto wa majirani lakini majina yenu nyuso zenu wanazijua fika. Mmetembea Tanzania mmezunguka mikoa yote vijiji kwa vitokoji. Tunawapa pongezi za dhati kwenye hili la kusimami sekta ya nishati msiyumbe kwa kweli mpo vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitajikita kwenye taasisi moja tu ya *TPDC*. Sambamba na pongezi zangu kwa Wizara na viongozi wa Wizara lakini pia ninapenda kwa namna ya pekee nimpongeze *Engeneer* Msomba pamoja na timu yake, mwenyekiti wa bodi Bakukula lakini pia wadada watatu ambao wameonekana kujituma sana katika taasisi ya *TPDC* nanyi pia mpokee pongezi za za dhati. Ninamfahamu Venosa lakini pia ninamfahamu Dorah, ninamfahamu Maria. Kwa kweli sisi kama wanawake vijana tunawapongezini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TPDC* kwa miaka ya nyuma ulikuwa ukiitaja hapa Bungeni, nafikiri hata kama michango ukiipata ni michango dhaifu, kwa sababu kila mtu alikuwa ame-*tend* ku-*withdraw*, hakuna mtu mwenye hamu ya kutaka kuisikiliza *TPDC* ni nini, lakini, kwa heshima na taadhima napenda kuipongeza Taasisi hii iliendа ikajitafakari ikaja na

*turnaround strategy* na leo ninathubutu kutaja mafanikio makubwa yaliyopatikana kwenye Taasisi hii ya *TPDC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kupitia Gesi ya Kinyerezi *I na II*, *TPDC* imeweza kufanya mambo makubwa katika nchi hii, umeme viwandani, kwa sasa Dangote analipa shilingi bilioni tano za Kitanzania kila mwenzi, lakini siyo hivyo *Goodwill Ceramic* analipa 2.2 bilioni kwenye uchumi wa Tanzania kutokana na Kinyerezi I na II. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Cocacola juzi amepewa umeme wa gesi, analipa shilingi milioni 150 kwa mwezi, ninapoongea hapa *Lodhia Steel*, lakini pia *NAF Industries* leo hii wanaenda kulipa shilingi milioni 512 kwa mwezi kwa sababu ya gesi ya Kinyerezi I na II. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambasamba na haya, *TANESCO* kwa mara ya kwanza kabisa na nitaomba ikikupendeza wenzetu hawa waweze kutafakari ni nini walichokiandika katika ukurasa wa sita kwa sababu wametuambia bado kwamba *TANESCO* inalipa *capacity charge*, huu ni uongo na ni upotoshaji mkubwa, nitaomba niweke rekodi hizi vizuri katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapoongea hapa kwa mara ya kwanza tumeondokana na *capacity charge* za *Aggreko,* tumeondokana na *capacity charges* za *Artumas*, tumeondokana na *capacity charges* ambazo tulikuwanazo kwenye *Richmond saga* katika Bunge lako hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Hizi ni pongezi za hali ya juu, sisi ni waumini katika...

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Hebu endelea.

**MBUNGE FULANI:** Endelea.

**MBUNGE FULANI:** Endelea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mmasi kuna taarifa. Mheshimiwa Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumpa taarifa mchangiaji, anasema tumeondokana na *TANESCO*, wameondokana na *capacity charge* wanazotoa kwenye makampuni yanayowauzia umeme, si kweli, anazungumzia *capacity charge* zinazoondolewa kwa wateja wadogowadogo, lakini *TANESCO* bado wanalipa *capacity charge* wanakonunua umeme kwenye makampuni mbalimbali, kwa hiyo anachoongea ni uongo kabisa huyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa pamoja na kwamba unachotoa ni taarifa Kanuni uliyotumia siyo, kama unaona anasema uongo, ungetumia Kanuni ya 63 ama 64. Mheshimiwa Ester Michael Mmasi.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, utamaduni na utaratibu wa Bunge lako tukufu ikiwa Mbunge anapotosha, ni sharti alete kithibitisho, niko radhi kuleta uthibitisho kwenye Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *capacity charge* aliyokuwa analipwa na Serikali, shilingi bilioni 6.9 imeondoka kwenye mahesabu ya *TANESCO* na huo ni uthibitisho tosha, *data* ninazo lakini haitoshi, mimi niko pamoja na wengine huko kwenye Kambi yenu, tunahudumu Kamati moja, haya masuala tunaongea kwenye Kamati, kwa nini nidanganye leo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asinipotezee muda, naikataa taarifa yake, Sambamba na matokeo chanya haya, lakini leo hii kwa mara ya kwanza mwaka wa tatu leo, *TANESCO* imeondokana na ruzuku ya bilioni 143 iliyokuwa inalipa kwa mwaka. Haya ni mafanikio makubwa, hakuna wa kubeza katika hili, sisi ni waumini wa maendeleo ya Taifa

hili, sisi ndiyo wabeba Ilani wa Taifa hili tupeni nafasi tufanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana *TPDC*, naupongeza uongozi, ampongeza Waziri na Naibu Waziri, kazi inaonekana, leo *TPDC* ina rekodi faida ya shilingi bilioni 9.57 na mpango wa miaka ijayo tunaenda kurekodi bilioni 59 na huu ni mpango wa miaka mitatu ijayo ni nani wa kubeza katika hili. Uthibitisho ninao, nitaleta mkinitaka nilete katika Bunge hili, *TPDC* kwa *turnaround strategy* imeenda kufanya mabadiliko makubwa sana kwenye sekta ya nishati ya gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu nitapenda niongelee Sheria ya Mafuta na Gesi, ya mwaka 2015, Sheria namba 21. Katika Sheria hii niseme tu kwamba nafikiri Wizara ipate muda iweze kufanya rejea na kuondokana na yale masharti hasi, ambayo yako katika ile sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii *TPDC* sharti la kwanza katika ile sheria inaitaka *TPDC* ifanye kazi kibiashara, ijiendeshe kibiashara, irekodi faida, lakini sharti lililowekwa katika sheria ile wanasema kwamba raslimali ya gesi na mafuta irudi Serikalini. Leo *TPDC* akitaka kununua mitambo, *either* katika kufanya utafiti wa *upper stream* or *downstream* ama katika kununua mitambo ya kusafirisha gesi itapaswa kupita kwenye utaratibu wa Kiserikali kuandika *minute sheet*, kuandika folios iende kwenye *Cabinet Ministers* ndiyo waweze kupata *approval*. Kwa sharti la kisheria kwamba hii *TPDC* iweze kujiendesha Kibiashara, nafikiri ni muhimu sana, Wizara ikaona umuhimu wa kuondokana na hizi *red tapes* hazitatusaidia. (Makofi)

Mheshishimiwa Naibu Spika, sambasamba na takwa hili la kisheria...

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Mmasi kuna taarifa. Mheshimiwa Salome Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante mimi napenda kumpa taarifa ndugu yangu Mheshimiwa Ester Mmasi kwamba taarifa zinazotolewa kwenye ripoti ya Kambi zinatokana na *sources* ambayo mojawapo ni ripoti ya *CAG.* Sasa tunaomba utufahamishe, hicho unachokisema unakitoa wapi? Usije ukawa unatulisha matango pori humu.

**MBUNGE FULANI:** *CAG* na wewe nani mwongo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salome Makamba unauliza swali huku unatoa taarifa, taarifa ni kwamba mtu kile anachokisema unakuwa unamwongezea kama hakijakamilika ama kimekaa namna fulani, sasa wewe unamuuliza swali ili aanze kujibizana na wewe jambo ambalo haliruhusiwi.

Mheshimiwa Ester Michael Mmasi malizia mchango wako.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kuna homa ambayo haijapata tiba, *dengue* leo inatiba, lakini homa ya kwetu humu ndani, haijapata tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko hivi *TANESCO* leo anaambiwa anarekodi hasara, si kila hasara ni hasara, mtu anapodaiwa si kosa la jinai na kudaiwa si hasara, nini kigumu katika hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niikatae taarifa ya rafiki yangu mpenzi, *comrade* wangu Salome, naomba niendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye masharti ya Sheria hii ya mwaka 2015 ya *Petroleum Act* inatuambia kwamba ni sharti kwamba Taasisi hii iweze kuwa Mfuko wa Rasilimali ya Gesi na Mafuta, ni sharti zuri sana, haina mjadala, lakini katika

masharti ya Mfuko huu, leo hii *TPDC* mwaka huu wa fedha peke yake imepeleka bilioni 66, lakini Mfuko huu una jumla ya bilioni 102, lakini toka *TPDC* imeanza kupeleka kule hakuna *a single coin* iliyoweza kutoka na kwenda kufanya *re-investment* kwenye masuala ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Waziri amesimama pale anasema kwamba anaenda kwenye mpango wa nyumba 200, baada ya hapo nyumba 1000, leo tunatakiwa tuongelee nyumba 10,000 au 20,000 leo tunatakiwa tusikie maendeleo ya kuleta nishati ya gesi Dodoma, lakini tuko Dar es Salaam pale tunahitaji Mfuko huu ufanye kazi Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, Mfuko wa *REA* unafanya kazi, tuondoe sharti la kisheria la asilimia tatu, halitatusaidia Mheshimiwa Waziri. Tunaomba sharti la asilimia tatu kama kifungo cha Waziri iondoke kwenye ile sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili, upo mkopo wa *EXIM Bank of China* ambayo ni shilingi 1.225 bilioni *US Dollars.* Kwa kuwa moja ya jukumu la Serikali katika kuandaa mazingira wezeshi ya *investors* ni pamoja na kuweka miundombinu. Leo hii Serikali imeenda imekopa pesa China inakuja inamwekea *TPDC* ina m-*charge* zile pesa. Leo hii *TPDC* ameandikiwa rekodi ya bilioni ya 340 kama rejesho lake, yaani huyu amepewa hesabu kama ni mdaiwa wa mkopo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jukumu la Serikali kuandaa miundombinu ili *TPDC* aweze hata kukopesheka akienda leo sokoni hawezi kukopesheka, kwa sababu anaonekana ana taarifa chafu. Naomba Mheshimiwa Waziri aje atuambie ni kwa nini asione umuhimu wa kuondokana na mkopo huu kwa Taasisi ya *TPDC* ili iweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imeshagongwa Mheshimiwa, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Shaabani Omari Shekilindi, Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba atafuatia na Mheshimiwa Hasna Sudi Mwilima ajiandae.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Nishati. Kwanza kabisa nimpongeze Waziri Mheshimiwa Dkt. Kalemani, Naibu wake, dada yangu Mheshimiwa Subira Mgalu kwa kazi anayoifanya, lakini pamoja na timu yao yote, wanafanya kazi kubwa sana kwa kweli mwenye macho haambiwi tazama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita kwenye mada moja tu, hususan katika kutaja vijiji vyangu vyote ambavyo havina umeme, pamoja na shule, pamoja na zahanati. Ni imani yangu kubwa kwamba Mheshimiwa Kalemani alifika Lushoto na akatoa maelekezo kwa Wakandarasi, lakini Mkandarasi yule, bado hajatekeleza ahadi ya Waziri mpaka leo. Sasa kwa kuwa leo timu nzima leo ipo hapa basi nami nianze Kijiji kimoja baada ya kingine ili wataalam wake wakusaidie kusukuma mambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na vijiji ambavyo havina kabisa umeme katika Jimbo la Lushoto ambavyo ni Vijiji vya kwanza Miegeo, Handei, Ngulwi, Kwemashai, Gare, Yamba, Kongei, Masange, Makanka, Milungui, Kireti, Kigumbe, Bombo Kamgobore, Kilole, Mazumbai, Ntambwe, Mavului, Mazashai, Mdando, Kweulasi, Bombo, Kwetango, Mbwaya, Kigulunde na Kwai. Hivyo ni vijiji kabisa ambavyo havina umeme kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vinavyofuata ambavyo ni vya kujaziliza ni Vijiji vya Chumbageni, Ngulwi, Kizara,

Yoghoi, Magamba, Kilangwi, Kwemashai, Boheloi**,** Migambo, Kwefingo, Kwemakame, Malibwi, Mbwei, Mshangai, Makole, Mlola, Ungo na Mhezi.

Mheshimia Naibu Spika, nimeamua kuyataja maeneo yangu kwa sababu Mheshimiwa Waziri alikuwa kila siku ananiambia nimletee orodha, kwa hiyo leo nimeamua kutaja orodha hii moja kwa moja kwa sababu wataalam wake wote wapo, basi waichukue na waendelee kumsukuma sana yule Mkandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee na sekondari ambazo hazina umeme ni Sekondari za Balozi Mshangama, Masange, Gare, Mkuzi, Kwai, Kwekanga, Mariam Mshangama, Makole, Mdando, Kweulasi na Mazashai. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo bila kupumzika niendelee na Vituo vya Afya na Zahanati. Kituo cha Afya Gare, Zahanati ya Makanka, Kituo cha Afya Ngwelo ambayo ni Kigulunde, Zahanati za Miegeo, Mavului, Mazumbai, Mbelei, Kweulasi na Mdando. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeyafanya hayo, maana nimechoka kuandika na *hansard* nayo ichukue ili Waziri akihitaji basi atachukua tu kiurahisi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeyataja hayo maeneo yote hayo lakini kila eneo nililolitaja hapo lina shule, lina Msikiti na Zahanati...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Vizuri sana Mheshimiwa, sasa nimemwona hapo Mheshimiwa Waziri alikuwa anaandika hivyo Vijiji vyote, Zahanati zote na Vituo vya Afya na Shule zote ameshaandika halafu dakika zako zimekwisha Mheshimiwa. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. *(Kicheko/ Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana na mimi huyo ni mchangiaji aliyevunja rekodi kwa siku ya leo. Ameshangiliwa na Bunge zima, *(Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Hasna Sudi Mwilima, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe ajiandae.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara ya Nishati, Wizara ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Dkt. Kalemani, kwa kazi kubwa anayoifanya kwenye Wizara hii; Naibu Waziri wetu ambaye ni Mheshimiwa Subira Mgalu; Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa *REA*, kwa kweli kazi wanayoifanya ni kazi ya uhakika nichukue nafasi hii kipekee kabisa kuwapongeza. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza kwa sababu gani, kwa kweli kwa kipindi kirefu, kumekuwa na tatizo kubwa la umeme, vijiji vingi katika nchi ya Tanzania vilikuwa havina umeme, lakini leo hii kutokana na taarifa ni vijiji vingi sasa vya Tanzania vimeweza kupatiwa umeme, vijiji zaidi ya 5,000 ni jambo ambalo la kipekee sana, tunapenda kupongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nipongeze kwa ajili ya mipango iliyopo, kwa sababu mpaka mwaka 2020 wanakusudia kufikia vijiji zaidi ya 10,278. Kwa hiyo mimi binafsi nina imani kubwa kwamba hata kwenye Jimbo langu la Busanda, vijiji vyote vitaweza kupatiwa umeme kwa mpango huu ambao wameuweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kanda ya Ziwa kuna Mradi mkubwa wa umeme wa kilovoti 220, kutoka Bulyanghulu kwenda Geita na mradi huu unapitia katika maeneo katika Jimbo langu la Busanda. Naomba sana, kwamba kupitia mradi huu viko vijiji 10 ambavyo vinatakiwa kupata umeme huu wa gridi ya Taifa, hivyo basi wakati ambapo utekekelezaji unavyoendelea naomba vijiji hivi viweze kupatiwa umeme mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo pia, jana nilikuwa napiga simu kule jimboni nimeambiwa tayari Wakandarasi wako wanafanya kazi maeneo ya Bujura. Kwa kweli, ni kiasi cha kupongeza kwa kazi kubwa ambayo Wizara inafanya kwa kweli wanafanya kazi njema sana kwa ajili ya Watanzania wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kwamba suala la umeme, ni suala muhimu sana, ili tuweze kufikia uchumi wa kati katika Taifa la Tanzania, lazima vijiji vyetu viweze kupata umeme wa uhakika na ndiyo kazi ambayo Serikali inafanya kwa sasa hivi. Kwa hiyo niombe Serikali iweze kuongeza bajeti kwenye Miradi ya *REA*, kwa sababu *REA* ndiyo ambayo tunaitegemea kuweza kusambaza umeme vijijini. Kwa hiyo niombe sana bajeti ya *REA*, iweze kuongezeka zaidi ili hatimaye basi vijiji vya Tanzania viweze kupatiwa umeme kupitia *REA. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda pia kuiomba Serikali kwamba wanapofanya utekelezaji wa miradi hii umeme vijijini wahakikishe kwamba zile sekta muhimu za umma kwa mfano, katika shule, Vituo vya Afya, pamoja na sekondari, kwenye huduma za kijamii, tuhakikishe kwamba umeme huu unapelekwa kipaumbele katika sekta hizo. Nasema hivyo kwa sababu, katika maeneo mengi ya vijijini ambako wamepata umeme, unakuta shule hazina umeme, Vituo vya Afya havina umeme, mfano tu Bukoli pale umeme wamepata umeme tangu mwaka 2014 lakini hivi sasa naongea Kituo cha Afya Bukoli hakijaweza kupatiwa umeme mpaka sasa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa Bukwimba, ahsante sana.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ili waweze kutekeleza miradi hiyo katika vijiji hivyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hasna Sudi Mwilima, hayupo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, atafuatiwa na Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele na Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya ajiandae.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa. Kwanza nitumie fursa hii kuishukuru Serikali kwa dhati kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nzega, kile kimeo cha pale Iguguta kimekwisha Naibu Waziri juzi alienda akazindua, Kashishi wameshatuzindulia, nina maombi machache kwa niaba ya wananchi wa Nzega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Mkandarasi anayefanya Mradi wa *REA* wa Nzega asimamiwe. Mradi tuliowasha katika Kijiji cha Ibushi tukiwa pamoja na Mheshimiwa Waziri, mpaka leo nyumba alizoishia ndiyo hizo hizo, wameshindwa kusogeza nguzo wala kupeleka waya. Kata ya Mbogwe mpaka leo umeme haujafika, Sekondari ya wasichana ya Mwanzoli mpaka leo umeme haujafika tumeshindwa ku-*enroll* watoto wa kike katika hiyo *boarding school* kwa sababu ya suala la umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Zahanati ya Idudumo mpaka leo umeme haujafika, wametoa *commitment by the end of July* ikishindikana *by the end July* Mkandarasi huyu kufanya kazi na Waziri amekuwa *very fair* kwake kwa sababu ya jinsia, tunaomba wachukue hatua kama Serikali kuhakikisha kwamba suala hili linatatuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nataka niseme, *fairly* kabisa mimi nawapongeza *TANESCO* na Serikali, suala la umeme *ration* na mgao wa umeme umepungua sana katika nchi sasa hivi, wamefanya hatua nzuri sana na ningetumia fursa hii kusema maneno machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama taifa tuna *plan* ya *energy mix,* na ukitazama *focus* ya vyanzo vya umeme ambavyo tunatarajia kupata kutokana na maji vyote tukifanya vitatupatia kama megawati 4,000; ukichukua na megawati 1600 tuliyonayo leo jumla tutakuwa tuna megawati 5600, *our target* ni kuwa na megawati 10,000 *by 2025.* Ni muhimu kama Serikali kuanza kujadili sasa hivi ni namna gani vyanzo vya *solar* vinaanza kutumika, na kama inawezekana tufanye *PPP* ili watu wa *private sector* waje wawekeze. Namna gani *themo* tunaanza kutumia, namna gani mradi wa Singida na Mradi wa Makambako unafufuka, namna gani Mradi wa Mchuchuma unaanza kutekelezwa ili *by 2025* tuwe na hizo 10,000 *megawati*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka niseme ni kuhusu *Stieglers*; kumekuwa na *national debate* kuhusu *stiegler's;* hapa tulipofika ni *point of no return stieglers must be implemented.* Sasa ushauri wangu kwa Serikali tuna mpango wa kuzalisha 2100 megawati kwenye mradi wa *Stiegler's.* Swali la kujiuliza *do we have a muster plan* ya namna gani tutakapoanza kuzalisha 2100 tuta-*maintain* kwa kipindi cha miaka 10-15 *production* 2100?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hatutakuwa na *grand plan* hiyo maana yake *investment* yote tunayowekeza pale itakuwa ni *waste,* ni lazima tuangalie namna gani vyanzo vya maji vinavyoenda kwenye Mto Ruaha na Mto Kilombero vinavyopeleka maji kwenye eneo la *Stiegler's* vinakuwa *protected* na namna gani shughuli za binadamu zilizoko katika *upper stream* zinakuwa *marginalized* ili vyanzo hivi vya maji viweze kwenda kule. Tusije kujikuta *ata the end of the day* baada ya miaka 5 *stieglers* ina-*produce 40 percent* ya *capacity.* Baada ya miaka 10 *stieglers* ina-*produce just 50 percent* ya *capacity.* Tuna *experience* ya Kihansi, tuna

*experience* ya nyumba ya Mungu, tuna *experience* ya haya mabwawa ya maji. Ni muhimu sana sasa Wizara ya Mazingira, Wizara ya Ardhi, Wizara ya Kilimo kuwa na *joint effort* ya kutengeneza *a grand plan* ya ku-*protect* mazingira katika maeneo haya. Suala la *Stiegler's is national decision* ni maamuzi ya nchi *we have to do it* na kama tunafanya *we do it rightly* ili ku-*attain efficiency and effectiveness.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru naunga mkono hoja *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza ajiandae.

Mheshimiwa Magdalena Hamisi Sakaya atafuatiwa na Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza, Mheshimiwa Rashid Mohamed Chua Chua ajiandae.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba ambayo ipo mbele yetu; na nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kuweza kusimama tena kwenye Bunge lako Tukufu. Naomba pia niungane na Wabunge kupongeza kazi ya *REA* inayofanyika maeneo mbalimbali ya kuweza kuongeza juhudi za umeme hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Mheshimiwa Waziri anazindua *REA III* mwaka 2017 kwanza alisema kwamba itaenda *speed,* alisema hata kwa wakandarasi aliokuwa anawapa maagizo; na pia kwamba ile *REA III* itakwenda mpaka kwenye vitongoji tofauti na *REA* awamu ya kwanza na *REA* awamu ya pili. *REA* hii awamu ya tatu kwanza inakwenda taratibu sana; na ingawa Mheshimiwa Waziri anatembelea maeneo mbalimbali lakini akishafika kule akitoka bado *speed* inakwenda *slow* vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Kaliua tulipewa vijiji saba tu *REA III,* lakini mpaka napoongea huu ni mwaka wa pili kilichowaka umeme ni kijiji kimoja tu na imewekwa transfoma moja tu; vijiji vingine vitatu wamepeleka nguzo nyaya bado na vijiji vingine 3 bado kabisa hawajafika. Sasa kwa *speed* hii tunayokwenda nayo Mheshimiwa Waziri itachukua miaka mingapi hata kwa hivyo saba tu kukamilika? Achana na vingine ambavyo bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, *speed* ya *REA* bado ni ndogo. Fedha hii ya *REA* ni *ring fenced,* iko pale, haifanyi kazi nyingine, lakini *speed* imekuwa ni ndogo sana kila siku kuna vikwazo. Kwanza walikuwa wanasema ni nguzo, nguzo zikija wanasema ni nyaya, nyaya zikija wanasema ni *tranfoma,* kwa hiyo kila siku ni matatizo. Namwomba Mheshimiwa Waziri, *speed* ile ambayo mlikuwa mmeanza nayo mara ya mwanzo kushinikiza wakandarasi wafanye kazi kwa muda wafuatiliwe wafanye kazi kwa muda. Mwaka jana wakasema ni mvua nyingi mwaka huu mvua haziko nyingi. Kwa kweli tunasikitika kwamba *speed* ya *REA* ni ndogo pamoja na kuwa fedha ya *REA* iko *ring fenced* kazi yake ni hiyo moja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, ndani ya Wilaya ya Kaliua umeme umekuwa ni kizungumkuti, imekuwa ni kumulimuli. Mheshimiwa Waziri kila siku ya kwa Mungu, hata leo, tunakosa umeme masa sita mpaka nane, kila siku. Kwa hiyo kwa maana nyingine ule uwepo wa umeme hauonekani, maana umeme ukiwepo usaidie jamii kunufaika, mashine zifanye kazi, *welding* wafanye kazi, saluni zifanye kazi, vile viwanda vidogovidogo vifanye kazi. Sasa kama wanafunga kwa muda wa masaa nane kwa siku hauna faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri tulikuwa na shida ya nguzo kwenye maeneo ambayo ni mbuga, ukaagiza tangu mwaka jana zibadilishwe; mpaka leo shida ya Kaliua katika umeme iko pale pale. Hivi navyoongea leo kuanzia saa moja asubuhi mpaka saa nane walikuwa hawana umeme; na huu ndio utaratibu, hiyo ndiyo historia ya Kaliua. Mheshimiwa Waziri umeme ni maendeleo, umeme

ni uchumi; leo uchumi wetu hauwezi kupanda kama vijana kwa masaa nane kwa siku hawafanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la kujenga *substation.* Kwenye bajeti ya mwaka jana Mheshimiwa Waziri alituambia kwamba vinajengwa vituo viwili kati ya Kaliua na Urambo na Kaliua na Uvinza; na nina imani kabisa inawezekana kujenga hiyo *substation* ukaweza kusaidia angalau umeme labda wakapokelea pale kwenye hiyo ki-*substation* ukawa umeme wa uhakika. Naomba, vile vituo Mheshimiwa Waziri havikujengwa kwenye bajeti ya mwaka jana, mwaka huu unapokuja ku-*windup* utuambie, je, mwaka huu vitajengwa? Ili angalau tuweze kuondokana na shida ya umeme. Leo umeme ni uchumi lakini kwa mwendo tunaoenda nao Kaliua, maeneo ya Urambo na maeneo mengine bado hatuoni faida kubwa sana kwa sababu tunaona nguzo na nyaya tu lakini umeme hautumiki kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala linguine, Mheshimiwa Waziri amekuwa anatamka hapa Bungeni, nje ya Bunge na hata ndani ya Bunge kwamba pale *REA* inapoishia *TANESCO* ipeleke umeme kwa shilingi 27,000 vijijini, lakini hilo halitekelezwi, sasa sielewi kwamba maagizo haya hawajapewa *TANESCO?* Wilaya ya Kaliua tuna zaidi ya watu 160 wameomba wafungiwe umeme, wamefanya *wiring* hawapelekewi umeme na shilingi 27,000 wanayo. Hiki kingine ambacho *TANESCO* wanasema kwamba lazima kuwepo na nguzo, Mheshimiwa Waziri inakuwa ni *double standard.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama *REA* imepeleka umeme mpaka maeneo fulani halafu kuanzia pale mwananchi anaambiwa alipe nguzo 338,000, kama ni nguzo mbili ni 480,000, kama ni nguzo tatu ni 900,000 ilhali mwenzake hapa jirani tu kafungiwa umeme kwa shilingi 27,000; hiyo ni *double standard.* Naomba Mheshimiwa Waziri utuhakikishie unapokuja ku-*windup* kesho hapa, utuambie namna gani wananchi wa vijijiini maeneo ambapo *REA* imeishia wanaweza kupata umeme kwa gharama ile ile unayosema kila siku, 27,000, kwa sababu ni haki ya kila mmoja kuweza

kupata umeme kwa bei ambayo ni *standard* na ambayo itakuwa ni haki kwa wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, limekuwepo tatizo lingine kwenye uwekezaji kwenye sekta ya mafuta. Tumekuwa tunalalamika kwamba kuna vikwazo vingi vingi kwenye masuala ya uwekezaji hapa Tanzania kwenye maeneo mbalimbali. Hata kwenye sekta ya mafuta pia lipo tatizo la uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapotaka kuwekeza kwenye sekta ya mafuta aidha kujenga kituo cha mafuta kuna milolongo mingi sana ya kupitia, pia kuna vibali vingi sana vya kupitia. Ukianza na NEMC wanachukua mwaka, ukienda halmashauri unaomba kibali miezi sita, ukitoka tena ukienda EWURA miezi 6, useme uende OSHA miezi sita. Miaka miwili na nusu unahangaika tu na kibali huujakipata uanze kujenga kwa mwendo huu mwekezaji yeyote aliyejiandaa ataweza? Hawezi kwa hiyo tunaomba kuwepo na *one stop center,* kama ni masuala yafanyike kwa pamoja ili mtu anapokuwa na lengo la kuwekeza aweze kuwekeza kwa kirahisi kwa sababu uwekezaji ndio uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine pia ambalo ni tatizo ni faini kubwa sana wanazopigwa watu wa mafuta. Sekta hii unakuta kwamba wale ambao ni wakubwa ndio wanaoweza kuwekeza tu, wale wadogo wanaojichomoza hawawezi; kwa sababu mtu mkubwa ana mitaji mikubwa, anaweza akawa anasubiri vibali huku anaendelea na mambo mengine; lakini kwa yule ambaye anayechipukia ambao ndio tunaowalenga, Watanzania wa chini wenye uwezo mdogo, waweze kunyanyuka, wanakwama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunaomba; wakati mwingine kuna faini kubwa sana zinapigwa kiasi kwamba mtu ana mtaji wa milioni 10, anapigwa faini milioni 20, umemuulia pale pale na bado unamdai. Faini tulizokubali ziwepo pale mtu anapofanya kosa ziendane na hali halisi kwa sababu tunapenda hawa wenzetu ambao ni wa chini pia waweze kunyanyuka kwa ajili ya kuhakikisha kwamba

wanachangia uchumi na ni sehemu ya maendelo ya taifa lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni hizi *criteria* za kampuni za mafuta au watu wanaofanya biashara za mafuta. Kumekuwepo na *criteria* mbalimbali, kuna watu wanaitwa CODO, kuna wengine wanaitwa DODO, na wengine ni wale wa chini kabisa. Unakuta mtu ambaye anaagiza mafuta kwa jumla na yeye pia anaruhusiwa tena kwenda kuuza kwa rejereja. Kwa hiyo wale wanaoagiza mafuta kutoka nje wanakuja wanauziana kampuni madogo ndogondogo nao pia wanaruhusiwa kufungua vituo vidogo vya mafuta wanauza reje reja; kwa hiyo ile *fair competition* inakosekana. Wakati huo umemuuzia mtu mdogo mdogo reje reja pembeni yake wewe unakwenda kufungua tena kituo kwa bei ya reja reja. Kwa hiyo wewe una faida kwa sababu kwanza ulishauza kwa bei jumla, pili unawezo wa kupunguza bei kwa sababi tayari unapata faida mara mbili. Mheshimiwa Waziri, kwa nini Wizara inaruhusu haya? Matokeo yake wale ambao ni wadogo hawawezi ku-*compete* kwenye biashara, mara nyingi unakuta wameondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ndiyo maana ukisoma kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri unakuta kuna mahali kuna vituo 73 baada ya mwaka vimefungwa vitano kwa sababu wanaofunga ni wale wadogo ambao wanashindwa ku-*compete* na biashara. Tunaomba hizi *criteria* ziheshimiwe; Kama mtu anaagiza mafuta nje; kama yeye ni mtu mkubwa na ana uwezo wa kuagiza mafuta nje abaki kuagiza mafuta nje. Mheshimiwa Waziri wale ambao ni CODO wanaoagiza mafuta nje akishamuuzia mwenzake na ile *criteria* nyingine waweze kuhakikisha kwamba wao wanawaachia kwenye sekta ile tena wauze. Wale wa chini kabisa kule ambao ndio DODO waweze kuwa na uwezo wa kuweza kuuza pia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga, ahsante sana.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza atafatiwa na Mheshimiwa Rashid Mohamed Chuachua, Mheshimiwa Hasna Sudi Mwilima ajiandae.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati. Niungane na Wabunge wenzangu waliotangulia kupongeza viongozi wetu Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara hii kwa kazi nzuri na kubwa wanayoifanya; tumepiga hatua kubwa. Ukijaribu kuangalia kulingana na taarifa *coverage* mpaka sasa hivi vijijini ni karibu asilimia 84 kwa maana ya kwamba kati ya vijiji 12,268 ni vijiji takribani 1990 tu ambavyo havijafikiwa na umeme na ambavyo nina uhakika kwamba 2020 basi tutakuwa tumefika maeneo yote hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika nikienda kwenye mradi wa *REA* hususan *REA* awamu ya tatu zipo changamoto ambazo tunaziona hususani katika *speed* kwa wakandarasi ambao wamepata zabuni hizi. Niombe katika Wilaya yangu ya Ngara usimamizi wa karibu kwa mkandarasi uweze kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama tulivyokuwa tumeanza kwamba tupeleke umeme kwenye maeneo kutokana na uhitaji ambapo kuna huduma za kijamii kama shule, afya n.k. Niombe kwamba katika Jimbo langu la Ngara kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ulipokuja; umeshakuja zaidi ya mara tatu; nimekuwa nikikulilia kwamba vile vijiji ambavyo vina huduma hizi, kama Kata ya Bukiriro kwa maana ya kijiji cha Bukiriro, Kijiji cha Mururama kwenda Kigarama, Mrusagamba Tanga, Kumbuga; kwa sababu ya umuhimu na huduma zilizoko kule tunahitaji kupata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vipo vijiji ambavyo vilipitiwa na umeme *REA* II lakini hakuna umeme unaopatikana; kwa mfano Kijiji cha Kenda ambapo line ya

kutoka Ngara Mjini kwenda Lusumo boda ilipita pale na ukafanyika uharibifu; kwa maana ya kwamba kuna mazao yaliyokatwa lakini watu hawa hawajaunganishiwa umeme; sawa na Kijiji cha Kata ya Mabawe, Kijiji cha Murugina ambapo pia ulipita line kubwa lakini mazao kama kahawa yalikatwa na bado mpaka sasa hivi wananchi hawa hawajaunganishiwa umeme basi tuweze kuwafikiria hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwamba tuliunganishwa kwenye *grid* ya taifa mwaka wa jana lakini mpaka sasa hivi takribani mwaka mzima huduma ya umeme imekuwa ni shida kutokana na msongo wa umeme unaokuja kuwa mdogo, ambao mara kadhaa umekuwa ukikatikana hata kushindwa kukidhi kutoa huduma. Hii imeathiri hata huduma ya maji kwa sababu pampu zinazotumia umeme kusukuma maji zimekuwa haziwezi kufanya kazi vizuri na hivyo kusababisha adha ya ukosefu wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao mradi wa njia ya kusafirisha umeme mradi wa kutoka Rusumo kuelekea Nyakanazi. Line hii ni line ambayo imepelekea kwamba sasa wananchi wanaopitiwa na mradi huo hawajapata fidia mpaka sasa hivi. Mwaka jana kulikuwa na *commitment* ya Serikali kwamba kufikia mwezi wa tano mwaka jana wangekuwa wamepata fidia lakini mpaka sasa hivi wananchi hawa wa Kijiji cha Kafua, wananchi wa maeneo ya Benako kwenda mpaka Rusumo hawajapata fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo mradi tunaoendelea nao katika Jimbo la Ngara ambao ni mradi wa nchi tatu, mradi wa maji wa Rusumo. Mradi huu umekuwa na changamoto kubwa kwa sababu wapo wananchi ambao mpaka sasa hivi ni mwaka wa tatu mradi umeanza hawajapata fidia. Kila ambapo wamekuwa wakijaribu kudai haki hiyo kumekuwa na uzungushwaji hususani Kampuni ya *NELSAP* ambao wanahusika moja kwa moja katika kuhakikisha kwamba watu hawa wanapata fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri katika hili ajaribu kufatilia kwa karibu ili wananchi ambao

wanadai fidia katika mradi huu waweze kupata stahiki yao. Ipo athari kubwa ya milipuko katika eneo hili la mradi ukizingatia kwamba wanapochoronga kwa ajili ya kutengeneza tanel kumekuwepo na mtikisiko mkubwa. Awali ilikuwa ifanyike *light blastaling* lakini sasa hivi ilipofikia takriban mita 380 ambazo zinatakiwa zichorongwe kwa *heavy blasting* kuna athari kubwa ambayo itajitokeza na athari ambayo haikuonekana wakati wa kuandaa *visibility study na detail design.*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba katika vikao ambavyo Mheshimiwa Waziri unahudhuria, vikao vya mawaziri wenye dhamana muweze kuangalia ni namna gani ya kuhakikisha kwamba watu wanapata fidia lakini pia kuangalia namna...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana. Mheshimiwa Dokta Rashid Mohamed Chuachua atafatiwa na Mheshimiwa Hasna Sudi Mwilima, Mheshimiwa Nagenjwa Livingstone Kaboyoka ajiandae.

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi nipate fursa ya kusema kidogo kwa ajili ya kuchangia Hotuba ya Waziri katika Wizara hii ya Nishati. Nianze na kumpngeza sana Mheshimiwa Dkt. Kalemani; ni mchapakazi kwelikweli yeye na Naibu Waziri wake wanafanya kazi usiku na mchana kuzunguka Tanzania kwenda kutatua matatizo ya wananchi wetu wanyonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Wizara kwa jumla kwa kazi kubwa wanayofanya, na niwapongeze sana kwa sababu ukisoma hotuba yao ukurasa wa 63 wanaonyesha wazi kwamba Tanzania kwa sasa ni nchi ya kwanza katika Afrika ya Mashariki katika kusambaza umeme vijijini; hili ni jambo kubwa sana, hatuwezi kukaa bila ya kuwapongeza. Pamoja na pongezi hizo ningependa nimfahamishe Mheshimiwa Waziri kwamba katika mikoa

anayoishughulikia kwenda kusambaza umeme hafahamu usiku na mchana anapotembea kwamba umeme katika Mkoa wa Mtwara umesambazwa katika vijiji vichache sana ukilinganisha na mikoa mingine. Huu ni ujumbe ambao Mheshimiwa Waziri anatakiwa awe anatembea nao wakati wote ili atuangalie kwa macho mawili katika Mkoa wa Mtwara namna ambavyo vijiji vichache sana vimepata umeme wa *REA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri, katika ziara yake aliyofanya kwenye Mkoa wa Mtwara amefika kwenye Wilaya ya Masasi na amefika kwenye jimbo langu. Mheshimiwa Waziri amewasha umeme katika Kijiji cha Mombaka katika Kata ya Mombaka pia kwa niaba ya wananchi amezungumza mambo mengi na matarajio makubwa ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri umetoa maelekezo ambayo nakuomba sasa uendelee kuyasimamia. Umetoa maelekezo kwamba umeme utapatikana kwa shilingi 27,500, uwe unasambazwa kwa njia ya *REA* au unasambazwa na *TANESCO;* naomba hili pia ulisisitize sana katika Bunge lako. Pia umetoa maelekezo kwamba wananchi wa Kata ya Sululu katika Kijiji cha Sululu washushiwe umeme, maelekezo haya naomba uendelee kuyasimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Waziri ametoa maelekezo katika Kata ya Chanikanguo, wananchi wa Kijiji cha Namakongwa wapelekewe umeme, aendelee kuyasimamia maelekezo hayo. Pia Mheshimiwa Waziri ametoa maelekezo wananchi wa Kata ya Mombaka, Kijiji cha Namikunda A na Namikunda B wapewe umeme, maelekezo hayo naomba Waziri aendelee kuyasimamia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba, katika Halmashauri yangu ya Mji wa Masasi ambayo ina vijiji takribani 31 na ina mitaa zaidi ya 48, ukijumlisha tuna maeneo mengi lakini zaidi

ya maeneo 40 ukijumlisha na vijiji 20 hatujapata kabisa umeme na zipo Kata ambazo hazijapati umeme hata kijiji kimoja. Sasa hivi kuna mkandarasi anaendelea kufanya kazi lakini ana vijiji sita (6) tu, hii inaonesha wazi kwamba kasi ya kusambaza umeme katika Jimbo langu hairidhishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ushauri; kwanza Wizara wanapopanga mipango yao wanaipanga kwa kuzingatia Tawala za Kiwilaya jambo ambalo wanatakiwa waende mbele zaidi. Wanatakiwa watambue kwamba wanapochukua vijiji kwenye wilaya, ndani yake kuna halmashauri na ndani yake kuna majimbo; kwa hivyo basi, wanapofanya mipango yao waende mbele zaidi wasiishie kwenye Wilaya kwa kuchagua vijiji, wanaacha tawala nyingine zenye uwakilishi. Kuna majimbo ndani ya kila wilaya lakini kuna halmashari, ili kuweza kugawa hizo rasilimali sawasawa wasiishie kwenye wilaya peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hasna Sudi Mwilima, atafuatiwa na Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mheshimiwa Augustine Vuma Holle ajiandae.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi. Kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na timu yote ya Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya. Natambua kwamba hawalali wanafanya kazi lakini sisi kama wawakilishi wa wananchi tunapoona wanapita huko mikoani lakini umeme hauwashwi kwenye vijiji lazima tuseme tunapopata nafasi hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Waziri umeme kwenye Kijiji cha Nyanganga wameshawasha na wananchi wanashukuru sana kwa jitihada alizozifanya. Hata hivyo, tuna tatizo kubwa katika Mkoa wa Kigoma, nguzo na vitendea kazi vingine bado havijawasili katika mkoa wetu. Sasa tunashindwa kufahamu, ni lini wakandarasi hawa

wataanza kupeleka nguzo Nguruka ili vijiji vyangu vya Chagu, Kijiji cha Mganza, Kijii cha Mtegowanoti, Kijiji cha Nyangabo, Kijiji cha Nguruka, Kijiji cha Bweru, Itebula, Mganza, Kasisi, Mlyabibi, Mpeta na kuendelea, lini watapelekewa nguzo ili angalau umeme sasa uweze kuwafikia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anatambua kwamba jiografia ya Jimbo langu ni mbaya, wananchi wa Ukanda wa Ziwa Tanganyika kwa maana ya Kata ya Mwakizeja, kuna vijiji kama viwili havijapelekewa umeme, lakini Kata ya Ilagala. Tatizo langu mimi kama mwakilishi wao, tangu *survey* ile ya kwanza waliyoifanya mpaka leo hakuna kinachoendelea. Sasa ninawiwa kwenye kushika shilingi na naomba kabisa niwekwe kwenye *list* ya kushika shilingi ili niweze kuambiwa ni lini vifaa vitapelekwa kwenye vijiji vyangu 24 ili sasa kazi ya kupeleka umeme iweze kuanza mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri afanye ufuatiliaji wa kina kwa mfano, tunacho Kitongoji cha Muyobozi na Kijiji cha Kabeba. Tangu mwaka jana mwezi wa Saba (7) wenzao wamewashiwa umeme, wao waliwashiwa siku moja, siku ya pili wakabeba *transformer* wakazipeleka Kigoma Mjini. Sasa swali langu, tangu nimelia kwa Waziri kwamba Muyobozi na Kabeba wawashiwe umeme hawajawashiwa umeme, basi waende wakang'oe nguzo. Wakang'oe nguzo, wakang'oe nyaya ili wananchi waache kuonga nyaya na nguzo kwa mwaka mzima, umeme hawawashiwi, tatizo liko wapi? Nimeshalalamika sana kwa Mheshimiwa Waziri, safari hii nitashika shilingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia kwenye vijiji vyangu vya Kata ya Kalya, tulikubaliana vizuri *REA* awamu ya tatu kwamba Kijiji cha Ubanda, Lufubu, Kashaguru, Tambusha, Kalya na Sibwesa watapata umeme kutoka Ikola au kutoka Mwese. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, hadi leo ninavyoongea hakuna *survey* yoyote iliyofanywa kwenye hivi vijiji sita, sasa wananchi wamenituma niulize, hii ndiyo bajeti ya mwisho. Bajeti hii tunalialia hapa kwa sababu bajeti

inayokuja tunakwenda kwenye uchaguzi, sasa Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa kuhitimisha nataka nijue hivi vijiji sita ndani ya Kata ya Kalya vinapata lini umeme kutoka Ikola au Mwese ili tujue *way forward.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa Hasna, ahsante sana kwa mchango wako.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, atafuatiwa na Mheshimiwa Augustine Hole Vuma na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab ajiandae.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Nishati. Kwanza nipende kusema kwamba naunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani. Pia nitaanzia pale Mheshimiwa Mwijage alipoachia alipojaribu kulinganisha barabara na bomba la gesi hili ya kutoka *Songas* na kuja Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba kwanza ukiangalia mradi wowote unaotakiwa kuanzishwa lazima uangalie *cost effectiveness* yake. Kwa maana yake lazima unaangalia *return to capital,* sasa anachotaka kututumainisha Mheshimiwa Mwijage ni kwamba haijalishi kama mtambo huu wa gesi unazalisha *full capacity* ama unazalisha *under capacity.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa gesi kutokana na ripoti ya *CAG* ambayo imetoka Machi, 2018, unakuta kwamba matumizi ya mtambo huu ni asilimia 24 tu

ukilinganisha na *installed capacity.* Kwa maana yake ni kwamba kwa asilimia 76 matambo huu una-*run under capacity,* maana yake ni nini, maana yake ni kwamba huu mtambo unaleta hasara maana *TPDC* lazima iendelee ku-*service* mradi ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, ukiangalia kama *TPDC* itandelea ku-*service* mtambo ambao hauzalishi maana yake nini, hapo hapo unganisha na *TANESCO. TANESCO* wanashindwa kulipa ankara za *TPDC* ambayo *TPDC* inaiuzia *TANESCO* gesi asilia kwa kuzalisha umeme wa Kinyerezi, Ubongo II, *Symbion Power Plus.* Ni wazi kwamba *TPDC* itashindwa kulipa mkopo wa *Exim Bank* ya China. Tumejua madhara ambayo wenzetu walioshindwa kulipa mikopo hii imekuwa ni nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia mkataba ule Kifungu Na.2 ni wazi kwamba *TPDC* watakaposhindwa kulipa mkopo ule, *Exim Bank* ya China itachukua huu mradi na ui-*run* na ukijua kwamba wenzetu wa China wana fedha za kumwaga ni kwamba wataufanya u-*run* kwenye *full capacity,* gesi yetu yote itakuwa inachukuliwa kwa Wachina na sisi tutakuwa tunabaki tukishangaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kusema tu kwamba, *TANESCO* wanajitahidi sana, lakini pamoja na jitihada hizo wanakumbwa na matatizo mawili. Kwanza *TANESCO* wanakuwa *controlled* na *EWURA, EWURA* ndiyo wanaopanga bei. Waheshimiwa Wabunge, wewe angalia una *product* yako unauza, lakini ni mtu mwingine anakupangia bei unategemea hiyo biashara iende kwa namna gani. Kwa mfano, *TANESCO* wananunua umeme kwa shilingi 544.65 kwa *unit* na kuuza kwa shilingi 279.35, haihitaji kwenda Chuo Kikuu kuchukua *economics* kujua kwamba kwa njia hii tunaiua *TANESCO*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili Mashirika ya Umma hawalipi madeni kwa *TANESCO, TANESCO* inadai fedha nyingi sana kwa mashirika mbalimbali ya umma. Pamoja na Mheshimiwa Rais kusema kwamba wakatie

umeme yale mashirika ambayo hayalipi umeme, napenda nikuulize wewe ambaye unailaumu *TANESCO.* Kama ingekuwa wewe uambiwe ukatie umeme Muhimbili, kwa ubinadamu ungeweza kuikatia Muhimbili umeme? Kama huwezi ina maana gani, kwa nini Serikali isichukue jukumu la kulipia mashirika yale ambayo wanajua hayatengenezi faida na hayawezi kulipia umeme. Ni wazi kwamba Shirika la *TANESCO,* kama halitaweza kusaidiwa na Serikali ni wazi kwamba litakufa katika muda mfupi ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo napenda kusema pamoja na Waziri amesema kwamba *TANESCO* hawahitaji ruzuku, lakini tujue kwamba kama Mashirika ya Umma hayalipi na sina hakika kama Wizara yenyewe ya Nishati wameshalipa deni lake kwa *TANESCO*. Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka kuipa ruzuku au kulipia yale mashirika ambayo yameshindwa kulipa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye *REA* namba tatu, kwanza niseme namshukuru Waziri amefanya jitihada sana kumpigia Meneja kwenye Jimbo langu kwamba waweke umeme kwenye vile vijiji alivyoahidi. Tulifanya ufunguzi wa mbwembwe wa Mkoa wa Kilimanjaro pale Mwanga, lakini unakuta sasa hivi kinachotokea *REA* wanapeleka nguzo wanaweka hapa halafu wanatoweka. Sasa wananchi wanaona hiki ni kiini macho au maana yake ni nini? Pia nipende kuuliza, kule kwangu Jimbo la Same Mashariki kuna mito mikubwa ambayo ina maporomoko ambayo tungeweza kutumia maji kuzalisha umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ya *PAC* ilipotembelea *Arusha Technical College* tuliona wanafunzi wale wanavyojaribu kuzalisha umeme lakini kwa kutumia *laboratory* na kutumia ndoo za maji. Kwa nini Serikali isisaidie vyuo kama hivi vikaenda kufanya majaribio au *practical* kwenye mito kama hii ambayo ina maporomoko na kwa ajili hiyo nisingemsumbua Waziri kwamba vijiji vyangu na vitongoji vyangu havina umeme. Kwa hiyo naomba kwanza akija kuhitimisha anieleze kwamba mpaka sasa hivi ule mkopo *Exim Bank* wa China umelipwa kwa asilimia ngapi. Pili, napenda

anieleze kwamba kama hawataweza kushinikiza mashirika ya umma yakalipa yale madeni, wanategemeaje *TANESCO* iendelee ku-*survive? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda nizungumzie tu kwamba katika ajira, katika Sekta ya Mafuta na Gesi inasikitisha kuona kwamba kampuni za ndani ziliweza kupata sehemu ya manunuzi au ya ku-*supply* vitu kwa asilimia tisa tu. Makampuni yote ya nje ndiyo yamefaidi miradi inayoletwa Tanzania. Ukiangalia mafunzo katika sekta hii yamefanywa kwa asilimia 20 tu kwa maana hiyo ina maana kwamba hatuna *personnel* ya kuweza ku-*run* gesi zetu au mitambo hii ya gesi. Ukiangalia katika wataalam waliofundishwa au walioelimishwa mpaka sasa labda wawe wameongezwa wengine kutokana na ripoti ya *CAG,* ni asilimia sita tu ambayo katika Sekta ya Gesi na Mafuta wameweza kupata masomo ambayo ndiyo *relevant* kwenye hii sekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunachotaka kusema, hivi Tanzania kwa nini sisi tunakumbatia mashirika ya nje hata kama mradi ume-*provide* kwamba mafunzo yafanyike, hayafanyiki. Matokeo yake watu wetu hawapati ajira, watu wetu hawafaidiki na fedha hizi ambayo ni mikopo kutoka nje ambayo italipwa na jasho la wananchi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Augustine Holle Vuma atafuatiwa na Mheshimiwa Adadi Rajab na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso ajiandae.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi hii ambayo nimeipata jioni ya leo kuchangia kwenye bajeti hii. Nipende kwanza kuipongeza Serikali, kwanza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli na nimtakie kila la kheri kwenye ziara

yake aliyopo nchini Namibia arudi salama, tunamuombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kumpongeza pia Waziri na Naibu Waziri na Timu nzima ya Wizara ya Nishati kwa kazi kubwa ambayo wanafanya kuhakikisha kwamba wanatuletea maendeleo katika sekta hii. Najua mkandarasi wa kule Kigoma na Katavi wameanza utekelezaji wa mradi ule *late* kidogo, lakini naamini kwamba kama Serikali ambavyo imekuwa ikielekeza wakandarasi kumaliza miradi kabla ya wakati nina imani kwamba mkandarasi ambaye anafanya kazi Mkoa wa Kigoma naye atamaliza kwa wakati na kuhakikisha kwamba Kata zangu za Nyachenda, Bugaga, Buzye, Kasangezi, Lusesa, Kalela, Lungompya na nyingine zinapata umeme kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende pia kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa na maamuzi magumu ambayo walifanya kwenye mradi wa *Rufiji Hydro Power.* Naomba niseme kitu kimoja, ndugu zangu nimekaa hapa nikiwa nasikiliza michango ya watu tangu mwaka jana na mwaka huu nimeona, hasa ndugu zetu wa upande wa pili. Niseme Rais wa Awamu ya Nne aliwahi kusema kwamba akili za kuambiwa changanya na za kwako, akimaanisha usiamini kila unachoambiwa. Sasa ndugu zangu kwa sababu mabeberu wamekuwa wanakataa mradi huu ambao ni *very potential* kwa Taifa letu, msiingie kwenye mgogoro wa kuwasapoti ili hali mnajitoa ufahamu kwa faida za mradi huu wa *Rufiji Hydro Power.* (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme tu kwa faida ya Watanzania, Mradi huu wa *Rufiji Hydropower* una faida nyingi sana kwa Watanzania na Taifa kwa ujumla. Faida ya kwanza kabisa tunaenda kupata umeme ambao tunaupata kwa bei ndogo kuliko umeme wa chanzo chochote katika nchi hii, namba moja kabisa. Tunaenda kupata umeme mwingi; kwa *study* iliyopo kwamba katika nchi yetu ya Tanzania hakuna chanzo chochote cha nishati ya umeme ambacho kinaweza kikatoa nishati ya bei ndogo lakini kwa wingi kama chanzo cha maji. Kwa hiyo uamuzi wa Serikali

kujikita kwenye miradi ya kuzalisha umeme wa maji ni uamuzi sahihi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, faida ya pili, mradi ule ukiusoma vizuri utaona kwamba kutakuwa na miradi ya uvuvi pia. Wanavyojenga lile bwawa kutakuwa kuna *potential* watu kufanya shughuli za uvuvi ambayo ni shughuli ya kiuchumi ikayoweza kuwasaidia wananchi ambao watafanya shughuli hiyo. Sababu ya pili au faida ya pili, tunategemea mradi ule kutakuwa na umwagiliaji, watu wanafanya kilimo cha mpunga na miwa na *study* inaonesha kwamba mpunga au mchele utakaotoka kule kwenye bonde lile utaweza kulisha Afrika Mashariki na Kati, sasa wanakataa nini kwenye mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye sababu nyingine, ule mradi kwa sababu ni wa kipekee nawahakikishieni ule mradi utakuwa ni kivutio cha utalii Afrika Mashariki. Wako watu ambao wakija Tanzania watataka kwenda kuona kule *Rufiji Hydro Power* namna ambavyo ilivyo na kujifunza. Pia huu mradi naamini, nitofautiane na wengi ambao wanaamini kwamba huu mradi unaenda kuharibu mazingira, niseme huu mradi unaenda kutunza mazingira kwa sababu gani, wananchi wengi vijijini kule wanatumia nishati ya kuni kwa ajili ya kuleta mwanga lakini pia na kupika. Kama haitoshi wanatumia vibatari kwa ajili ya nishati ya mwanga. Sasa umeme unapokuwa umeenda tunaamini kwamba matumizi ya kuni yatapungua lakini na matumizi ya vibatari yatapungua. Huo utakuwa ni utunzaji wa mazingira kupitia mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme huu mradi mimi naufananisha na *three gorges* ya China, huu mradi ulianzishwa na Rais wa kwanza wa China ambaye alikuwa anaitwa Sun Yat-Sen. Huu ni kama vile mradi wetu huu ilivyokuwa wazo la Mwalimu Nyerere vilevile na ulibuniwa zaidi kabla ya mwaka 1980, huu wa *three gorges.* Sasa kwa sababu ya figisu figisu kama ambazo tunasema hapa kwetu Tanzania, huu mradi ulianza kutekelezwa kuanzia miaka 1990.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutekelezwa kwa mradi huu kulitokea baada ya Bunge la China kupiga kura kwamba kama nchi inahitaji mradi huu au haihitaji. Walivyopiga kura theluthi mbili ya Wabunge wa China wakakubali kwamba mradi huu wanautaka kama Taifa. Sasa niseme sisi wameleta bajeti hapa Wizara mwaka jana kuomba bilioni 700 kwa ajili ya mradi huu, sisi Wabunge wa CCM nadhani na wa *CUF* ambao ni zaidi ya robo tatu, zaidi ya idadi ya ile ya Wachina ambao ilipisha mradi ule tulisema tunahitaji Mradi wa Rufiji *Hydro Power.* Kwa hiyo niwaambie Serikali, hili jambo lina baraka ya Bunge na ndiyo maana mwaka jana tuliwapa bilioni 700 na nina imani hela zimefanya kazi ipasavyo na tunawaunga mkono katika hilo.

Mheshimiwa Spika, na niseme, lazima Serikali muwe imara, msiyumbishwe na miluzi. Kule China wakati wanajenga mradi huu kuna watu baada ya kupiga kura Bungeni, ilitolewa amri ya Serikali kwamba hairuhusiwi mtu yeyote kupinga mradi huu na mtu aliyekuwa anajaribu kupinga kuna watu ambao walifungwa jela. Sasa mimi siwaambii Serikali mkawafunge wanaopinga mradi huu lakini niwaambieni wapuuzeni chapeni kazi tunahitaji Mradi wa Rufiji *hydropower* kwa ajili ya manufaa ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso. Mheshimiwa *Engineer* Gerson Hosea Lwenge ajiandae.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi ningependa kushukuru sana kupata nafasi hii kuweza kuchangia hoja hii ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningependa kumpongeza sana Waziri na Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wote; kazi ambayo wanaifanya kwa kweli ni kubwa sana na inahitaji kupongezwa. Nakumbuka wiki

iliyopita nilikuwa na Waziri kwenye kijiji change kimoja ambacho aliloa tope kabis akutokana na mvua, lakini aliweza kudiriki kuweza kuwasha umeme kwenye baadi ya vijiji. Nakushukuru sana, na namshukuru pia Naibu Waziri ambae ni mwenyeji sana Muheza na tumempa kadi pale kwa hiyo karibu sana na wametembelea sana Jimbo langu la Muheza.

Mheshimiwa Naibu Spika, *REA* awamu ya tatu Muheza tulibahatika kupata vijiji 19 lakini nasikitika kusema, na Naibu Waziri na Waziri wana habari kabisa kwamba mkandarasi ambaye yuko pale Radi ni mkandarasi ambaye ni mbovu sijawahi kuona. Kati ya vijiji 19 katika muda wa miezi 10 ameweza kuwasha umeme kwenye vijiji vitano tu. Kwakweli inasikitisha lakini Mheshimiwa Waziri nilikumbuka na nilikuambia kwamba tafadhali sana naomba vijiji vingine ambavyo vingekuja labda kwenye awamu ambayo itakuja Awamu ya Pili, *REA III* vijiji 28 basi uweze kuniwekea na uweze kunitafutia mkandarasi ambaye kwakweli ni mzuri. Nitakushukuru sana endapo utatimiza ahadi hiyo. Isipokuwa nakushukuru sana kw ajuhudi za kuweza kum-*force* huyu mkandarasi aweze kuweka umeme kwenye sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri kwenye Awamu ya III ya *REA round* ya pili hii mikataba ya hawa wakandarasi ikaangaliwa vizuri; na ni vizuri kama masuala ya *transformer,* masuala ya nguzo na nyaya basi ikanunuliwe moja kwa moja kwenye makampuni ambayo yanahusika badala yake kunakuwa na mikataba mingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ningependa kujikita sasa kwenye mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia *(LNG),* mradi huu ni mkubwa na muhimu sana, Mheshimiwa Waziri na Wizara yako ni vizuri sasahivi mkajielekeza kwenye gesi asilia kwenye huu mradi wa *LNG.* Serikali haijaipa uzito unaostahili mradi huu. Mradi huu ni muhimu sana, na mimi nakumbuka kabisa kwamba mradi huu unaweza ukainua uchumi wa nchi hii kwa nafasi kubwa sana. Makampuni ambayo yalikuwa kwenye huu mradi baadhi yao wameshaondoka na wamekwenda Msumbuji.

Mheshimiwa Waziri, Msumbiji, mradi huu wa *LNG* sasahivi Msumbiji wanauzindua mwezi ujao tarehe 18, iko kwenye *press,* na mradi utakuwa ni *plant* moja kubwa sana katika Afrika na Ulaya. Sasa hatuwezi kuacha hiyo nafasi tukaanza kucheza mradi huu. Nakuomba kabisa Mheshimiwa Waziri elekeza nguvu sasa kwenye huu mradi wa *LNG* tuweze kuinua huu uchumi kwa bidii sana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele imeshagonga Mheshimiwa. Ahsante sana.

**MHE. BALOZI. ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Moshi, Selemani Kakoso atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Gerson Hosea Lwenge tutamalizia na Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru sana kupata nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote niipongeze Serikali kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya ya kupeleka huduma ya Nishati hasa kwenye miradi ya *REA* ambayo kila eneo katika nchi yetu imeweza kufanyika. Nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri kwa jitihada kubwa na juhudi ambazo amezifanya kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo Jimbo la kwangu amefika zaidi ya mara tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri ameenda kijiji cha Kasekese, alipata mapokezi mazuri, makubwa lakini amefanya jitihada za makusudi kusukuma umeme kwenye vijiji vya Majalila, Kijiji cha Ifukutwa, Kijiji cha Kabungu na kwenye eneo la Gereza la Kilimo Kalilangurukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi letu sisi wananchi wa Mkoa wa Katavi, Kigoma na Rukwa hatuna umeme wa *grid* ya taifa, umeme huu ndiyo umeme ambao utakuwa suluhisho la kudumu kwenye maeneo mbalimbali ya mikoa hii mitatu na mr adi wa *grid* ya taifa ni wa muda mrefu toka mwaka 2010 ulianza kuzungumzwa kwenye vitabu mbalimbali vya Wizara. Niwaombe sasa kuwe na jitihada za maksudi ule umeme wa *kilovolt* 400 ambao tunategemea utoke Tunduma hadi Nyakanazi Mkoa wa Kigoma. Uwekwe kwenye mpango ambao na msukumo mkubwa ili uweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme huu utawasaidia wananchi wa Mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma. Tuombe sana Serikali ipeleke fedha kwa ajili ya kuanza mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme wa *REA phase III.* Tunapongeza jitihada za Serikali zilizofanyika lakini kasi ya wakandarasi waliopewa nafasi ya kuandaa miundombinu ya umeme wa *REA III* bado si ya kuridhisha. Pamoja na jitihada nzuri zinazofanywa na Wizara lakini bado uhitaji wa miradi hii kutekelezwa kwa wakati ni mkubwa sana. Nikuombe Mheshimiwa Waziri, umeenda pale Kijiji cha Mchakamchaka umezindua umeme, lakini baada ya kuondoka jitihada zile ambazo zilikuwa zinahitajika kusukuma ili miradi iweze kwenda kwa haraka bado hazijafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimkumbushe Mheshimiwa Waziri alipofika eneo la Kasekese na alipofika Ifukutwa aliwaahidi wananchi wa Wilaya ya Tanganyika kwamba vijiji vyote vitapata umeme wa *REA phase III.* Niombe sana eneo la Mishamo na vijiji vyote vilivyoko kwenye eneo hilo naomba upeleke umeme na mkandarasi umuagize ahakikishe vile vijiji vinapata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liko eneo la ukanda wa ziwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, kengele imeshagonga, ahsante sana.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa *Engineer* Gerson Hosea Lwenge atafuatiwa na Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii ya Nishati kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya. Ninapongeza kwa mambo makubwa manne, kwanza kwa kuweza kuzalisha umeme na tukawa na ziada ya *megawatt* 300, kwa maana kwamba sasa hatuna mgao wa umeme. Jambo lingine ninalokupongeza ni kuanzisha ujenzi wa mradi wa Rufiji *hydropower* ambao tutapata *megawatt* zaidi ya 2115. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la usambazaji wa umeme kwa mradi huu kabambe wa *REA* ambao tunategema kwamba vijiji vyote ikiwezekana vijiji zaidi ya 2,012 vitapata umeme. La mwisho pia nakupongeza kwa kuamua kwamba uunganishaji wa umeme maeneo yote vijijini itakuwa ni 27,000 japokuwa hili lina changamoto hasa pale ambapo wanapaswa wananchi kununua nguzo kwa shilingi 319, kwa mfano kama Mkoa wa Njombe, kwakweli naona kama hii bei ya nguzo kwa mwananchi kuweza kuunganisha umeme ni kubwa. Halafu akiunganisha yeye ile nguzo inakuwa ni mali ya *TANESCO* wale wengine wanakuwa wanaunganishwa kwa 27,000. Mheshimiwa Waziri, mimi naomba jambo hili uliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika huu mradi kabambe wa usambazaji umeme vijijini mwaka jana nilichangia, kwamba kweli ni kazi kubwa tunapeleka miundombinu katika vijiji 12,000 lakini kujenga miundombinu yake na kufanya matengenezo kuwa na uendelevu wa ile miradi lazima tuwe

na mfumo wa taasisi kwa ajili ya matengenezo *(Maintenance)* kama hakuna mfumo mzuri wa *maintenance* miradi hii ita-*collapse.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikichukuliwa mfano kwa Wilaya ya Wanging'ombe, mwaka jana nilisema, kulikuwa na *transformer* 30 zimeungua sasa kama huna mfumo wa kibajeti wa kuweza kumsaidia huyu mtu wa *TANESCO* ina maana kwamba wananchi wataendelea kuwa gizani pamoja na kwamba kazi kubwa mmeifanya. Kwa hiyo naomba sana muangalie mfumo wa kitaasisi wa *maintenance.* Ukichukulia mfano kwenye *TANROADS* tumeweka Mfuko wa Barabara katika Mfuko wa Barabara asilimia 90 zinaenda kwenye matengenezo na ndiyo maana barabara zinakuwa nzuri muda wote lakini kwenye kitabu hiki sijaona mfumo wowote wa *maintenance* wa hii Programu Kabambe ya Usambazaji wa Umeme Vijijini. Naomba jambo hili uliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye Wilaya yangu ya Wanging'ombe, hivi leo ninavyoongea kuna vijiji 54 havina umeme kabisa. Katika programu hiyo inayoendelea kuna vijiji 38 vina matumaini ya kupata umeme. Mkandarasi aliyepo wa Mkoa wa Njombe anaitwa Mufindi *Power joint venture* na *Hagie* kwakweli kasi yake ni mbovu na sidhani kama ataweza kumaliza hiyo December ambayo ndiyo mwisho wa mkataba wake kwa sababu mpaka sasa kwenye wilaya yangu ameweza kuwasha vijiji vinne tu na vitongoji vitano. Kati ya viji na vitongoji 48 sasa kwenye miezi sita nina wasiwasi kwamba sidhani kama anaweza kumaliza. Naomba Mheshimiwa Waziri uangalie namna gani mikataba hii ilivyoingiwa na namna inavyosimamiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimeona kuna udhaifu wa usimamizi. Meneja wangu wa *TANESCO* hana hata gari ya *supervision* anafikaje kwenda kuona huyo mkandaras anavyofanya? Maeneo mengi nguzo zimewekwa wanasema hawana waya na sehemu nyingine wanasema nguzo ndogo hakuna. Sasa kwa mkoa kama Njombe ambapo tunazalisha nguzo ninashangaa kwanini hili linatokea? Kwenye mikataba

najua kuna kipengele kwamba ndani ya siku 30 mtu akileta *certificate* lazima Seriakli ilipe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Kengele imeshagonga, ahsante sana.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Marwa, Ryoba Chacha.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana. Naomba na mimi nichangie kwenye Wizara hii ya Nishati na Madini. Nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Nishati kwa kazi nzuri anayofanya; Mungu akubariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niseme, kama taifa tunahitaji umeme mwingi, na kama ingewezekana leo tukawa na uwezo wa kuzalisha *megawatt* 10,000 ingelipendeza zaidi. Mimi nimpongeze sana Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye ni muasisi wa taifa letu. Mwalimu Nyerere alikuwa na maoni ya kama Taifa la Tanzania tuwe na utoshelevu wa Nishati ya umeme na Mwalimu Nyerere wakati ule alikuwa na maono ya *Stiegler's Gorge.* Sasa bahati mbaya sana wakati ule kama Taifa tulikuwa tunahitaji *megawatt* 100 na uwekezaji kwenye *Stiegler's Gorge* usingewezekana kwa sababu gharama ilikuwa kubwa. Lakini wakati ambao tunao ni wakati mwafaka wa kuwa na umeme unaotokana na *Stiegler's Gorge. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wana hoja dfhaifu sana. Hivi wanataka watuambie kwamba Mwalimu Nyerere alikuwa mjinga, kwamba hakuwa na maono sahihi? Mimi nikuambie, kama kuna mtu anapingana na maono ya Mwalimu Nyerere huyo mtu amelaaniwa. Mwalimu Nyerere alikuwa ni mtu wa *principle,* mwalimu Nyerere alikuwa ni mtu

wa maono, amekufa mzee wa watu hana chochote hana lolote kwa sababu alikuwa na uzalendo mkubwa na nchi hii. Leo nani anayeweza akasema mimi ni mzalendo kuliko Nyerere? Leo watu wanasema *issue* ya mazingira, mazingira kitu gani? Wananchi wa Tanzania wangapi wanatumia kuni na mkaa? Misitu mingapi inafyekwa kwa ajili ya mkaa na kuni? Tuambizane hapa kwa kuja na takwimu. Mimi huko ninakotoka kila mtu anatumia mkaa, kila mtu anatumia kuni, misitu inafyekwa kila leo. Leo sehemu ambayo inafyekwa kwa ajili ya kuwekeza ni sehemu ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme wa maji ni umeme wa gharama ndogo. Unajua mimi kitu siwaelewi watu wa kule upinzani, hawaji na *statistics, research.* Leo tuambieni umeme wa gharama ndogo ni upi kwa *research* ni upi? Umeme wa gharama ndogo ni umeme wa maji; shilingi 36. Sasa ukiwasikiliza hivi hawa wako sawasawa kweli? *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bahati nzuri unajua mimi nimetokea kule unajua kule ili mtu achangie mpaka ale ile kitu ya kwao Heche kule Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanasema waemacha gesi, wameacha gesi wapi? Kwa taarifa yako asilimia 50 ya umeme tunaoutumia unatokana na gesi. Hawasemi hilo, hawasemi kabisa. Leo nimepigiwa simu, kuna watu wana magari yanatumia gesi, hiyo hiyo gesi yanatumia, na kesho Mheshimiwa Waziri amesema wayalete hapa Bungeni Wabunge waone magari yanayotumia gesi yetu. Sasa labda hawajui *master plan* ya nishati yetu. *Our master plan is power mix, energy mix.* Labda tu niwaamabie kwa dondoo kidogo ili waelewe. Upepo kwa *research* iliyofanyika utazalisha *megawatt 500,* solar 500, maji *megawatt* 5,000. Sasa uache umeme wa maji 5,000 uende kwenye nini? Wewe tulia, huelewi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji wa umeme huu wa *Stiegler's Gorge* ndio rahisi kulingana na mazingira ya kiuchumi tuliyonayo. Huwezi kujigamba kwenda kuwekeza

kwenye umeme wa ghali ilhali tuna shida nyingine. Tuwekeze kwenye huu ambao ni *very cheap* lakini umeme mwingi halafu utashuka bei; unajua hofu ni 2020 inawatesa wale jamaa wa kule ng'ambo. Ikifika 2020 wataenda kusema nini? Sasa hivi *REA* kila kijiji watakuwa wamepata umeme au nasema uongo? Kila kijiji watakuwa wamepata umeme, kwa hiyo wanahaha, wenzenu wana shida kweli kweli, hawalali! Sasa wewe unafikiria mtu kama yule Mnyika, atarudi wapi? Au yule Sugu, anarudi wapi? He! *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikwambie kinachowatesa ni hofu ya kutokurudi 2020; na kwa kazi ambayo anaifanya Rais Magufuli mimi nasema Rais Magufuli kamua twende. Nilikuwa nasoma kwenye kitabu cha Kambi ya Upinzani yaani ni kituko. Yaani kweli, taarifa gani hii? Uongo mtupu!

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa najua Mnyika ni Padri kumbe anasema uongo. Hebu sikiliza hii, eti Mnyika anaema *TANESCO* ina madeni inashindwa kujiendesha sijui kitu gani. Hebu sikiliza, *TANESCO* enzi za nyuma ilikuwa inapewa kila mwaka bilioni 143 ruzuku ya Serikali, mwanaume Magufuli alipoingia akasema hakuna cha ruzuku mtajiendesha wenyewe; kwa kuwa ninyi ni Shirika la Serikali, lazima mzalishe faida. Mwaka 2017 *TANESCO* mapato ambayo imekusanya ziada 1.5 ziada! Na wanalipa kila wiki *9 billion TPDC,* wewe unasema nini? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chacha, ahsante sana muda wako umekwisha. Ahsante sana. Muda umeisha.

**MHE. CHACHA M. RYOBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Mheshimiwa Kalemani songa mbele, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha mchana. Wako wachangiaji

ambao hawakupata fursa ya kuchangia leo. Nitawataja hapa kwa sababu hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati inaendelea kesho ili majina yao yaweze kupata fursa kwa ajili ya uchangiaji kesho. Mheshimiwa Bahati Ally Abeid, Mheshimiwa Venance Methuselah Mwamoto, Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo moja la wageni ambao hawakupata fursa ya kutangazwa asubuhi na hawa ni wageni 23 wa Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani, Waziri wa Nishati ambao ni wadau mbalimbali wa Sekta ya Nishati wakiwemo *IOCS TAREA, USAID, JICA, Norway Embassy* na *EDPG.* Karibuni sana. Wageni hawa walikosa fursa ya kutangazwa asubuhi.

Jambo lingine dogo ni la kukumbushana Waheshimiwa Wabunge, hasa wa upande wa upinzani. Kwamba hoja huwa inakuwa ni moja tu kwa hivyo nawakumbusha, ukisema unaunga mkono maana yake unaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo niwapongeze kwa kuunga mkono hiyo hoja; kwa sababu kuna tofauti ya kuunga mkono na kukubaliana na maoni ya Kambi ya Upinzani. Hiyo si hoja, hoja inakuwa ni moja tu na sasa hoja ni ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati. Kwa hiyo nawakumbusha tu kwamba hoja ni ya Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema haya...

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nikiwa nimesimama hamruhusiwi kuongea, kwa hiyo hata kama unaomba mwongozo huruhusiwi kuomba nikiwa nimesimama ndiyo kanuni zetu zinavyosema. Kwa hiyo, huruhusiwi kuongea nikiwa naongea. Sasa kwa sababu huwa kuna utaratibu wa kuvunja kanuni hivi, watu huwa wanarahisisha mambo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho asubuhi saa tatu kamili.

*(Saa 12:00 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 29 Mei, 2019 saa Tatu asubuhi)*